

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Januari, 2019

(Saa Tatu Asubuhi Bunge Lilianza)

WIMBO WA TAIFA

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Mbunge afuataye aliapa:-

Mhe. Abdallah Ally Mtolea

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa taarifa kwenu kwamba katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Bunge lilipitisha Muswada wa mmoja wa Sheria uliokuwa ukiitwa Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za za Kifedha wa Mwaka 2018 (*The Microfinance Bill, 2018*). Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari

Muswada huo umepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na kwa hiyo, imekuwa imekuwa ni sheria ya nchi inayoitwa Sheria ya Huduma Ndogo za Kifedha Na. 10 ya Mwaka 2018 (*The Microfince Act No. 10 of 2018*)

Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za kuwasilishwa mezani Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:-**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

Toleo Na. 44 la tarehe 02 Novemba, 2018;
Toleo Na. 45 la tarehe 09 Novemba, 2018;
Toleo Na. 46 la tarehe 16 Novemba, 2018;
Toleo Na. 47 la tarehe 23 Novemba, 2018;
Toleo Na. 48 la tarehe 30 Novemba, 2018;
Toleo Na. 49 la tarehe 07 Desemba, 2018;
Toleo Na. 50 la tarehe 14 Desemba, 2018;
Toleo Na. 51 la tarehe 21 Desemba, 2018;
Toleo Na. 52 la tarehe 28 Desemba, 2018;
Toleo Na. 01 la tarehe 04 Januari, 2019;
Toleo Na. 02 la tarehe 11 Januari, 2019; na
Toleo Na. 03 la tarehe 18 Januari, 2019.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tunakushukuru. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Bado ya Wizara.

SPIKA: Aah bado, *okay* malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 [*Political Parties (Amendments) Bill, 2018*].

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kuwasilisha huo Muswada mbele yetu. Nilichanganya kidogo mambo. Unajua leo asubuhi palikuwa bundi; bundi *original*, siyo..., hapo juu hapo. Kwa Dodoma, bundi wa mchana hana tatizo, ila wa usiku ndiyo shida. (*Kicheko*)

Waheshimiwa tunaendelea. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria tafadhali. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Mchengerwa. Karibu. (*Makofii*)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na ushauri wa kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 [*Political Parties (Amendments) Bill, 2018*].

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

**MHE. CATHERINE N. RUGE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZI MKUU, SERA,
BUNGE, KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kuhusu Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018
[The Political Parties (Amendments) Bill, 2018].

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linalelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ilivyo kawaida, linaulizwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 1

**Baadhi ya Kampuni Binafsi Kukandamiza
Wafanyakazi**

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI (K.n.y. MHE. MUNIRA
MUSTAPHA KHATIB)** aliuliza:-

Baadhi ya Kampuni binafsi zimekuwa zikiwafanyisha kazi Watumishi wao zaidi ya muda wa saa za kazi, kutowapa chakula na kuwalipa kima kidogo cha mshahara:-

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu suala hilo linalowakandamiza Wafanyakazi hao ambao wengi wao ni vijana?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA
VIJANA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inasimamia ipasavyo mahusiano ya kikazi sehemu zote za kazi ikiwa ni pamoja na kampuni binafsi. Kupitia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, Serikali inasimamia viwango stahiki nya kazi ikiwa ni pamoja na masaa ya kazi, likizo mshahara na kazi staha kwa wafanyakazi wa sekta zote.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Mwajiri kutii matakwa ya sheria kwa kumlipa mfanyakazi wake mshahara na maslahi stahiki. Hivyo, mwajiri anayekiuka matakwa ya sheria hii anastahili adhabu.

Aidha, katika kuimarisha uwajibikaji upande wa waajiri, mwaka 2016, Bunge letu Tukufu lilifanya marekebisho katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya Mwaka 2004 na kuimarisha mfumo wa kaguzi za kazi mahali pa kazi kwa kuruhusu kutoa adhabu za papo kwa papo (*compounding of offences*) kwa waajiri wanaokiuka matakwa ya sheria, ikiwa ni pamoja na kutowalipa wafanyakazi malipo ya ziada kwa saa za ziada walizofanya kazi na kulipa mshahara chini ya kiwango cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itaendelea kusimamia sheria na kuimarisha mahusiano kati ya waajiri na wafanyakazi na kufanya kaguzi za kazi sehemu za kazi ili waajiri watimize wajibu wao kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Khadija Nassir.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile bado malalamiko ya waajiriwa ni mengi sana nchini na bado utaratibu haujafafanua vizuri ni namna gani ambavyo waajiriwa hawa wanaweza kupata stahiki zao na usalama wao wakati

wakiwa katika maeneo ya kazi, Serikali ina kauli gani juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa vile bado ajira zetu za ndani hazina sheria ya moja kwa moja ambayo inawalinda waajiriwa, Serikali pia inasema nini juu hili?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Spika, katika swali la kwanza kuhusu malalamikio, Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikiyafanya kazi malalamiko na taarifa mbalimbali zinazowahusu wafanyakazi kwa kufanya kaguzi mbalimbali ambazo lengo la kaguzi hizi ni kutaka waajiri wote nchini wafuate utaratibu wa sheria unavyoolekeza kwa maana ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria Na. 7 ya mwaka 2004 ambazo zimetoa haki na wajibu kwa wafanyakazi pamoja na waajiri.

Mheshimiwa Spika, ofisi yetu imeendelea kuchukua hatua kwa waajiri wote ambao wanakiuka sheria na mpaka ninavyozungumza hivi sasa, tayari tumeshawafikisha Mahakamani zaidi ya waajiri 19 katika kipindi cha mwaka 2017/2018 ambao wamekiuka utaratibu wa sheria. Ndiyo maana Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuelpukana na malalamiko haya ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya swali lake Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua kuhusu sheria ya kuwalinda wafanyakazi. Kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 2004, imainisha bayana haki za mfanyakazi na wajibu wa mwajiri. Sheria hii ndiyo inayotumika katika kuwalinda wafanyakazi. Ndiyo maana Bunge lako Tukufu mwaka 2016 liliifanya marekebisho ili kuongeza meno zaidi katika Idara ya Kazi katika kuwalinda wafanyakazi kwa kuhakikisha kwamba ikitokea mwajiri anakiuka taratibu za

kisheria kuhusu mikataba na masaa ya kazi, Afisa Kazi akienda kumkagua atakuwa na uwezo wa kumtoza faini hapo hapo ambayo ni kiasi cha fedha, ambapo pia baadaye atakuwa na *compliance order* haya yote yaende kwa pamoja. Lengo ni kufanya sheria hiyo iwe na meno na wafanyakazi wetu waweze kulinda haki zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda Mbunge wa Handeni, kwa Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Kigoda, tafadhali.

Na. 2

Majengo ya Madarasa Yaliyotokana na Nguvu za Wananchi

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali kupitia Halmashauri itakamilisha majengo ya madarasa yaliyotokana na nguvu za wananchi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Abdala Kigoda, Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua juhudzi za wananchi na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Elimu ikiwa ni pamoja na kusaidia ujenzi wa miundombinu ya shule kama vile vyumba vya madarasa, madawati, matundu ya vyoo, nyumba za Walimu, mabwalo na maabara.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Handeni ina maboma yapatayo 15 ya vyumba vya madarasa yaliyoanza kwa nguvu za wananchi na kati ya hayo, maboma sita yako katika hatua ya lenta. Hadi Januari, 2019 Halmashauri imepokea jumla ya shilingi 46,600,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma yaliyoanza kwa nguvu za wananchi ili yaanze kutumika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau kupitia Programu ya Lipa kwa matokeo (*EP4R*) na Programu ya kuimarisha ubora wa Elimu Tanzania (*EQUIP-T*) itaendelea kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Aidha, Halmashauri zinahimizwa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyopo kabla ya kuanzisha miradi mipyta. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Nimekuona Mbunge wa Handeni, swali la nyongeza.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na suala la elimu bure, imeleta changamoto ya kuwa wanafunzi wengi sana ambao wamejiandikisha, lakini kuna uhaba mkubwa sana wa Walimu ambao unasababisha hawa wanafunzi wasipate elimu bora: Je, Serikali ina mpango gani mkakati wa kuajiri Walimu wengi zaidi ili hawa wanafunzi waweweza kupata elimu bora? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, elimu bora Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala Mikoa na Serikali za Mtaa, Mheshimiwa Mwita Mwkwabe Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba elimu ya msingi bila

malipo imeleta chachu ya maendeleo na mwamko mypa na wanafunzi wengi wamejiandikisha na kuingia katika mfumo wa elimu Tanzania. Hili ni jambo jema na kupongezwa kwa maamuzi thabiti ya Mheshimiwa Rais kwa Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo ni kwamba tunao Walimu zaidi ya 11,000 katika Shule za Sekondari, ambao hawa tunaona kwamba mzigo wao siyo mkubwa sana, tumeomba kibali washushwe waje kufundisha Shule za Msingi ili waweze kuziba *gap* la uchache wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kumekuwa na wale Walimu ambao wanastaifu na wengine wanapata makosa ya kinidhamu kazini na wengine wanafariki dunia, lakini hapa katikati kumekuwa na mkwamo kidogo, Mheshimiwa Rais amesharuhusu kuajiri angalau kila mwaka kupunguza *gap* hili.

Mheshimiwa Spika, mpango wa tatu, tumepata kibali cha kuajiri Walimu zaidi za 6,000 ambao wakiajiriwa watapunguza upungufu wa Walimu katika Shule zetu za Msingi. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, tunaenda swalii la tatu, bado tupo TAMISEMI, litaulizwa na Mheshimiwa Gibson Blasius Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swalii la tatu, bado tupo TAMISEMI litaulizwa na Mheshimiwa Gibson B. Ole Maisemeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi.

Na. 3

Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Lami Kilometra 12

MHE. GIBSON B. OLE MEISEYEKI aliuliza:-

Mheshimiwa Rais Mstaifu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi ujenzi wa

barabara yenye urefu kwa kilomita 12 katika Jimbo la Arumeru Magharibi na sasa imepita miaka 10 bila kutekelezwa ahadi hiiyo:-

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hiyo hasa ikitiliwa maanani kuwa katika Jimbo la Arumeru Magharibi hakuna barabara ya lami hata nusu kilomita?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gibson Blasius Ole Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Maghari kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara ya lami kilomita 12 Arumeru Magharibi mwezi Novemba, 2012 kwenye uzinduzi wa Hospital ya Wilaya ya Oltrumeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaanza utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais Msaafo ambapo kati ya mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2017/2018 barabara zenye urefu wa kilomita 3.55 kwa kiwango cha lami zimejengwa Arumeru Magharibi kwa gharama ya shilingi billioni mbili. Barabara zilizojengwa ni kama ifuatavyo: Mianzini-Timbolo kilomita 0.8; Sarawani-Oldonyosapuk kilomita 0.7; Tribunal Road kilomita 2.5; na Sekei-Oglai kilomita nne (4). Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami kwa kadiri fedha zinavyopatikana.

SPIKA: Swali la nyongeza nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru Magharibi.

MHE. GIBSON B. OLE MEISEYEKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimekuwa nikisubiria majibu ya swali hili kwa miaka mitatu sasa, lakini majibu niliyopewa siyo ya barabara ambazo Mheshimiwa Rais aliziahidi. Rais alipokuwa anaomba

kura mwaka 2005 alitoa ahadi ya kilomita 12 ya bararaba inayoanzia Ngaramtoni kupitia hospitali ya Selian mpaka kwa Luhijo kilomita 12. Alipochaguliwa 2012 akatuongeza barabara nyingine inayokwenda Hospitali ya Oltrumeti. Barabara zote hizi hazina lami mpaka sasa. Je, ni lini sasa Serikali itapata fedha ili iweze kuteleza ahadi hiyo ya Rais kwa barabara hizo ambazo alituahidi hizi nyingine alizozisema Mheshimiwa Waziri hazihusiani na swali langu?

Mheshimiwa Spika, pia ametaja kwamba barabara ya Sarawani inatengenezwa, ni kweli, lakini imekuwa ikitengenezwa kilomita 0.8 kwa takriban mwaka mzima sasa hajakamilika. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongoza na mimi kwenda Arumeru Magharibi tukaangalie maendeleo na ubora wa barabara hii ya Sarawani - Oldonyosapuk ambayo kwa zaidi ya mwaka mzima inatengenezwa na bado hajakamilika? (*Makofii*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mbunge unauliza maswali ya 2005 leo 2019 uliza maswali ya Awamu ya Tano, ndiyo Mawaziri wakujibu. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, nilikuwa na wasiwasi kwamba Mheshimiwa Mbunge angesema barabara hizo hajijaja kwenye jimbo lake lakini na yeye tunakubaliana kwamba barabara hizo zimejengwa kwenye jimbo lake, kwa hiyo, naamini kuwa Mheshimiwa Mbunge ana kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa kujenga barabara hizo ndani ya jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi ambazo tumetoa ni ahadi thabiti na kwa kadri uhitaji wa wakati unavyoruhusu ndio tunaenda kwenye barabara hizo. Kwa hiyo naomba nimhakikishie kwamba ahadi za Rais wetu aliyetangulia ambaye sasa amepokea kijiti Rais tuliyenayo bado ni ahadi za CCM, tutazitekeleza kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaomba fursa nikatazame hiyo barabara ambayo imekuwa ikitengenezwa ya kilomita 0.8, nalo ni jambo la kushukuru kwa sababu angeniambia kuwa hajaanza kutengenezwa kabisa *then* hata kuongea kwake ingekuwa tofauti. Naomba nimhakikishie kwa kadiri ratiba itakavyokuwa inaruhusu mimi nipo tayari kuambatana naye.

SPIKA: Tunaendelea na swali la nne linaulizwa na Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi kuelekea Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu hili, naomba uniruhusu kwa sekunde chache kukushukuru wewe kutoka katika sakafu ya moyo wangu kwa jinsi unavyosimamia suala la umeme la VAT Zanzibar na kuondoshewa mzigo huu na hatimaye Zanzibar kuweza kuvuta pumzi baada ya kuwa *ICU* kwa muda mrefu. Nikushukuru na nawashukuru vilevile waliokupa nafasi ya kuwa mlezi upande wa Zanzibar, nasema hawakukosea, matatizo yao mengi na naamini utatusaidia.

Baada ya maelezo hayo, naomba swali langu lijibiwe.

SPIKA: Ahsante sana. Shukrani hizo ziende kwa Baraza la Mawaziri pamoja na Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa kulimaliza jambo hili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhalii.

Na.4

ATCL Kuanzisha Safari za Ndege - Zanzibar- Dodoma

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuza:-

ATCL Corporation ni Shirika la Ndege la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na limekuwa likifanya vizuri chini ya Uongozi wa Mkurugenzi Mkuu *Engineer Matida*:

(a) Je, kwa nini ATCL kila Jumatatu inapoondoka Dar es Salaam kwenda Dodoma isipitie Zanzibar ili viongozi pamoja na wananchi wanaotaka kwenda Dodoma wapate huduma hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa safari za ATCL kutoka Dar es Salaam zipitie Zanzibar kwa Jumatatu zote kupunguza tatizo la usafiri kwa wananchi wa Zanzibar wanaotaka kwenda Dodoma kwa shughuli mbalimbali?

(c) Je, ni lini safari hizo zitaanza ili viongozi, wananchi wa watalii kutoka Zanzibar waone kuwa Serikali yao inawajali na inadumisha Muungano wetu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, dhumuni la Serikali kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ni kuhakikisha wananchi wote wa Tanzania Bara na Visiwani wanapata huduma ya usafiri wa anga kwenye kituo (*destination*) chochote chenye maslahi ya kibiashara. Aidha, ATCL inatumia kituo cha Dar es Salaam kama kitovu ili kuwa na muunganiko wa kupeleka abiria sehemu nyingi na kukidhi mizania ya kibiashara kwani bila kufanya hivyo inaweza kukosa abiria wa kutosha kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, Serikali kupitia ATCL imebaini kuwa Zanzibar ni moja ya vituo ambavyo kuna maslahi kibiashara. Hivyo, imesharekebisha ratiba zake ili kuhakikisha wasafiri kutoka Zanzibar wanakuwa na uwezo wa kusafiri kwenda Dodoma kupitia kitovu (*hub*) cha Dar es Salaam kwa kuwa na ndege ya siku ya Ijumaa kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam ambapo abiria hao wataweza

kuunganisha safari kwenda Dodoma kwa ndege ya alasiri siku hiyo hiyo ya Ijumaa Aidha, *ATCL* ina ndege ya Jumapili inayotoka Zanzibar kuja Dar es Salaam asubuhi ambayo itaungaisha na ndege inayokwenda Dodoma.

(b) Kama nilivyoeleza kwenye jibu la kipengele (a) cha swali hili, hivi sasa siyo wakati muafaka kwa kila Jumatatu ndege ya *ATCL* inapoondoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ipitie Zanzibar. Aidha, utaratibu huo wa safari za *ATCL* kutoka Dar es Salaam kupitia Zanzibar kwa kila Jumatatu utaanza pindi muunganiko wa kupeleka abiria Zanzibar kutoka Dar es Salaam na sehemu zingine kwa siku ya Jumatatu utakidhi mizani ya kibiashara.

(c) Safari za *ATCL* kila Jumatatu kutokea Dar es Salaam kwenda Dodoma kupitia Zanzibar kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali (b) zitaanza pindi muunganiko wa kupeleka abiria sehemu zingine kupitia Zanzibar utakapokidhi mizani ya kibiashara.

Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawajali viongozi, wananchi na Watalii kutoka Zanzibar na ndio maana inajitahidi kwa kila hali kuhakikisha kuwa Viongozi, Wananchi na Watalii kutoka Zanzibar wanapata usafiri wa kuunganisha kutoka kituo cha Dar es Salaam kama kitovu kwenda Dodoma kwa kadiri inavyowezakana.

SPIKA: Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru Naibu Waziri huyu ambaye amekuwa akishughulika sana kwa suala la Muungano, mara utamkuta Pemba mara Unguja na mambo mengi ni sare ya Muungano anaileta Baraza la Wawakilishi, ni Waziri Naibu wa pekee na niombe Manaibu Mawaziri wengine mfuate nyayo zake huyu bwana na hana kiburi hata kidogo. Mheshimiwa Naibu Waziri sikusifu kwa kuwa upo mbele yangu lakini kiburi huna na Manaibu Waziri na Mawaziri wafuate nyayo zake.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ndege kuondoka kule Ijumaa na Jumapili nimwambie kuwa ndege kule inaondoka saa mbili na kufika hapa 2.30 kutoka saa tatu mpaka saa 10 jioni huoni ni *fatigue* na ni adhabu hii kwa Wazanzibari: Sasa, swalii la kwanza, je, ni lini atafanya utaratibu huu wa kujipanga upya kuona Zanzibar ni haki yao ya msingi katika Shirika hili la Ndege la Air Tanzania na hii Tanzania ni mmiliki kutokana na muungano wa Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania?

Mheshimiwa Spika, *ATCL* tokea mwaka 2007 inadaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar shilingi milioni 241 na amekiri humu ndani kuwa watalipa na mpaka hii leo ikiwa mimi ni mjumbe wa Kamati hii hawajalipa deni hili? Pia je, ni sababu gani zilizopeleke Wajumbe wa Bodii ya *ATCL* hata upande mmoja...

SPIKA: Mheshimiwa Jaku maswali yanazidi mawili yanakuwa mengi sana. Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshasikia, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali, usijibu zaidi ya mawili chagua tu katika hayo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba abiria wa kutoka Zanzibar kuja Dodoma wakipitia Dar es Salaam huwa wanachukua muda mrefu sana wakisubiri ndege ya kuwaunganisha, hilo tumeliona na kwa kweli tunalifanya kazi, kama mnakumbuka juzi wakati tunapokea ndege yetu nyingine tumeahidiwa na Mheshimiwa Rais kuwa tutakuwa na ndege za Viongozi ili tuziweke kwenye *ATCL* ili tuweze kuhudumia.

Mheshimiwa Spika, lengo la *ATCL* ni kuhudumia Watanzania wote bila usumbufu wowote. Kwa hiyo, tukapozipata hizo tutahakikisha wasafiri wa Zanzibar kuja Dodoma hawachukui muda mrefu sana pale uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Jaku ameuliza kuhusu deni la shilingi milioni 241 ambayo *ATCL* inadaiwa kama *landing fee* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Ni kweli hilo deni tunalikumbuka na tunalifahamu na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa linafanyiwa kazi na Mamlaka za Ukaguzi; tukishalihakiki tutalipa. Tunaendelea kulipa madeni kwasababu *ATCL* ina madeni mengi na inaendelea kuyalipa baada ya kuyahakiki.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum.

Na.5

Kupanua Jengo la Mama na Mtoto – Muhimbili

MHE. ANATROPIA L. THEONEST aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ambalo hata akinamama wajawazito wawili hawawezi kupishana kwenye *corridor*?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kupanua eneo la jengo hilo kutaenda sambamba na kuhamasisha wanaume kwenda kliniki na wenza wao na kupata ushauri pamoja?

(c) Katika eneo la kujifungulia la akinamama ni rahisi kuona kitanda cha jirani yako; je, Serikali haioni hali hii ni udhalilishaji pamoja na kuingilia uhuru wa mwingine kujihifadhi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naombaa kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuboresha huduma za akinamama wajawazito, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, mnamo mwaka 2016 alielekeza kuwa Ofisi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zilizokuwa eneo la Hospitali ya Taifa Muhimbili kuhama na jengo hilo kutolewa kwa Hospitali ya Taifa ili kupunguza msongamano wa akinamama wajawazito katika jengo la *Maternity*. Hivyo basi, ikumbukwe kuwa jengo hili lilikuwa ni Ofisi na libadilishwa matumizi kuwa jengo la mama na mtoto, hivyo, miundombinu ya jengo hili hairuhusu kufanyiwa upanuzi.

Mheshimiwa Spika, jengo hili limewekwa viti vyakutosha katika *corridor* ambayo vinatosheleza kukaa akinamama pamoja na wenza wao. Natoa rai kwa wanaume kuambatana na wenza wao kliniki ili kupata elimu ya kutunza ujauzito; maandalizi ya kujifungua na matunzo ya mtoto ajaye, mwitikio kwa sasa kwa wanaume sio wa kuridhisha.

Mheshimiwa, Spika huduma za akinamama hasa za kujifungua zinahitaji usiri mkubwa. Hiki ni kipaumbele cha Serikali na kwa Watumishi wa Afya katika vituo mbalimbali nchini. Hivyo, katika jengo hili eneo la kujifungulia lina vitanda 20 ambavyo vimetenganishwa na mapazia imara (*screen folds*) ambapo akinamama hawaonani wakati wa kujifungua na hivyo kutunza faragha zao.

SPIKA: Mheshimiwa Anatropia, wewe ulionaje kuwa wanaonana? Swalii la nyongeza tafadhalii.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru swalii la nyongeza la kwanza, ni ukweli kwamba idadi ya akinamama wanaoendelea kujifungua kulingana na takwimu inaendelea kuongezeka, lile jengo kusema ukweli bado ni finyu sana kiasi cha kupelekea akinababa kushindwa kuandama na wenza wao, kinyume na alivyosema Naibu Waziri. Sasa swalii langi sio kweli kwamba jengo lile halijezi kubadilishwa, jengo linaweza likaondolewa likajengwa ghorofa angalau moja au likajengwa ghorofa moja sehemu

nyingine Serikali ipo tayari kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga eneo angalau la ghorofa moja kuweza kuwa-*accommodate* watu hawa ambao wanabanana kwenye *corridor*?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kujifungua ni tendo la faragha sana, wote mtajua Madaktari akinamama wanavyoenda kwenye hicho kitendo wengine wanaweza kutoka vinyesi, wengine wanapata kifafa cha mimba, wengine wanatokwa na maneno ya ajabu na shida nyingine kama hizo ambao wamepitia uzazi wanajua, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza vyumba ambavyo *concrete* au ku-*separate*vile vitanda na *concrete* au kujenga *partition* ambazo mwanamke mmoja na mwengine hawawezi kuonana tofauti na ilivyo leo kwamba mmeweka pazia ambazo kiukweli wanaonana na inadhalilisha utu wao. Naomba sasa Serikali ituambie ni lini ipo tayari kutengeneza *partition* kwa ajili ya kustiri utu wa mwanamke pale anapokwenda kujifungua.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya haya maswali ya kujifungua hutaweza bwana wewe hujawahi ku..., mwachie mwenyewe. Mheshimiwa Waziri wa Afya tafadhli maana maswali nyeti haya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatriopia. Kwanza suala kwa nini tusiongeze jengo lingine Muhimbili Mheshimiwa Mbunge alitakiwa kutushukuru kwa sababu lile ni jengo la ziada, baada ya Mheshimiwa Rais mara tu baada ya kuapishwa alikuta mrundikano wa wangojwa akatunyang'anya ofisi Wizara ya Afya na jengo lile tukaliboresha na kuwa ni jengo la Wazazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru umenipa fursa ya kujibu hili swalii. Muhimbili *National Hospital*, tumefuta kliniki za mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Muhimbili. Pale tunapeleka wajawazito ambao wana matatizo ya kujifungua. Kwa hiyo hata ule mrundikano wa wagonjwa wataenda Mwananyamala, wataenda Amana, wataenda

kwenye vituo vya afya 350 ambavyo Serikali imeviboresha ili kuvivezesha kutoa huduma. Nitoe wito kwa wanawake, Muhimbili ni *National Hospital* sio mtu yoyote unaenda tu kwa ajili ya *chek up*.

Mheshimiwa Spika, suala la pili anataka *partition*, Mheshimiwa Mbunge angetembelea vituo vya afya tunavyojenga, asingeuliza hili swali, tunajenga kwa kuhakikisha tumeweka *partition* kwa vituo vya afya vyote. Lengo letu sisi anachosema ufaragha, tunafikiria iliwezekana hata baba amsindikize mama anapotaka kwenda kujifungua. Kwa hiyo tumeliona kama Wizara na tumeweka *partition* zenyenye staha katika vituo vya afya. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo na ninavyoangalia angalia Tanga kule hakuna machaka kabisa. Anatropia amefurahi amepata majibu ya uhakika kabisa.

Sasa tunaingia Wizara ya Nishati, swali linaulizwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe (*Makofii*)

Na. 6

Utekelezaji wa REA III Mwanga

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE aliuliza:-

Awamu ya III ya *REA* ilizinduliwa Wilayani Mwanga mnamo Julai, 2017 lakini hadi sasa utekelezaji wake haujaanza;

Je ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijiji katika Wilaya ya Mwanga kuitia REA awamu ya tatu ulianza mwezi Oktoba, 2017 ukifanywa na Mkandarasi Kampuni ya *Urban and Rural Engineering Service Limited*. Katika mzunguzuko wa kwanza vijiji 14 vya Wilaya ya Mwanga vitapatiwa umeme vikiwemo Vijiji vya Ndorwe, Kinghare, Kigoningoni, Kiriche, Mangulai, Kirya, Lungurumo, Mangara, Kiverenge, Kichwa, Chang'ombe, Vuchama Ngofi na Ngujini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Vijiji vya Wilaya ya Mwanga inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 10.98, njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 24, ufungaji wa transfoma 12 za KVA 50 pamoja na kuwaunganisha wateja wa awali 347. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi za awali ikiwemo uchimbaji wa mashimo na kusimika nguzo katika Kata ya Kirya. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo itakamilika mwezi Juni, 2019. Gharama ya mradi ni Sh.1,350,000,000.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Maghembe, Mbunge wa Mwanga, nimekuona, tafadhali.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru sana Wizara na Waziri wa Nishati na Madini, kwa jibu zuri sana ambalo ametupatia. (Makofsi)

Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika maeneo ambayo tayari yamepatiwa umeme kule vijijini, wako wananchi wengi sana ambao bado hawajapatiwa umeme kinyume na ahadi ambazo tumepewaa hapa Bungeni kwamba kila mmoja atakayepitiwa na nguzo au waya za umeme na yeze atapata umeme. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba hawa watu ambao wamepitwa bila kufungiwa umeme wanafungiwa umeme kama wenzao waliofungiwa awali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Tarafa yetu ya Jipe ambayo ina urefu wa kilomita 70 kuanzia mwanzo mpaka mwisho, viko vijiji viwili ambavyo bado havijahudumiwa na mradi wa *REA* ambavyo ni Vijiji vya Kwanyange na Karambandea. Serikali ina mpango gani wa kuvihudumia vijiji hivi na kuvipatia umeme?

SPIKA: Karibu sana Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalo, sijui kama vijiji hivyo utakuwa unavifahamu lakini jaribu kujibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayofanya katika Jimbo lake. Nilifanya ziara mwaka jana mwezi kama huu niliona namna ambavyo anashughulika na kero za Nishati katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kwenye maeneo ambayo yamepitiwa na miundombinu ya umeme mkubwa lakini baadhi ya wananchi hawajapata kuunganishiwa umeme, napenda nimtaarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imepanga Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili baada ya mafanikio ya Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa Ujazilizi Awamu ya Pili ambaao utaanza Machi, 2019 unahuisha mikoa tisa ya awali ikiwemo Mkoa wa Kilimanjaro lakini baadaye mwezi Julai, 2019 tutaanza Awamu ya Pili katika mikoa iliyosalia. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi ambaao hawajapata umeme katika vijiji ambavyo miundombinu ya umeme imefika kupitia Mradi wa Ujazilizi watafikiwa na huduma hii ya nishati.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linahusiana na vijiji katika Tarafa ya Jipe ambapo Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Jimbo la Mwanga anasema bado havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba licha ya Mradi wa Ujazilizi, Serikali pia kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) imeanza Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili ambapo upembuzi yakinifu umeanza na hivyo vijiji viwili vitafikiwa na miundombinu ya umeme baada ya mradi huo kuanza. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, bado tuko Wizara ya Nishati, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

Na. 7

**Maporomoko ya Maji na Jotoardhi Kuzalisha
Umeme Busokelo**

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Halmashauri ya Busokelo ina maporomoko ya maji (*waterfalls*) maeneo mbalimbali na jotoardhi (*geothermal*):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia maporomoko hayo ya maji (*waterfalls*) na jotoardhi (*geothermal*) kuweza kuzalisha umeme ili kupunguza changamoto ya umeme nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Busokelo kuna maeneo yenye maporomoko ya maji yanayoungana na maporomoko yaliyoko Wilaya ya Makete katika Mto Rumakali. Upembuzi yakinifu katika maeneo hayo ulifanywa na Serikali mwaka 1998 kwa ushirikiano na Serikali za Norway na Sweden.

Mheshimiwa Spika, kulingana na upembuzi yakinifu huo maporomoko ya Mto Rumakali yanaweza kuzalisha umeme wa MW 222. Kwa sasa *TANESCO* inaendelea na kazi ya kuhuisha upembuzi yakinifu kuititia ufadhili wa Benki ya Dunia kabla ya kuanza hatua za utekelezaji. Utekelezaji wa mradi utaanza Aprili, 2020 na kukamilika Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya jotoardhi ya Ngozi, Kiejo-Mbaka Mkoani Mbeya na Songwe Mkoani Songwe. Miradi hili yote imefikia hatua ya uchorongaji visima vya majoribio ili kuhakiki kiasi na ubora wa rasilimali ya jotoardhi katika maeneo hayo. Aidha, *TANESCO* kuititia Kampuni Tanzu ya Jotoardhi inaendelea na utafiti wa vyanzo vya umeme wa jotoardhi katika eneo la Mbaka katika Halmashauri ya Busokelo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo yataonyesha hali halisi ya uwezo wa kuzalisha umeme kwa nguvu za jotoardhi itakayopatikana katika eneo husika. Kazi ya utafiti na uchorongaji huo inatarajiwa kukamilika mwaka 2022.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, swali tafadhalii.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nimpongeze pia Waziri mwenye dhamana kwa namna ambavyo waliweza kutembelea Jimbo langu la Busokelo na kufanya mikutano mingi na wananchi wale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa mradi huu umechukua muda mrefu, ni zaidi ya miaka 21 sasa tangu upembuzi yakinifu ufanyike, je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha mradi huu ili ifikapo 2022 uweze kukamilika badala ya mwaka ambao Mheshimiwa Waziri ameusema? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa umeme wa jotoardhi ni umeme endelevu kwa maana ya *renewable* na tumeona katika nchi yetu na tafiti zimeonyesha tunaweza kupata *megawatts* zaidi ya 5,000 kwa vyanzo vyote ambavyo vimeainishwa kwa nchi nzima ya Tanzania. Je, Serikali ina mpango gani wa kuviedeleza vyanzo hivyo ili Tanzania ifikapo 2025 iwe ni nchi ya uchumi wa kati? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe Dkt. Kalemani, tafadhalii.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya awali ambayo ametoa ufanuzi mzuri sana katika mradi wa kuzalisha umeme wa jotoardhi. Sambamba na shukrani kwa Naibu Waziri wangu, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mwakibete kwa anavyofuatilia masuala ya rasilimali ya jotoardhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakibete, la kwanza amesema imechukua muda mrefu kufanya utafiti kwa takribani miaka 21. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge lakini niwape taarifa Watanzania kwamba katika hatua za utekelezaji wa upembuzi yakinifu, mradi ambao umeenda kwa kasi katika miradi ya jotoardhi ni pamoja na mradi huu wa Ngozi ambao utatuzalishia MW 20. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida miradi ya jotoardhi, upembuzi yakinifu huchukua takribani miaka 25 - 40. Kwa hatua hii, ndiyo maana tunasema tumekwenda kwa kasi na tuna matumaini ya kukamilisha mapema mwaka uliotajwa wa 2023 tutapata MW 30.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili, nchi yetu ina rasilimali nyingi sana na madini ya jotoardhi (*geothermal*) kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Rasilimali tullyonayo inaweza kutuzalishia *megawatt* zaidi ya 5,000, ingawa kwa sasa tathmini zinavyoonyesha tunawenza tukaanza kuzalisha MW 200 kwa kuanzia ifikapo miaka mitano ijayo. Tutaanza na MW 30 ambayo itatoka kwenye eneo la Ngozi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini nieleze tu kidogo, niwapongeze sana wananchi wa Mbozi na wananchi wengine wa maeneo yanayozunguka mradi huu kwa sababu wametupa ushirikiano mkubwa wa kufanya tathmini. Hivi sasa tunaendelea na kufanya tathmini ya maeneo mengine mengi nchini ikiwemo eneo la Majimoto kule Katavi ambayo nayo itatuzalishia *megawatt* za uhakika. Kwenye mradi wetu tutapata MW 5,000 miaka kumi au ishirini ijayo lakini itakuwa ni umeme wa uhakika ambaa uta-*stabilize* sana upatikanaji wa umeme hapa nchini. Ahsanteni sana.

SPIKA: Tunaelekeea Kilimo, swalii linaulizwa na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Gimbi tafadhalii.

Na. 8

Bei Ndogo ya Pamba

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwapangia wakulima wa pamba bei ndogo wakati wa mavuno bila kuzingatia gharama kubwa walizotumia kipindi cha uzalishaji:-

Je, Serikali haioni sasa wakati umefika kuwaacha wakulima wauze pamaba kwa bei kubwa wanayotaka wao? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo la Mheshimiwa Gimbi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L.
BASHUNGWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, kwa ridhaa yako, naomba nitumie nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kuweza kusimama hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kipekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na wasaidizi wake kwa kuniamini na kunitfea katika hii nafasi ya Naibu Waziri wa Kilimo. Namuahidi Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake, nitafanya kazi kwa uadilifu na kwa maarifa yangu yote katika kutekeleza majukumu ambayo wamenikabidhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kukushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa *support* yenu mpaka nikawenza kufika hapa. Ninawaahidi ushirikiano na naamini mtanipa ushirikiano katika kutimiza majukumu yangu. Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wananchi wa Karagwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwapangii wakulima bei ya kuza pamba bali huratibu upatikanaji wa bei nzuri ya pamba kwa wakulima. Sheria ya Pamba Na.2 ya mwaka 2001 inaipa Serikali kupitia Bodi ya Pamba jukumu la kukaa na wawakilishi wa wakulima na kampuni za kununua pamba kukubaliana bei elekezi ambayo inazingatia gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani gharama za uzalishaji wa ekari ya pamba inakadiriwa kuwa Sh.488,000.

Ekari moja iliyotunzwa vizuri hutoa wastani wa kilo 1,000 sawa na kuzalisha kilo moja kwa Sh.488. Bei iliyopangwa na wadau wa pamba yaani bei elekezi ya msimu wa mwaka 2018/2019 ilikuwa Sh.1,100 ambapo kwa mkulima aliyezalisha kwa tija ya kilo 1,000 kwa ekari na kuuza kwa bei hiyo hakuza chini ya gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa pamba ni wadau muhimu katika kupanga bei ya pamba kwa kila msimu. Serikali inatambua umuhimu huo, hivyo imefanya maboresho katika mfumo wa uuzaji kwa kufufua na kuimarisha vyama vya ushirika kwa lengo la kuongeza fursa ya wakulima kushiriki katika soko kupitia ushirika wao. Upangaji wa bei ya pamba huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo bei ya pamba nyuzi katika soko la dunia, kiwango cha kubadilishia fedha, bei ya mbegu za pamba, gharama za usafirishaji, uchambuaji na uwiano katil ya nyuzi na mbegu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika mwezi Septemba, 2018, baadhi ya wakulima wa Mkoa wa Simiyu waliuza pamba kwa Sh.1,200 kwa kilo juu ya bei elekezi kutokana na mabadiliko ya bei ya pamba katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, fursa ya wakulima wa pamba kuza bei wanayotaka itaongezeka kwa kuwa Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya pamba hasa kuongeza viwanda vya kuchakata pamba hapa nchini. Aidha, Serikali inaendelea kujenga uwezo wa wakulima ili kuongeza tija katika zao la pamba na hatimaye kuongeza uzalishaji na pato la mkulima mmoja mmoja.

SPIKA: Swali la nyongeza, mwenye swali lake Mheshimiwa Dotto tafadhali.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali yasiyokuwa na afya, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wananchi wamekuwa wakilalamikia kuhusu suala la dawa zinazoua wadudu. Mwaka huu Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba tunapata dawa ambazo zinaua wadudu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kumekuwa na changamoto kipindi cha kugawa dawa za kuua wadudu kwamba mkulima ambaye amelima na akatupia mahindi kidogo hapewi dawa badala yake anaambiwa alipie dawa hizo wakati mMkulima ambaye hajachanganya na zao lolote anapewa dawa bure. Ni kwa nini Serikali imekuwa ikianza na adhabu kwa wananchi badala ya kutoa elimu ndiyo ianze kuwaadhibu wananchi? Nakushukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Gimbi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Gimbi anasema viuatilifu ambavyo wamekuwa wakipewa wakulima haviuwi wadudu. Azma ya Serikali ni kuhakikisha viuatilifu vinavyoingizwa nchini vinaua wadudu kama inavyotakiwa. Tayari Serikali kupitia Taasisi ya Kudhibiti Viuatilifu nchini tumewaelekeza kuhakikisha viuatilifu vinavyoingizwa nchini, Sheria ya Udhhibiti Ubora wa Viuatilifu unazingatiwa. Mimi katika ziara zangu nimehakikisha viuatilifu vinavyoingizwa kwa msimu huu wa pamba wa mwaka wa 2018/2019 vinazingatia Sheria ya Udhhibiti Ubora wa Viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko makini na msimu huu wa pamba tutahakikisha viuatilifu vyote vinavyoingizwa nchini vinafaa kwa ajili ya kuua wadudu. Sambamba na hili, Wizara imeelekeza Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na taasisi nyingine ndani ya Wizara kutoa elimu kwa wakulima ili

wakulima wetu wajue namna bora ya kutumia hivi viuatilifu kuweza kupata matarajio ya kuua wadudu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

WABUNGE FULANI: Bado swali la pili.

SPIKA: Ahsante sana. Bado tuko kwenye Wizara hii hii na swali linalofuata pia ni la mambo ya pamba, la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 9

Bei ya Pamba Msimu wa Mwaka 2019/2020

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Kwa kuwa msimu wa pamba wa mwaka 2018/2019 ulikuwa na bei elekezi ndogo ya Sh.1,100 na kwa kuwa mara nyingi bei hizo elekezi zinapendekezwa kwa msukumo wa bei ya pamba duniani:-

(a) Je, Serikali katika msimu wa mwaka 2019/2020 ina mkakati gani wa kuinua bei ya wakulima kutoka Sh.1,100 hadi Sh.2,500?

(b) Kwa kuwa kuna Vyama vyaya Ushirika na Benki ya Wakulima, je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la usambazaji wa mbegu za pamba katika Wilaya ya Bunda na hasa Jimbo la Bunda ambapo kila mwaka kunakuwa na uhaba wa mbegu na kutofika kwa wakati?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, linahusu mambo ya pamba, kama ulibakiza kule mwanzo unaweza ukajumlishia hapa hapa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L.
BASHUNGWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bei za mazao na bidhaa mbalimbali hutegemea nguvu ya soko kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji (*supply*), mahitaji (*demand*), ubora na viwango vinavyohitajika katika masoko ya ndani na nje na ushindani uliopo katika masoko husika.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei ya pamba kutoka Sh.1,100 hadi Sh.2,500 katika msimu wa ununuzi wa 2019/2020 kutategemea nguvu za soko hususani kupanda kwa bel ya pamba katika soko la dunia. Aldha, pamoja na kutegemea nguvu ya soko la dunia, Serikali inatekeleza mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika Viwanda vya Nyazi na Nguo ili kuimarisha soko la ndani na ushindani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua ya kuongeza upatikanaji wa mbegu za pamba nchini, ambapo katika msimu wa mwaka 2018/2019 jumla ya tani 27,851 zilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima ikilinganishwa na tani 20,496 zilizozalishwa msimu wa mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 36. Aidha, kati ya mbegu zilizozalishwa mwaka 2018/2019, tani 1,075 zimesambazwa katika Wilaya ya Bunda ikilinganishwa na tani 688 zilizotumika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo inahudumia sekta ya kilimo kwa ujumla wake kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu ukilinganisha na benki zingine. Aidha, Benki ya Kilimo inatarajia kushiriki katika ununuzi wa pamba sambaba na benki nyingine zilizopo nchini kwa kutoa mikopo kwa kampuni zitakazoshiriki katika ununuzi wa pamba kama ilivyofanyika msimu wa ununuzi wa mwaka 2018/2019.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Bunda.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuiliza maswali mawili ya nyongeza, nimshukuru kwanza Naibu Waziri wa Kilimo, Ndugu yangu Bashungwa kwa uadilifu wako, nadhani Mungu atakusaidia utafika unakoenda. Napenda kuiliza maswali mawili ya nyongeza la kwanza, na hili niliseme wazi kwa Waziri aliyopo na wewe mwenyewe, na kwa Wabunge wote nadhani unalijua hili, tatizo kubwa la pamba ni mambo mawili tu, la kwanza ni bei ya pamba, la pili ni usambazaji wa pembejeo kwa wakati ambao haufai.

Mheshimiwa Spika, suala la bei, naomba kujua kupata ufanuzi, ni kwa nini sasa Serikali isitafute masoko ya ndani na masoko ya nje kwa wakati muafaka kwa msimu unaofaa, ili Wakulima wa pamba wapate bei nzuri ya kutosha?

Swali la pili kwa kuwa mwaka jana kwa msimu 2018/2019 Serikali ilikuja hapa Bungeni ikatuomba wakate shilingi mia kwa kilo ya pamba kwa wakulima, na lengo lilikuwa kupunguza au kufuta kabisa kero ya usambazaji wa mbegu za pamba au madawa kwa wakati muafaka, nini kimetokea mpaka leo Wakulima wa pamba wanateseka na mbegu hazipatikani kwa wakati na madawa hayapatikani kwa wakati, nini tatizo? Tatizo ni ubovu wa bodi ya pamba? au ni mikakati mibovu ya Wizara ya Kilimo?

SPIKA: Majibu Naibu Waziri Mheshimiwa Innocent Bashungwa, unatakiwa uchague kati ya mawili, ubovu wa bodi ya pamba au ubovu wa Wizara ya Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Boniphace Getere kwa namna anavyohangaikia changamoto za Wakulima Jimboni kwake Bunda hususani zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, tatizo la bei na usambazaji tayari Serikali chini ya mfumo wa ushirika tunaendelea kuimarisha ushirika ili ushirika uweze kuwajibika kwa Mkulima kwa kuhakikisha Mkulima anapata pembejeo kwa wakati anazingatia ubora na tayari Wizara yetu kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini ya Wizara tunaendelea kutoa elimu ili wakulima wetu wa pamba wazingatie kupanda kwa kutumia kamba ambayo ina vipimo.

Mheshimiwa Spika, pia, sambasamba na hilo usambazaji wa pembejeo hususani viuatilifu kwa misimu iliyopita vilikuwa vikichelewa lakini tayari Wizara tumeshakaa na kuhakikisha tuna mkakati wa kuhakikisha msimu huu viuatilifu vina wafikia wakulima wetu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Getere ni kuhusu masoko ya ndani na nje nimuhakikishie Mheshimiwa Getere kwa vile ni mfuatiliaji mzuri tutakaa naye pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mikoa inayolima pamba na kuhakikisha tunakuwa tuna mfumo mzuri ambao utamuhakikishia mkulima kupata bei nzuri lakini na shilingi mia moja ambayo wanakatwa tutaangalia namna ya kuangalia mfumo mzuri ili makato ya mkulima yamsaidie katika kuwa na Kilimo cha tija, ili aweze kupata pato zuri katika msimu wa kuza pamba, nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana, swali la mwisho siku ya leo la Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini.

Na. 10

Changamoto katika Uuzaji wa Zao la Korosho

MHE. MAFTAH A. NACHUMA aliuliza:-

Zao la Korosho pamoja na kuingiza mapato makubwa Serikalini bado lina changamoto nyingi sana katika uuzaji wake kwa upande wa Wakulima:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa changamoto hizo ili kuleta tija kwa Wakulima?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Omary Tebweta Mgumba, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma Mbunge wa Jimbo la Mtwara mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli zao la Korosho ni mojawapo ya mazao ya Kilimo yanayoliingizia Taifa mapato ambapo katika kipindi kilichoishia Oktoba, 2018, zao la Korosho liliingizia Taifa fedha za kigeni za Kimarekani zaidi ya dola milioni mia tano sabini na tano pointi sita sawa na zaidi fedha za Kitanzania trillioni moja nukta tatu ikilinganishwa na mazao mengine ya biashara. Aidha, pamoja na mchango wa zao hilo katika uchumi wa Taifa, zao la Korosho limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali ambapo Serikali imekuwa ikizitafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo ni pamoja na kuyumba kwa bei ya zao la Korosho katika soko la dunia kutokana na Korosho kuuzwa ikiwa ghafi bila kuongezewa thamani; Tija ndogo katika uzalishaji wa wakulima; baadhi ya wakulima kutotumia miche bora na matumizi hafifu ya pembejeo ikiwemo viuadudu kama *sulphur*; wakulima kutozingatia Kanuni bora za Kilimo katika uzalishaji, uvunaji na uhifadhi hafifu wa Korosho; uwezo mdogo wa maghala ya kuhifadhia Korosho na baadhi ya wakulima kuchanganya Korosho na mawe na mchanga kwa ajili ya kuongeza uzito wakati wa mavuno ambaa unashushia ubora.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeboresha mfumo wa uuzaji wa

Korosho kwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kuanzia ngazi ya vyama vyama msingi, maghala makuu, maghala ya hifadhi na kutoa elimu kwa wakulima; kurejesha Kiwanda cha BUCCO cha Mkoani Lindi cha kubangua Korosho ujenzi wa maghala matatu ya kuhifadhi Korosho katika Mikoa ya Ruvuma, Pwani na Tanga ili kuongeza Kiwango cha kuhifadhi na ubora wa Korosho pamoja na kuzalisha miche bora zaidi ya milioni kumi na kuisambaza kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuimarisha mnyororo wa thamani katika zao la Korosho ili kuongeza uzalishaji, kuimarisha usambazaji wa pembejeo za Kilimo kwa wakati, kutoa huduma za ugani pamoja na kuweka mazingira wezeshi na kuwajengea uwezo wabanguaji wa ndani wa Korosho kwa lengo la kuongeza thamani ya Korosho inayozalishwa nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini, swalil la nyongeza.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, asante, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado kuna changamoto moja ameiacha katika Korosho ambayo ni changamoto ya malipo kwamba mpaka leo Serikali inasuasua kuwalipa Wakulima waliouza Korosho zao. Wapo Wakulima ambao wamepeleka Korosho zao ghalani lakini wamelipwa pesa ambayo haikidhi au hailingani na kiwango walichopeleka. Lakini pia wapo Wakulima ambao mabodi *display* zinaonesha kwamba wamelipwa tayari lakini wakienda benki pesa hizo hazipo, kwa hiyo kuna malipo hewa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kujua Serikali kwa nini haielezi ukweli juu ya malipo ya Korosho kwa Wakulima wa Korosho.

Mheshimiwa Spika, swalil la pili nilikuwa naomba kujua kwamba Serikali imekusanya Korosho hizi zikawekwa kwenye maghala Mtwara na Lindi na maeneo mengine na Korosho zinahifadhiwa haizidi miezi mitatu, Korosho zimeanza kuota

hivi sasa zingine. Je, Serikali haioni kwamba inalitia hasara Taifa hili kwa kuziweka Korosho hizi bila kuzibangua? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, majibu ya maswali hayo ya Mbunge wa Mtwara Mjini.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swalii la nyongeza kwa Mheshimiwa Nachuma. Kwanza sisi kama Serikali au Taasisi ya Serikali iliyopewa jukumu hili bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko tunalipa pesa kwa wakulima, na mpaka jana kiasi cha Korosho tulizokusanya ni zaidi ya tani laki mbili kumi na tatu na tumeshafanya uhakiki zaidi ya tani laki moja na ishirini na tisa na tani laki moja na kumi na sita ndizo tulizozilipa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ajue kufahamu kwamba malipo hatuwezi kuanza kulipa kabla ya kujiridhisha katika uhakiki na pesa hii niwahakikishie kwamba pesa zipo na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Waziri Mkuu tumetoka juzi huko ambaa kulikuwa kweli na changamoto hasa kwenye malipo ya daraja la pili ambaa mwanzo pale tuliona mkazo kuanza daraja la kwanza lakini kuanzia jana wameanza kulipwa pia na Korosho daraja la pili hasa Mikoa ya Pwani na Mikoa ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili anazungumzia kuhusu hasara ambayo kwa kuweka Korosho muda mrefu, kwanza ni kweli Korosho sio kama zabibu kwa sababu zabibu ukiweka muda mrefu ndio ukali wake unaongezeka lakini Korosho kila unavyoiveka ubora wake unazidi kushuka. Hilo tunalifahamu na ndio maana tumeshaingia mikataba na wabanguaji wa ndani wameshaanza kubangua na sasa hivi tuko kwenye mazungumzo ya mwisho kwa ajili ya kuuza tani zaidi ya laki mbili kwenye masoko ya Kimataifa muda sio mrefu Korosho zitaanza kusafirishwa nje ya nchi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Nape utamalizia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, asante nilitaka kuuliza swali la nyongeza, suala la ununuzi wa Korosho unaendana sambasamba na ulipaji wa wadau wanaoshiriki katika suala zima la Korosho, ununuzi unaoendelea mpaka sasa hivi halmashauri hazijapewa pesa yao ya ushuru hata senti tano. Nilitaka kuiuliza Serikali yangu, kwa kuwa Serikali imeamua kununua Korosho ni lini italipa ushuru wa halmashauri ili Bajeti zetu ziende kama tulivyozipanga?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mgumba tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijiji, kwanzani kweli kuna watoa huduma mbalimbali katika zao la Korosho, na sisini kama Serikali tullona mwanzoni kutokana na mkanganyiko uliokuwepo tuliweka mkazo zaidi kulipa kwamba wakulima kabla ya watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, na mpaka sasa tulishalipa wakulima zaidi ya asilimia 59 sasa hivi tumeshaanza kulipa na watoa hudma wengine wakiwemo hao watu wa halmashauri, mpaka jana tulishalipa zaidi ya bilioni nne kwa wasafirishaji lakini tumeshalipa watanza maghala zaidi bilioni sita na tushalipa pia watoa huduma wengine wasambazaji wa magunia zaidi ya bilioni nne nukta nane.

Kwa hiyo na hiyo ya Halmashauri tunaifahamu tushawaambia watu wa vyama vikuu na vyama vya msingi watunze rekodi zao vizuri wote tutawalipa kwa sababu halmashauri na Serikali kuu wote ni wadau katika hili, Serikali kuu *export levy* na hawa hizo fedha za halmashauri zote Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi zipo kwenye mikakati na tutazilipa. Lakini la mwisho, nitoe ufanuzi katika hili, ni kweli Serikali tunanunua Korosho lakini sio kwamba Serikali yenyewe ndio inanunua Korosho ni Taasisi ya Serikali ya Bodi ile ya nafaka ya mazao mchanganyiko ndio inayonunua Korosho, kama zinavyofanya biashara Taasisi zingine kama TTCL na zingine sio Serikali kuu.

SPIKA: Mheshimiwa Nape swali la mwisho kwa siku ya leo.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na maelezo mazuri ya Serikali itakumbukwa kwamba siku nne tano zilizopita Mheshimiwa Waziri Mkuu alikiri kwamba zoezi la uhakiki limegubikwa na vitendo vya rushwa. Sasa ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kuwachukulia hatua wale ambao wameshiriki zoezi hili na kujihusisha na vitendo vya rushwa, ambayo kwa kweli kwa sehemu kubwa ndiyo imevuruga zoezi hili na kulikosesha maana na matokeo yake wakulima wameathirika sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Ooohh! Tafadhalii karibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla ya kujibu hili swali, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kwa kunitfea katika nafasi hii na kuniamini kwamba naweza kufanya kusaidia katika maendeleo. (*Makofii*)

Pia nichukue nafasi kuwashukuru viongozi wengine wote wanaomsaidia Mheshimiwa Rais lakini pia, wewe Mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa malezi mazuri, ambayo ndiyo yamenifanya nifikie katika nafasi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimjibu Mheshimiwa Nape Nnauye kama ifuatavyo, ni kweli kabisa kwamba wakati tunaendelea na hili zoezi la uhakiki katika maeneo mengi kumekuwa na maneno katika baadhi ya maeneo kwamba baadhi ya viongozi na baadhi ya wafanyakazi ambao wako kwenye Kamati za uhakiki wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa. Sisi kama Wizara tuliposikia tu hatukusubiri tupate ushahidi, tuliposikia baadhi ya wafanyakazi wanashiriki kwenye rushwa tumechukua hatua na naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwenye upande wa Wizara na bodi zake.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wanne tumeshawachukulia hatua tumeshawasimamisha na hivi sasa tunakusudia kuwapeleka Mahakamani kutokana na kudhihirika kwamba wamejihuisha na vitendo nya rushwa. Lakini pia kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wako TAMISEMI ambao tunawasiliana ndani ya Serikali ili nao waweze kuchukuliwa hatua zinazokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba Serikali haitavumilia wafanyakazi wote ambao watakuwa wanajihuisha na vitendo nya rushwa na pale ambapo Waheshimiwa Wabunge mnazo takwimu au mmepata taarifa kwamba mfanyakazi wetu ye yeyote anajihuisha na rushwa tunaomba mtupatite hiso taarifa na kama Serikali tutachukua hatua mara moja. Ahsante.

SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge niwaambie tu Watu wa kusini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa huko Mtwara juzi tu hapa na ametoka kutatua matatizo haya haya akishirikiana na watu wake wa Kilimo na TAMISEMI na wengine wote kwa hiyo, wakulima wa Korosho wawe na utulivu mambo yatacaa sawa.

Matangazo kuhusu wageni kwanza tunaye mgeni, Kaimu Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dkt. Ihmi Paterson, karibu sana, Mheshimiwa Balozi, karibu Bungeni na bahati nzuri Mheshimiwa Balozi, anaongea Kiswahili kizuri sana, kwa hiyo naamini ameweza kufuatilia kinachoendelea Bungeni bila kuhitaji Mkalimani, karibu sana Balozi Inmi. Lakini amefuatana na maofisa wake wa Ubalozi akiwemo afisa wa masuala ya siasa ndugu Laurean Ladenson, karibu (*Makofi*).

Msaidizi wa Masuala ya siasa ndugu Chikulupi Kasaka, huyu ni binti yetu tumekuwa naye hapa Bungeni siku zilizopita. Balozi wa Sweden nchini Tanzania Andres Sjoberg, karibu sana Mheshimiwa Balozi, huyo ni Balozi wa Sweden tuko naye hapa leo, Afisa Ubalozi ndugu Ludvig Bontell karibu sana. Lakini pia tunaye Afisa Ubalozi Victor Harvey, karibu sana na wengine kama wapo waliofuatana na Waheshimiwa Mabalozi hawa,

tunawakaribisheni sana, hapa Dodoma na hapa Bungeni. Lakini pia nina wageni maalum hapa leo katika jukwaa langu la Spika, ninaye Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi Ndugu Humphrey Polepole, (*Makofi*).

Asante sana, makofi haya yanaonesha kazi nzuri unayofanya, lakini pia ninaye Katibu wa NEC Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa Chama cha Mapinduzi Kanali Ngemera Luhinga, (*Makofi*).

Ninaye Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Ndugu Maimuna Tarishi. (*Makofi*)

Ninao wageni sita kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, wakiongozwa na Msajili mwenyewe wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wabunge sijui kama mniamfahamu Msajili wa Vyama vya Siasa.

WABUNGE FULANI: Hatumjuiii!

SPIKA: Hamumfahamu eehhe! Naomba nimtambulisse tena Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Francis Mutungi. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sijui kama mniamfahamu Msajili wa Vyama vya Siasa.

WABUNGE FULANI: Hatumfahamu.

SPIKA: Hamumfahamu eeh? Naomba nimtambulisse tena Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Francis Mutungi, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa Ndugu Sistyl Nyahoza, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa Ndugu Piencia Kiure, karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini pia nina wageni 17 kutoka vyama vya siasa ambaa ni Mwenyekiti wa Chama cha TLP Dkt. Augustine Mrema, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia Makini -

Mheshimiwa Mohamed Abdulla, Katibu Mkuu wa Chama cha *DPNdugu* Abdul Mluya, Katibu Mkuu wa *NRA* - Ndugu Hassan Almas, Katibu Mkuu wa Chama cha *Wakulima AFP* - Ndugu Rashid Rai, Katibu Mkuu wa Chama cha *SAU*- Ndugu Leopald Mahona, Katibu Mkuu wa Chama cha *UDP* Ndugu Saumu Rashid, Katibu Mkuu wa Chama cha *ADC* - Ndugu Doyo Hassan Doyo na Naibu Katibu Mkuu (Bara) wa Chama cha *ADC* - Ndugu Queen Sendiga. (*Makofi*)

Aah, natafuta Makatibu Wakuu wa Vyama vingine sijui wengine hawana Makatibu Wakuu maana yake siwaoni hapa, hivi vyama vingine inakuwajekuwaje hii. Tuna mgeni kutoka Taasisi ya *Alliance for Development Organization (ADO)* - Ndugu Habib Mchange. (*Kicheko/Makofi*)

Kuna wanafunzi wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Bethany Ndugu Lisa na Mese, karibuni pale mlipo.

Kuna wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaao ni kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Simon Mwakifamba ambaye ni Rais wa Shirikisho la Filamu Tanzania, yule pale ahsante sana na wenzake kutoka Shirikisho la Filamu na wageni wao, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 44 wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea kutoka Jijini Dar es Salaam ambaao ni mke wa Mheshimiwa Mtolea Bi. Fatma Aboubakari, shemeji hatujakuona! Aah sawasawa, eeh kutoka TMK, ameambatana na viongozi wa Wilaya kutoka Temeke hawa ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Temeke Ndugu Al-Mish Azad, Meya wa Temeke Ndugu Abdallah Chaurembo, Mkurugenzi wa Temeke Ndugu Lusubilo Mwakibibi, Mwenyekiti wa Wazee wa Dar es Salaam Ndugu Mohamed Mtulia na Mwenyekiti wa Wazee wa Temeke Mzee Mitande Mbonde. (*Makofi*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Salum Khamis ambaao ni wapiga kura wake wakiongozwa na Ndugu Aberi Msabila, karibuni sana.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mgeni Kadika ambao ni watoto wake kutoka Visiwani Zanzibar nao ni Ndugu Badria Ally na Ndugu Saida Omary, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, wale pale karibuni sana Wanamaombi mtuombee. (*Makof*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Taufiq, ni wana kikundi wa *VICOBA Faraja* kutoka Nkuhungu, karibuni sana.

Kwa ajili ya mafunzo tuna wanafamilia tisa kutoka Chidachi, Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Farida Kyendo na Ndugu Shabani Bunduki ambaye ni mstaifu kutoka Mkoani Tabora.

Huo ndio mwisho wa wageni.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona hata kwenye maswali yetu ya leo sikuruhusu maswali ya nyongeza kwa sababu ya muda, muda wetu ni mdogo sana awamu hii ya Mkutano huu, kwa hiyo, tunajaribu kutunza muda na kwenda kwa kadri tunavyoweza. Kama mlivyoona jana tulivyokuwa tunaiangalia ratiba yetu.

Mwisho nina tangazo la Mheshimiwa Anna Lupembe kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote mnaohusika na masuala ya maombi kwamba leo mchana, tarehe 29 Januari kutakuwa na ibada katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Wabunge mnaohusika Mwenyekiti wenu wa ibada Mheshimiwa Anna Lupembe anawaomba saa 7.00 mchana mukutane kwenye Ukumbi wa Msekwa.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mwongozo wa Spika.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mwongozo wa Spika, Kanuni ya 68(7)...

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mwongozo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Katibu, washa chombo hicho.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

SPIKA: Hoja ya kutengua kanuni, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nitoe maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge ulioanza leo tarehe 29 Januari, 2019 umepangwa kumalizika tarehe 8 Februari, 2019. Shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu haziwezi kukamilika iwapo Vikao vya Bunge vitafanyika katika siku za kazi peke yake yaani Jumatatu mpaka Ijumaa na iwapo tutatumia muda wa kawaida wa Vikao vya Bunge.

Kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) Bunge linakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo hurejea tena saa 11.00 jioni; na kwa kuwa Kanuni ya 28(15) inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko na kwa kuwa Kamati ya Uongozi iliyokaa jana tarehe 28 Januari, 2019 na kuridhia kwamba katika Mkutano wa Kumi na Nne Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana lirejee tena saa 10.00 jioni na kwamba siku ya Jumamosi tarehe 2 Februari, 2019 Bunge likutane kwa ajili ya kufanya kazi.

Hivyo basi, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji bora wa shughuli za Bunge, naomba Bunge lako liridhie Kanuni ya 28(2) na Kanuni ya 28(15) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana lirejee saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge lirejee saa 10.00 alasiri kuanzia leo Jumanne tarehe 29 Januari, 2019; na Kanuni ya 28(15) itenguliwe ili kuruhusu siku ya Jumamosi ya tarehe 2 Februari, 2019 itumike kwa ajili ya Vikao vya Bunge isipokuwa kwamba katika siku hiyo Bunge litaanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa kwamba kwa awamu hii kwa kipindi cha jioni tuenze shughulli zetu kuanzia saa 10.00 jioni. Nitawaomba sana ushirikiano kwa wakati huo maana yake tutaanza saa hiyo hata kama tupo wawili/watatu tutaanza, lakini pia inapendekezwa kwamba siku ya Jumamosi tufanye kazi. Na niwahakikishie kwamba siku za Jumamosi mambo yanayohusu utaratibu yatazingatiwa. Sasa ninawahojii. (*Makofii*)

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Naamini walioafiki wameshinda. Basi kwa hiyo huo ndio utaratibu katika awamu hii, tutajitahidi tufanye kazi kwa saa moja zaidi ili tuweze kukidhi mahitajio ya kazi zetu za Mkutano huu wa Kumi na Nne. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho kwa niaba yenu nimepokea mwaliko kuja kwenu kutoka kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania akiwaalika kuhudhuria Maonesho ya Wiki ya Sheria yanayofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 31 Januari hadi tarehe 4 Februari, 2019 saa 2.00 asubuhi mpaka saa 11.00 jioni. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria pamoja na Wabunge wengine mnaombwa mjumuike pamoja na

wananchi wa Dodoma mtembelee mabanda ya maonesho yatakayokuwa eneo la *Nyerere Square*, Dodoma.

Kauli mbiu ya safari hii ya wiki hiyo ya sheria nchini inasema; "utoaji wa haki kwa wakati wajibu wa mahakama na wadau." Sasa tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Kwa sababu ya muda kama nilivyosema naomba tuokoe miongozo yote tutaichukua kesho, Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA YA SERIKALI

MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 (*The Political Parties (Amendment) Bill, 2018*)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2016 naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama za Siasa wa mwaka 2018 kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe kwa mara pili na ya tatu na Bunge lako tukufu lijadili na hatimaye lipitishe muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu muswada huu, ninaomba nianze kwa kuwatakia sana Wabunge wote heri ya mwaka mpya pamoja na wewe mwenyewe. Tumshukuru Mungu kwa sababu ameweza kutufikisha mwaka huu mpya wa 2019. Pia nakushukuru sana

kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuhudumu kwenye nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa uongozi shupavu katika kusimamia utekelezaji wa llani ya chama chetu Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, maelekezo na miongozo anayotupatia...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tusikilizane, tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: ...anayotupatia ambao inatuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu mliouwezesha kukamilisha muswada huu. Pia nimshukuru sana Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge pamoja na wasaidizi wake wote kwa msaada waliotha katika kufanikisha maandalizi ya muswada wetu.

Mheshimiwa Spika, adiha, nampongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mbunge) kwa kuteuliwa kuhudumu

kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji. Vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Doto Biteko Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini.

Nichukue nafasi hii ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Temeke kwa uamuzi wake wa kujunga na Chama cha Mapinduzi na hatimaye kuapishwa kuwa Mbunge wa Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa pekee ninawashukuru sana wasaidizi wangu wapendwa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira na Mheshimiwa Stella Ikupa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye masuala ya wenye ulemavu. Nawashukuru pia Makatibu Wakuu Bi. Maimuna Tarishi, Bwana Andrew Massawe na Bi. Dorothy Mwaluko ambaye ni Katibu Mkuu mpya ndani ya ofisi yetu na nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa kuteuliwa kwake.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza Makatibu Wakuu na watendaji wengine wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi mbalimbali ikiwemo Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu. Ninawatachia utekelezaji mwema wa dhamana waliyokabidhiwa kuwatumikia watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu Prof. Adelardius Kirangi na watumishi wote wa ofisi yake kwa ushirikiano waliotupatia. Kwa nafasi ya pekee kabisa ninaomba kumshukuru sana Msajili wa Vyama vyta Siasa, Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi na Naibu Msajili Bwana Mohamed Ally Ahmed pamoja na watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia vizuri mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini pamoja na utayarishaji wa muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba

na Sheria chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Najma Giga pamoja na wajumbe wote wa Kamati na Wajumbe walioalikwa kwenye kamati hiyo kwa kazi kubwa ya kupitia na kuchambua muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba nilihakikishie Bunge lako tukufu wametupatia ushirikiano mkubwa, ushauri, maoni na mapendekezo ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha muswada kama inavyoonekana katika jedwali letu la marekebisho tuliloliwasilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee salamu zangu za shukrani ziwafikie wadau wote ambao walijitokeza mbele ya Kamati ili kutoa maoni ya muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018 unapendekeza kufanya marekebisho, kuongeza na kuondoa baadhi ya vifungu vya Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya mwaka 1992 Sura ya 358. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuondoa upungufu uliojitekeza wakati wa kuitumia sheria hii ili kuboresha utekelezaji wake na kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yanayofanyika sasa ni ya kawaida kwani sheria hii imeshafanyiwa marekebisho mara saba tangu kutungwa kwake mwaka 1992 kwa lengo la kukuza demokrasia ya vyama vingi vya siasa hapa nchini na kukabiliana na changamoto na kuzingatia mahitaji ya wakati husika tulionao sasa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018 ulianza toka mwaka 2013 wakati maoni ya wadau yalipoanza kukusanya. Mwaka 2014 vyama vya siasa vilipendekeza mchakato huo kusimama kupisha mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya.

Vilevile mwaka 2015 mchakato huo ulisimama kupisha Uchaguzi Mkuu. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yameandaliwa baada ya kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ikiwemo wadau wakuu ambao ni vyama vyaa siasa.

Mheshimiwa Spika, muswada huu umezingatia taratibu zote za kisheria na kikanuni katika uandaaji wake. Ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 9 Novemba, 2018 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali tarehe 16 Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ya muswada inaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la sheria liliofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya muswada inapendekeza kufanya marekebisho kuitia Muswada huu katika vifungu vyaa sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha pili cha muswada kinakusudia kurekebisha Kifungu cha Tatu cha Sheria ya Vyama vyaa Siasa kwa kuongeza tafsiri ya maneno yaliyotumika katika baadhi ya masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tatu cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha nne cha Sheria ya Vyama vyaa Siasa ili kubainisha majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vyaa Siasa ambayo ni pamoja na kutoa elimu kuhusu demokrasia ya vyama vingi vyaa siasa na sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vyaa Siasa, kuratibu elimu ya uraia inayotolewa kwa vyama vyaa siasa na wadau mbalimbali; kusimamia mienendo ya vyama vyaa siasa na kusimamia utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kufanya majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vyaa Siasa yafahamike kwa urahisi kuliko ilivyo sasa ambapo hayajawekwa katika sehemu moja ndani ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tano cha muswada kinakusudia kuongeza kifungu kipyga cha 5(a) na 5(b) katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Kifungu kipyga cha 5(a) kinamtaka mtu binafsi ama taasisi za ndani na nje zenye nia ya kutoa elimu ya uraia na mafunzo ya aina yoyote ile kwa vyama vya siasa kumtaarifu Msajili.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuratibu elimu itakayotolewa kwa vyama vya siasa ili kudumisha umoja wa Kitaifa, kukuza uzalendo wa nchi yetu na kuzuia elimu inayolenga kupandikiza chuki mionganoni mwa jamii na mifarakanano kati ya vyama vya siasa inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, kifungu kipyga cha 5(b) kinamwezesha Msajili kupata taarifa stahiki kutoka kwa chama cha siasa au klongozi wa chama cha siasa. Lengo ni kumwezesha Msajili wa Vyama vya Siasa kutekeleza vyema jukumu lake la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kuwa na mamlaka ya kuhitaji taarifa zinazomwezesha kutekeleza vyema jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 cha muswada kinaongeza sehemu mpya ya 2(a) na Kifungu cha 6(a), (b) na (c) katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Sehemu ya 2(a) inahusu uundwaji wa vyama vya siasa. Kifungu kipyga cha 6(a) kinavita vyama vya siasa kufuata matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na sheria nyengine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia kuzingatia masuala ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuainisha mwongozo unaopaswa kuzingatiwa wakati wa kuanzisha na kuendesha chama cha siasa ili kuwe na vyama vya siasa ambavyo vinaaheshimu sheria za nchi na maslahi ya Taifa. Vilevile, kifungu hicho kinaweka msisitizo wa vyama vya siasa kuzingatia misingi na alama muhimu za Taifa na Utaifa wetu kama vile Muungano, Mapinduzi ya Zanzibar, mapambano dhidi ya rushwa, uzalendo, Mwenge wa Uhuru, amani na

utulivu wa nchi yetu, masuala ya jinsia, masuala ya vijana na masuala ya wenyewe ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hicho pia kinaelekeza utaratibu wa kutunga na kurekebisha Katiba za vyama vyaya siasa. Lengo ni kuhakikisha majukumu ya kutunga na kurekebisha Katiba za vyama vyaya siasa, kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Taifa, kuteua Mgombea Urais, kuchagua au kuteua Katibu Mkuu na viongozi wengine wa Kitaifa hayatakasimiwa kwa vikao vyaya chini vyaya chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho pia kinaeleza masuala ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na chama wakati wa uundwaji na uendeshaji wake ili kuhakikisha vyama vyaya siasa nchini vinazingatia na kuheshimu masuala ya Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6(b) kinaweka sifa za mtu anayeomba kusajili chama cha siasa. Lengo ni kuhakikisha mtu anayeomba kusajili chama cha siasa ni raia wa Tanzania mwenye sifa zinazostahili kuanzisha chama cha siasa, kwani chama cha siasa ni taasisi muhimu sana ya Umma ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6(c) kinaweka vigezo vyaya mtu anayestahili kuwa mwanachama wa chama cha siasa ili kuhakikisha kila mwanachama wa chama cha siasa ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na kupiga marufuku raia wa kigeni kushiriki katika kufanya maamuzi ya chama.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8 cha muswada kinarekebisha kifungu cha nane cha Sheria ya Vyama vyaya Siasa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) baada ya kifungu cha 8(4) ili kuweka masharti ya jina la chama na ukomo wa usajili wa muda kwa vyama vyaya siasa vilivyoomba usajili wa muda. Lengo ni kuainishaa vyema ukomo wa cheti cha usajili wa muda wa chama cha siasa chenye usajili wa muda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, muswada unaweka utaratibu utakaowezesha chama cha siasa chenye jina linalostahili au lisilostahili au linalofanana na chama kingine au taasisi yoyote kutosajiliwa ili kuepusha vyama vyama siasa kuwarubuni au kuwachanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 8(a) cha Sheria ya Vyama vyama siasa ili kutega *register* ambazo zitatunzwa na Msajili wa Vyama vyama siasa. *Register* hizi zitajumuisha *register* ya vyama vyama siasa, *register* ya Viongozi wa Kitaifa wa vyama na *register* ya Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Siasa. Lengo ni kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vyama siasa kuwa na taarifa muhimu za vyama vyama siasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 8(b) cha Sheria ya Vyama vyama siasa kwa kuainisha adhabu kwa kitendo cha kukiuka masharti ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 cha muswada kinakusudia kuongeza vifungu vipyta vyama siasa 8(c), (d) na (e) katika Sheria ya Vyama vyama siasa. Kifungu cha 8(c) kinaweka utaratibu wa kutunza kumbukumbu za viongozi na wanachama wa chama cha siasa kwa kikitaka kila cha cha siasa kuwa na *register* ya taarifa hizo. Lengo ni kumwezesha Msajili wa Vyama vyama siasa kujua kama chama cha siasa kinakidhi matakwa ya usajili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8(b) kinaeleza mambo ya msingi yatakayopaswa kuwamo katika katiba ya chama cha siasa. Lengo ni kufanya Katiba za Vyama vyama siasa kuwa bora na kukidhi matakwa ya sheria.

Kifungu cha 8(e) kinaweka katazo kwa chama cha siasa kuanzisha kikundi cha ulinzi na usalama au kuendesha mafunzo ya kutumia nguvu au silaha ya aina yoyote kwa wanachama wake au mtu yeyote. Lengo ni kuzuia vikundi hivyo kuingilia kazi za vyombo vyoma ulinzi na usalama vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 9 cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kuwa uanachama katika vyama vya siasa uko wazi kwa watu wenye ulemavu. Lengo ni kukomesha ubaguzi kwa watu wenye ulemavu katika vyama vya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 cha muswada kinarekebisha Kifungu cha 10 cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuboresha Masharti ya Usajili wa Vyama vya Siasa kwa kikitaka chama cha siasa kinachoomba usajili wa kudumu kuwa na wanachama wasiopungua 200 wenye sifa za kusajiliwa kuwa wapiga kura kutoka nusu ya mikoa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo ni kuhakikisha kila chama cha siasa kinachosajiliwa kinakuwa ni cha Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 10(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kuongeza sifa za mtu anayestahili kuchaguliwa au kuwa Kiongozi wa Kitaifa wa Chama cha Siasa. Lengo ni kuwa na Viongozi wa Kitaifa wa Vyama vya Siasa wenye sifa zinazokubalika katika jamii ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 cha muswada kinakusudia kuweka Kifungu kipycha 10(b) katika Sheria ya Vyama vya Siasa ili kumpa Msajili wa Vyama vya Siasa mamlaka ya kuhakiki chama cha siasa wakati wowote. Lengo ni kuhakikisha chama cha siasa kinakuwa na sifa za usajili muda wote, uhai wake na kueleza bayana mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kuhakiki muda wote utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kila chama cha siasa kinazingatia na kutekeleza masharti ya usajili.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 11 cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kujumuisha uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika masharti ya kifungu hicho. Lengo ni kuboresha suala la Muungano katika Sheria ya Vyama vya Siasa kwani Sheria ya Vyama vya Siasa ni ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 cha muswada kinakusudia kufuta kifungu cha 11(a) na (b) cha Sheria ya Vyama vyा Siasa. Vilevile, kifungu hicho cha Muswada kinakusudia kuweka kifungu kipyा cha 11(c) kitakachoweka masharti na utaratibu wa vyama vyा siasa kushirikiana. Lengo ni kuhakikisha vyama vyा siasa vinaacha kabisa mazoea ya kufanya ushirikiano kiholela ili kuviepusha kuvunja sheria nydingine za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 11(c) cha Sheria ya Vyama vyा Siasa kinachozua vyama vyा siasa kusimika na kupeperusha bendera kwenye maeneo yaliyokatazwa na Kifungu cha 12 cha sheria hiyo. Lengo ni kuhakikisha bendera za vyama vyा siasa hazipeperushwi katika maeneo ambayo Sheria ya Vyama vyा Siasa imekataza siasa kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 12 cha Sheria ya Vyama vyा Siasa. Vilevile, kifungu cha 20 cha muswada kinakusudia kufuta Kifungu cha 12(a) cha Sheria ya Vyama vyा Siasa. Lengo ni kuboresha kifungu kidogo kinachokataza mtu au chama cha siasa kufanya siasa katika Taasisi za Umma kwa kufuta kifungu cha 12(a) na kuweka maudhui yake katika kifungu cha 12, kwani maudhui ya vifungu hivi viwili yanafanana.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21 cha muswada kinakusudia kuweka kifungu kipyा cha 12(c) cha Sheria ya Vyama vyा Siasa ili kuvitaka vyama vyा siasa kuwasilisha kwa Msajili tamko la mapato na matumizi. Lengo ni kumwezesha Msajili wa Vyama vyा Siasa kujua mapato na vyanzo vyा mapato na matumizi ya chama cha siasa wakati wa mchakato wa usajili ili kudumisha suala la uwazi katika mapato na matumizi ya vyama vyा siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu muswada kiboko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 13 cha Sheria ya Vyama vyta Siasa ili kujumuisha vyanzo vyta mapato ya chama cha siasa ya ndani ya nchi katika vyanzo vyta mapato vinavyopaswa kuwekwa wazi kwa Msajili. Lengo ni kuwezesha Msajili wa Vyama vyta Siasa kuratibu vyema mapato na matumizi ya vyama vyta siasa. Pia kuvitaka vyama vyta siasa kuteua Afisa Masuuli atakayesimamia mali za chama.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuwezesha kila chama cha siasa kuwa na mtu anayewajibika katika mapato na matumizi ya chama ili kukidhi matakwa ya mfumo wa uwajibikaji katika utunzaji wa mali za taasisi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 15 cha Sheria ya Vyama vyta Siasa kwa kutaka kila chama cha siasa kinachopata ruzuku ya Serikali kuwa na akaunti maalum ya benki kwa ajili ya kuweka na kutumia fedha za ruzuku. Lengo ni kuhakikisha chama cha siasa kinachopata ruzuku hakichanganyi mapato na matumizi ya fedha za ruzuku na fedha kutoka katika vyanzo vingine ili kuhakikisha fedha za ruzuku zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 18 cha Sheria ya Vyama vyta Siasa ili kumpa Msajili mamlaka ya kusitisha ruzuku kwa chama cha siasa kilichoshindwa kusimamia matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kulinda fedha za Umma zisitumike vibaya. Vilevile kumpa Msajili mamlaka ya kumwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa mapato na matumizi ya chama cha siasa. Lengo ni kumwezesha Msajili kubaini upungufu uliopo katika mapato na matumizi ya chama cha siasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25 cha muswada kinakusudia kufuta na kuweka kifungu kipyä cha 18(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuweka sharti kwamba mwaka wa fedha wa kila chama cha siasa unapaswa kuwa sawa na mwaka wa fedha wa Serikali. Pia kikitaka kila chama cha siasa kuwasilisha taarifa za hesabu zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi, kisha kuwasilisha taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa Msajili. Lengo ni kuboresha utaratibu wa kukagua hesabu za vyama vya siasa ili uendane na ratiba ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 28 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 21 cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuzuia Viongozi wa Chama cha Siasa kuwa ni Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama husika. Lengo ni kuwepo kwa uwajibikaji katika kutunza mali za chama.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 29 cha muswada kinakusudia kufuta kifungu cha 21(a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuondoa mgongano wa kiutendaji kati ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Kabidhi Wasii, yaani Msajili wa Wadhamini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 30 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 21(b) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuainisha vyanzo vya fedha za kuendesha Baraza la Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 31 cha muswada kinakusudia kuongeza kifungu kipyä cha 21(d) na 21(e) katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Kifungu kipyä cha 21(d) kinaainisha makosa na adhabu za jumla kwa makosa ambayo hayana adhabu maalum katika Sheria ya Vyama vya Siasa. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna kosa katika Sheria ya Vyama vya Siasa ambalo halina adhabu ili kuhakikisha sheria hiyo inatekelezwa ipasavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kifungu kipywa cha 21(e) kinaweka utaratubu wa kumdhiliti mwanachama wa chama cha siasa anapokiuka Sheria ya Vyama vywa Siasa. Lengo ni kumwajibisha mwanachama wa chama cha siasa aliyejiku sheria kwa kufanya kitendo ambacho hakistahili na kuepuka kukiadhibu chama kwa kosa ambalo anastahili kuadhibiwa mwanachama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 32 cha muswada kinakusudia kurekebisha kifungu cha 22 cha Sheria ya Vyama vywa Siasa kwa kuondoa baadhi ya maneno ili kuwezesha kuweka mpangilio mzuri wa kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa mara nyingine tena, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu sana ya kuwasilisha hoja hii mahsus i sana kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vywa Siasa wa mwaka 2018 (*The Bill for an Act to Amend the Political Parties Act of 2018*).

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu kuupitisha katika hatua ya kusomwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye marekebisho yaliyopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Tunakushukuru sana sana.

ISSN 0856 - 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 4E

16th October, 2018

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.4E. Vol.99 dated 16th October, 2018

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE POLITICAL PARTIES (AMENDMENT) ACT, 2018

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.

PART II
GENERAL AMENDMENTS

2. Amendment of section 3.
3. Amendment of section 4.
4. Amendment of section 5.
5. Addition of new sections 5A and 5B.
6. Repeal and replacement of section 6.
7. Addition of Part IIA.
8. Amendment of section 8.
9. Amendment of section 8A.
10. Amendment of section 8B.
11. Addition of sections 8C, 8D and 8E.
12. Amendment of section 9.
13. Amendment of section 10.
14. Amendment of section 10A.
15. Addition of section 10B.

16. Amendment of section 11.
17. Repeal and replacement of sections 11A and 11B.
18. Amendment of section 11C.
19. Amendment of section 12.
20. Repeal of section 12A.
21. Addition of section 12C.
22. Amendment of section 13.
23. Amendment of section 15.
24. Amendment of section 18.
25. Repeal and replacement of section 18A.
26. Amendment of section 19.
27. Addition of section 19A.
28. Amendment of section 21.
29. Repeal of section 21A.
30. Amendment section 21B.
31. Addition of sections 21D and 21E.
32. Amendment of section 22.

—————
NOTICE
—————

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
15th October, 2018

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL

for

An Act to amend the Political Parties Act.

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

Cap.258

- 1.** This Act may be cited as the Political Parties (Amendment) Act, 2018 and shall be read as one with the Political Parties Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

PART II
GENERAL AMENDMENTS

Amendment of
section 3

2. The principal Act is amended in section 3 by inserting in its appropriate alphabetical order the following new definitions:

“political party general meeting” means the highest administrative organ of the party, made by delegates based on the party structure prescribed in the party constitution;

“National Executive Committee” means a party organ or any similar organ comprised of party national leaders and party representatives from each region where the party has administrative organ or representative elected in accordance with party constitution;

“founding member of a political party” means a person who participates in the formation of a political party and who is among the first members of the party.

Amendment of
section 4

3. The principal Act is amended in section 4, by-

(a) adding immediately after subsection (4) the following:

“(5) Without prejudice to subsection (4), the functions of the office of the Registrar shall be to-

- (a) register political parties in accordance with this Act and any other written law;
- (b) supervise the administration and implementation of this Act;
- (c) monitor intra-party elections and nomination process;
- (d) disburse and monitor accountability of Government subvention to political parties which qualify under this Act;
- (e) monitor income and expenditures of political parties and accountability of party resources;
- (f) provide civic education regarding multiparty democracy, laws governed by the Registrar and related matters;

- (g) regulate civic education provided to political parties;
 - (h) advise the Government on issues related to political parties and multiparty democracy;
 - (i) facilitate communication between political parties and the Government;
 - (j) undertake research on political parties, multiparty democracy and political parties financing;
 - (k) provide secretariat to the Political Parties Council; and
 - (l) undertake any other functions conferred by this Act or any other written law.
- (b) renumbering subsection (5) as subsection (6).

Amendment of
section 5

4. The principal Act is amended in section 5 by deleting the words “assistant registrars” appearing in the marginal note and in the contents of section 5 and substituting for them the word “directors”.

Addition of new
sections 5A and
5B

5. The principal Act is amended by adding immediately after section 5 the following new sections:

“Regula-
tion of
civic
education

5A.-(1) A person or institution registered within or outside the United Republic wishing to conduct civic education or any kind of capacity building training or initiative to a political party, shall prior to conducting such training, inform the Registrar in writing stating the objective and kind of training, training programme, persons involved in such training, teaching aids and expected results.

(2) Upon receipt of information under subsection (1), the Registrar may disapprove the training or capacity building programme and give reasons for such disapproval.

(3) Any person who contravenes this section, commits an

offence and is liable, on conviction to a fine of not less than one million shillings but not exceeding five million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding twelve months or to both.

(4) Any institution which contravenes this section, commits an offence and is liable, on conviction to a fine of not less than five million shillings but not exceeding thirty million shillings.

(5) Any person or institution which contravenes this section shall, in addition to penalties under this section be ordered by the Registrar to submit the information on the training or training programme within such period as prescribed by the Registrar.

(6) A person or institution which fails to comply with an order under subsection (5) commits an offence.

Powers of
Registrar to
demand
information
from political
parties

5B.-(1) The Registrar may, in the execution of functions and responsibilities under this Act, demand from a political party, a leader or a member any information as may be required for implementation of this Act.

(2) A political party which contravenes this section shall be liable to a fine of not less than one million shillings but not exceeding ten million shillings.

(3) Any person, being a person having the mandate of his political party, who contravenes this section or provides false information to the Registrar, commits an offence and is

liable, on conviction to a fine of not less than one million shillings but not exceeding three million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding twelve months or to both.

(4) Any person or institution which contravenes this section shall, in addition to penalties under this section be ordered by the Registrar to submit the information within such period as prescribed by the Registrar.

(5) The Registrar may, where a political party contravenes subsection (4), suspend or deregister such political party.”

Repeal and
replacement of
section 6

6. The principal Act is amended by repealing section 6 and replacing for it the following:-

“Protection
of officers

6. No suit shall lie against the Registrar, Deputy Registrar, Director or other officers under the Registrar for anything done or omitted to be done in good faith in the performance of any function under this Act.”

Addition of new
Part IIA

7. The principal Act is amended by adding immediately after Part II the following new Part:-

**“PART IIA
FORMATION OF POLITICAL
PARTIES**

Formation of
political party

6A.-(1) A political party may, subject to the Constitution of the United Republic and this Act, be formed to further objectives and purposes which are not contrary to the

Constitution of the United Republic, the Constitution of Zanzibar or any other written law in the United Republic.

- (a) adhere to the rules and procedures of the political parties relating to the formation of coalition;
- (b) be sanctioned by the general meeting of the political parties entering into the coalition and shall –
 - (i) be in writing and duly executed by authorized national party leaders; and
 - (ii) be commissioned by a commissioner of oaths of the submitted to the Registrar.
- (c) state-
 - (i) parties which are members of the coalition;
 - (ii) policies and objectives of the coalition;
 - (iii) overall structure of the coalition;
 - (iv) organisation structure and management of the coalition;
 - (v) criteria or formula for sharing of positions in the coalition structure, roles and responsibilities within the coalition;
 - (vi) coalition nomination rules;
 - (vii) coalition election rules;
 - (viii) decision making structure, rules and procedures;
 - (ix) process and mechanisms upon which the coalition agreement may be amended;
 - (x) policy initiation, policy consultation and policy decision making structure, rules and procedures;
 - (xi) code of conduct of coalition including values and principles guiding the performance of individuals and the member parties within the coalition;
 - (xii) dispute resolution mechanisms and procedures;
 - (xiii) procedures for appeal;
 - (xiv) enforcement and sanction mechanisms and procedures for breach of any of the provisions of the agreement;
 - (xv) role of general meeting and political party organs of the individual member parties of the coalition in the running of the affairs of the coalition;

- (xvi) formula and mechanism of sharing subvention from the government and other sources; and
- (xvii) grounds and procedure upon which the coalition may be dissolved .

Dodoma,
....., 2019

KMM
WM

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu mawili/matatu kabla hatujaendelea, nayo ni kwamba nawaomba sana kwa sababu ya muda wale wote wenye hotuba zao hapa, ni vizuri kujikita zaidi katika yale mambo muhimu ili tusije kuyakosa badala ya kusoma kama ilivyo, matokeo yake unafika mwisho unajikuta umeacha labda mambo ambayo ultaka kuyasema ili Waheshimiwa Wabunge wasikie.

La pili, uchangiaji wetu utakaoanza muda sio mrefu utakuwa ni wa dakika 15 kwa sababu hatukuwa tumepata mapendekezo tangu jana kwenye Kikao chetu cha jioni kwamba labda tupunguze muda ili wachangiaji wawe wengi. Kwa hiyo, kwa majina ambayo nimeshaletewa na vyama, ukipata hizo dakika zako 15 basi uzitumie vizuri. Ukiweza kutumia chini ya hapo, tutashukuru maana itatuongzea idadi ya wachangiaji.

Muda siyo mrefu tutapata *schedule of amendments*, kulikuwa na ucheleweshaji fulani, kwa hiyo, zikipita ni vizuri kuangalia *schedule of amendments* hasa ya Serikali na nyingine kwa sababu marekebisho ni makubwa na ni mengi, *yame-accommodate* mambo mengi ambayo labda mtu ungependa kusema hapa kumbe yameshafanyiwa kazi na Kamati yetu ya Katiba na Sheria ambayo napenda kuipongeza na pia naipongeza Serikali kwa kukubali baadhi ya marekebisho muhimu tayari. (*Makofii*)

Baada ya kusema hayo, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. (*Makofii*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakushukuru sana wewe kwa kuendelea kuniimarisha kwa kuridhia Muswada huu kufika mbele ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 6 Novemba, 2018, wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa (*The Political Parties (Amendment) Bill, 2018*)] ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza. Baada ya hatua hiyo, ulizingatia Masharti ya Kanuni ya 84(1) pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili uchambuliwe. Hivyo, kwa masharti hayo, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa uniruhusu kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, niwasilishe Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa (*The Political Parties (Amendment) Bill, 2018*). Katika uwasilishwaji, ili kubainisha misingi ya maoni haya nitaeleza kwa muhtasari mambo makuu mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu Maudhui ya juu ya Muswada kama ilivyozingatiwa wakati wa majadiliano kwenye Kamati na jambo pili ni namna Kamati ilivyofanyia kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya ujumla ya Muswada; kwa ujumla Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ili kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria hii. Utatuzi huu ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (a) Kubainisha majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo yanajumuisha kusajili vyama vya siasa, kutoa elimu ya uraia, kusimamia mienendo ya vyama vya siasa na kusimamia utekelezaji wa sheria za nchi;
- (b) Kuzitaka taasisi zenyе nia ya kutoa elimu ya uraia kumtaarifu Msajili na pia kumwezesha Msajili kupata taarifa

kutoka kwa chama chochote cha siasa. Lengo na marekebisho hayo ni kumwezesha Msajili kuratibu utoaji wa elimu ya uraia; na

(c) Kuongeza sehemu mpya itakayohusu uundwaji wa vyama vyta siasa, ambapo inapendekezwa kuwa sheria ivitake vyama vyta siasa kufuata masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vyta Siasa nchini. Vile vile inapendekezwa kuwa Sheria iweke vigezo vyta mtu anayeweza kuomba kusajili chama cha siasa na vigezo vyta mtu kuwa mwanachama wa chama cha siasa pamoja na kuweka masharti yanayozuia mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika shughuli za chama cha siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo, marekebisho ya sheria yanayopendekezwa, yanalenga kuimarisha Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa. Uimarishaji huo unapendekezwa kwa kuiongezea mamlaka ya kuratibu na kusimamia uanzishwaji, utekelezaji wa majukumu ya Vyama vyta Siasa nchini kwa ufanisi zaidi tena kwa namna inayozingatia ipasavyo, masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyofanya kazi; katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana kwa muda wa wiki mbili katika Ofisi za Bunge ambapo ilijielekeza katika shughuli zifuatazo:-

(a) Kujadiliana na kuainisha mambo mbalimbali yanayofanikisha uchambuzi wa Muswada huu ili kupata maoni yatakalolisaidia Bunge kutunga sheria yenye tija;

(b) Kupokea na kujadili Wasilisho la Sekretarieti kuhusu Ulinganisho wa Dhana ya Usimamizi Uratibu wa Vyama vyta Siasa wa Tanzania na Mfumo ya kisheria katika nchi nyingine. Lengo lilikuwa ni kuwezesha Kamati kupata uzoefu wa mifumo mingine ya kisheria katika nchi tofauti ili kujiridhisha na uzingatiaji wa masuala ya msingi katika Muswada huu.

Aidha, Kamati ilipokea na kujadili uchambuzi wa awali wa Sekretarieti kwa lengo la kupata uelewa wa Muswada husika kwa mujibu wa Kanuni ya 21(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;

(c) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu madhumuni na sababu za Muswada ambayo yaliwasilishwa na mtoa hoja, Mheshimiwa Jenesta Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Walemavu);

(d) Kupokea maoni huru yaani (*Expert Opinion*) kuhusu dhana na mambo makuu yanayojitokeza katika Sheria inayopendekezwa. Shughuli hii iliwezeshwa ipasavyo na Ofisi ya Bunge, chini ya Utaratibu wa Mradi wa *LSP Awamu* ya II;

(e) Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau yaani (*Public Hearing*) kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Jumla ya Taasisi kumi na nne (14) kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilitumiwa Mialiko rasmi ili zifike au zitume maoni yao kuhusu Muswada huu. Vile vile mamia ya Wadau walifika kutoa maoni yao kwa tangazo la Ofisi ya Bunge kwa umma waliweza kusikilizwa na maoni yao kufanyiwa kazi;

(f) Kwa kuzingatia uhusika wa vyama vya siasa katika mapendekezo ya Sheria hii, Kanuni ya 84(2) ilipendelea kuzingatiwa pamoja na ushauri wa Mheshimiwa Spika uliusika kutoa fursa mahsus kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa kumi na tisa (19) vyenye usajili wa kudumu hapa nchini. Vyama hivyo pia vilisikilizwa kuititia viongozi waliofika mbele ya Kamati kwa ajili hiyo;

(g) Kuchambua maoni ya wadau wote kwa kulinganisha na sababu, mantiki na madhumuni ya Muswada ili kupata msimamo na mwelekeo wa Kamati katika hoja mbalimbali zinazojitokeza katika Muswada huu. Katika vikao hivyo, Wabunge kuititia vyama mbalimbali vyenye uwakilishi Bungeni ambaeo ni wajumbe wa Kamati mbalimbali walifika

na kushiriki kwenye mijadala kwa lengo la kuuboresha Muswada huu na hatimaye Kamati ilipata mambo kadhaa ya kujadiliana na Mtoa hoja; na

(h) Kujadiliana na Serikali kuhusu hoja mbalimbali za Kamati kabla ya kuhitimisha uchambuzi wa Muswada katika Kamati. Kutokana na uzito wa hoja zilizotolewa, nafurahi kulijulisha Bunge kuwa Serikali ilikubali na kuahidi kuwa itakuwa na Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*) kama ambavyo limewasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa vikao vyakopokea na kusikiliza maoni ya wadau; kama nilivyoeleza hapo awali, Katibu wa Bunge aliwaalika Wadau kwa njia ya barua na kupitia vyombo vyakopokea na habari ili kuiwezesha Kamati kupata maoni yatakayosaidia kuboresha Muswada huu. Kwa sababu hiyo, Jumla ya Taasisi ishirini na moja (21) na watu binafsi mia nne na kumi (410) walifika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao na wengine waliwasilisha kwa njia ya maandishi. Wadau hao walitoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa kumbukumbu za Bunge lako Tukufu orodha ya Taasisi hizi ni kama inavyoonekana katika tarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kibali chako, tarehe 19 hadi tarehe 20 Januari, 2019, Viongozi wa Vyama vyakopokea na tisa (19) vyenye usajili wa Kudumu hapa nchini, walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao ya vyama vyao. Orodha ya Vyama husika vilivyowasilisha maoni mbele ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

United Democratic Party (UDP), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo), Union for Multiparty Democracy (UMD), Democratic Party (DP), Chama cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Labour Party (TLP), Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Alliance for Democratic Change (ADC), Alliance for African Farmers (AAFP), National Convention for Construction and Reform (NCCR-Mageuzi), United Democratic Party (UPDP), African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA), DEMOKRASIA MAKINI, Sauti ya Umma

(SAU), *National League for Democracy (NLD)*, Chama cha Kijamii (CCK), *National Reconstruction Alliance (NRA)* na *The Civic United Front (CUF)*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Vikao vya Kamati vya kuchambua maoni; kwa kuzingatia Kanuni ya 117(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilijiwekea utaratibu wake kwa lengo la kuiwezesha kuelewa maudhui na mantiki ya kila Ibara ya Muswada sambamba na namna bora ya uratibu wa vikao vya Maoni ya Wadau. Kamati inaishuruku sana Ofisi ya Bunge iliyotumia Mradi wa *LSP* kuwezesha uelewa, upatikanaji na uzoefu wa kutosha pamoja na mambo mengine ya msingi kwa kuchambua Muswada huu. Utaratibu uliotumika wa kuiwezesha Kamati kupata maoni huru ya Kitaalam (*Expert Opinion*) umeisaidia sana Kamati kuwa na uelewa mkubwa uliowezesha kuchambuzi wa Muswada kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu huo katika uchambuzi wa Muswada huu, Kamati inakiri kuwa utaratibu wa kujenga uelewa kwa Wajumbe kuhusu Muswada (*Bill awareness*) na ule wa kupata maoni huru ya kitaalam (*Expert opinion*) unafaa kuendelezwa kwa Miswada yote inayochambuliwa na Bunge lako Tukufu. Kufanya hivyo kunalihakikishia Bunge uchambuzi wa Miswada kwa viwango vinavyoridhisha. Yote hayo yalifanikishwa kwa miongozo yako kila tulipohitaji na kwa ushirikiano mkubwa na wa dhati ambao ulisaidia kufanikisha hatua zote za uratibu wa maoni ya Wadau katika kuheshimu misingi ya demokrasia ya vyama vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba itoshe kusema kuwa, Kamati yangu imeutendea haki Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Bunge, busara na hekima pamoja na mashauriano ya karibu ya aina ya Kamati, Serikali na Sekretarieti ya Bunge. Mambo haya kwa pamoja yameiwezesha Kamati kukamilisha uchambuzi na kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii, kwa kuzingatia ratiba ya Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ulinganisho wa Dhana ya Mamlaka ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Vyama vyा Siasa Tanzania pamoja na Mifumo ya Kisheria ya baadhi ya nchi nyingine; mara baada ya Kamati kubaini na kuainisha maudhui ya jumla ya muswada huu, iliona ni vyema iwapatie masuala ya msingi yanayopendekezwa katika Muswada huu kwa kulinganisha matumizi yake katika mifumo ya kisheria kutoka katika nchi nyingine, hususan kutoka katika nchi za Jumuiya ya Madola zenyе utaratibu angalau unaokaribiana na kufanana na mfumo unaotumika hapa Tanzania katika demokrasia ya vyama vingi. Lengo ilikuwa ni kujielimisha na kujiridhisha kuhusu dhana zenyе kuainisha misingi ya usimamizi na uratibu wa vyama vyा siasa hapa nchini. Katika kufanya hivyo, Kamati ilibaini kuwa dhana zinazoonekana mpya katika muswada huu, zimekuwa zikitumika katika nchi nyingine kwa muda mrefu sana. Maboresho yameendelea kufanyika kulingana na hatua za maendeleo ya nchi husika na kwa wakati unaohusika.

Mheshimiwa Spika, nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa Kamati iliweza kujifunza kuhusu dhana za uratibu wa vyama vyा siasa katika nchi ya Uingereza, Ufaransa, Afrika ya Kusini, Ghana na Kenya na hatimaye kuainisha mifumo ya kisheria ya nchi za Ghana na Kenya kama mfano kifani (*Case Study*) kwa rejea ya Kamati. Ulinganisho huo unaonesha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchini Ghana chini ya Sheria ya *Political Parties Act*, ya mwaka 2000; Kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Vyama vyा Siasa nchini Ghana kikisomwa pamoja na Ibara ya 55(7) ya Katiba ya Ghana, kinaiipa Tume ya Uchaguzi Wajibu wa Kusajili Vyama vyा Siasa kwa kuitambua Tume hiyo kuwa ndicho chombo chenye mamlaka na wajibu wa kusajili Vyama vyा Siasa.

Aidha, Kifungu kidogo cha (1) cha Sheria hiyo kinatoa sharti kuwa Chama cha Siasa kinaweza kuanzishwa endapo hakikinzani na misingi ya Katiba na Sheria nyingine za nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, Kifungu cha (26) cha Sheria hiyo kinatamka kuwa, Mtu asiye na sifa ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Ghana aruhusiwi kuanzisha Chama cha Siasa au kuwa Kiongozi wa Juu wa Chama cha Siasa nchini Ghana. Hivyo, sifa za Mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge zimetumika kama kigezo cha Sifa za Mtu anayetaka kuanzisha Chama cha Siasa au kujishughulisha na masuala ya Siasa kwa kuzingatia misingi iliyoainishwa katika Katiba ya Nchi ya Ghana.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilibaini kuwa, lipo sharti linalowekwa na Kifungu cha 2(2) cha Sheria hiyo nchini Ghana, kinazuia Mtu au kwenye Kikundi/Taasisi fulani kwa sababu ya uhusika wake katika Taasisi au Kikundi hicho na kujunga na Chama cha Siasa kwa kutumia umaarufu wake aliokuwa nao kwenye taasisi au kikundi husika.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 13 na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Ghana, Tume ya Uchaguzi ya Ghana ina mamlaka ya kufuta usajili wa Chama cha Siasa baada ya kuthibitika kukiuka masharti ya Sheria na Katiba ya nchi ya Ghana na kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Kamati ilijifunza kuwa, Sheria ya Ghana haiainishi wazi masuala ya uratibu wa Elimu ya Uraia, isipokuwa Kifungu cha 27 kinatoa sharti kwa Chama chochote cha Siasa kinapofanya mikutano au tukio lolote kizingatie masharti ya Sheria ya *Public Order Act* ya mwaka 1994 (*Act Na. 491*) ya nchini Ghana.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 23 hadi 25 vya Sheria ya Ghana, Vyama vya Siasa haviruhusiwi kufadhiliwa na wafadhili wa nje. Ufadhilli wa Vyama vya Siasa unaoruhusiwa ni ule unaokidhi sharti la kutohana na raia wa Ghana tu au kampuni ambayo inamiliikiwa na Mghana kwa asilimia 100 au kwa angalau asilimia 75 ya umiliki wa raia wa Ghana na mtu ye yote ambaye siyo raia wa Ghana ambaye akibainika kufadhili shughuli za Vyama vya Siasa nchini Ghana, atachukuliwa kama mhamiaji haramu na atafukuzwa ndani ya nchi hiyo kwa mujibu wa *The Aliens Act* ya mwaka 1963, *Act No.160*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kamati ilibaini kuwa dhana nyingi zinazotumika katika Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Siasa nchini Ghana unafanana kwa kiasi kikubwa na dhana mpya zinazopendekezwa katika Muswada huu wa Sheria ya Vyama vya Siasa hapa nchini, isipokuwa tu, katika kuungana kwa vyama vya siasa haukuwekwa ukomo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kenya, *Political Parties Act* ya mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016. Kifungu cha 11 cha Sheria hiyo, kimempa Msajili wa Vyama vya Siasa mamlaka ya usajili, usimamizi na uratibu wa Vyama vya Siasa. Aidha, Sehemu ya II ambayo kwa kiasi kikubwa inarejea Ibara za Katiba ya Kenya, ambapo pamoja na mambo mengine, ili uwe wanachama au kiongozi wa Chama cha Siasa sharti uwe raia wa Kenya na mtu asiye raia wa Kenya haruhusiwi kujishughulisha na masuala ya kisiasa nchini humo. Pia, Msajili ana Mamlaka ya kutoruhusu usajili wa Chama cha Siasa endapo majina ya chama hicho au nembo zake zinakinzana na matakwa ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Sharti la chama kusajiliwa nchini Kenya katika Kifungu cha tatu (3) cha Sheria hiyo, linajumuisha kuwa na idadi ya wanachama wasiopungua 1000 kutoka nusu ya *Counties* zote za Wanachama wawe wamejiandikisha kupiga kura na wawe wametoka kwenye Makabila/jamii mbalimbali kutoka pande zote za nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, Kifungu cha 23 kinaanzisha Mfuko wa Vyama vya Siasa ambao ndiyo chombo pekee cha kufadhili shughuli za Vyama vya Siasa nchini Kenya. Mfuko huu umewekwa chini ya uratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa na unafadhiliwa kwa kupokea aslimia 0.3 ya Bajeti ya nchi inayopitishwa na Bunge. Mfuko huo umeruhusiwa kukusanya michango ya ufadhili kutoka vyanzo vingine halali kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 cha Sheria hiyo, kinaanzisha vyanzo vingine vya fedha ya mapato ya Chama

cha Siasa nchini Kenya kuwa ni michango ya Wanachama pamoja na ufadhili mwingine usiotokana na Taasisi za nje ya nchi au mtu asiyre raia wa Kenya na kila Chama cha Siasa nchini Kenya kina wajibu wa kuweka wazi vyanzo vyake vya fedha na kutoa taarifa husika kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Ispokuwa, Chama cha Siasa kitaruhusiwa kushirikiana na Taasisi za nje ya nchi kwa masuala ya kiufundi na kitikadi pasipo na kufadhili fedha, rasilimali kwa Chama cha Siasa nchini humo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo ya Kenya, pamoja na mambo mengine muhimu kinatoa sharti kuwa, hakuna Mtu au Taasisi kutoka ndani ya nchi anayeruhusiwa kufadhili Chama cha Siasa zaidi ya asilimia tano ya Bajeti ya matumizi ya Chama husika kwa mwaka na endapo chama kitathibitika kupokea ufadhili zaidi ya ukomo ullowekwa na sheria, kiasi hicho kilichozidi kitachukuliwa yaani kitataifishwa kuwa mali ya Serikali na akishindwa kufanya hivyo anaweza kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili jela au faini na kifungo kwa wakati mmoja. Aidha, Kifungu cha 31 na 32 cha Sheria ya Kenya, vinampa Msajili wa Vyama vya Siasa, mamlaka na wajibu wa kusimamia mapato na matumizi ya fedha za vyama vya siasa nchini humo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejifunza pia kuwa, Kifungu cha 18 Kama kilivyo kwa mapendekezo ya Muswada huu, Msajili nchini Kenya ana mamlaka ya kuhitaji taarifa yoyote kutoka Chama cha Siasa na Kiongozi wa Chama cha Siasa kwa lengo la kutekeleza matakwa ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, baada ya kuitia mifumo ya kisheria kutoka nchi Kenya na Ghana pamoja na nchi nyingine kama nilivyojitaja hapo awali, Kamati imeridhika pasipo shaka kuwa, wakati umefika sasa kwa Tanzania kuboresha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuimarisha usimamizi na uratibu wa Vyama vya Siasa kwa lengo la kuweka misingi thabiti yenye kuimarisha na kuendeleza demokrasia ya vyama vingi nchini kwa haki na usawa wa mujibu wa Sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kamati

ina maoni kuwa Tanzania tumechelewa sana kuenenda na mabadiliko mbalimbali yanayotokea na kuacha changamoto mbalimbali ndani ya nchi katika uratibu na usimamizi wa shughuli za vyama vya siasa hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kuzungumzia masuala ya awali yanayojenga msingi wa maoni ya Kamati, sasa naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati ambavyo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Serikali wakati wa mashauriano, kama yanavyooneka katika Jedwali la Marekebisho. Maoni hayo yanaelezwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Vyama vya Siasa hapa nchini illitungwa mwaka 1992 ulipoanzishwa mfumo wa vyama vingi. Sheria hii kwa ujumla inaweka masharti ya uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa vyama vya siasa hapa nchini. Sheria imekuwa ikifanya marekebisho mbalimbali ili kuboresha na kuondoa changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hii na mifumo ya vyama vingi nchini.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mwisho ya Sheria hii ni ni yale marekebisho yaliyofanywa miaka kumi iliyopita. Hivyo, bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa mfumo wa vyama vingi unafanya kazi kwa tija, kwa kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa wananchi pamoja na kukuza demokrasia nchini. Dhamira hiyo, inahitaji mfumo wa sheria inayosimamia vyama vya siasa ulio madhubuti. Kwa sababu hiyo, Kamati ina maoni kuwa Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho unatatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria inayorekebishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhia kuwa kama Bunge litapitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama tulivyokubaliana na mtoa hoja, mfumo wa Sheria nchini utaweza:-

(a) Kubainisha majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ni pamoja na usajili wa vyama vya siasa, kutoa elimu ya uraia, kusimamia mienendo ya vyama vya siasa na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi;

(b) Kumwezesha Msajili wa Vyama vya siasa kuzitaka Taasisi zenye nia ya kutoa elimu ya uraia kumtaarifu Msajili na pia kumwezesha Msajili kupata taarifa kutoka kwa chama chochote cha siasa. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Msajili kuratibu utoaji wa elimu ya uraia; na (*Makofi*)

(c) Kuwa na masharti mazuri yaliyo dhahiri kuhusu uundwaji wa vyama vya siasa hapa Nchini. Aidha, masharti ya vyama vya siasa kufuata matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vya Siasa yatazingatiwa.

Vilevile, mfumo wetu wa sheria utakuwa na vigezo vya mtu anayeweza kuomba kusajili chama cha siasa na vigezo vya mtu kuwa mwanachama wa chama cha siasa hata kuzuia mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika shughuli za chama cha siasa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, marekebisho ya sheria hii yanayopendekezwa, yataimarisha utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuipa mamlaka zaidi, kuratibu na kusimamia ufanisi zaidi uanzishwaji na utekelezaji wa majukumu ya vyama vya siasa nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, masuala yaliyopendekezwa kurekebisha na kufutwa. Kutokana na uchambuzi wa Kamati ilibaini masuala ambayo endapo yasipofanyiwa marekebisho au kuondolewa yangekwamisha utekelezaji wa sheria hii. Miongoni mwa masuala hayo ni pamoja na:-

(a) Msajili kupewa mamlaka makubwa zaidi ya yale anayotakiwa kuwa nayo kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya nchi.

(b) Msajili kupewa jukumu la kuwa mshauri wa Serikali kwa masuala ya demokrasia ya vyama vingi nchini, hatua ambayo ingeweza kuhatarisha demokrasia nchini kwa kumpa mtu mmoja kuamua hatma ya misingi ya Katiba ya nchi.

(c) Adhabu kubwa zenyeye kukosa uhalisia na ambazo zinakosa misingi wake wa Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria nyingine nchini zinazopendekezwa katika baadhi ya Ibara za Muswada huu zingekosa mantiki ya busara ya sheria inayopendekezwa.

(d) Sababu za kufuta usajili wa Chama cha Siasa ambazo kimsingi ni kinyume na sababu zilizoainishwa na Katiba ya nchi kwa mujibu wa Ibara ya 20(2).

(e) Masharti yenye kubeba misingi ya Katiba za Vyama na masuala yote ya demokrasia ya Vyama vingi kutungiwa Kanuni na Waziri badala ya kuainishwa kwenye Majedwali ndani ya Muswada husika.

(f) Masuala mbalimbali ya kiuandishi kwa baadhi ya Ibara za Muswada ambayo yalihitaji kuandikwa upya ili kuleta mantiki ya kimaudhui iliyokusudiwa.

(g) Masharti ya uunganishwaji vyama (*merging*) yenye mwelekeo wa kufuta Ofisi ya Rais, hali ambayo inaweza kuingiza nchi kwenye mgogoro wa Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, masuala yanayopendekezwa kuendelea kuwepo katika Muswada huu. Yapo masuala ya misingi ambayo kwa maoni ya Kamati ndiyo yaliyobeba mantiki ya kimaudhui ya jumla ya Muswada husika, ambayo Kamati ilitambua nia njema ya Serikali na ikapendekeza yabaki kama yalivyo. Baadhi ya masuala hayo ni pamoja na:-

- (a) Masharti ya kuzuia ufadhili holela kutoka nje ya nchi kwa Vyama vyta Siasa na umuhimu wa kutumia Mfuko wa Baraza la Vyama vyta Siasa.
- (b) Uainishwaji mzuri wa majukumu ya Msajili wa Vyama vyta siasa tofauti na ilivyo katika Sheria ya sasa pamoja na kuainisha jukumu la usimamizi wa chaguzi ndani ya vyama vyta siasa.
- (c) Uainishwaji mzuri wa usimamizi wa Vyama vyta Siasa chini ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta siasa kwa ujumla wake.
- (d) Zuio la Vyama vyta Siasa kuwa na vikundi vyta ulinzi badala yake vyama vipate haki ya ulinzi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vyta Siasa. (*Makofi*)
- (e) Udhibiti wa maudhui ya elimu ya uraia na masuala yenye kuendana na hilo kutoka na mtu au taasisi ndani au nje ya nchi.
- (f) Uainishwaji bora wa masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika Katiba za Vyama vyta Siasa ikiwemo mgawanyo mzuri wa kufanya maamuzi mbalimbali kwa vyombo mahsus ni ndani ya chama husika.
- (g) Uainishwaji mzuri wa masharti ya vyama kuungana yaani *merging* na kuunda ushirika yaani *coalition* pamoja na maboresho ya Kamati kuhusu jambo hili.
- (h) Maeneo yote ambayo hayakukinzana na misingi ya Katiba ya nchi, Sheria ya Vyama vyta Siasa au Sheria nyingine za Nchi.
- Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kubainisha mapungufu mbalimbali katika mfumo wa kisheria nchini katika usimamizi na uratibu wa Vyama vyta Siasa nchini kwa kuandaa marekebisho na kuyawasilisha kwenye Bunge lako Tukufu kuititia Muswada huu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Vyama

vya Siasa na kuimarisha misingi ya nidhamu ndani ya Vyama vya Siasa hususan matumizi ya fedha za umma, kulinda na kuimarisha misingi ya utaifa kwa Vyama vyote kama ilivyoasisiwa na Waasisi wa Taifa letu na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ustawi wa Demokrasia ya Vyama vingi na kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda sitaweza kusoma mapendekezo ya kila Ibara kwa kuwa Ibara nyingi zimependekezwa kurekebishwa na baadhi yake kufutwa kama inayoonekana katika Jedwali la Marekebisho, hivyo naomba maoni yote mahsus kama yalivyo kwenye taarifa hii yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kuainisha baadhi ya marekebisho yanayopendekezwa na Kamati yenye kutokana na mvutano mkubwa wakati wa kuchambua maoni ya wadau ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya demokrasia, amani na utulivu nchini na katika utekelezaji wa sheria hii. Kamati ilikuabaliana na Serikali baadhi ya Ibara hizo zibaki kama zinavyopendekezwa na Serikali na baadhi zirekebishwe kwa kufutwa au kuandikwa upya kama inavyojonyesha.

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika Ibara ya 3 ambayo inaongeza Kifungu kidogo cha (5) inayohusu majukumu ya Msajili, Kamati inapendekeza:-

(a) Katika Ibara ya 3 ambayo inaongeza kifungu kidogo cha (5) inayohusu majukumu ya Msajili, Kamati inapendekeza katika Ibara ya 3(5)(c) neno “monitor” libaki kama lilivyo ili kumwezesha Msajili kufuatilia na kusimamia chaguzi za ndani za vyama vya siasa kwa lengo la kupunguza uwezekano wa migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kwenye vyama hivyo.

(b) Mapendekezo ya Ibara ya 3(5)(g) kuhusu Msajili kuratibu elimu ya uraia katika Vyama vya Siasa yabaki kama yalivyopendekezwa na Serikali ili kuhakikisha elimu

inayotolewa inaendana na maadili, tamaduni za Mtanzania na pia kuhakikisha usalama wa nchi unalindwa. (*Makofii*)

(c) Kufutwa maneno "*and multi party democracy*" katika Ibara ya 3(5)(h) kwa kuwa siyo majukumu ya Msajili.

(d) Kufutwa Ibara ya 3(5)(i) kwa kuwa majukumu ya Msajili yameainishwa na sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu vyeo vipyta vyta Wakurugenzi vinavyoendekezwa katika Ibara ya 4 ya Muswada, Kamati inashauri vyeo hivyo vifutwe na cheo cha Msajili Msaidizi kibaki kama kilivyo kwenye sheria ili kuakisi jina la Ofisi na majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika Ibara ya 5 kuna mapendekezo ya kuboresha kama ifuatavyo:-

(a) Katika Ibara ya 5(5A)(1) inayoweka masharti kuwa mtu au taasisi inayotaka kutoa elimu ya uraia kumjulisha Msajili irekekebishwe kwa kufuta neno "*registered*" ili kuondoa utata kwa kuwa vinginevyo kuna utata kuhusu mtu aliyesajiliwa. Aidha, uandishi uboreshwe kwa kuainisha "muda wa siku 30" kwa mtu au taasisi kutoa taarifa kabla ya siku ya kutoa elimu husika. Sababu za pendelekezo hilo ni kumwezesha Msajili kupata muda wa kupitia maudhui ya kupitia andiko linalowasilishwa na mwombaji.

(b) Katika Ibara ya 5(5A)(2) inapendekezwa vigezo vinavyotumiwa na Msajili kukataa kuitisha maombi ya kutoa elimu ya uraia viainishwe.

(c) Katika Ibara ya 5(5A)(3) na (4) inashauriwa adhabu zipunguzwe na kuondoa adhabu ya shilingi milioni moja na badala yake kuweka adhabu ya shilingi laki tano. Aidha, adhabu inayopendekezwa ya kifungo cha miezi sita iondolewe na badala yake iwekwe adhabu ya kifungo cha miezi mitatu.

(d) Katika Ibara ya 5(5B)(1) maneno "or a member" yaondolewe ili taarifa zitolewe na chama au viongozi wa chama.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa sababu ya muda siku ya leo mambo ni mengi, nakushukuru sana sana, ndiyo maana nilishauri mwanzoni kwamba muanze na yale ambayo ndiyo yenyewe halafu yale mengine yawe yanamalizia. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana.

MAONI NA SHAURI WA KAMATI KUHSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA WA MWAKA 2018 [THE POLITICAL PARTIES (AMENDMENT) BILL, 2018]
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 6 Novemba, 2018, wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama Vya Siasa (*The Political Parties (Amendment) Bill, 2018*] ulisomwa Bungeni mara ya kwanza. Baada ya hatua hiyo, ulizingatia Masharti ya Kanuni ya 84(1) pamoja na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, na kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili uchambuliwe. Hivyo, kwa masharti hayo, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba sasa uniruhusu kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, niwasilishe Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama Vya Siasa ([*The Political Parties (Amendment) Bill*, 2018]. Katika uwasilishaji, ili kubainisha msingi wa maoni haya nitaeleza kwa muhtasari mambo makuu mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu Maudhui ya jumla ya Muswada kama ilivyozingatiwa wakati wa majadiliano kwenye Kamati. Na la pili ni namna Kamati ilivyofanyia kazi Muswada huu.

1.1 Maudhui ya Jumla ya Muswada

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Muswada huu, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ili kutatua changamoto mbalimbali zillizojitokeza katika utekelezaji wa sheria hii. Utatuzi huo ni pamoja na:-

- a) Kubainisha majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo yanajumuisha kusajili vyama vya siasa, kutoa elimu ya uraia, kusimamia mienendo ya vyama vya siasa na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi.
- b) Kuzitaka taasisi zenyе nia ya kutoa elimu ya uraia kumtaarifu Msajili na pia kumwezesha Msajili kupata taarifa kutoka kwa chama chochote cha siasa. Lengo la marekebisho haya ni kumuwezesha Msajili kuratibu utoaji wa elimu ya uraia, na
- c) Kuongeza sehemu mpya itakayohusu uundwaji wa vyama vya siasa, ambapo inapendekezwa kuwa sheria ivitake vyama vya siasa kufuata masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vya Siasa. Vile vile inapendekezwa kuwa sharia iweke vigezo vya mtu anayeweza kuomba kusajili chama cha siasa na vigezo vya mtu kuwa mwanachama wa chama cha siasa pamoja na kuweka masharti yanayozuia mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika shughuli za chama cha siasa hapa nchini.

Kwa madhumuni hayo, marekebisho ya sheria yanayo pendekezwa, yanalenga kuimarisha Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Uimarishaji huo unapendekezwa kwa kuiongezea mamlaka ya kuratibu na kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa Majukumu ya Vyama vya Siasa nchini kwa ufanisi zaidi tena kwa namna inayozingatia ipasavyo, masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nydingine za Nchi.

1.2 Namna Kamati ilivyofanya kazi

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana kwa muda wa wiki mbili katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilijielekeza katika shughuli zifuatazo:-

- a) Kujadiliana na kuainisha mambo mbalimbali yanayofanikisha uchambuzi wa Muswada huu ili kupata maoni yatakalolisaidia Bunge kutunga sheria yenye tija.
- b) Kupokea na kujadili Wasilisho la Sekretarieti kuhusu Ulingenisho wa Dhana ya Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Siasa kwa Tanzania na Mifumo ya kisheria katika Nchi nydingine. Lengo lilikuwa ni kuwezesha Kamati kupata uzoefu wa mifumo mingine ya kisheria katika nchi tofauti ili kujiridhisha na uzingatiaji wa masuala ya msingi katika Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea na kujadili uchambuzi wa awali wa sekretarieti kwa lengo la kupata uelewa wa Muswada husika kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.
- c) Kupokea maelezo ya Serikali kuhusu madhumuni na sababu za Muswada ambayo yaliwasilishwa na mtoa hoja, Mhe. Jenesta Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemauvu.
- d) Kupokea maoni huru (*Expert Opinion*) kuhusu dhana na mambo makuu yanayojitokeza katika Sheria inayopendekezwa. Shughuli hii iliwezeshwaa ipasavyo na Ofisi ya Bunge, chini ya Utaratibu wa Mradi wa LSP (II).

- e) Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau (*Public Hearing*) kwa mujibu Kanuni ya 84 (2) pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Jumla ya Taasisi Kumi na nne (14) kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilizotumiwa Mialiko rasmi ili zifike au zitume maoni yao kuhusu Muwasda huu. Vile vile mamia ya Wadau waliofika kutoa maoni yao kwa tangazo la Ofisi ya Bunge kwa Umma waliweza kusikilizwa na maoni yao kufanyiwa kazi.
- f) Kwa kuzingatia uhusika wa vyama vya siasa katika mapendekezo ya Sheria hii, Kanuni ya 84(2) iliendelea kuzingatiwa pamoja na usahauri wa mheshimiwa Spika uliohusu kutoa fursa mahsus kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa Kumi na Tisa (19) vyenye usajili wa Kudumu hapa nchini. Vyama hivyo pia vilisikilizwa kupitia viongozi waliofika mbele ya Kamati kwa ajili hiyo.
- g) Kuchambua maoni ya wadau wote kwa kulinganisha na sababu, mantiki na madhumuni ya Muswada ili kupata msimamo na mwelekeo wa Kamati katika hoja mbalimbali zinazojitokeza katika Muswda huu. Katika vikao hivyo, Wabunge kupitia vyama mbalimbali vyenye uwakilishi Bungeni ambao ni wajumbe wa Kamati mbalimbali walifika na kushiriki kwenye mijadala kwa lengo la kuuboresha Muswada huu na hatimae Kamati ilipata mambo kadhaa ya kujadiliana na Mtoa hoja.
- h) Kujadiliana na Serikali kuhusu hoja mbalimbali za Kamati kabla ya kuhitimisha uchambuzi wa Muswada katika Kamati. Kutokana na uzito wa hoja zilizotolewa, nafurahi kulijulisha Bunge kuwa Serikali ilikubali na kuahidi kuwa itakuwa na Jedwali la Marekebisho. (*Schedule of Amendments*).

2.0 Uratibu wa Vikao vya kupokea na kusikiliza Maoni ya wadau

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Katibu wa Bunge iliwaalika Wadau kwa njia ya barua na kupitia vyombo vya habari ili kuiwezesha Kamati kupata maoni

yatakayoisaidia kuboresha Muswada huu. Kwa sababu hiyo, Jumla ya **Taasisi ishirini na moja (21)** na **Watu binafsi Mia Nne na Kumi (410)** walifika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao na wengine waliwasilisha kwa njia ya maandishi. Wadau hao walitoka **Tanzania bara na Tanzania Zanzibar**. Kwa kumbukumbu za Bunge lako tukufu naomba kuzitaja Taasisi zilizowasilisha maoni yao kama ifuatavyo:-

- i) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*)-LHRC,
- ii) *Stallion Attorneys*,
- iii) Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (*Tanganyika Law society*)-TLS,
- iv) *Zanzibar Law Society*,
- v) *Centre for Good Governance and Democracy in Tanzania*(CEGODETA)
- vi) Tanzania Women Lawyers Association-TAWLA
- vii) Tanzania Women Crosspaty Platform (ULINGO)
- viii) TWaweza
- ix) Alliance for Development Organisation
- x) Jukwaa la Katiba Tanzania(JUKATA),
- xi) Tanzania Network of Legal Aid Providers-TANLAP,
- xii) Youth Partnership Countrywide (YPC)-Pwani,
- xiii) Women Wake UP (WOWAP)-Dodoma,
- xiv) Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA)-Dar es Salaam,
- xv) NGONEDO-Dodoma,
- xvi) ICISO-Iringa,
- xvii) PLAJC-Dodoma,
- xviii) *Zanzibar Youth Forum* (ZYF)-Zanzibar,na
- xix) Wana mtandao wa Wanawake na Katiba,
- xx) *African Centre for International Affairs* (ACIA), na
- xxi) *Tanzania Citizens Information Bureau* (TCIB)

Mheshimiwa Spika, kwa kibali chako, tarehe 19 hadi 20 Januari, 2019 Viongozi wa Vyama vya Siasa Kumi na Tisa (19) vyenye usajili wa Kudumu hapa nchini, walifika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni ya vyama vyao. Orodha ya Vyama vya siasa viliviyowasilisha maoni mbele ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

- i) United Democratic Party (UDP),
- ii) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),
- iii) Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo),
- iv) Union for Multiparty Democracy (UMD),
- v) Democratic Party (DP),
- vi) Chama cha Mapinduzi – CCM,
- vii) Tanzania Labour Party (TLP),
- viii) Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA),
- ix) Alliance for Democratic Change (ADC),
- x) Alliance for African Farmers Party (AAFP),
- xi) National Convention for Construction and Reform (NCCR-Mageuzi),
- xii) United Peoples Democratic Party (UPDP),
- xiii) African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA),
- xiv) DEMOKRASIA MAKINI,
- xv) Sauti ya Umma (SAU),
- xvi) National League for Democracy (NLD),
- xvii) Chama cha Kijamii (CCK),
- xviii) National Reconstruction Alliance (NRA), na
- xix) The Civic United Front (CUF).

3.0 Uratibu wa Vikao vya Kamati vya kuchambua Maoni ya Wadau

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilijiwekea utaratibu wake kwa lengo la kuiwezesha kuelewa maudhui na mantiki ya kila Ibara ya Muswada sambamba na namna bora ya uratibu wa vikao vya Maoni ya Wadau. Kamati inaishuruku Ofisi ya Bunge iliyotumia Mradi wa LSP (II) kuwezesha uelewa, upatikanaji wa uzoefu wa kutosha pamona na mambo mengine ya msingi kwa uchambuzi wa Muswada huu. Utaratibu uliotumika wa kuiwezesha Kamati kupata maoni huru ya Kitaalam (*Expert Opinion*) umeisaidia Kamati kuwa na uelewa mkubwa uliowezesha uchambuzi wa Muswada kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kutohana na uzoefu huo katika uchambuzi wa Muswada huu, Kamati inakiri kuwa utaratibu wa kujenga uelewa kwa Wajumbe kuhusu Muswada (*Bill*

awareness) na ule wa kupata maoni huru ya kitaalamu (*Expert opinion*) unafaa kuendelezwa kwa miswada yote inayochambuliwa na Bunge lako tukufu. Kufanya hivyo kunalihakikishia Bunge uchambuzi wa Miswada kwa viwango vinayvyordhisha. Yote hayo yalifanikishwa kwa miongozo yako kila tulipohitaji na kwa ushirikiano mkubwa na wa dhati ambao ulisaidia kufanikisha hatua zote za uratibu wa maoni ya Wadau katika kuheshimu Misingi ya Demokrasia ya Vyama vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba itoshe kusema kuwa, Kamati yangu imeutendea haki Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Bunge, *busara na hekima pamoja na mashauriano ya karibu baina ya Kamati, Serikali na Sekretarieti ya Bunge. Mambo hayo kwa pamoja yamewezesha Kamati kukamilisha uchambuzi na kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako tukufu leo hii, kwa kuzingatia ratiba ya Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge.*

4.0 Ulinganisho wa Dhana ya Mamlaka ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Vyama Vya Siasa Tanzania pamoja na Mifumo ya Kisheria ya Baadhi ya Nchi Nyingine;

Mheshimiwa Spika, mara tu baada ya Kamati kubaini na kuainisha maudhui ya jumla ya Muswada huu, iliona ni vyema ipatie dhana na masuala ya msingi yanayopendekezwa katika Muswada huu kwa kulinganisha matumizi yake katika Mifumo ya kisheria kutoka katika nchi nyingine, hususan kutoka katika Nchi za Jumuiya ya Madola zenyе utaratibu angalau unaokaribiana au kufanana na mfumo unaotumika hapa Tanzania katika demokrasia ya vyama vingi. Lengo ilikuwa ni kujielimisha na kujiridhisha kuhusu dhana zenyе kuainisha misingi ya usimamizi na uratibu wa Vyama vya siasa. Katika kufanya hivyo, Kamati ilibaini kuwa dhana zinazoonekana mpya katika Muswada huu, zimekuwa zikitumika katika nchi nyingine kwa muda mrefu sasa. Maboresho yameendelea kufanyika kulingana na hatua za maendeleo ya nchi husika na kwa wakati unaohusika.

Mheshimiwa Spika, nilijulishe Bunge lako tukufu kuwa Kamati iliweza kujifunza kuhusu dhana za uratibu wa vyama vyaa siasa katika Nchi ya Uingereza, Ufaransa, Afrika ya Kusini, Ghana na Kenya na hatimaye kuainisha Mifumo ya kisheria ya nchi za Ghana na Kenya kama mfano kifani (*Case Study*) kwa rejea ya Kamati. Ulinganisho huo unaonesha kama ifuatavyo:-

4.1 Nchini Ghana chini ya Sheria ya Political Parties Act, 2000;

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 cha Sheria ya vyama vyaa siasa nchini Ghana kikisomwa pamoja na **Ibara ya 55(7)** ya Katiba ya Ghana, kinaipa Tume ya Uchaguzi Wajibu wa Kusajili Vyama vyaa siasa kwa kuitambua Tume hiyo kuwa ndicho chombo chenye Mamlaka na Wajibu wa Kusajili Vyama vyaa siasa. Aidha, **Kifungu cha 1(1)** cha Sheria hiyo kinatoa sharti kuwa Chama cha Siasa kinaweza kuanzishwa endapo hakikinzani na misingi ya Katiba na Sheria nyiningine za nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, **Kifungu cha 26** cha Sheria hiyo kinatamka kuwa, Mtu asiye na sifa ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Ghana asiruhusiwe kuanzisha Chama cha Siasa au kuwa Kiongozi wa Juu wa Chama cha Siasa nchini Ghana. Hivyo, sifa za Mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge zimetumika kama kigezo cha Sifa za Mtu anayetaka kuanzisha Chama cha Siasa au kujishughulisha na masuala ya Siasa kwa kuzingatia misingi iliyoainishwa katika Katiba ya Nchi ya Ghana.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilibaini kuwa, lipo sharti linalowekwa na **Kifungu cha 2 (2)** cha Sheria hiyo nchini Ghana, kinazuia Mtu kutoka kwenye Kikundi/Taasisi fulani kwa sababu ya uhusika wake katika Taasisi/Kikundi hicho na kujunga na Chama cha Siasa kwa kutumia umaarufu wake aliokuwanao kwenye taasisi/kikundi husika.

Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 13** na **Kifungu cha 14** cha Sheria ya Ghana, Tume ya Uchaguzi ya Ghana ina Mamlaka ya kufuta usajili wa Chama cha Siasa baada ya

kuthibitika kukiuka masharti ya Sheria na Katiba ya nchi ya Ghana na kwa kuzingatia utaratibu ulioainshwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Kamati ilijifunza kuwa, Sheria ya Ghana haiainishi wazi masuala ya uratibu wa Elimu ya Uraia, isipokuwa **Kifungu cha 27** kinatoa sharti kuwa Chama chochote cha Siasa kinapofanya mikutano au tukio lolote (*an event*) kizingatie masharti ya **Sheria ya Public Order Act 1994 (Act 491)** ya Nchini Ghana.

Mheshimiwa Spika, katika **Kifungu cha 23** hadi 25 vya Sheria ya Ghana, Vyama vya Siasa haviruhusiwi kufadhiliwa na wafadhili wa nje ya nchi. Ufadhili wa Vyama vya Siasa unaoruhusiwa ni ule unaokidhi sharti la kutokana na Raia wa Ghana tu au Makampuni ambayo yana milikiwa na Waghana kwa asilimia 100% au walau kwa asilimia 75% ya Umiliki wa Raia wa Ghana, na Mtu yejote ambaye siyo Raia wa Ghana ambaye akibainika kufadhili shughuli za Vyama vya Siasa nchini Ghana, atachukuliwa kama mhamiaji haramu na atafukuzwa ndani ya nchi kwa mujibu wa Sheria ya the Aliens Act, 1963 (Act 160).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati ilibaini kuwa dhana nyingi zinazotumika katika Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Siasa nchini Ghana inafanana kwa kiasi kikubwa na dhana mpya zinazopendekezwa katika Muswada huu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, isipokuwa tu, kuungana kwa vyama vya siasa hakujawekewa ukomo.

4.2 Sheria ya Kenya ya Political Parties Act (2011) kama ilivyorekebishwa mwaka 2016

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 cha Sheria hiyo, kimempa Msajili wa Vyama vya Siasa Mamlaka ya usajili, usimamizi na uratibu wa Vyama vya Siasa. Aidha, **Sehemu ya II** ambayo kwa kiasi kikubwa inarejea Ibara za Katiba ya Kenya, ambapo pamoja na mambo mengine, ili uwe mwanachama au kiongozi wa Chama cha Siasa sharti uwe Raia wa Kenya na mtu asiye Raia wa Kenya haruhusiwi kujishughulisha na masuala ya kisiasa nchini humo. Pia, Msajili ana Mamlaka ya kutoruhusu usajili wa Chama cha Siasa

endapo majina ya chama hicho au nembo zake zinakinzana na matakwa ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Sharti la chama kusajiliwa nchini Kenya katika **Kifungu cha 3** cha Sheria hiyo, inajumuisha kuwa na idadi ya wanachama wasiopungua elfu moja kutoka nusu ya Counties zote na Wanachama hao wawe wamejandikisha kupiga kura na wawe wametoka kwenye Makabila/jamii mbalimbali kutoka pande zote za Nchi ya Kenya (*diversities*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, **Kifungu cha 23** kinaanzisha Mfuko wa Vyama vya Siasa ambao ndicho chombo pekee cha kufadhili shughuli za Vyama vya Siasa nchini Kenya. Mfuko huu umewekwa chini ya uratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa, na unafadhiliwa kwa kupokea aslimia 0.3% ya Bajeti ya nchi inayopitishwa na Bunge. Mfuko huo umeruhusiwa kukusanya michango na ufadhili kutoka vyanzo vingine halali kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 cha Sheria hio, kinaainisha vyanzo vingine vya Fedha na mapato ya Chama cha Siasa nchini Kenya kuwa ni Michango ya Wanachama pamoja na ufadhili mwingine usiotokana na Taasisi za nje ya nchi au mtu asiyé Raia wa Kenya na kila Chama cha Siasa nchini Kenya kina wajibu wa kuweka wazi vyanzo vyake vya Fedha na kutoa taarifa husika kwa Msajili wa Vyama. Ispokuwa, Chama cha Siasa kitaruhusiwa kushirikiana na Taasisi za nje ya nchi kwa masuala ya kiufundi na kiitikadi pasipo kutoa/kufadhili Fedha/Raslimali kwa Chama cha Siasa nchini humo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo ya Kenya, pamoja na mambo mengine muhimu kinatoa sharti kuwa, hakuna Mtu/Taasisi kutoka ndani ya nchi anaruhusiwa kufadhili Chama cha Siasa zaidi ya asilimia 5% ya Bajeti ya Matumizi ya Chama husika kwa Mwaka, na endapo Chama kitathhibitika kupokea ufadhili zaidi ya ukomo uliowekwa na Sheria, kiasi hicho kilichozidi kitachukuliwa/

kitataifishwa kuwa mali ya Serikali na akishindwa kufanya hivyo anaweza kuhukumiwa kifungo cha Miaka 2 au faini ya kiasi hicho cha ziada na Kifungo kwa wakati mmoja.

Aidha, **Kifungu cha 31 na 32** vya Sheria ya Kenya, vinampa Msajili wa Vyama vya Siasa, Mamlaka na wajibu wa kusimamia Mapato na Matumizi ya Fedha za Vyama siasa nchini humo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejifunza pia kuwa, **Kifungu cha 18** Kama ilivyo kwa mapendekezo ya Muswada huu, Msajili nchini Kenya ana Mamlaka ya kuhitaji taarifa yoyote kutoka Chama cha Siasa na Kiongozi wa Chama cha Siasa kwa lengo la kutekeleza matakwa ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, baada ya kupitia mifumo ya kisheria kutoka nchi ya Ghana na Kenya pamoja na nchi nyiningine kama nilivyo zitaja hapo awali, Kamati imeridhika pasipo shaka kuwa, wakati umefika kwa Tanzania kuboresha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuimarisha Usimamizi na Uratibu wa Vyama vya Siasa kwa lengo la kuweka misingi thabiti yenyeye kuimarisha na kuendeleza Demokrasia ya Vyama vingi nchini kwa haki na usawa kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati ina maoni kuwa Tanzania tumechelewa kuenenda na mabadiliko mbalimbali yanayotokea na kuacha changamoto mbalimbali ndani ya nchi katika uratibu na usimamizi wa shughuli za vyama vya siasa.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya awali yanayojenga msingi wa maoni ya Kamati, sasa naomba nitoe maoni na Ushauri wa Kamati ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Serikali wakati wa mashauriano, kama yanavyooneka katika Jedwali la Marekebisho. Maoni hayo yanaelezwa kama ifuatavyo:-

5.1 Maelezo ya Jumla ya Muswada

Mheshimiwa Spika, Sheria ya vyama vya siasa hapa nchini ilitungwa mwaka 1992 ulipoanzishwa mfumo wa vyama

vingi. Sheria hii kwa ujumla inaweka masharti ya uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa vyama vyा siasa nchini. Sheria imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali ili kuboresha na kuondoa changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria na mfumo wa vyama vingi nchini, na marekebisho ya mwisho katika Sheria hii ni ya tangu mwaka 2009, takribani Miaka Kumi (10) iliyopita.

Hivyo, bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa mfumo wa vyama vingi unafanya kazi kwa tija, kwa kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa wananchi pamoja na kukuza demokrasia nchini. Dhamira hiyo, inahitaji mfumo wa sheria zinazosimamia vyama vyा siasa ulio madhubuti. Kwa sababu hiyo, Kamati ina maoni kuwa Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho unatatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake wa Sheria inayorekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika kuwa kama Bunge litapitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama tulivyokubaliana na Mtoa hoja, mfumo wa Sheria nchini utaweza:

- a) Kubainisha majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vyा Siasa ambayo ni pamoja na usajili wa vyama vyा siasa, kutoa elimu ya uraia, kusimamia mienendo ya vyama vyा siasa na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi,
- b) Mumwezesha Msajili wa Vyama vyा siasa kuzitaka taasisi zenyе nia ya kutoa elimu ya uraia kumtaarifu Msajili na pia kumwezesha Msajili kupata taarifa kutoka kwa chama chochote cha siasa. Lengo la marekebisho haya ni kumuwezesha Msajili kuratibu utoaji wa elimu ya uraia, na
- c) Kuwa na masharti mazuri yaliyo dhahiri kuhusu uundwaji wa vyama vyा siasa. Aidha, masharti kwa vyama vyा siasa kufuata matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vyा Siasa yatazingatiwa. Vilevile, mfumo wetu wa sheria utakuwa na vigezo vyा mtu anayeweza kuomba kusajili chama cha siasa

na vigezo vya mtu kuwa mwanachama wa chama cha siasa na hata kuzuia mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika shughuli za chama cha siasa hapa nchini.

Hivyo, Marekebisho ya Sheria hii yanayopendekezwa yataimarisha Utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuipa mamlaka zaidi ya kuratibu na kusimamia kwa ufanisi zaidi uanzishwaji na utekelezaji wa Majukumu ya Vyama vya Siasa nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria nyingine za Nchi.

5.1.1 Masuala yaliyopendekezwa kurekebishwa au kufutwa

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi, Kamati ilibaini masuala ambayo endapo yasingefanyiwa marekebisho au kuondolewa yangekwamisha utekelezaji wa Sheria. Miongoni mwa masuala hayo ni pamoja na:

- a) Msajili kupewa mamlaka makubwa zaidi ya yale anayotakiwa kuwa nayo kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya nchi,
- b) Msajili kupewa jukumu la kuwa mshauri wa Serikali kwa masuala ya Demokrasia ya Vyama vingi nchini, hatua ambayo ingeweza kuhatarisha demokrasia nchini kwa kumpa mtu mmoja kuamua hatima ya misingi ya Katiba ya Nchi,
- c) Adhabu kubwa zenyе kukosa uhalisia na ambazo zinakosa misingi wake chini ya Sheria ya vyama vya Siasa pamoja na Sheria nyingine za nchi zinazopendekezwa katika baadhi ya Ibara za Muswada huu zingekosa mantiki ya busara ya Sheria inayopendekezwa;
- d) Sababu za kufuta usajili wa Chama cha Siasa ambazo kimsingi ni kinyume na sababu zilizoainishwa na Katiba ya nchi,
- e) Masharti yenye kubeba misingi ya Katiba za Vyama na masuala yote ya demokrasia ya Vyama vingi kutungiwa

Kanuni na Waziri badala ya kuainishwa kwenye Majedwali ndani ya Muswada husika,

f) Masuala mbalimbali ya kiuandishi kwa baadhi ya lbara za Muswada ambayo yalihitaji kuandikwa upya ili kuleta mantiki ya kimaudhui iliyokusudiwa, na

g) Masharti ya uunganishwaji vyama (*merging*) yenye muelekeo wa kufuta Ofisi ya Rais, hali ambayo inaweza kuingiza nchi kwenye mgogoro wa Kikatiba.

5.1.2 Masuala yanayopendekezwa kuendelea kuwepo katika Muswada huu

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ya msingi ambayo kwa maoni ya Kamati ndiyo yaliyobeba mantiki ya kimaudhui ya jumla ya Muswada husika, ambayo Kamati ilitambua nla njema ya Serikali na ikapendekeza yabaki kama yalivyo. Baadhi ya masuala hayo ni pamoja na:-

a) Masharti ya kuzuia ufadhili holela kutoka nje ya nchi kwa vyama vya siasa na umuhimu wa kutumia Mfuko wa Baraza la Vyama vya Siasa,

b) Uainishwaji mzuri wa majukumu ya Msajili wa Vyama vya siasa tofauti na ilivyo katika Sheria ya sasa pamoja na kuainisha jukumu la usimamizi wa chaguzi ndani ya vyama vya siasa,

c) Uainishwaji mzuri wa usimamizi wa vyama vya siasa chini ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa kwa ujumla wake,

d) Zasio la vyama vya siasa kuwa na vikundi vya ulinzi na badala yake vyama vipate haki ya ulinzi kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa,

e) Udhibiti wa Maudhui ya Elimu ya Uraia na masuala yenye kuendana na hilo kutoka kwa mtu au taasisi ndani au nje ya nchi;

- f) Uainishwaji bora wa masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika Katiba za Vyama vya siasa ikiwemo mgawanyo mzuri wa kufanya maamuzi mbalimbali kwa vyombo mahsusini ndani ya Vyama husika,
- g) Uainishaji mzuri wa masharti ya Vyama kuungana(*merging*) na kuunda ushirika (*coalition*) pamoja na maboresho ya Kamati kuhusu jambo hili, na
- h) Maeneo yote ambayo hayakukinzana na Misingi ya Katiba ya nchi, Sheria ya Vyama vya Siasa au sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubainisha mapungufu mbalimbali katika mfumo wa kisheria nchini katika usimamizi na uratibu wa Vyama vya Siasa nchini kwa kuandaa marekebisho na kuyawasilisha kwenye Bunge lako Tukufu kuititia Muswada huu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na kuimarisha misingi ya nidhamu ndani ya Vyama vya Siasa hususan matumizi ya fedha za umma, kulinda na kuimarisha misingi ya utaifa kwa Vyama vyote kama ilivyoasiwi na Waasisi wa Taifa letu na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ustawi wa Demokrasia ya Vyama vingi na kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu kwa ujumla.

5.2 Maoni mahsusini kwa kila Ibara

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Demokrasia, amani na utulivu nchini na katika utekelezaji itakuwa vema iwapo baadhi ya Ibara zitarekebishwa kwa kuongeza maneno, kufuta maneno au kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:-

- 1) Katika Ibara ya 3 ambayo inaongeza Kifungu kidogo cha (5) inayohusu majukumu ya Msajili, Kamati inapendekeza:-

- a) kufuta Ibara ya 3(5)(a) kwa kuwa jukumu hili lipo katika Kifungu cha 4(4) cha sheria ya vyama bya siasa,
 - b) Katika Ibara ya 3(5)(c) neno "**monitor**" libaki kama lilivyo ili kumwezesha msajili kufuatilia na kusimamia chaguzi za vyama vya siasa kwa lengo la kupunguza uwezekano wa migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kwenye vyama hivyo,
 - c) Maudhui ya Ibara ya 3 (5) (d) yabaki kama yalivyo pendekezwa na Serikali ili kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa vyama kusimamia matumizi bora ya fedha za umma,
 - d) Kuongezwe maneno "**provide guidelines and**" kabla ya neno monitor katika Ibara 3(5) (e),
 - e) Kufutwa neno "**governed**" katika Ibara ya 3(5)(f) na badala yake kuweka neno "**Administered**" ilikuendana na majukumu ya msajili yaliyo kusudiwa,
 - f) Mapendekezo ya Ibara ya 3 (5) (g) Kuhusu Msajili kuratibu elimu ya Uraia katika vyama vya Siasa yabaki kama yalivyopendekezwa na Serikali, ili kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na maadili, tamaduni za kitanzania na pia kuhakikisha usalama wa nchi unalindwa,
 - g) Kufutwe maneno "**and multi party democracy**" katika Ibara ya 3(5)(h) kwa kuwa siyo majukumu ya msajili, na
 - h) Kufutwe Ibara ya 3(5)(l) kwa kuwa majukumu ya msajili yameainishwa na sheria.
- 2) Kuhusu vyeo vipyta vya Wakurugenzi vinavyoendekezwa katika ibara ya 4 ya Muswada, Kamati inashauri vyeo hivyo vifutwe na cheo cha msajili msaиди kibaki kama kilivyo kwenye sheria ili kuakisi jina la Ofisi na Majukumu yake.
- 3) Katika Ibara ya 5 kuna mapendekezo ya kuboresha kama ifuatavyo:-

a) Katika Ibara ya 5(5A)(1) inayoweka masharti kwa mtu au taasisi inayotaka kutoa elimu ya uraia Kumjulisha msajili irekekebishwe kwa kufuta neno "*registered*" ili kuondoa utata kwa kuwa vinginevyo kuna utata kuhusu mtu aliyesajiliwa.

Aidha, uandishi uboreshwe kwa kuainisha **muda wa siku 30** kwa mtu au taasisi kutakiwa kutoa taarifa kabla ya siku ya kutoa elimu husika. Sababu za pendekero hilo ni kumwezesha Msajili apate muda wa kupitia maudhui ya kupitia andiko linalowasilishwa na mwombaji.

b) Katika Ibara ya 5 (5A)(2) inapendekezwa vigezo vinavyotumiwa na msajili kukataa kupitisha maombi ya kutoa elimu ya uraia viainishwe,

c) Katika Ibara ya 5(5A) (3) na (4) inashauriwa adhabu zipunguzwe kwa kuondoa adhabu ya **shilingi milioni moja** na badala yake kuweka adhabu ya **shilingi laki tano**. Aidha, adhabu inayopendekezwa ya **kifungo cha miezi sita** iondolewe na badala yake iwekwe adhabu ya **Kifungo cha miezi mitatu**.

d) Katika Ibara ya 5(5B) (1) maneno "**or a member**" yaondolewe ili taarifa zitolewe na chama au viongozi wa chama,

e) Maneno "**this section**" yafutwe katika Ibara ya 5(5B)(2) na badala yaandikwe maneno "**subsection one**" ili kuweka rejea inayokusudiwa,

f) Maneno "**person, being a person having the mandate of his political party**," katika Ibara ya 5(5B)(3) yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "**leader of a political party**". Aidha, Kamati inapendekeza kufuta maneno "**one million shillings**" na badala yake yaandikwe maneno "**five hundred thousands shillings**". Vilevile inapendekezwa kufuta maneno **six months** na badala yake yaandikwe maneno "**three months**", na

g) Ibara ya 5(5B)(5) kifutwe kwa kuwa kinaweka vigezo visivyozingatia masharti ya Ibara ya 20(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

h) Ibara ya 6(6) ifutwe na badala yake ibaki kama ilivyo katika sheria ya vyama vyasiasa kwakuwa ndicho kinacho zingatia masharti ya ***in good faith*** na ***without negligence***.

4) Katika Ibara ya 7 inapendekezwa kuwa:

a) Ibara ya 7 (6A)(2) iboreshwe kwa kuongeza maneno "***on account of***" mara baada ya neno "***discrimination***" ili masharti hayo yaweze kueleweka vizuri kimantiki.

b) Ibara ya 7 (6A)(4) iboreshwe kwa kuongeza kazi za msingi za chama ambazo hazitakasimiwa ambapo:

i. Yataongezwa maneno yanayozingatia kazi ya kuchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mgombea Urais Kwenye kifungu cha 6A (4)(a) mara baada ya neno "***constitution***"; na

ii. Katika Kifungu cha 6A (4)(b) baada ya neno "***rules***" yaongezwe maneno yanayozingatia kazi ya kumchagua Katibu Mkuu na Viongozi wa chama wa ndani ya chama wa kitaifa.

c) Ibara za 7 (6A)(6)(7) kuhusu ***Pressure group/Activist group*** ifutwe kwa kuwa inakosa mantiki ya utekelezaji wake.

d) Maneno "***both parents***" katika Ibara ya 6B(a) inayohusu sifa za uraia kwa mtu kuanzisha Chama cha Siasa, yafutwe ili kuwa na maudhui ya Ibara ya 39 (1) na Ibara ya 47 (4)(a) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)

e) Katika Ibara ya 6B(c), maneno "***declared bankrupt***" yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "***un discharged***".

- f) Katika Ibara ya 6B (d) maneno "*twenty one*" yafutwe na badala yake liandikwe neno "**eighteen**".
- g) Ibara ya 7 (6B)(e) irekebishwe kwa kuongeza maneno "**or english**" baada ya neno **Kiswahili** ili kuepuka Kifungu hiki kukinzana na Ibara ya 67 (1)(a) ya Katiba ya nchi,
- h) Katika Ibara 7(6B)(f) yaongeza maneno "*and gender biased violence*" baada ya maneno "**evading tax**",
- i) Katika Ibara ya 6C (1) (b) maneno "*age of majority*" yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "**eighteen years**". Lengo ni kuepuka tafsiri zaidi ya moja, na
- j) Katika Ibara ya 7(6C)(6) maneno "*the provision of this section*" yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "*subsection (4)*".

5) Katika Ibara ya 8, Kamati inapendekeza kufuta Ibara ya 8 (6) na kuiandika upya kama ifuatavyo:-

"where in an application for registration of a political party it is apparent that the proposed name of a political party, the abbreviation of its name or symbol is

(a) is obscene or offensive;
(b) is used by another political"
(c) has been used by a political party whose certificate of registration has been cancelled or its certificate of provisional registration has been lapsed in accordance of the provision of this Act, the Registrar shall, within 14 days from the date of receipt of the application, inform the applicant accordingly.

6) Katika Ibara ya 10(3) maneno "**one million shillings**" yafutwe na badala yake yaandikwe maneno "**five hundred thousands shillings**" na kufuta maneno "**five million shillings**" na badala yake kuweka maneno "**two million shillings**".

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo mengine ni kuwa:

7) Ibara ya 11 irekebishwe ifuatavyo:-

a) Katika Ibara ya 11(8C) (4) rejea iwe ni kifungu kidogo cha (4) badala ya Kifungu cha (3) ili kuondoa makosa ya kiuchapaji,

b) Maneno ya pemberi "*marginal note*" katika Ibara ya 11(8D) yarekebishwe kwa kufuta neno "*rules*" na badala yake kuandika neno "*regulations*" ili kuendana na maudhui ya Ibara,

c) Kamati inapendekeza masuala yanayotamkwa katika Ibara ya 11(8D) (1) yaainishwe kwenye Jedwali ndani ya Muswada huu,

d) Ibara ya 11 (8D) (4) ifutwe kwa kuwa haikidhi vigezo vilivainishwa na Katiba ya nchi katika Ibara ya 20(2), na

8) Ibara ya 12 (2) (f) (g) ifutwe kwa kuwa maudhui ya kifungu hiki hayaendani na maudhui ya Ibara ya 20(2) ya Katiba ya nchi.

9) Ibara ya 13 (b) iandikwe upya ikiwemo kufuta maneno "*from each zone*" yaliyotumika katika Ibara ya 13(b) (ii), kwa kuwa hakuna Sheria yenye kuanzisha ukanda hapa nchini Tanzania.

10) Katika Ibara ya 14(e) kufutwe neno '*bankruptcy*' na badala yake kuongezwe neno "*un discharged*" mara baada ya neno "*declared*".

11) Katika Ibara ya 15(10B)(2) yafutwe maneno "*at any time*" na badala yake yaandikwe maneno "*within twenty one days*" mara baada ya neno "*may*".

12) Katika Ibara ya 17 ya Muswada, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Maudhui ya Ibara ya ya 17(11B) (1) (2) inayotoa sharti la viongozi na wanachama kupoteza nafasi zao za uongozi

na uanachama baada ya vyama husika kuungana "**merging**" yabaki kama yalivyopendekezwa na Serikali. Hata hivyo, kamati inashauri kuwa, marekebisho yafanywe katika Ibara ya 11B(4) kuhusu tafsiri ya "**Political Leader**" kwa kuiondoa Ofisi ya Rais, Kwa kuwa kwa Ibara 42(3) (a) ya Katiba ya Nchi inaweka sharti kuwa Rais atashika madaraka mpaka siku atakapo apishwa Rais mteule. Hivyo, vifungu vifanyiwe marekebisho kumuondoa Rais kupoteza cheo chake endapo ikitokea Chama chake kikiungana na Vyama vingine kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Nchi kuhusu vigezo vinavyosababisha Rais kupoteza sifa za kuwa Rais , ambapo uunganishwaji wa vyama siyo sehemu ya vigezo hivyo,

b) Ibara ya 17 (11C) (2) kuhusu mamlaka ya waziri kutunga kanuni zinazoweka utaratibu wa kuunda ushirika wa vyama "**coalition**" ifutwe na badala yake utaratibu wa kuunda ushirika uainishwe kwenye jedwali katika muswada huu. Aidha, Kamati inashauri Jedwali hili lizingatie mambo muhimu yafuatayo:-

i. Masuala ya kuzingatia katika utaratibu wa kuingia mashirikiano kabla ya Uchaguzi na Masuala ya kuzingatia katika utaratibu wa kuingia mashirikiano baada ya Uchaguzi;

ii. Maamuzi ya mashirikiano yafanywe na mukano mkuu wa chama; na

iii. Makubaliano ya mashirikiano yawekwe kwenye maandishi na yawasilishwe kwa msajili, na

c) Kuwepo na mpangilio mzuri wa Ibara ya 17(11C) na Ibara ya 18 ilikuepuka na kuwa na vifungu viwili vinavyofanana,

13) Katika ibara ya 24, Kamati inashauri maboresho yafuatayo:-

a) Katika Ibara ya 24(6) Irekebishwe kwa kufuta maneno "**or unspecified**" ili libaki maneno "**specified period**".

Kwa lengo la kuainisha muda maalum kwa msajili kusimamisha ruzuku kwa chama cha siasa. Aidha, neno *believes* ifutwe na badala yake kuandikwe neno 'evidence',

b) Katika Ibara ya 24(7) maneno "***Qualified Audit Report***" yafutwe na badala yake yabaki maneno "***Disclaimer Audit Report***". Lengo ni kumpa mamlaka msajili ya kusitisha ruzuku ya chama kilichopata hati chafu tu.

c) Ibara ya 24(9) ifutwe kwa kuwa maudhui yake yameainishwa katika Kifungu cha 22(2)(d) cha Sheria ya Vyama vyta Siasa.

14) Ibara ya 26(2) ifutwe kwa kuwa kifungu hiki hakina mantiki kwa kuzingatia kuwa msajili alishajihakiki kuhusu taarifa za chama husika kabla ya kutoa usajili wa kudumu. Aidha, masharti haya siyo sehemu ya masharti yaliyo ainishwa katika Ibara ya 20(2) ya Katiba ya nchi.

15) Ibara ya 27 iandikwe upya ili kuakisi mantiki ya maudhui iliyokusudiwa kwa kuzingatia majukumu ya Msajili kwa mujibu wa Sheria ya vyama vyta Siasa na misingi ya Katiba ya Nchi. Hii ni pamoja na haki ya Chama kupata taarifa kabla ya Msajili kuchukua hatua stahiki.

16) Ibara ya 31 iandikwe upya ili kuepuka maudhui yake yasirudie maudhui ya Ibara ya 5(5B)2 na 5B(3). Aidha, Maneno ya pembeni ya ibara ya 31(21E) yarekebishwe ili yabebe maudhui ya ibara husika, na Ibara ya 21E(3) ifutwe kwa kuwa Sheria ya Vyama vyta Siasa tayari imeshaainishwa utekelezaji wa majukumu yenyе kufanana na hayo.

17) Ibara ya 32 (k) ifutwe na badala yake masuala haya yawekwe kwenye jedwali katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati iliutendea haki Muswada huu kwa kufanya uchambuzi wa kina ibara kwa ibara na kifungu kwa kifungu, kufanya mashauriano na Serikali kwa kuzingatia misingi ya Katiba ya nchi na Sheria nyingine

za nchi, na hatimaye Serikali kuridhia maoni na ushauri wa Kamati kama ambavyo inaonekana kwenye Majedwali ya Marekebisho.

5.3 Msingi wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi ya Katiba ya nchi na Misingi iliyokwishaainishwa chini ya Sheria ya Vyama vyta Siasa na Sheria nyiningine za nchi, maoni na Mapendekezo ya Kamati ni kuwa, Ibara zote na vifungu vyote viliviyobainika kukinzana na misingi ya Katiba ya nchi vifutwe na vifungu vyenye kasoro za kiuandishi viboreshw. Ushauri huu ulizingatiwa na Serikali iliandaa Jedwali na kukubaliana na Kamati. Sababu ni kuizingatia misingi ya Kikatiba, ustawi wa Demokrasia ya Vyama vingi nchini na uandishi bora wa Sheria yenyе maoni jumuishi inayoteklezeka.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyiningine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili iweze kuufanya kazi Muswada pamoja na kuwezesha ushiriki wa Vyama vyote vyta Siasa katika mchakato wa kuuboresha Muswada huu. Viongozi wa vyama hivyo kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar waliweza kufika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao, ambayo mengi yamezingatiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenesta Joakim Mhagama, (Mb) pamoja na Watendaji wake bila kumsahau Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) kwa usikivu na ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanya kazi maoni na mapendekezo ya Kamati kama yalivyoainishwa katika Majedwali ya Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, naomba ni kutambua na kuwashukuru wadau mbalimbali, Viongozi wa Vyama vyote vyta Siasa vyenye usajili wa kudumu hapa nchini pamoja na Waheshimiwa Wabunge kutoka Kamati mbalimbali za Bunge, waliofika na kutoa maoni na ushauri wao mbele ya kamati pamoja na wengine waliotoa maoni kwa maandishi. Maoni hayo yalisaidia kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nitambue mchango mahsusini wa Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa weledi wake na ushauri wake ambao ulisaidia Kamati kufanya uchambuzi na kufanya uamuzi stahiki katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD) pamoja na taarifa yote hii inayowasilisha maoni ya Kamati. Majina ya Wajumbe hao ni:-

- 1) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
- 2) Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – Makamu /Mwenyekiti
- 3) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
- 4) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
- 5) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
- 6) Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
- 7) Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
- 8) Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
- 9) Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
- 10) Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
- 11) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;-
- 12) Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
- 13) Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
- 14) Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
- 15) Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
- 16) Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb- Mjumbe;
- 17) Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
- 18) Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
- 19) Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
- 20) Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
- 21) Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
- 22) Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
- 23) Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe

24) Mhe. Dkt. Suzan Kolimba, Mb – Mjumbe

Mheshimiwa Spika, namshukuru saana Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndg. Leocardo Kapongwa, Ndg. Hawa S. Manzurya, Ndg. Rehema Kipera.

Kipekee kabisa nawashukuru saana Makatibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa na Ndg. Victor Leonard pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Samwel waliofanikisha kazi ya Uchambuzi, Ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati kwa juhudu kubwa na kujituma kwa hali ya juu ili kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ipasavyo. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
29 JANUARI, 2019

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja linahusiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tumepata mawasiliano mazuri kwamba sasa yeye siyo Dokta tena ni Profesa. Ameimarika zaidi, kwa hiyo, yeye sasa ni Profesa Adelardus Kilangi. Naomba Makatibu pia mzingatie hilo na wenzagu tunaokaa hapa Mezani tuzingatie hilo.

Waheshimuwa Wabunge, kwa hatua hii sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Spika aendelee na sehemu hii inayofuata mchana huu. (*Makofii*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya mawasilisho hayo, tutaendelea na maoni ya Kambi Rasmi

ya Upinzani, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ester Bulaya. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha, naamini Kiti chako kitatumia busara kutenda haki, kupokea Jedwali la Mabadiliko la Wabunge wa Upinzani kuhusiana na Muswada huu. Wamewahi kwa mujibu wa Kanuni, Ofisi ya Katibu wa Bunge imekataa kuyapokea na imepokea ya Mbunge mmoja tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, napenda kuwasilisha Mabadiliko ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2018 [*The Political Parties (Amendments) Bill, 2018*].

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza katika mwaka huu mpya wa 2019 nasimama hapa kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Vyama vya Siasa 2018, sina budi kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kutuepusha na majanga mbalimbali katika mwaka uliopita na kutuwezesha kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba Muswada huu ambao kimsingi unatakiwa kuweka mazingira rafiki ya kufanya siasa na kujenga mustakabali mwema wa uendeshaji wa siasa za nchi yetu unaletwa Bungeni huku wadau muhimu wa siasa kama vile Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Nje wakiwa Gerezani yapata miezi miwili sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla hata ya kupitishwa kwa Muswada huu ambao kwa kiwango kikubwa unaharamisha na kufanya shuguhli za kisiasa kuwa makosa ya jinai hapa nchini, tayari viongozi wa vyama vyaa siasa wamekuwa wakiandamwa na kesi za kisiasa wakiwemo takriban viongozi wote wa juu wa CHADEMA nikiwemo na mimi mwenyewe ninayesoma hotuba hii, Kiongozi wa ACT Wazalendo - Mheshimiwa Zitto Kabwe ambaye leo yuko Mahakamani na Mheshimiwa Selemani Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali hii ya CCM ikatambua kwamba siasa ni mfumo unaogusa maisha ya watu moja kwa moja. Kwa sababu hiyo, inapoleta Muswada kandamizi kama huu, madhara yake hayatavikumba vyama vyaa siasa peke yake ambavyo Serikali imepanga kuvidhibiti, bali yataathiri maisha ya wananchi kwa ujumla wake ikiwa ni pamoja na hata wale wasio na vyama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu miongozo yote ya uendeshaji wa sekta zote ambazo hugusa maisha ya watu moja kwa moja, kwa njia moja ama nyingine hutolewa na vyombo au taasisi ambazo chimbuko lake ni siasa. Mathalani, uamuzi juu ya namna ya nchi inavyotakiwa kuendeshwa kuanzia kwenye utungaji wa sheria, na upangaji wa matumizi ya rasilimali za uendeshaji wa nchi hufanywa na Bunge ambalo kwa ukamilifu wake ni chombo cha kisiasa. Kwa muktadha huo, kitendo cha kuweka vikwazo vyaa aina yoyote katika uendeshaji wa siasa ni kuleta athari katika sekta zingine zozote za kijamii na kichumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muswada huu umelenga kudhibiti vyama vyaa siasa, ni vema kueleza nini maana ya chama cha siasa na malengo yake. Chama cha Siasa ni muunganiko wa watu wenye mawazo na malengo yanayoshabihiana ya kisiasa ambayo hutafuta kushawishi sera za umma ili kuungwa mkono kwa minajili ya kuongoza Serikali. Chama cha siasa kina majukumu makuu manne, ambayo ni: Kuunganisha watu pamoja; kuunda sera zenye maslahi kwa chama na umma ili kuungwa mkono na umma;

kugombea nafasi za uongozi ili kupata uwakilishi; na mwisho ni kuongeza wanachama. Hivyo basi, katika kutimiza majukumu hayo, kila chama kina mbinu zake za kuflikia malengo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chama cha siasa hai wakati wote ni wakati wa harakati kwa lengo la kuwashawishi wanachama na umma na kuisimamia Serikali iliyopo madarakani kwa minajili ya kuikosoa na kushauri mawazo mbadala. Kwa dhana hiyo, sheria au kanuni yoyote inayokusudia au inayolenga kwa namna yoyote kuzuia uhuru wa chama cha siasa kutekeleza majukumu, malengo hayo manne, ni batili na kandamizi kwa sababu inanyang'anya na kufifisha uhuru na haki za msingi za vyama vya siasa na wananchi na inaua demokrasia kwa ujumla wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kutoa utangulizi huu juu ya umuhimu wa kuwa na taasisi za siasa zilizo imara. Uimara wa taasisi ni uwepo wa mazingira ambayo yanavutia au kuhamasisha watu wengi wenye maono kuingia kwenye siasa na kuweza kutoa mchango wao bila ya uwepo wa tishio la kupelekwa jela au kulipishwa faini na vitu vingine kama hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Muswada huu kwa kiasi kikubwa ulifanya kazi ya siasa kuwa ni kosa la jinal au sawa na uhalifu mwingine kama vile ubakaji, wizi, ulaji rushwa na kadhalika. Aidha, faini zilizowekwa kwenye sheria hiyo zinaidhalilisha sana tasnia ya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu ambao kwa njia moja au nyingine ni wadau wakubwa na tunafahamu umuhimu wa kuwa na siasa ilio huru, kuwatendea haki wananchi wa Tanzania kwa kuviondoa vipengele vyote vya Muswada huu vinavyokwenda kinyume na Katiba na vinavyonyima haki na uhuru mionganini mwa vyama vya siasa. Narudia, ni wajibu wetu sote ambao kwa njia moja au nyingine ni wadau wakubwa na kufahamu umuhimu wa kuwa na siasa ilio huru, kuwatendea wananchi wa Tanzania

haki kwa kuviiondoa vipengele vyote vya Muswada huu vinavyokwenda kinyume na Katiba na vinavyonyima haki na uhuru mionganoni mwa vyama vya siasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalisihi Bunge kutumia madaraka yake kuwatetea wananchi wa Tanzania kwa kutunga sheria bora itakayodumu vizazi hata vizazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mwafaka sasa sisi Wabunge tukatafakari kwa kina juu ya nia ya Serikali inapoletwa Miswada ya Sheria hapa Bungeni. Ni lazima nia njema inayohusu mustakabali mpana wa maendeleo ya nchi yetu ioneckane na siyo nia ya kuhakikisha kikundi fulani cha watu kinashikishwa adabu au kumkomoa mtu fulani. Kama Bunge tukikubali kushiriki katika nia ovu za watu fulani ili kuwahakikishia watu hao usalama wa kisheria katika matendo yao yasiyo na nia njema kwa nchi hii tutakuwa tunafanya makosa makubwa sana na huo utakuwa ni usaliti kwa wananchi tunaowawakilisha. Tunawatahadharisha kama kikokotoo na madhara yale miliyaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana kuu ya Muswada huu ni kumpa Msajili wa Vyama vya Siasa nguvu kubwa ya kuingilia uendeshaji wa Vyama vya Siasa na hadi kuwavua uanachama na viongozi wa vyama. Nguvu hii inapitiliza na inampa uwezo zaidi ya ule ambao Katiba za vyama zinautoa kwa wanachama na viongozi wake. Msajili ni mlezi wa vyama, katika hilo tulitarajia angalau alete Muswada ambao utaweza kutatua mizozano baina ya viongozi ndani vyama, baina ya vyama na vyama na Serikali au Tume ya Uchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wenzetu wa Kenya Kifungu cha (38) cha sheria yao ya vyama vya siasa namba 11 ya mwaka 2011 iliyofanyiwa marejeo ya mwaka 2012 kinaanzisha kitu kinachoitwa Kamati Patanishi ya Vyama vya Kisiasa. Lengo la kamati hii ni kutoa nafasi ya mazungumzo baina ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa, Tume Huru ya Uchaguzi pamoja na Vyama vya Kisiasa. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Kamati ya Upatanishi ambayo ni muhimu katika kutatua mizozo ya

kisiasa ikawekwa kwani Msajili mwenyewe hana uwezo wa kutatua mizozo hiyo ya kisiasa badala yake ataikuza na ishindwe kutatulika na hivyo kuendelea kulemaza shughuli za kisiasa na mwisho wa siku ni kushindwa kujenga taasisi zilizo imara katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwanzo wa Muswada katika vifungu vyote vinavyotoa adhabu, hakuna kifungu chochote kinachotoa haki ya kusikilizwa na haki ya kukata rufaa pale mhusika anapoona kuwa hakutendewa haki. Tukumbuke kuwa haki ya kusikilizwa na kukata rufaa ni haki ya msingi kwa mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo ni kwamba Muswada huu wa Msajili ni dhahiri umekuja na dhamira ambayo anaijua yeye na sio kwa ustawi wa demokrasia katika vyama vya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia utangulizi huo ni kwamba Muswada huu ni uonevu mkubwa dhidi ya vyama vya siasa. Sisi Wabunge tuna uwezo mkubwa wa kuzuia uonevu huu ikiwa tutapenda kufanya hivyo. Askofu Desmond aliwahi kusema ukikaa kimya wakati mtu anayeonewa inamaanisha unamuunga mkono mtu yule anayemuonea mwensiwe. Albert akasema dunia imekua mahali hatari pa kuishi, si kwa sababu ya kuwepo na watu wabaya, bali kwa sababu ya kuwepo kwa watu wema wanaokaa kimya uonevu unapotendeka au unapotaka kutendeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya vifungu mbalimbali katika Muswada ulio mbele yetu, Kifungu cha 3(c) cha Muswada huu kinatoa mamlaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuingilia mfumo wa uchaguzi wa ndani ya chama, jambo ambalo linapunguza uhuru wa vyama kufanya chaguzi bila mashinikizo kutoka katika ofisi ya msajili wa vyama vya siasa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu hicho kifutwe na badala yake msajili awe na jukumu la kukuza demokrasia na utawala bora ndani na mionganoni na vyama vya siasa. Kwa

maana hiyo kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo, " *to promote democracy and good governance within and among political parties*". (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 3(g) na kikisomwa pamoja na kifungu cha 5A vyote vinazungumzia kuhusu elimu ya uraia. Wakati kifungu cha 3(g) kinampa mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa kudhibiti elimu ya uraia, kifungu cha 5A kinaweka masharti ya namna ya utoaji wa elimu ya uraia.

Mheshimimiwa Naibu Spika, kwanza, elimu ya urai ni haki ya kila mtanzania bila kujali kama ni mwanachama wa chama chochote cha siasa au la. Aidha, elimu hiyo hutolewa kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Kwa mantiki hiyo, hii siyo kazi ya msajili wa vyama vya siasa kwa kuwa elimu ambayo imekuwa ikitolewa na Serikali kuititia Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Hata kama Muswada huu unamaanisha elimu ya Mpiga kura, bado jukumu hilo lingekuwa chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na siyo Msajili wa Vyama vya Siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5A(1) kinatoa masharti ya namna ya utoaji wa elimu ya uraia kwa kumtaka mtoaji wa elimu hiyo, iwe ni mtu ye yote au taasisi ya ndani au nje ya nchi kutoa taarifa ndani ya kipindi cha siku 30 kwa Msajili wa Vyama vya Siasa iklainishaa aina ya mafunzo, watakaohusika na mafunzo, dhana za kufundishia, pamoja na malengo yanayolengwa kufikiwa na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti hayo hayakutilia maanani kuwa vyama vya siasa vina mahusiano ya kiitikadi na vyama rafiki toka nje ya nchi, na ni haki yao ya msingi ya kueneza Itikadi za vyama vyao bila kujali mipaka ya nchi. Aidha, kifungu kidogo cha (2) kinaweka masharti kwamba msajili anaweza kukataa maombi ya kutoa mafunzo hayo na kutaja sababu za kukataa. Muswada huu haujaainisha popote sababu za Msajili wa Vyama kukataa maombi ya kutoa mafunzo hayo chini ya kifungu cha 5A(1). Huu ni upungufu mkubwa kwani msajili anaweza kukataa tu

kutokana na matashi yake bila kuongozwa na sheria inayopendekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5A pia kimejaa adhabu za faini na vifungo kwa atakayekiuka masharti ya kifungu hicho. Yote haya tunayatafsiri kama ni hila mbaya ya kuvizua hasa vyama vya upinzani, kushirikiana na vyama rafiki katika kueneza itikadi zao na kupata mafunzo ya namna bora ya kuendesha siasa za kistaarabu na kushamiri. Kwa sababu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba kifungu chote cha 5(a) na vipengele vyake vifutwe yaani vifyekelewe mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipyta ya 5B cha Muswada kinampa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama kutaka taarifa yoyote kutoka kwenye Chama au Kiongozi wa Chama. Kambi Rasmi ya Upinzani inapinga msajili kutaka taarifa yoyote kwani taarifa nyingine ni siri kwa ajili ya maslahi na ustawi wa chama. Mathalani haitakuwa afya chama cha siasa kikatakiwa kutoa taarifa za mikakati yake ya ushindi ya uchaguzi na kuitoa kwa mamlaka za Serikali iliyoko madarakani. Kwani hiyo, ni vema Muswada huu ukaainisha aina taarifa zinazotakiwa kutolewa kwa msajili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipyta cha 6A(3) kinaingilia utaratibu wa Katiba za Vyama kwa kutoa sharti kuwa Mkutano Mkuu au Kamati Kuu visikasimu madaraka yake. Huku ni kuingilia utaratibu wa kawaida wa Vyama kwa mujibu wa katiba zao. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki hakileti afya kwa siasa za vyama vingi, hivyo kifutwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6B(a) kinaeleza kwamba kila mtu aweze kusajili chama cha siasa, ni lazima wazazi wake wote wawili wawe ni raia wa Tanzania. Kifungu hiki kinatoa taswira ya ubaguzi na kuonyesha kuwa Tanzania kuna raia ambaye uraia wake ni wajuu kuliko wa mwenzake *first and second class citizen*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaamini kuwa kama mtu ni raia wa Tanzania basi haina haja tena ya kuangalia

uraia wa wazazi wake. Aidha, Ibara ya 13(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kuwa, ni marufuku kwa sheria yoyote inayotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taadhira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sasa wawe tu ni raia wa Tanzania bila sharti la kuzaliwa, hoja ya msingi hapa ni kwamba ikiwa mtu ni mtanzania kwa mujibu wa sheria ya uraia na amekidhi masharti ya kusajili chama cha siasa apewe fursa hiyo na tusianze kutenganisha aina za uraia kwani huo ni ubaguzi na hatima yake tunabomoa tunu za umoja wa mshikamano wa kitaifa tunaoubiri kila siku na mwisho kuingiza Taifa katika mpasuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusisitiza, Ibara ya 39 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa pamoja na Ibara ya 47(4)(a) zinatoa masharti ya mtu anayetaka kugombea Urais au Makamu wa Rais wa Tanzania kwamba atatakiwa kuwa raia wa Tanzania tu kwa kuzaliwa lakini masharti hayo hayakuwekwa kwa wazazi wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji, ikiwa mtu anayewania nafasi ya juu kabisa ya uongozi wa Taifa hili wazazi wake hawawekewi masharti ya uraia na Katiba iweje mtu anayesajili chama cha siasa awekewe masharti haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinakwenda kinyume na katiba na kina hila mbaya ya kuweka mazingira magumu ya kuanzisha vyama vyaa siasa hapa nchini kutokana na woga wa Serikali hii ya CCM kuondolewa madarakani kwa njia ya demokrasia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11, kinaanzisha vifungu vipyaa vyaa 8C, 8D na 8E. Kifungu cha 8C(1) na (2) kinatoa masharti kwamba chama cha siasa lazima kiwe na orodha halisi iliyohuishwa *the updated register* ya wanachama na viongozi wa chama katika ngazi mbalimbali za chama husika, na kwamba Msajili anaweza kudai kupatiwa orodha hizo wakati wowote na taarifa

zozote kuhusu *register* hizo kwa muda atakaoamua katika *notice* atakayokipatia chama husika kuwasilisha taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *register* ya orodha ya wanachama na viongozi wa chama ni mojawapo ya nyaraka muhimu za mikakati ya ushindi wa chama chochote cha siasa. Kwa maneno mengine, idadi ya wanachama ni mtaji na hazina kwa chama cha siasa. Kuiweka idadi hiyo hadharani ni sawa na kuweka hadharani mikakati ya ushindi katika chaguzi mbalimbali na hivyo kuvivezesha vyama pinzani kutumia taarifa hizo katika kujipanga upya. Mbalii na unyeti wa taarifa za wanachama na viongozi wa chama husika, pia ni changamoto kuhifadhi na kuweza kuwasilisha kwa msajili *register* ya wanachama mathalani milioni sita au kumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo baya zaidi ni kwamba kushindwa kutekeleza masharti haya, chama kitapewa adhabu atakayeshindwa kuwasilisha taarifa hizo atakuwa ametenda kosa, na hivyo atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tatu au kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kifungu kipywa cha 8(2) kinampa mamlaka Msajili kuamuru chama fulani kufuta au kurekebisha kifungu cha Katiba yake . Kifungu hiki kinakiuka haki za watu kujumuika na kuamua mambo yao ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya masharti ya kifungu hiki ni kwamba Katiba za vyama vyote zitakuwa sawa kwa kuwa Katiba hizo zitakuwa zimeandikwa kwa mtindo mmoja kwa kufuata orodha ya mambo yaliyopangwa na Serikali kuingizwa kwenye Katiba hizo za vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipywa cha 8E kinazuia vyama kuwa na kikundi cha Ulinzi. Kifungu hiki ni kibaya kwa sababu ulinzi ni jukumu la kila mtu kwa mujibu wa Katiba. Kuanzia vyama visijilinde ikiwa ni pamoja na

kulinda mali na viongozi wake ni kutoa nafasi kwa kushambuliwa na watu wasiojulika na wasiokuwa na nia njema na vyama vyetu. Kwa mtazamo wetu jambo hili lina nia ovu dhidi ya vyama vyetu ikiwa ni pamoja na wanachama, mali na viongozi wetu. Nyie wenyewe mashahidi, kuna viongozi wetu kwenye chaguzi wameuawa wengine vilema na wengine wamepoteza maisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kifungu cha 17, kinachoanzisha vifungu vipyta ya 11A, 11B na 11C, Serikali imeleta marekebisho kwa kifungu cha 11A kwa kuingiza kifungu kipyta cha 16 kwamba masharti ya vyama kuungana au kushirikiana yaliyopo kwenye kifungu cha 11A hayatakihusu chama kilichopo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yanaonyesha ubaguzi wazi wazi wa kisiasa na kwamba sheria hii haihusu chama Tawala kwani kuna tatizo gani CCM kuungana na CHADEMA, kuna tatizo gani CHADEMA kuungana na CCM na vyama vingine kwani mnaumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 19 cha Muswada kinachofuta kifungu cha 12(2) cha sheria na kukiandika upya, kinapiga marufuku shughuli zozote za kisiasa katika Taasisi za Umma, ikiwemo katika Vyuo vya Umma, majengo ya Serikali, sehemu za Ibada, maeneo ya kazi nakadhalika.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa Msajili amesahau kuwa kuna fani inayohusiana na siasa zinafundishwa katika vyuo vya Umma na kupolekea ili mwanafunzi awe mzuri katika taaluma hiyo itamlazimu kufanya mafunzo ya vitendo kwenye vyama vya siasa ili kulinganisha nadharia za darasani na uhalisia katika vyama. Na unatenganisha vipi wanafunzi na wakufunzi wa siasa vyuoni na siasa halisi? Wengi ni mashahidi hasa mmetokea katika siasa za vyuoni na sasa ni viongozi wazuri na wale ambao hawakuwa wanasiasa vyuoni mnaweza kuona aina ya uongozi wao katika hali halisi ya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24 cha Muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha (18) kwa kuongeza vifungu vidogo vyoye vya 6, 7, 8 na 9. Kifungu cha 6 kinaongozwa na hisia za msajili na hivyo kupelekea kusitisha ruzuku kwa chama cha siasa. Jambo hilo la kutokuwa na ushahidi usiokuwa na mashaka bali hisia ni jambo la hatari sana katika nchi inayoendeshwa kwa misingi ya utawala bora.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya kengele ya pili imegonga dakika mbili umalizie.

MHE. ESTER A. BULAYA-MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo yote yaliyobaki yaingizwe kwenye *hansard*.

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU, AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI HIYO, KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA WA MWAKA 2018 (*THE POLITICAL PARTIES (AMENDMENTS) ACT, 2018*) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge-Toleo la January 2016

1. UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza katika mwaka huu mpya wa 2019 nasimama hapa kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Vyama vya Siasa 2018, sina budi kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kutuepusha na majanga mbalimbali katika mwaka uliopita na katuwezesha kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba, Muswada huu ambao kimsingi unatakiwa kuweka mazingira rafiki ya kufanya siasa na kujenga mustakabali mwema wa mwenendo wa siasa za nchi yetu; unaletwa Bungeni huku wadau muhimu wa siasa kama vile Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mwenyekiti CHADEMA Taifa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Nje wakiwa gerezani yapata miezi miwili sasa.

Mheshimiwa Spika, Kabla hata ya kuitishwa kwa muswada huu, ambao kwa kiwango kikubwa unaharamisha na kufanya shuguhli za kisiasa kuwa makosa ya jinai hapa nchini, tayari viongozi wa vyama vya siasa wamekuwa wakiandamwa na kesi za kisiasa wakiwemo takriban viongozi wote wa juu wa CHADEMA, Klongozi wa ACT Wazalendo Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Selemani Bungara - Mbunge wa Kilwa Kusini.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali hii ya CCM ikatambua kwamba siasa ni mfumo unaogusa maisha ya watu moja kwa moja. Kwa sababu hiyo, inapoleta muswada kandamizi kama huu, madhara yake hayatavikumba vyama vya siasa peke yake ambavyo serikali imepanga kuvihhibit, bali yataathiri maisha ya wananchi kwa ujumla wake ikiwa ni pamoja na hata wale wasio na vyama.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu miongozo yote ya uendeshaji wa sekta zote ambazo hugusa maisha ya watu moja kwa moja, kwa njia moja au nydingine hutolewa na vyombo au taasisi ambazo chimbuko lake ni siasa. Mathalani, uamuzi juu ya namna nchi inavyotakiwa kuendeshwa kuanzia kwenye utungaji wa sheria, na upangaji wa matumizi ya rasilimali za kuendesha nchi hufanywa na Bunge – ambalo kwa ukamilifu wake ni chombo cha kisiasa. Kwa muktadha huo kitendo cha kuweka vikwazo vya aina yoyote katika uendeshaji wa siasa ni kuleta athari katika sekta zingine zote za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada huu umelenga kudhibiti vyama veya siasa; ni vema kueleza nini maana ya chama cha siasa na malengo yake. Chama cha Siasa ni *"muunganiko wa watu wenyewe mawazo na malengo yanayoshabihiana ya kisiasa ambao hutafuta kushawishi sera za umma ili kuungwa mkono kwa minajili ya kuongoza serikali"*.

Mheshimiwa Spika, chama cha siasa kina majukumu manne, ambayo ni; Kuunganisha watu pamoja, Kuunda sera zenye maslahi kwa chama na umma ili kuungwa mkono na umma, Kugombea nafasi za uongozi ili kupata uwakilishi na mwisho ni kuongeza wanachama. Hivyo basi, katika kutimiza majukumu hayo, kila chama kina mbinu zake za kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, chama cha siasa hai wakati wote ni harakati, kwa lengo la kuwashawishi wanachama na umma na kuwa msimamizi(watch dog) wa Serikali iliyopo madarakani kwa minajili ya kuikosoa na kuishauri mawazo mbadala.

Mheshimiwa Spika, kwa dhana hiyo, sheria au kanuni yoyote inayokusudia au inayolenga kwa namna yoyote kuzuia uhuru wa chama cha siasa kutekeleza majukumu/malengo hayo manne, ni batili na kandamizi kwa sababu inanyang'anya na kuffifisha uhuru na haki za msingi za vyama veya siasa na wananchi na inaua demokrasia kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutoa utangulizi huo juu ya umuhimu wa kuwa na taasisi za siasa zilizo imara. Uimara wa taasisi ni uwepo wa mazingira ambayo yanavutia au kuhamasisha watu wengi wenyewe maono kuingia kwenye siasa na kuweza kutoa mchango wao bila ya uwepo wa tishio la kupelekwa jela au kulipishwa faini na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kama nilivyoeleza hapo awali, Muswada huu kwa kiasi kikubwa unaifanya kazi ya siasa kuwa ni kosa la jinai au sawa na uhalifu mwingine kama vile ubakaji, wizi,

ulaji rushwa nk. Adhabu na faini vilivyowekwa kwenye sheria hiyo zinaidhalilisha sana tasnia ya siasa.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sote ambao kwa njia moja au nyingine ni wadau wakubwa na tunafahamu umuhimu wa kuwa na siasa iliyo huru, kuwatendea wananchi wa Tanzania haki kwa kuviondoa vipengele vyote vya muswada huu vinavyokwenda kinyume na katiba na vinavyominya haki na uhuru mionganini mwa vyama vya siasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliishi Bunge kutumia madaraka yake kuwatetea wananchi wa Tanzania kwa kutunga sheria bora itakayodumu vizazi hata vizazi.

Mheshimiwa Spika, ni muda mwafaka sasa sisi Wabunge tukatafakari kwa kina juu ya nia ya Serikali inapoleta miswada ya sheria hapa bungeni. Ni lazima nia njema inayohusu mustakabali mpana wa maendeleo ya nchi yetu ionekane na sio nia ya kuhakikisha kikundi fulani cha watu kinashikishwa adabu, au kumkomoa mtu fulani. Kama Bunge tukikubali kushiriki katika nia ovu za watu fulani ili kuwashakikishia watu hao usalama wa kisheria katika matendo yao yasiyo na nia njema kwa nchi hii, tutakuwa tunafanya makosa makubwa sana na huo utakuwa ni usaliti kwa wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, dhana kuu ya muswada huu ni kumpa Msajili wa vyama vya siasa nguvu kubwa ya kuingilia uendeshaji wa vyama vya siasa na hadi kuwavua uanachama wanachana na viongozi wa vyama. Nguvu hii inapitiliza na inampa uwezo zaidi ya ule ambao Katiba za vyama zinautoa kwa wanachama na viongozi wake. Msajili ni mlezi wa vyama, katika hilo tulitarajia angalau alete muswada ambao utaweza kutatua mizozo baina ya viongozi ndani vyama, baina ya vyama na baina ya vyama na Serikali na au Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa Wenzetu wa Kenya Kifungu cha 38 cha sheria yao ya vyama vya siasa namba 11ya mwaka 2011 iliyo fanyiwa marejeo mwaka 2012 kinaanzisha kitu kinacho itwa "Political Parties Liaison Committee" **Kamati**

Patanishi ya Vyama vya Kisiasa. Lengo la kamati hii ni kutoa nafasi ya mazungumzo baina ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka pamoja na Vyama vya Kisiasa. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Kamati ya Upatanishi ambayo ni muhimu katika kutatua mizozo ya kisiasa ikawekwa kwani Msajili Mwenyewe hana uwezo wa kutatua mizozo hiyo ya kisiasa badala yake ataikuza na ishindwe kutatulika na hivyo kuendelea kulemaza shughuli za siasa na mwisho wa siku ni kushindwa kujenga taasisi zilizo imara katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwanzo wa muswada katika vifungu vyote vinavyotoa adhabu, hakuna kifungu chochote kinachotoa haki ya kusikilizwa na haki ya kukata rufaa pale mhusika anapoona kuwa hakutendewa haki. Tukumbuke kuwa haki ya kusikilizwa na kukata rufaa ni haki ya msingi kwa mhusika.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo ni kwamba "muswada huu wa msajili" ni dhahiri umekuja na dhamira ambayo anajua yeye na sio kwa ustawi wa demokrasia katika vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia utangulizi huo ni kwamba muswada huu ni uonevu mkubwa dhidi ya vyama vya siasa. Sisi wabunge tuna uwezo mkubwa wa kuzuia uonevu huu ikiwa tutapenda kufanya hivyo. Askofu Desmond Tutu aliwahi kusema ukikaa kimya wakati mtu anaonewa inamaanisha unamuunga mkono yule anayemuonea mwenziwe (oppressor). Albert Einstein akasema dunia imekua mahali hatari pa kuishi, si kwa sababu ya kuwepo kwa watu wabaya, bali kwa sababu ya kuwepo kwa watu wema wanaokaa kimya uonevu unapotendeka au unapotaka kutendeka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawasihi wabunge wote bila kujali itikadi za vyama vyao, kuongozwa na maneno ya hekima ya Askofu Desmond Tutu na Albert Einstein na kukataa kuunga mkono uonevu kwa kufuta vipengele vyote kandamizi vilivyopo katika muswada huu.

2. MAPITIO YA VIFUNGU MBALIMBALI KATIKA MUSWADA ULIOMBELE YETU

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3(c) cha Muswada huu kinatoa mamlaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuingilia mfumo wa uchaguzi wa ndani ya Chama, jambo ambalo linapunguza uhuru wa vyama kufanya chaguzi bila mashinikizo kutoka katika ofisi ya msajili wa vyama vya siasa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu hicho kifutwe na badala yake msajili awe na jukumu la kukuza demokrasia na utawala bora ndani na miongoni mwa vyama vya siasa. Kwa maana hiyo kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo: *"to promote democracy and good governance within and among political parties"*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3(g) na kikisomwa pamoja na kifungu cha 5A vyote vinazungumzia kuhusu elimu ya uraia. Wakati kifungu cha 3(g) kinampa mamlaka Msajili wa Vyama vya siasa kudhibiti elimu ya uraia, kifungu cha 5A kinaweka masharti ya namna ya utoaji wa elimu ya uraia.

Mheshimimiwa Spika, kwanza, elimu ya urai ni haki ya kila mtanzania bila kujali kama ni mwanachama wa chama chochote cha siasa au la. Aidha, elimu hiyo hutolewa kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Kwa mantiki hiyo, hii siyo kazi ya msajili wa vyama vya siasa kwa kuwa elimu ambayo imekuwa ikitolewa na Serikali kuititia wizara ya elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Hata kama muswada huu ulimaanisha elimu ya Mpiga kura, bado jukumu hilo lingekuwa chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na siyo Msajili wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5A (1) kinatoa masharti ya namna ya utoaji wa elimu ya uraia kwa kumtaka mtoaji wa elimu hiyo, iwe ni mtu yejote au taasisi ya ndani au nje ya nchi kutoa taarifa ndani ya kipindi cha siku 30 kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ikainisha aina ya mafunzo, watakaohusika na mafunzo, zana za kufundishia, pamoja na malengo yanayolengwa kufikiwa na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, masharti hayo hayakutilia maanani kuwa vyama vya siasa vina mahusiano ya kiiitikadi na vyama rafiki toka nje ya nchi, na ni haki yao ya msingi ya kueneza Itikadi za vyama vyao bila kujali mipaka ya nchi. Aidha, kifungu kidogo cha (2) kinaweka masharti kwamba msajili anaweza kukataa maombi ya kutoa mafunzo hayo na kutaja sababu za kukataa. Muswada huu haujaainisha popote sababu za Msajili wa Vyama kukataa maombi ya kutoa mafunzo hayo chini ya kifungu cha 5A(1). Huu ni upungufu mkubwa kwani msajili anaweza kukataa tu kutokana na matashi yake bila kuongozwa na sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5A pia kimejaa adhabu za faini na vifungo kwa atakayekiuka masharti ya kifungu hicho. Yote haya tunayatafsiri kama hila mbaya ya kuvizuia hasa vyama vya upinzani, kushirikiana na vyama rafiki katika kueneza itikadi zao na kupata mafunzo ya namna bora ya kuendesha siasa za kistaarabu na kushamiri. Kwa sababu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba kifungu chote cha 5A na vipengele vyake kifutwe.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipyta ya 5B cha muswada kinampa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama kutaka taarifa yoyote kutoka kwenye Chama au Kiongozi wa Chama. Kambi Rasmi ya Upinzani inapingga msajili kutaka taarifa yoyote kwani taarifa nyingine ni siri kwa ajili ya maslahi na ustawi wa chama. Mathalani haitakuwa afya chama cha siasa kikatakiwa kutoa taarifa ya mikakati yake ya kushinda uchaguzi na kuitoa kwa mamlaka za Serikali iliyoko madarakani. Kwa hiyo, ni vema muswada huu ukaainisha aina taarifa zinazotakiwa kutolewa kwa msajili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipyta cha 6A(3) kinaingilia utaratibu wa Katiba za Vyama kwa kutoa sharti kuwa Mkutano Mkuu au Kamati Kuu visikasimu madaraka yake. Huku ni kuingilia utaratibu wa kawaida wa Vyama kwa mujibu wa katiba zao. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki hakileti afya kwa siasa za vyama vingi, hivyo kifutwe.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 6A (5) kinachohusu ulazima wa chama cha siasa kuenzi na kudumisha uwepo wa mwenge wa Uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba kazi na madhumuni ya mwenge wa uhuru yалиshakamilika, ila ni muhimu kuweka kumbukumbu hiyo katika makumbusho ya taifa na katika vitabu vya historia ila si kwenye sheria. Vilevile Kutambua au Kukumbuka Mapinduzi ya Zanzibar ni jambo jema kwa kuwa ni sehemu ya historia ya nchi yetu, na vizazi vijavyo vitakuwa na haki ya kujua histora hiyo, ila Kambi Rasmi haionti mantiki ya kuweka suala hilo kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6B (a) kinaeleza kwamba ili mtu aweze kusajili chama cha siasa, ni lazima wazazi wake wote wawili wawe ni raia wa Tanzania. Kifungu hiki kinatoa taswira ya ubaguzi na kuonesha kuwa Tanzania kuna raia ambaye uraia wake ni wajuu kuliko wa mwenzake (first and second class citizen). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaamini kuwa kama mtu ni raia wa Tanzania basi haina haja tena ya kuangalia uraia wa wazazi wake. Aidha, Ibara ya 13 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kuwa "Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake"

Mheshimiwa Spika, jedwali la marekebisho lilioletwa na Serikali halijabadili mantiki ya uraia wa wazazi wa mtu anayeomba kusajili chama cha siasa. Hii ni kwa sababu kabla ya marekebisho yaliyoletwa, sharti lilikuwa ni wazazi wote wawili wawe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa, ila marekebisho ya sasa wawe tu ni raia wa Tanzania (bila sharti la kuzaliwa). Hoja ya msingi hapa ni kwamba ikiwa mtu ni mtanzania kwa mujibu wa sheria ya urai, na amekidhi masharti ya kusajili chama cha siasa, apewe fursa hiyo na tusianze kutenganisha aina za uraia kwani huo ni ubaguzi na hatma yake tunabomoa tunu za umaja na mshikamano wa kitaifa tunaouhubiri kila siku na mwisho kuliingiza taifa katika mpasuko.

Mheshimiwa Spika, kwa kusitiza, ibara ya 39 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa pamoja na ibara ya 47(4)(a) zinatoa masharti ya mtu anayetaka kugombea urais au Makamu wa Rais wa Tanzania kwamba atatakiwa kuwa raia wa Tanzania kwa kuzaliwa lakini masharti hayo hayakuwekwa kwa wazazi wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji, ikiwa mtu anayewania nafasi ya juu kabisa ya uongozi wa taifa hili wazazi wake hawawekewi masharti ya uraia na Katiba iweje mtu anayetaka kusajili chama cha siasa awekewe masharti hayo?

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kinakwenda kinyume na katiba na kina hila mbaya ya kuweka mazingira magumu ya kuanzisha vyama vya siasa hapa nchini kutookana na woga wa Serikali hii ya CCM kuondolewa madarakani kwa njia za kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11, kinaanzisha vifungu vipyta vya 8C, 8D na 8E. Kifungu cha 8C (1) na (2) kinatoa masharti kwamba chama cha siasa lazima kiwe na orodha halisi iliyohuishwa (the updated register) ya wanachama na viongozi wa chama katika ngazi mbalimbali za chama husika, na kwamba Msajili anaweza kudai kupatiwa orodha hizo wakati wowote na taarifa zozote kuhusu rejista hizo kwa muda atakaoamua katika notisi atakayokipatia chama husika kuwasilisha taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, rejista ya orodha ya wanachama na viongozi wa chama ni mojawapo ya nyaraka muhimu za mikakati ya ushindi wa chama chochote cha siasa. Kwa maneno mengine, idadi ya wanachama ni mtaji na hazina kwa chama cha siasa. Kuiweka idadi hiyo hadharani ni sawa na kuweka hadharani mikakati ya ushindi katika chaguzi mbalimbali na hivyo kuviwzesha vyama pinzani kutumia taarifa hizo katika kujipanga upya. Mbali na unyeti wa taarifa za wanachama na viongozi wa chama husika, pia ni changamoto kuhifadhi na kuweza kuwasilisha kwa msajili rejista ya wanachama mathalani milioni sita au kumi.

Mheshimiwa Spika, jambo bay a zaidi ni kwamba kushindwa kutekeleza masharti hayo, chama kitapewa adhabu ya kusimama kufanya kazi za siasa na pia Kiongozi wa chama aliyeshindwa kuwasilisha taarifa hizo atakuwa ametenda kosa, na hivyo atakabiliwa na adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni 1 na isiyozidi milioni 3 na kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote kwa pamoja. Mambo yote haya yanaonekana kuwa na hila mbaya za kufifisha na kudumaza shughuli za vyama vyama siasa na kimsingi vyama vinavyolengwa na sheria hii ni vyama vyama Upinzani. Kwa mantiki hiyo, tunashauri kifungu hicho kifutwe.

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu kipyra cha 8D(2) kinampa mamlaka Msajili kuamuru Chama fulani kufuta au kurekebisha kifungu cha Katiba yake . Kifungu hiki kinakiuka haki za watu kujumuika na kuamua mambo yao ya ndani. Hii ni kwa sababu kabla Chama hakijasajiliwa lazima kiwasillishe pamoja na mengine Katiba yake kwa Msajili. Na ukweli ni kwamba; Katiba za vyama zinaamuliwa na mikutano mikuu ya vyama husika; na mikutano mikuu kwa vyama hukaa kila baada ya miaka mitano. Kwa muktadha huo, ni kwamba kifungu hiki hakitekelezeki kwa kuwa kinapoka mamlaka ya Mikutano Mikuu ya Vyama kufanya marekebisho ya katiba zao. Aidha kifungu hiki kinatoa shinikizo kwa vyama kufanya marekebisho ya katiba zao hata kama marekebisho hayo hayaungwi mkono na vyama hivyo. Ikiwa kifungu hiki hakitaondolewa, basi katiba za vyama zitakuwa ni katiba za Msajili/Serikali kwa kuwa zitakuwa zimetungwa kukidhi matakwa ya Serikali na sio ya vyama.

Mheshimiwa Spika, athari nyingine ya masharti ya kifungu hiki ni kwamba katiba za vyama vyote zitakuwa sawa kwa kuwa katiba hizo zitakuwa zimeandikwa kwa mtindo mmoja kwa kufuata orodha ya mambo yaliyopangwa na Serikali kuingizwa kwenye katiba hizo. Kwa sababu hiyo hakutakuwa na tofauti kati ya chama A na chama B kwa kuwa maudhui ya katiba zao yanafanana. Hii ni kumnyima mwananchi fursa ya kuchagua kuijunga na chama A kutokana na ubora wa katiba yake kuliko chama B. Kwa ujumla, kifungu hiki kinapunguza wigo wa ubunifu wa vyama katika

kuboresha katiba zao ili kuwavutia wanachama wengi zaidi. Aidha, kifungu hiki kinaondoa kabisa dhana ya ushindani mionganoni mwa vyama vyaya siasa kwa kuwa muundo, katiba na shughuli mbalimbali za vyama vyaya siasa hazitakuwa na tofauti yoyote.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipyaa cha 8E kinazuia Vyama kuwa na kikundi cha Ulinzi. Kifungu hiki ni kibaya kwa sababu ulinzi ni jukumu la kila mtu kwa mujibu wa Katiba. Kuzuia Vyama visijilinde ikiwa ni pamoja na kulinda mali na viongozi wake ni kutoa nafasi kushambuliwa na watu wasiokuwa na nia njema na vyama vyetu. Kwa mtazamo wetu jambo hili lina nia ovu dhidi ya vyama vyetu ikiwa ni pamoja na wanachama, mali na viongozi wetu. Nyie ni mashahidi wa jambo hili, viongozi wetu wameshambuliwa mchana kweupe, katika chaguzi mbalimbali wanachama wameshambuliwa na wengine kuuawa na wengine hadi sasa ni vilema.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa tuna vyombo vyaya ulinzi na usalama; lakini vyombo hivi vimekuwa vina ubaguzi wa kuwalinda viongozi wa chama tawala na upande mwingine vyama vyaya upinzani vinaonekana kama vile ni wahaini na watu wasiotakiwa. Na hii inatokana na mfumo wa utawala uliopo wa kuwa na chama dola, katika mazingira hayo ambayo uwanja wa siasa hauko sawa; wale ambaa ulinzi na usalama wao unaonekana kuwa hatarini kwa nini wahesabiwe kuwa wametenda kosa wakijilinda. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba, kifungu hiki kifutwe.

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu cha 17, kinachoanzisha vifungu vipya vyaya 11A, 11B na 11C, Serikali imeleta marekebisho kwa kifungu cha 11A kwa kuingiza kifungu kipyaa cha 11A (6) kwamba masharti ya vyama kuungana au kushirikiana yaliyopo kwenye kifungu cha 11 A hayatakihusu chama kilichopo madarakani.

Mheshimiwa Spika, mapendelekezo haya yanaonyesha ubaguzi wazi wa kisisasa na kudhihirisha kwamba chama tawala hapa kwetu Tanzania si mionganoni mwa vyama vyaya

siasa na kwamba sheria hii tunavitungia vyama vingine. Mapendekezo haya ya Serikali yanaonyesha kwamba CCM ambayo ndiyo chama tawala hapa kwetu hakifungwi na masharti ya sheria hii na kwamba hakipaswi kufuata taratibu za vyama vya siasa jambo ambao linaashiria kwamba hata kisiposhinda uchaguzi kitaendelea kung'ang'ania madaraka. Huu ni udikteta mkubwa ambao tunataka kuhalalisha kisheria. Kambi ya Upinzani inayapingga kwa nguvu zote mapendekezo haya ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha muswada kinachofuta kifungu cha 12(2) cha sheria na kukiandika upya, kinapiga marufuku shughuli zozote za kisiasa katika taasisi za umma, ikiwemo katika vyuo vya umma, majengo ya Serikali, sehemu za Ibada, maeneo ya kazi n.k. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa Msajili amesahau kuwa kuna fani inayohusiana na siasa zinafundishwa katika vyuo vya umma na tunapoelekea ili mwanafunzi aweze kuwa mzuri katika taaluma hiyo itamlazimu kufanya mafunzo ya vitendo kwenye vyama vya siasa ili kulinganisha nadharia za darasani na uhalsia katika vyama. Na unatenganisha vipi wanafunzi na wakufunzi wa siasa vyuoni na siasa halisi? Wengi ni mashahidi hapa mmetokea katika siasa za vyuoni na sasa ni viongozi wazuri na wale ambao hawakuwa wanasiasa vyuoni mnaweza kuona aina ya uongozi wao katika hali halisi ya siasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 24 cha muswada kinachofanya marekebisho kifungu cha 18 kwa kuongeza vifungu vidogo vya (6),(7),(8) na (9). Kifungu cha (6) kinaongozwa na hisia za msajili na hivyo kupelekeea kusitisha ruzuku kwa chama cha siasa. Jambo hili la kutokuwa na ushahidi usiokuwa na mashaka bali hisia ni jambo la hatari sana katika nchi inayoendeshwa kwa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27, kinachoanzisha vifungu vipyta vya 21D na 21E. Katika kifungu cha 21E kinampa Msajili mamlaka ya kumfkuza Mwanachama wa Chama cha Siasa. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa Katiba za vyama

kwa sababu Msajili anakuwa juu ya Katiba na Vikao nya Chama. Jambo hili linamfanya kuwa juu ya wanachama wakati ye ye sio mwanachama wa chama husika na hivyo anakosa uhalali wa kuwa maamuzi ya kufukuza au kusajili kiongozi wa chama husika.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, sheria nzuri ni sheria zinazotungwa bila hila wala nia ya kuwaadabisha baadhi ya watu au kundi fulani la watu. Tukumbuke kuwa sheria inayoitungwa leo, kesho inaweza kutuathiri sisi wenye we tulioitunga. Tukumbuke kuwa katika siasa hakuna uadui; na mwanasiasa ambaye anadhani siasa ni uadui basi huyo yuko katika fani tofauti kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaelewa vyema kuwa wakati wa mchakato wa utunzi wa Katiba mpya kila mmoja wetu alikuwa anaegemea upande gani na wengi wenu mliokuwa katika Bunge la Katiba mnafahamu kabisa ni jambo gani lilichokuwa mnataka katika Katiba mpya na wangapi mionganoni mwenu walikuwa ni UKAWA na sasa hivi ni wangapi ambao hawataki kabisa kusikia neno Katiba mpya ya wananchi ikisikika masikioni mwao.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo, kwa kuwa siasa ni tasnia inayokua na kuvutia watu wengi kushiriki, hivyo katika kufanya hivyo ni wajibu wetu sisi watunga sheria kuweka mazingira wezeshi ili shughuli za kisiasa zishamiri na tuwe na wanasi siasa na sio wachumia tumbo au waganga njaa.

Mheshimiwa Spika, ni muda mwafaka wa Bunge hili chini ya uongozi wako likaandika historia kwa vizazi vijavyo kwa kutumia madaraka yake chini ya ibaara ya 63 ya Katiba, kwa kuvikataa vipengele vyote vilivyo katika muswada huu vinavyoonekana dhahiri kwamba vina nia ya kudumaza demokrasia ya vyama vingi hapa nchini kwa kuwa vinakwenda kinyume na Katiba ambayo imetoa uhuru wa kuwa na vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Ester Amos Bulaya (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU**

29 Januari, 2019

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tumemaliza mawasilisho sasa tutaendelea na uchangiaji ila niwaombe mpitie jedwali liloletwa na Serikali kwa sababu kuna mambo ambayo yameshaondolewa tayari hilo ni moja.

La pili ni la kuhusu kupokelewa marekebisho ya upande wa vyama vya upinzani hapa mezani pengine wengine hamna nakala lakini ninayo nakala ambayo wameileta ofisini na inapokelewa Mheshimiwa Anatropia Theonest na huyu ni Mbunge wa Upinzani sasa ya kwake alipokelewaje mengine yameachwa. Kwa hiyo, ninayo hapa mbele huenda wengine ya kwao yanakuja ama kama hayaji basi taarifa mtapewa lakini tuiseme kana kwamba ni wote wamekataliwa yako hapa ya Mheshimiwa Theonest. Kwa hiyo, tutandeelea Waheshimiwa Wabunge ninazo orodha hapa za kutoka vyma vyote vinavyowakilishwa humu Bungeni tutaendelea na uchangiaji.

Kwa upande wa Chama cha Wananchi (CUF) majina yako matatu na mtu anayetakiwa kuchangia ni mmoja kwa hiyo nitakavyoita majina mtachangia dakika tano, tano, kwa upande wa CHADEMA majina yako matatu nafasi ziko mbili kwa hiyo maana yake mtagawana dakika kumi majina yote matatu. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kolimba, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia muswada ambao ni muhimu sana kwa demokrasia, amani na utulivu wa Taifa letu. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuleta muswada huu mahususi ambao unakwenda kulijenga Taifa lenye nidhamu, demokrasia, amani na utulivu; na sifa hizo zote zitabaki sifa za kudumu kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba nieleze masikitiko yangu. Kambi ya Upinzani imetumia muda mrefu sana kwenye jukwaa lako na ndani ya Bunge hili tukufu kupoishaa umma. Hotuba nzima ya Kambi ya Upinzani ukiisikiliza au wanapotosha kwa makusudi Watanzania au hawajaelewa huu muswada. Sasa mimi naomba nifanya *assumption* kwamba wenzetu Kambi ya Upinzani hawajaelewa huu muswada na nichukue jukumu la kizalendo kabisa la Mtanzania anayewajibika katika Taifa lake kuufafanua huu muswada, hasa maeneo yale muhimu ambayo nimeona yamepotosha kwa makusudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya manufaa makubwa ambayo muswada huu unayaleta kwetu na kwa Watanzania wote ni dhana ya uwazi na uwajibikaji, kwa lugha ya kigeni tungesema *transparency and accountability*. Hizi dhana nilizozzungumza hapa unazona kwenye Ibara ya 21 ambayo inataka vyama vyote vyaa siasa vitoe tamko la mali na madeni ya taasisi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Ibara ya 22 kuhusu dhana ya uwazi na uwajibikaji kwa vyama vyaa siasa inavitaka vyama vyaa siasa viwe na Afisa Masuuli (*Accounting Officer*) na Ibara ya 23 katika hiyo dhana ya uwazi na uwajibikaji inavitaka vyama vyaa siasa viwe na akaunti maalum ambayo itatumika kwa ajili ya kuhifadhi fedha za ruzuku. Ibara ya 25 kwenye hiyo hiyo dhana ya uwazi na uwajibikaji inamtaka mkaguzi Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akague hesabu za vyama vyote vyaa siasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya naomba niyafafanue, hii dhana ya uwazi na uwajibikaji na Watanzania wajue kwamba wenzetu ambao walikuwa wanaendesha

vyama nya kisiasa kwa mfumo wa ukaranja, kwa mfumo wa udanganyifu, wenzetu baadhi yao wamekuwa wanavitumia vyama nya siasa sio kama taasisi za kwenda kujenga nchi isipokuwa kama *SACCOS*ili waweze kujinufaisha na fedha za ruzuku. Fedha hizi Serikali imetambua kwamba, ni fedha za Watanzania; fedha hizi zinapatikana kwa kupitia kodi. Hii ruzuku inayopelekwa kwenye vyama nya siasa lazima isimamiwe, na ndiyo mantiki ya kuleta muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusiupotoshe umma kuhusu jambo hili. Hili linakwenda kuwasaidia Watanzania, fedha zao na kodi zao zinakwenda kusimamiwa vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nimeliona linapotoshwa, lakini limebeba maudhui muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu ni Ibara ya 5(5)(A)(1). Ni kuhusu uratibu wa elimu ya uraia na programu za kujengea uwezo vyama nya siasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unajua vizuri kwamba hata shule zetu tunazipelekea *curriculum*, wanachofundishwa tunakijua, tumejisimamia. Vyama nya siasa ni matanuru ya kupika viongozi, hawa viongozi wakishaiva katika chama ndio wanaokwenda kuliendesha Taifa hili. Kwa hiyo, haki na wajibu wetu kama Watanzania ni kujiridhisha juu ya maudhui ya mambo yote ambayo yanakwenda kwenye vyama nya siasa ili yale yanayokwenda kufundishwa katika vyama nya siasa yaendane kwanza na utamaduni wetu, yalandane pamoja na mila na desturi zetu za Kitanzania. Dunia yetu imebadilika, *values* zetu hazifanani hata kama nchi zetu ni za kiafrika bado kuhusu tunu tunatofautiana, *values* zetu zinatofautina. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika imani tunu zetu zinatofautiana. Mataifa haya tunu zao zinatofautiana, tunazo mila, tunazo tamaduni zetu na tunazo desturi zetu hizo lazima tuzisimamie kufa na kupona. Kwa hiyo, muswada

huu unakuja na hiyo kwamba, mtu ye yeyote au taasisi yoyote, iwe ya ndani au iwe ya nje, itakayokwenda kutoa elimu ya uraia kwa chama cha siasa, itakayokwenda kufanya programu yoyote ya kuwezesha kujengea uwezo vyama vya siasa lazima itoe taarifa kwa Msajili na ipeleke maudhui. Iwapo Msajili wa Vyama vya siasa ataona kwamba maudhui yaliyokusudiwa hayalindi utamaduni wetu, mila na desturi zetu, hailijengi Taifa letu katika umoja, amani na maendeleo yake atazuia na huo ndio wajibu wake. Kwa hiyo, hilo mimi naomba tusilipotoshe na Watanzania wote walijue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kupanua wigo wa Watanzania kushiriki katika masuala ya siasa bila kujali ukanda wala ukabila. Tunavyo vyama ambavyo ukivitazama vinatafsirika kama vyama vya ukanda, wakati mwingine vinatafsirika kama vyama vya kabilia fulani. Sasa tukiendelea na utaratibu huu tutalimaliza Taifa letu, tutaliangamiza Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muswada huu umelitazama hilo, Ibara ya 13 ya muswada huu inamtaka yeyote anayesajili chama cha siasa, kwanza wanachama wapya wasipungue 200...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alitahadharisha kuhusu muda mfupi tulionao. Kwa hiyo, taarifa na miongozo na kila kitu havitaruhusiwa isipokuwa utaratibu kama mtu anavunja kanuni.

Mheshimiwa Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Katika kipengele hiki ambacho tunataka tulijenge Taifa lenye umoja, Taifa la Kitanzania, ambapo vyama vyote

vya siasa viwe na uwiano sawa wa aina za wanachama waliopo katika vyama vyao ili Tanzania ibaki kuwa moja imetutaka Ibara ya 13 tuhakikishe kwamba wanachama wanatoka kwenye nusu ya mikoa ya Tanzania.

Vilevile pili imetutaka watoke walao kwa mikoa miwili ya Tanzania Zanzibar. Katika Tanzania Zanzibar walau Mkoa wa Pemba na Mkoa mmoja wa Zanzibar ya Unguja. Sasa tunataka nini Watanzania, tunataka kujenga Taifa moja na huu ndio uzuri mkubwa wa huu muswada na tusijikite kwenye vitu vidogo vidogo, tujikite kwenye mambo makubwa yanayokwenda kulijenga taifa la kujivunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni kuimarisha utawala bora ndani ya vyama vya siasa. Moja katika tatizo tunalolipata sisi Watanzania tulijisahau. Usipojenga dhana ya utawala bora kwenye chama huwezi kuupata utawala bora kwenye Serikali, kwa sababu ye yote anayekwenda kulitumikia hili kama Waziri, atakayeshika nafasi ya urais, atakayeshika nafasi ya Uwaziri Mkuu, ametoka kwenye chama. Sasa tukiwa na chama ambacho hakina utawala bora utajenga Taifa gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyo vyaa ambavyo Mwenyekiti ndiye *Accounting Officer*, ndiye huyo huyo Afisa Masuuli, ndiye huyo huyo katibu, ndiyo msemaji wa chama. Sasa huyo huyo akipata nafasi ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutakuwa na taifa gani katika nchi hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba, Watanzania tuuelewe muswada huu katika upana. Tusiende kwenye *details* ambazo hazina tija, tuangalie maudhui mapana ya taifa ambayo yanakwenda kulijenga Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhagama inavyoonekana mchango wako ni matata, naona umepigwa chapuo pande zote. Mheshimiwa Susan Kolimba atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae.

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwa Taifa langu katika Bunge lako hili tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu wa jumla ninaomba kwanza niseme kwamba ninaunga mkono hoja iliyowekwa mezani. Ninaposema kwamba, ninaunga mkono hoja iliyowekwa mezani, sababu za kuiunga mkono ninazo. Labda watu tujiulize kwamba muswada huu wale wanaoupinga kwa masaa mawill na wanaukubali baada ya masaa matatu, wanatafuta nini ndani ya muswada huu? Na wao ni akina nani? Ni wananchi, ni wazalendo au ni watu wa aina gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimeshaona sasa ni mara ya pili watu wanapinga muswada huu, lakini wakati huo huo wanaungu mkono wanasesma kwamba muswada huu ni mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kabla sijaenda kwenye ya kwangu ninaomba kwanza nijaribu kuuweka sawa ukweli. Wakati Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anawasilisha hoja/taarifa yake kutoka kwenye chama chake, Mheshimiwa Ester Bulaya, nilikuwa ninashangaa sana kwa sababu mambo mengi ambayo alikuwa anayazungumza ni mambo ambayo Serikali pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria kwa ujumla wao, kwa uzalendo wao na kwa uyakinifu wao wameyaona kabisa kwamba haya yanapingana na Katiba na yatolewe na yamekubalika. Sasa unapokuwa unazungumza kitu ambacho kimekwishatolewa halafu uko ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watu wengine Wananchi wako huko nje wanakusikiliza inakuwa si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye hoja. Muswada huu ulioletwa katika Bunge lako tukufu, ukuona kwa macho ya kizalendo ni muswada ambao unakwenda kutatua changamoto tulizonazo katika uendeshaji wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu watu wengi waliokuwa wanachangia, wadau na baadhi ya Wabunge ndani ya Bunge hili na baadhi ya taarifa wanasema Msajili wa Vyama vya Siasa amepewa majukumu makubwa sana au mamlaka makubwa saa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wengine wamejaribu kuzungumza kwamba huyu Msajili wa Vyama vya Siasa amepewa mamlaka mpaka ya kuingilia vyama, lakini nadhani wangeusoma muswada huu vizuri wangeweza kuelewa; kwa sababu tangu sheria ya kuendesha vyama vya siasa ilipotengenezwa mwaka ule wa 1992 mabadiliko kama saba yametokea na kila mabadiliko yalipotokea na mimi nilipofuatilia historia nimeona kabisa kwamba, lengo la Serikali ilikuwa ni kujenga demokrasia iliyio makini na kwa ajili ya watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tukija kwenye muswada huu ukiyaangalia marekebisho mengi ya Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo yamefanya kwa kipindi cha kama mara saba, lakini hayakuweza kuweka bayana na kuainisha majukumu halisia ya msajili wa vyama vha siasa, lakini muswada huu umefanya kazi hiyo. Kwa hiyo mtu anapokuwa anaupinga mimi ninamshanga, kwa sababu kwa kuweka bayana majukumu ya msajili wa vyama vya siasa yanamfanya msajili wa vyama vya siasa aweze kuongozwa na kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi na vilevile kujenga demokrasia makini na kuvilea vyama vya siasa ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninasema kwamba, mimi ninaunga mkono muswada huu, muswada huu kwanza unaorodhesha majukumu ya msajili wa vyama vya siasa na yako bayana na hii inamsaidia kufanya *good*

governance kwa sababu atakuwa haendi nje ya utaratibu uliowekwa ndani ya sheria, sasa kama mtu anapinga hilo mimi simwelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili inaweka muongozo mzuri wa mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na vyama vyaa siasa ndani ya vyama vyao vyaa siasa kwa kuangalia wanatakiwa kutengeneza sera za namna gani na utaratibu gani wa kuviedesha vyama vyao vyaa siasa. Mimi ninashangaa sana pale ninapoona baadhi ya ya Wabunge au baadhi ya wadau wanapoppinga kwamba vyama hivi vyaa siasa vinapotengeneza sera zao na majukumu yao na shughuli zao za kuendesha vyama vyao vyaa siasa hivi vyama visihakikishe kwamba muungano wetu unakuwepo, au umoja unakuwepo, au utu unakuwepo, au uzalendo unakuwepo na haya yote yameelekezwa katika kifungu kile cha 3 cha muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niende katika kifungu kingine ambacho kinaangalia utawala bora. Ni kile ambacho kinatoa mamlaka au kinaelekeza kwamba, katika vyama vyaa siasa, kiongozi yejote wa chama cha siasa hataweza kuwa mjambe katika Bodi ya Wadhamini na hiyo ni *good governance* kwa sababu, wale watakuwa wanakisimamia chama, lakini kama akiwa ni kiongozi wa chama cha siasa ndio ambaye anakuwa kwenye bodi ya udhamini inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niende katika kifungu ambacho kinazungumzia kinaweka makatazo kwenye vyama vyaa siasa. Vyama vyaa siasa ni vyama vyaa siasa, lakini vyama vyaa siasa haviwezi kuwa vyama vyaa ulinzi. Nimeona watu wamezungumzia sana kuhusu suala la vikundi vyaa ulinzi kuwepo katika vyama vyaa siasa. Mimi nafikiri hekima itutume kwamba kwenye suala la ulinzi tuwachie majeshi, tuachie vyombo vyaa ulinzi na usalama vifanye kazi yake. Hatuwezi kuchanganya masuala ya chama cha siasa kuwa masuala ya ulinzi, ni aidha uchague wewe ufanye kazi ya kuunda vikundi vyaa ulinzi kama kampuni za ulinzi au uwe chama cha siasa. Sasa muswada huu unaweka wazi na sisi

kama Kamati tumependekeza kwamba pale ambapo vyama vya siasa vitahitaji ulinzi nchi ipo, Serikali ipo na chama kitalindwa kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kuhusu ukaguzi wa hesabu za vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu ukaguzi wa hesabu za vyama vya siasa. Mimi bado naendelea kukubaliana na hoja hii ya Serikali iliyowekwa kuhusu kuhakikisha kwamba ukaguzi na kudhibiti ruzuku ambazo zinatolewa na Serikali kwenye vyama vya Siasa, inaangaliwa vizuri na inasimamiwa na jinsi itakavyokuwa inatumika. Nakubaliana na kifungu hiki kama Kamati yetu ilivyokuwa imetoa mapendekezo kwamba kibaki kama kilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie suala la Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia utaratibu wa uchaguzi kwenye vyama vyetu vya siasa. Mimi sioni kama ni tatizo, kwa sababu ye ye anapokuja kwenye kusimamia utaratibu unaofanywa na vyama vya siasa hana maana kwamba atakwenda kumpandikiza kiongozi ndani ya chama husika, ye ye anaangalia Katiba yako inasemaje? Imefuata Kanuni? Imefuata Katiba ya nchi na utaratibu uliowekwa? Tunapopotosha kusema kwamba Msajili anapokwenda kuhakikisha kwamba utaratibu umefuatwa, maana yake ameingilia na amepandikiza au amechagua viongozi kwenye chama husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala ambalo limezungumzwa kwenye taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani na Waziri Kivuli wa Wizara hii ya sekta, amesema kwamba kuna mambo mengi yapo ndani ya Muswada huu ambao yanakinzana na Katiba. Naomba nimtaarifu rasmi, sisi ndani ya Kamati ya Katiba na Sheria tumepitia vifungu vyote na tumejadili. Kama Mwenyekiti wangu alivyosema, tumejadili na kuviondoa vifungu vyote ambavyo vilikuwa vinakinzana na Katiba. Kwa hiyo, unaposema kwamba bado viro, ni kwamba unapotosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linapotoshwa ni la kuhusu pale mwanachama wa chama cha siasa anapofanya kosa na hatua zinapochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upotoshaji unaofanywa hapa ni kusema kwamba Msajili anamfuta chama. Hapana. Msajili hata kwenye jedwali na hata kwenye mapendekezo yetu tumesema kwamba utaratibu utafuata kama ulivyowekwa kwenye chama usika, ila Msajili atakachokuwa amefanya ni kukitaarifu chama juu ya kosa alilolifanya mwanachama husika ili wao wachukue hatua ya kum-suspend.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo chama cha siasa kitashindwa, bado atawaandikia kwa sababu hapa inaonekana kama hawapewi nafasi ya kujieleza; bado watamwandikia na kumkumbusha kuhusu hilo. Wakishindwa kabisa, basi hatua nydingine za sheria ya nchi yetu itachukua nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kile kifungu cha 8(c) ambacho kinazungumzia kuhusu chama cha siasa kutunza kumbukumbu za Wajumbe na vikao vya chama husika ili pale ambapo Msajili wa Vyama vya Siasa atakapohitaji taarifa, waweze kumpa. Mimi sioni kama ni jambo baya, ni jambo zuri tu kwa sababu ni lazima ajue kama chama hiki je, bado ni hai au kimekufa? Atajuaje kama hawezikupewa hiyo register?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde, Wajumbe wako wanansumbua sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Susan Kolimba. Ahsante sana.

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza niweke sahihi upotoshaji ambao umefanya na mdogo wangu Mheshimiwa Mhagama pale. Kambi ya Upinzani katika hotuba yetu, hakuna mahali popote ambapo tumepinga ukaguzi wa Hesabu za Serikali asifanyie ukaguzi fedha za Umma. Ni muhimu Mheshimiwa Mhagama akajua kuna shida ya kukarishwa vitu vya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Mheshimiwa Mhagama akajua; na rekodi za Bunge hili za mwaka 2009, ni Kambi ya Upinzani kuitia Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe tulileta mabadiliko hapa ya Sheria ya Vyama vya Siasa kutaka Mkaguzi akague ruzuku. Tena CCM walikuwa wanapinga. Usilete upotoshaji hapa, eti tunapinga hii sheria ama Muswada wa Vyama vya Siasa kwa sababu tunaogopa kukaguliwa. Hatujawai kuogopa kukaguliwa jana, juzi, leo na kesho. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuache kudanganya Watanzania kwamba tuna uchungu na tuna mapenzi na kinachoitwa fedha za Umma. CCM mmepewa dhamana nchi, hii lakini leo Hazina (hati chafu), Serikali ya Jamhuri ya Muungano (hati chafu) na Jeshi (hati chafu). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasubiri taarifa ya ukaguzi maalum kuhusiana na *1.5 trillion*, utaona vituko vya kiwango gani Hazina haitulii, inachezewa na Chama cha Mapinduzi. Tusitumie *propaganda* zisizokuwa na kichwa wala miguu kuweza kuhalalisha masuala ya msingi yenye maslahi ya Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu amezungumza hapa kwamba ni mambo madogo. Tunajadili mambo madogo madogo. Hivi suala la Katiba ni jambo dogo? Suala la kuvunja Katiba ya Nchi, ni jambo dogo? Unatambua kuna kazi imefanywa na Kamati vizuri, wala hatupingi. Tunatambua kuna kazi zimefanywa na Serikali ndani na nje vizuri. Tunachotaka turekebishe Muswada uwe bora, tusije tukajidanganya hata siku moja kwamba hii Miswada mnaitungia *CUF*, CHADEMA, ama *ACT*ama *NCCR-Mageuzi*. Hamjui lini mtakuwa wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Katiba, ibara ya 8(c) kuna uvunjaji wa Katiba, naunganana na hoja ya Mheshimiwa Msemaji wa Kambi. Kifungu cha 8(c) kinasema, vyama vinatakiwa viweke *register* mpaka ngazi ya Uongozi, sawa. Tunasema, Msajili anaweza akataka *register*, anasema, anafikiria chama chenye wanachama millioni sita, unataka kiwe kina *register* kila mwanachama, wanachama ambao wanaingia leo au wanaoingia kesho. Kwa maana hiyo wanaingia na kutoka. Hicho chama kitakuwa hakina kazi nyingine zaidi ya kuweka kumbukumbu za wanachama milioni sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8(c)(3) uwezekano siyo shida, kwa sababu vyama makini vina viongozi mpaka kule chini. Mnasema eti Msajili wa chama kinachowenza kushindwa ku-*comply* 8(c)(3) hakijarekebishwa mpaka sasa, labda mniambie Serikali imerekebisha usiku, maana tumepata *Amendments* saa 4.00. Yaani tumepata *Amendment* mpya saa 4.00 asubuhi na saa 4.00 hiyo hiyo mnataka tuchangie na kujumuisha mabadiliko ya Serikali. Wakati wote tumepeleka *Amendment* saa 2.30 mmekazana kutaka kuona huyu bundi, *this is nonsense*. Kifungu hiki kinasema eti chama kikishindwa kupeleka nakala ya wanachama wake Msajili akifute. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Mwanasheria, Ibara ya 20 (2)...

MHE. ESTER A. BULAYA: Na mwalimu wako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mwalimu wangu uliyenismamia *Thesis*. Ibara ya 20(2) ya Katiba (a) - (e) na Ibara 20 (3) inasema mazingira ambayo Msajili anaweza akakinyima chama usajili ama kukifutia, suala la *register* ya mwanachama siyo sehemu ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua Kamati mlifika Kifungu cha 5B mlifika Kifungu cha 8, tunaomba Serikali kwa mantiki hiyo hiyo hiki Kifungu cha 8C(3) kifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Katiba kuna jamaa hapa anasema mambo madogo madogo; usikubali kukaririshwa someni Muswada. Ibara inasema, "ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote na Jamhuri ya Muungano kuweka sharti ambalo ni la ubaguzi. Kasema hapa Mheshimiwa Bulaya, mabadiiiko ya Serikali yanasema kwamba "*a person is citizen of the United Republic by birth and birth parents of that person are citizens of United Republic.*" Katiba inatuambia uraia wa kuzaliwa tu. Hizi *story* za wazazi Katiba haitambui, uvunjwaji wa pili wa Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunjwaji wa Katiba siyo jambo dogo. Tunataka Mheshimiwa Waziri Jenista akija afanye marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vikosi kwa ulinzi wa chama, hivi nani asiyejua leo, kama ni wakweli wanajiamini, kwamba Jeshi la Polisi la nchi hii linafanya kazi ya Chama cha Mapinduzi kwenye uchaguzi. Nani asiyejua? Safari hii kwenye nchi hii tumefika hatua, mimi nimeshudia askari wanaiba kura wanaiba mabox ya kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kifungu kisingekuwa na shida kama majeshi yetu yangesimama katikati. Hiki kifungu kina shida. Kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mnadhimu anapigwa risasi Dodoma Makao Makuu kwenye ulinzi, Serikali imeshindwa kulinda.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 64 inazungumzia kwamba Mbunge hatatoa taarifa ndani ya Bunge ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji amezungumzia kwamba Katiba haina sehemu ambayo inazungumzia uraia wa mtu wa kuzaliwa. Nataka nimkumbushe kwamba Ibara 39 ya Katiba inazungumzia eneo hilo kwamba kiongozi ambaye anachaguliwa ni lazima awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimsaidie tu mwanasheria aweze kuliona hilo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika...

MJUMBE FULANI: Ilikuwa ni Kuhusu Utaratibu au Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

Mheshimiwa Mchengerwa amesimama kwa mujibu kanuni ya 64 akitoa...

Waheshimiwa Wabunge, someni kanuni Hamwelewi tofauti ya mwongozo na utaratibu, mbona mnakuwa hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani, tafadhali sana. Tusikilizane.

Kanuni ya 64 inayozungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, kwa sababu ya muda tulionao, sikusudii kurudia aliyojasema, lakini Mheshimiwa Mchengerwa anaeleza kwamba vipo vifungu ambavyo vinazungumzia mgombea kuwa raia na nafasi mbalimbali nyingi zilizotajwa kwenye Katiba. Naye Mheshimiwa Halima Mdee anavyo vifungu vyake ambavyo anavizungumzia. Kwa hiyo, amevitumia vifungu hivyo kuongea kuhusu hoja yake.

Mimi nadhani kwenye hili kwamba Kanuni imevunjwa, kanuni haijavunjwa. Mheshimiwa Mchegerwa atakapopata muda wa kutoa hoja yake, naye atatumia vifungu anavyoona vinaendana na hoja yake.

Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kumsaidia bwana mdogo, mimi sijasema kwamba... (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, ngoja kwanza. Humu ndani kikanuni wote ni Waheshimiwa na mwanzoni umeanza na Mbunge mwingine naye umemwita dogo, sasa punguza hiyo munkari kidogo. Humu ndani wote ni Waheshimiwa, waite Waheshimiwa, tafadhali.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa na ninashukuru kwa kumwelewesha. Nadhani akienda kusoma vizuri Katiba atanielewa nilikuwa namaanisha nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kama ambavyo Serikali imeleta mabadiliko imefanya ubaguzi kwa sababu Katiba yetu inatoa ruhusa ya kugombea nafasi yoyote kushiriki shughuli yoyote ukiwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa, haizungumzii biashara ya wazazi. Sasa ubaguzi wa kipengele hiki kinagusa wazazi kinyume na Katiba. Kwa hiyo, kohoa kidogo kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nilikuwa namalizia kwamba ni muhimu Mheshimiwa Waziri akaeleza hiki kifungu kinagaubaga kwamba je, vyama vya siasa haviruhusiwi kuwa na ulinzi binafsi? Tafsiri ya walinzi ni nini? Kwa sababu tuna Waziri wa Jeshi hapa, tuna Waziri wa Mambo ya Ndani hapa, wanajua taratibu za kumiliki silaha nchi hii zikoje. Siyo rahisi chama cha siasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Umemaliza muda wako Mheshimiwa Halima Mdee, dakika kumi. Mheshimiwa Sixtus Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Kama muda utaturuhusu, basi tutamsikia Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu asubuhi ya leo. Kabla sijajikita kwenye vifungu, naomba niweke kumbukumbu sahihi kwenye Bunge lako Tukufu. Chama cha siasa ni taasisi kubwa sana. Chama cha siasa ndiyo taasisi inayotoa uelekeo wa nchi katika maana ya uongozi na kupanga mambo yote ya maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chama cha siasa ndiyo walezi wa viongozi. Kwa namna yoyote ile, chama cha siasa kinahitaji kuwa na wanachama. Siyo tu kuwa na wanachama, kuwa na wanachama wanaojulikana na wanaofahamika kwenye nyaraka zao za chama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana, nchi yetu ya Tanzani tupo milioni 50 na ushee. Tunaofanya kazi za kisiasa katika maana ya idadi ya wanachama wa vyama vyote 19 vilivyosajiliwa, hatufiki milioni 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana, katika nchi yetu ya Tanzania tuko milioni hamsini na ushee, tunaofanya kazi za kisiasa katika maana ya idadi ya

wanachama wa vyama vyote 19 vilivyosajiliwa hatufiki milioni 13. Chama cha Mapinduzi kina zaidi ya milioni nane na hawa wote wapo kwenye *register*, Kanisa Katoliki duniani kina wafuasi wake dunia nzima na *register* ya Wakatoliki yote ipo Roma, ni ajabu sana, ni ajabu sana mwanasiasa anayetarajia kuwa kiongozi aseme kuwa na idadi, kuwa na majina ya wanachama wake ni jambo dogo. Hili jambo si dogo hata kidogo, tunataka tuongoze chama cha aina gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waungwana wana sema historia ni Mwalimu, naomba hoja yangu nijenje ni kikikita kwenye historia ya chimbuko la demokrasia ya nchi yetu. Mnamo mwaka 1992, nchi yetu iliamua kwa makusudi kuanzisha mfumo wa vyama vingi uliotokana na sheria ya vyama vya siasa mwaka 1992 na imefanyiwa marekebisho mara saba na leo haya yataenda kuwa ya nne, miaka 26 ni mingi sana na inatosha kwa Taifa letu kufanya tathmini na kuona tunakwendaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 92 nchi yetu ilipoamua kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi ilikuwa na malengo makubwa matatu. Lengo la kwanza tulikwenda kwenye mfumo wa vyama katika vingi ili kupanua demokrasia ya nchi yetu. Jambo la pili, tulikwenda katika mfumo wa vyama kwa ajili ya kuimarisha umoja wetu kama Taifa na jambo la tatu tuliamua kwenda katika mfumo wa vyama vingi ili kuifanya nchi yetu iwe huru na iendeshwe kama Taifa huru linalojitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka 26 tafiti zimeonesha vyama vyetu vya siasa katika ujumla wake vingi havikuwahi kuendeshwa kidemokrasia ingawa lengo la msingi ilikuwa ni kuendeshwa kidemokrasia. Jambo la pili, watafiti wanakwambia umoja wa kitaifa wa nchi yetu katika kipindi hiki cha miaka 26 umekuwa unayumba ukilinganisha na tulipokuwa na mfumo wa chama kimoja. Katika hali ya kawaida kwa watu ambao wenye pumzi zenye uhai, lazima wajitafakari, nchi yetu imejitafakari imeona miaka 26 kuna hitilafu kwenye hii sheria, inahitaji

iongezewe nguvu ili iende sambamba na matarajio tulioanzisha 1992, kuifanya nchi yetu ikue kidemokrasia, kuifanya nchi yetu iwe na umoja wa Kitaifa, kuifanya nchi yetu iwe huru na ilinde uhuru wake na isiingiliwe na mtu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakuja kuvifanya vyama vya siasa viendeshe shughuli zake kwa ubora zaidi na kulinda demokrasia, kifungu cha Muswada cha 6(1) – (5) kinaweka mambo ambayo yatavifanya vyama vya siasa vifanye kazi yake vizuri kwa kulinda demokrasia ya nchi na demokrasia ya vyama vyao. Hivi nani asiyejua kulikuwa kuna utaratibu mtu akikaa akiona mwaka huu ni uchaguzi pengine nitaguswa guswa mimi kama Mwenyekiti basi hahitaji mkutano mkuu, wanakutana wahuni wachache wanabadili Katiba. Sheria hii inakwambia mamlaka ya kubadili katiba ni ya mkutano mkuu, , hii ni *experience* ya miaka 26 ya uholela. Uholela ukizoleka sana unakuwa uholela halali na tusiifakishe nchi kwenye uholela halali.

Muswada huu unakwenda kuimarisha muungano na kuvifanya vyama vyetu viwe vyama vya kitaifa, nani asiyejua, nani asiyejua kuna utaratibu mpya anachukua kachama kake kwenye mkoa fulani akatafuata watu watatu akapata usajili. Kwa sheria hii sasa utatakiwa uwe na wanachama 200 nusu ya Tanzania Bara na sharti upate Mkoa mmoja wa Pemba na Mkoa mwingine wa Unguja. Hilo ndio *spirit behind*, huu ndio moyo uliotufanya tuingie katika mfumo wa vyama vingi, tuwe chama cha kidemokrasi cha Kitaifa. Siyo unakuwa chama cha kidemokrasia Mwenyekiti baba, Katibu mama, Mtunza Fedha mtoto na mjomba ndio anakuwa pale Mwenezi; hatuwezi kwenda kwa *style* hiyo. Miaka 26 imetupa haya mafundisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unatutengenezea utaratibu mzuri wa udhibiti wa rasilimali za chama na udhibiti wa rasilimali za umma zinazotokana na ruzuku. Hapa naomba tuelewane vizuri, hapa hatuongelei ruzuku ambayo Mheshimiwa Halima Mdee amesema, hapa tunakwenda zaidi ya hapo, kuna vyama Mwenyekiti ndiye

Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa Chama, anatoa hela kwenye mfuko A anapeleka kwenye mfuko B. Ikkumbukwe meli ya chama ni wanachama na wanachama ni Watanzania tulivyoamua kujiweka ili tueleze mambo yetu yanayotugusa kwa kupitia vyama vya siasa haiondoi kwamba kile chama cha siasa kina hati miliki ya Mwenyekiti, wanachama wana haki na wangapi wamelalamika, wakilalamikia viongozi wao kwamba wanakula ruzuku na mengine, mara ngapi wamelalamika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ngapi wamelalamika kwamba viongozi wao wanawakopesha hela zile zile za ruzuku halafu wanawalipa, mara ngapi? Mbona wanajitaa fahamu kwenye hili, Mheshimiwa Mwenyekiti huu mfumo ndio unatufanya sisi tuwe viongozi wanachi, tukaguliwe, tusimamie rasilimali zetu na tusimamie rasilimali za watu wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalinda maslahi mapana ya nchi, naomba nirudie, maslahi ya mapana ya nchi. Nchi yetu ni bado Taifa changa sana, linabidi kulelewa na kutunzwa, rasilimali zetu hizi zinapaswa kulindwa na kutunzwa na viongozi ambao tunawajua pasipo kuwa na shaka lolote ni Watanzania safi. Naomba ileweke kifungu cha 6B(a) hata kama wakikipotoshwa katika maana yoyote kinasimamia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu, watasema lakini mwishoni tukitoka nje tutakubaliana ndio mwarobaini wa kuondoa uhasama unaotakokana baina ya vyama vya siasa. Kwa sisi ambao tumefanya hizi chaguzi nydingi na ndugu zangu mtakuwa mashahidi, ilifika hatua vijana wetu badala ya kutulinda wanageuka kuwa wanamgambo kama *Al-qaida*. Tunakwenda kwenye chaguzi vijana wanamwagiana tindikali, tunakwenda kwenye chaguzi vijana wanakatana masikio, wanakatana migongo *for the extent of the party*. Hii sheria inakwenda kuwaondoa hawa, si lugha nzuri, wahuni kama kiningiki vile, inaondoa hawa wahuni kukifanya chama kiwe chama cha kisasa, maana yake uhuru tuliuopata kwa kuongea tukiwatengeneza vijana wetu wawe

wanamgambo, leo hawana silaha ila kuna siku wakiwa na *skills* silaha kwa kuipata watajua wao wenyewe. Nishukuru sana Muswada huu unatuweka sisi na wenzetu tuwe tunakaa vizuri bila kugombana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Muswada huu unakwenda kutatua matatizo na migogoro inayoendeshwa na vyama vyaya siasa. Ninyi mtakuwa mashaidi, rafiki yangu Mheshimiwa Bobali atakuwa shahidi, Mheshimiwa Ally Saleh atakuwa shahidi, wote wanajua kilichotokea kwa *CUF A* na *CUF B*. Msajili alipowaambia nipeni nyaraka za kumfukuza kiongozi wetu, hakuna hata mmoja aliyeweza kutoa muhtasari. Leo Msajili anakuja kuwaambia jamani tunzeni nyaraka za vikao vyenu pamoja na maamuzi ili yakiwa magumu mkirudi kwangu niwaambie kuwa haya ni maamuzi yenu, leo hawaalewani, mbingu na dunia havikutani, *CUF Lipumba* na *CUF Maalim* ni vurugu tupu kwa sababu ya hiki kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka hiki kifungu tuna uhakika vyama hivi sasa vitakuwa na utaratibu mmoja. Nazidi kukumbusha hawa sio malaika ni binadamu kama sisi na sifa ya kuwa binadamu, binadamu wana sifa kubwa mbili; sifa ya kwanza ni furaha na sifa ya pili ni machungu. Mtu akibanwa katika machungu hutafuta njia yoyote kuwa na furaha. Tumethibitisha katika kuendesha vyama vyao, haviendeshi kidemokrasi ushahidi upo, tumeona wamekuwa na migogoro isyoisha ushahidi upo. Hakuna hoja yoyote ile itakayoweza kuja kusimama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho, Muswada huu unatupeleka kuwa Taifa huru linalojitambua, linalojitegemea na lenye uhuru kamili usioingiliwa na mtu ye yote ndani na nje ya nchi. Tumepata mfano kutoka nchi nyingi, elimu ya uraia imekuwa ikitumika kufarakanisha watu. Kuna mataifa ya kutosha yaliyokuwa kama *paradise* leo kama yamekuwa kama Somalia, wote mnajua nini kilitokea Libya, wote manajua nini kilitokea Tunisia, wote mnajua nini kilitokea Egypty. Hii yote ilisababishwa kwenda sehemu ambapo sipo.

Mheshimiwa Naibu Spika....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sixtus Mapunda muda wako umekwisha.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofj*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk dakika tano, atamalizia Mheshimiwa Najma Giga dakika tano.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha tukutane kwenye Bunge letu hili na kuweza kuzungumzia leo Sheria ya Vyama vyा Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimjibu mzungumzaji aliyemaliza kuzungumza sasa kwamba akisema vyama vyetu havina demokrasia yawezakana kwao ni zaidi. Nimuulize swalii moja tu, swalii moja la kumuuliza hawa Wabunge waliotoka CHADEMA na CUF wakaenda CCM ni vikao vipi vilivyokaa vikawapitisha. Kwa hiyo kama ni demokrasia huko hakuna zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalotaka kulisema ni kwamba, nishukuru kwamba leo tunapitisha Muswada wa Sheria ya Vyama vyा Siasa na asubuhi hapa tumesikia wakitajwa, yupo Balozi wa Marekani na yupo Balozi wa Sweden amba ni wafadhili wetu wakubwa, najua wamekuja makusudi kuja kuangalia namna gani tunavyojadili Muswada huu. Sasa nawapa tahadhari tu kwamba, sheria tunayopitisha hii yawezekana kama ni nzuri itadumu miaka hamsini ijayo, lakini kama mbaya yawezekana hata isifike 2020 mambo yakavurugika. Kwa hiyo niwambie ipo siku CCM itakuwa chama cha upinzani sheria hii itawahusu na ushahidi wa hilo, juzi Kongo nani alijua kuwa wapinzani watachukua uongozi katika nchi ya Kongo. Nani alijua kwamba Zambia itaongozwa na upinzani, nani alijua kwamba Malawi itaongozwa na upinzani, kwa maoni

yangu naamini sisi wanyonge Mungu atatupa haki yetu.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitangulie kusema kwamba, anayejua 2020 ni Mwenyezi Mungu na naamini kulinga na mambo yanavyokwenda wananchi wa Tanzania wanalisikiliza Bunge hili hata iwe usiku linaooneshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na kifungu cha 5 hiki kinachosema kwamba kutoa taarifa ya mafunzo ndani ya siku 30 na kutoa taarifa ya vifaa, wahusika, aina ya mafunzo na kadhalika kama ni yule *RC* ya Tabora ningesema kifungu hiki fyeklea mbali. Kwa sababu gani nasema hivi? Hiki kifungu haiwezekani sisi leo mpaka tuzungumze tukatumia *maker pen*, tupeleke orodha ya wanaotaka kupewa mafunzo, tupeleke Walimu wa hayo mafunzo, wakati vyama vyetu vina vyama rafiki nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi *CUF* kuna chama ambacho kipo Ujerumanu inaitwa *FNF* hawa tunafanya nao mafunzo mbalimbali, lakini hakuna mafunzo yoyote mabaya waliyoyatoa kwa vyama vyetu na mafunzo yanayotolewa yametusaidia kupata ushindi mkubwa katika uchaguzi uliopita mwaka 2015. Pia kwenye nchi ya Denmark kuna chama kinaitwa *Radikale Venstre* nacho Kimesaidia kutupa mafunzo ambayo yametuwezesha mpaka tumekuwa viongozi bora katika chama yetu cha *CUF*. Sasa watakapoona kwamba kuna masharti magumu kama haya, ulete orodha ya mafunzo aina na vifaa itakuwa ni sharti ambalo halina msingi wowote. Kwa hiyo kifungu hiki cha tano 5A(1) fyeklea mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuwa, kuvinyima vyama vyaa kisiasa vikosi vyaa ulizi ambavyo havitumii silaha hawana hata kiwembe, ni mikono tu yamezidi mafunzo ya kareti, naona kama itakuwa sio sawa na kwa nini tunatetea hivi vikundi vyaa ulinzi? Kwa sababu tumeona uchaguzi unapofika wenzetu wa Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba kuna

watu wanaitwa Janjawid wanatesa watu, wanapiga watu, wanaua watu na hata ikitolewa taarifa Polisi, wale wanalindwa badala ya kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kifo cha Mheshimiwa Mawazo kilipotokea katika uchaguzi, haya yamefanywa na vikundi ambacho ni vya baadhi ya vyama. Sasa na sisi vyama vya upinzani ni lazima tuwe na vikundi vya ulinzi. Vikundi vyetu havitumii silaha, vikundi vyetu vitatumia tu taaluma ya mikono, kwa hiyo mimi nataka vyama vyetu vya siasa viruhusiwe kuwa na vikundi vya ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kuzuia ruzuku kwa vyama pale itakapoonekana kuna dosari; tukukumbuke vyama vinaendeshwa kwa fedha, vyama vina magari, vyama vina ofisi, vyama vinatumia maji, vyama vinatumia umeme. Sasa inapotokea imetokea kosa dogo unavinyima vyama ruzuku ni kuvuia vyama vya siasa na kuitukana demokrasia.

MHE. NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, dakika tano.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba moja kwa moja nianze kwa kusema kwamba, marekebisho ambayo tunayafanya leo ya Muswada wa Sheria hii yana malengo makuu mawili naomba tuelewe hivyo Watanzania wote. Lengo la kwanza ni kuhakikisha kwamba katika mfumo wetu wa vyama vingi katika Tanzania, lazima amani na utulivu idumu daima milele. Hili ndilo lengo la kwanza la sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la pili ni kuhakikisha kwamba vyama vya siasa vyote Tanzania vinashiriki kikamilifu katika hatua ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Hiyo inathibitishwa katika vifungu vyote, lakini naomba niende na kifungu kimoja kutokana na muda. Kwa mfano, *Section 6A(5)* ukurasa wa nane inazungumzia ulazima wa chama cha siasa

kuenzi na kudumisha mambo yote ya kitaifa ambayo yameorodheshwa katika Muswada huu na yamelenga katika maeneo matatu ya vyama vya siasa katika kuunda sera zake za chama cha siasa, lakini katika uteuzi wa wagombea na pia katika uchaguzi wa viongozi, lazima udumishe na kuenzi mambo haya ambayo yametajwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza moja baada ya moja. Naanza na Muungano, naamini muungano hakuna atakayepinga hapa, muungano lazima udumishwe kwa heshima zote katika ya Taifa, ni tunu ya pekee ya nchi hii. La pili ni Mapinduzi ya Zanzibar, Mapinduzi ya Zanzibar ni uhuru wa Wazanzibari, mapinduzi ya Zanzibar ndio alama inayothibitisha uhuru wa Zanzibar, ni lazima iweipo na ienziwe maisha na maisha. Chama chochote ambacho kitakuwa kimekwenda nyuma na makubaliano ya Mapinduzi ya Zanzibar hakifai katika sheria hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye demokrasia wote tunakubaliana hakuna anayepinga, tulikuwa tunapiga kelele demokrasia hakuna, sijui nini na nini, sheria imethibitisha kwamba demokrasia iko ndani ya sheria na vyama vyote vitastahiki kuhakikisha kwamba vinakwenda kwa mujibu wa demokrasia inavyotakiwa. Utawala bora hakuna anayekataa, sheria imeweka wazi mambo yote yanakwenda kwa namna ambayo vyama vinatakiwa vifanye utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija rushwa hakuna mtu anayetaka rushwa, sidhani kama kuna kuna mtu anakubaliana na rushwa, kila chama kinatakiwa kiheshimu hayo. Pia tunakwenda kulinda maadili na misingi ya maadili ya Taifa letu, ndio utakuta kuna vifungu vya utoaji wa elimu, tunadhibiti namna gani elimu ya uraia, vinaingia hapa hapa. Kwa hiyo lazima tulinde maadili ya Taifa letu kupitia sheria hii. Vilevile tunakwenda kwenye uzalendo, jamani uzalendo si rangi, si kabila wala si dini, uzalendo ni kulipenda Taifa lako, kulitetea kwa hali yoyote, kuhakikisha kwamba unaleta maendeleo katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine, Mwenge wa Uhuru, Uhuru *torch*, Uhuru *torch* ni *symbolization* ya Uhuru wa Tanganyika, ile pale, ni alama ambayo itabidi ienziwe milele, daima. Si hivyo, malengo ya mwenge wa uhuru hayajaisha Tanzania. Malengo ya mwenge wa uhuru ni kuleta upendo kwenye chuki na ni kuleta heshima kwenye dharau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amani na utulivu halina mjadala, lakini tumeongezewa jembe vyama vyetu havifuati, vina mfumo dume. Kuna chama humu kina Wabunge karibu Ishitini kutoka Zanzibar, hakina mwanamke hata mmoja jimboni, lakini vijana wameingizwa huku kwa sababu ndio Taifa la kesho. Kwa hiyo chama ambacho hakijali vijana hakitakiwi kwenye sheria hii. (*Makofi*) (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jamani naomba nirudie tena kusema, vifungu vyote vya sheria hii vinaendeleza vyama kushiriki kikamilifu katika Taifa letu. Naunga mkono mkono Muswada huu kwa maana hiyo ambayo nimeieleza. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa wabunge tumemaliza kipindi chetu cha asubuhi. Sasa nisome majina ya Wabunge watakaochangia mchana tunaye Mheshimiwa Zainab Katimba, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Said Kubenea, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 10.00 Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Zainab Katimba. (*Makofi*)

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vyta Siasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa uhuru wa kushirikiana na wengine yaani *freedom of association*. Ibara ya 20(2) inatoa masharti na vigezo na mipaka ya Vyama vyta Siasa kutumia nafasi yake kufanya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, Ibara ya 20(3) imetoe mamlaka kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga sheria itakayohakikisha Vyama vyta Siasa vinazingatia masharti yaliyowekwa katika Ibara ya 20. Hivyo, napenda kuipongeza kwa dhati Serikali kwa kufanya mchakato wa kuiangalia Sheria hii ya Vyama vyta Siasa na kuona haja ya kuleta marekebisho ya yatakayofafanua na kusisitiza masharti yaliyoainishwa katika Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika taratibu za kutunga sheria, tunafahamu kwamba sheria huwa inaanza na Muswada. Muswada siyo sheria ni mapendekezo ya awali ya sheria au maboreshao ya sharia. Muswada ule unasomwa hapa Bungeni kwa Mara ya Kwanza Wabunge wote wa vyama vyote wanapewa Muswada ule wausome, wauangalie waone kuna maeneo gani ambayo wao wanaweza kuja kutoa mapendekezo yao ya maboresho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kamati husika ambayo kwa muktadha huu ni Kamati ya Katiba na Sheria, inakaa kuujadili, kuusoma, kupendekeza maboresho ya Muswada huo kwa Serikali. Mapendekezo hayo hayaishii hapo Muswada ule unasomwa kwa Mara ya Pili katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wanapata muda

wa kuujadili na kutoa maoni yao kuhusiana na kuboresha Muswada ule ili baada ya kupita katika mchakato huo ukisainiwa uweze kuwa sheria bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme naipongeza sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi yake kubwa iliyofanya katika kutoa mapendekezo ya kuboresha Muswada huu. Tutambue kwamba kwenye Kamati hiyo ya Katiba na Sheria, kuna uwakilishi wa Wabunge kutoka vyama vyote, japokuwa Wabunge walio wengi kwenye Kamati hiyo ni Wabunge wa CCM. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri sana kufahamu kwamba Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na ni vizuri kufahamu Tanzania inaheshimu uhuru wa kutoa maoni. Hiyo imedhihirika kwa mchakato mzima wa Muswada huu kwa kuweza kuchukua maoni kutoka kwa wadau tofauti tofauti lakini hata kuchukua maoni na mapendekezo kutoka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria na ndiyo maana leo hii Serikali imeleta Jedwali la Marekebisho ya Muswada huu na ukiangalia Jedwali hili limezingatia mapendekezo ya Kamati. Kwa hiyo, hii inadhihirisha ni kiasi gani nchi yetu inaheshimu uhuru wa maoni lakini ni nchi ya kidemokrasia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda nitoe mifano michache tu ya maeneo ambayo Kamati ilitoa mapendekezo lakini na Serikali ikayapokea mapendekezo ya maboresho hayo ya Muswada huu. Kwenye *clause 7* ambayo imanzisha kifungu cha 6B katika Sheria ya Vyama vya Siasa, utaona kwamba kifungu hiki kimeweka sifa ya mwanzilishi au sifa ya mtu atakayetaka kuanzisha chama cha siasa. Kwenye Muswada sifa ya mtu huyu ilikuwa imewekwa kwamba awe ni raia wa Tanzania lakini na wazazi wake wote wawili wawe raia wa Tanzania. Hata hivyo, Kamati kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 13(1),(2) na (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikatoa mapendekezo ya maboresho ya kifungu hiki na Serikali yetu kwa sababu ni sikiu, Serikali yetu inaheshimu uhuru wa maoni, imepokea maoni yao na ndiyo maana yanaonekana kwenye Jedwali

la Marekebisho ya Muswada huu ambalo limeletwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, kuna kifungu ambacho kimeanzishwa cha 6B(d) ambacho kinazungumzia umri wa mwanzilishi wa chama cha siasa. Hapo awali iliwekwa sharti iwe miaka 21 lakini kwa mapendekezo ya wadau mbalimbali ikiwemo na Kamati ya Katiba na Sheria, ikapendekeza kwamba kwa kuzingatia mashari ya kikatiba Ibara ya 5 na 21 ambayo inatoa na kufafanua umri wa mtu kuweza kushiriki katika shughuli za kisiasa ikiwemo kuchaguliwa na kuchagua lakini kujihuisha na shughuli za umma ikiwemo shughuli za kisiasa, basi mapendekezo yakatoka umri ule uzingatie Katiba na uwe miaka 18. Serikali imechukua mapendekezo hayo na ndiyo maana yanaonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Sheria. Kwa hiyo, nasema na nasisitiza kwamba tutambue kwamba demokrasia ya kweli ipo lakini uhuru wa kutoa maoni upo na mchakato huu mzima umedhihirisha hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *clause 31* ambayo imeenda kuanzisha kifungu kipywa cha 21E ambacho kilikuwa kinatoa mamlaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kumfuta uanachama wa Chama cha Siasa au kumuondolea uanachama wake mwanachama wa Chama cha Siasa pale atakapokuwa amevunja Sheria ya Vyama vya Siasa. Kamati ikapendekeza kwamba yafanyike marekebisho ili mipaka ya mamlaka haya ya Msajili wa Vyama vya Siasa iishie kwenye kutoa na kutaka chama husika kimchukulie hatua ya kidhamu mwanachama wake kwanza. Siyo hivyo tu, kama mwanachama huyo au chama kikishindwa kumchukulila hatua mwanachama wake kwa kukinzana na matakwa ya Sheria ya Vyama vya Siasa basi Msajili wa Vyama vya Siasa atoe taarifa na mhusika au mtuhumiwa apewe muda wa kujitetea na baada ya muda wa kujitetea ndiyo adhabu ambayo Msajili wa Vyama vya Siasa atatoa iwe ni kumsimamisha asifanye shughuli za kisiasa. Mapendekezo hayo yamepokelewa na Serikali na ndiyo maana yanaonekana katika Jedwali hili la Marekebisho ya Sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye clause 11 ambayo imeanzisha Kifungu cha 8E katika Sheria hii ya Vyama vya Siasa. Utaona kwamba kifungu hiki kimetoa katazo la vyama vya siasa kuanzisha vikosi vya kijeshi au vikosi vya ulinzi na usalama. Napenda kurejea sheria mama yaani Sheria ya Vyama vya Siasa (*The Political Parties Act*) kwenye kifungu cha 3 na naomba nkinukuu, kimetoa tafsiri ya chama cha siasa (*political party*), kinasema hivi: "*political party*" means any organized group formed for the purpose of forming a government or a local government authority within the United Republic through elections or for putting up or supporting candidates to such election".

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya chama cha siasa siyo kikosi cha ulinzi na usalama, masuala ya ulinzi na usalama yametolewa katika Ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na naomba niisome. Ibara ya 147 ya Katiba inasema: "Ni marufuku kwa mtu ye yeyote au shirika lolote au kikundi chochote cha watu, isipokuwa Serikali kuunda au kuweka Tanzania jeshi la aina yoyote". (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaki kuishia hapo, ukisoma sheria mama, Sheria ya Vyama vya Siasa kifungu cha 11 kinasema kama ifuatavyo: "*Every party which has been provisionally or fully registered shall be entitled-*

b) to the protection and assistance of the security agencies for the purposes of facilitating peaceful and orderly meetings".

Mheshimiwa Spika, lakini kifungu hiki chote cha Sheria hii kimetoa haki kwa kila mwanachana na kila chama cha siasa kupatiwa ulinzi na usalama kwa vyombo ambavyo vimeanzishwa kikatiba. Kwa hiyo, naomba kusisitiza sana kifungu hiki ni muhimu na ye yeyote ambaye anapinga kifungu hiki maana yake anapinga Katiba kwa sababu sheria hii inaenda kufafanua masharti ambayo yamewekwa kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Ibara ya 20(2)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

inasema: "Bila kujali masharti ya Ibara ndogo ya (1) na ya (4), haitakuwa halali kwa chama chochote cha siasa kuandikishwa ambacho kutokana na katiba au sera yake, hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa vipindi na kwa njia za kidemokrasia." Muswada wa Sheria hii unakuja kukazia katika matakwa ya kikatiba. Ndiyo maana Msajili wa Vyama vya Siasa amepewa mamlaka ya kusimamia demokrasia ndani ya vyama. Demokrasia ya kweli inaanzia kwenye vyama vyetu sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafahamu kwamba Wabunge wataridhia na wataona umuhimu wa kuzingatia Katiba waunge mkono mapendekezo ya Muswada huo wa kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa ili tuweze kupata sheria bora itakayosimamia misingi iliyowekwa kikatiba katika siasa za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katimba, umetoa shule kwelikweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Ally Saleh baada ya shule hiyo kweli bado una cha kusema. Haya endelea, una dakika tano. (*Kicheko*)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, makubaliano siyo hayo, nimechukua dakika tano alizonipa Mheshimiwa Bobali kwa hiyo ni kumi.

SPIKA: Nakuruhusu dakika kumi.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naanza kwa kunukuu kauli zako mbili ulizosema jana wakati wa Kikao cha *Briefing*, mojawapo ni ile ya kushangaa kuja kwa Sheria ya Maji kwa namna ilivyokuja ukawa unasema hivi hawa watu wanaishi dunia gani. Pili, nataka nипитie kauli yako ya leo asubuhi au jana pia uliposema kwamba sheria inatungwa kwa kufanya *amendments*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nianze kutiririka. La kwanza ni kwamba kwa mshangao mkubwa pamoja na kauli yako ya jana leo asubuhi *amendments* za Upinzani zimekataliwa kuingia Bungeni. Mpaka sasa sijui kama zimeingia au hazijaingia. Kanuni inasema kwamba tupeleke mapema na tulipeleka mapema lakini tukakwepwakwepwa, nanong'onezwa hapa kama zipo lakini kitendo hicho kimeonyesha nia ovu. Baada ya kusema sisi ndiyo pengine zimekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu kauli yako ile ya maji inanishangaza kwamba Muswada huu umekuja kama ulivyo, kwamba umepita kwa wataalam, Makatibu Wakuu na Cabinet na ukaja Muswada ambao nitataja kasoro zake hata usingetarajia uje kama ulivyokuwa hapa, hii ni dalili ya nia ovu.

Mheshimiwa Spika, Muswada ule umekuja na vifungu vingi ambayo ni *unconstitutional*/ambapo unashangaa kama umepita hatua zote lakini bado mnaleta Muswada ambao ni *unconstitutional*. Pili umekuja Muswada una *lack view process*, sehemu hii ndiyo inampa mamlaka mtu bila ya kuhoji aamue mengine *in belief*, akiamini tu anaweza akafanya utashangaa kwa nini umekuja hivi lakini kwa sababu kulikuwa na nia ovu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni *criminalization of politics*. Vifungu vingi vimekuja ku-*criminalize politics* wakati tunajua huu ndiyo uwanja mpana wa watu kushiriki na ni *politically space* inafaa kutumiwa vizuri lakini we have *criminalized a big part of it*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni suala la ubaguzi. Utashangaa Muswada ambao umepita kwa Makatibu Wakuu na Cabinet unakuja na vifungu vyta ubaguzi, lakini yote kwa sababu ulikuwa nia ovu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme wapinzani hatusemi tusiwe na sheria na anayesema hivyo anajidanganya kwa kusema kwamba wapinzani mnataka

nini, tunataka *a lot* siyo hii, tunataka sheria ambayo itatupeleka mbele. Baada ya miaka 50 ya Uhuru hungetarajia kwamba ungekuwa na sheria ya aina hii. Baada ya miaka kadhaa ya vyama vingi hungetarajia kuwa na sheria kama hii. Kuna mifano mingi ya majirani zetu ya kuitazama, kuna maeneo mengi tu ya kuyatazama, wakija pale wanakupa mifano ya Ghana ukiwaambia kwa nini hukuchua hili wanakwambia kwa nini tuige yote lakini mazuri huwezi kuchukua? *What is the harm kuchukua good practice za wengine?*

Kwa mfano tumesema unachukua vyama unafanya waungane au unachukua vyama unafanya kitu lakini kuna kitu tume-suggest kizuri tu *tribunally disputes certain month tribunally*ya vyama ili mtu akikwaza na Msajili awe na pahala pa kwenda, hata hilo mnalikataa? Hata hilo linakataliwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hii kama vile hawa wanaishi nchi nyngine na hawa wanaishi nchi nyngine *we are lived in the same country?* Na tuna haki ya kufanya siasa kama wengine wanavyofanya siasa. Kama ambavyo kimekuja kipengele kimoja kwa heshima zote kwenye *merge* tunaambiya kwamba chama tawala hakitahusika kwenye *merge* kwa nini kisihusike? Yaani CCM hawatarajii kama wanaweza wakaungana na mtu? Yaani CCM wanafikiri watakuwa hivi hivi kila siku? Alisema Mheshimiwa Mbarouk asubuhi hapa mifano gani, kwani alitarajia kama Mori angeondoshwa, nani alitarajia kama Kaunda angeondoshwa, nani alitarajia kama Kamuzu Banda angeondoshwa, msitarajie msitengeneze mazingira kwa kuona leo *look ahead.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tizameni vizazi vyenu, tizameni usalama wa nchi, mnachukua kifungu mnasema kwamba hakuna kuunda Majeshi, nani kasema vyama vya Upinzani vinataka kuunda Jeshi? Katiba ilishasema kwamba hakuna kuunda Majeshi, nani ataunda Jeshi, sasa unawaambia utalindwa, hivi kweli mnatulinda? Hivi kweli nchi hii inalinda Wapinzani, hivi kweli ingekuwa Wapinzani wanalindwa? Hivi

kweli kungekuwa na haki Wapinzani wanalamika pote hapa kwamba wanachotaka angalau *minimum*. Angalau usalama wao, nani kasema wataunda vikundi nya Kijeshi, kwani Sheria hazipo, kwani usalama wa Taifa haupo, kwa hivyo mnafanya vitu ambavyo mnafikiri mtaishi milele katika siasa.

Mheshimiwa Spika, hamtaishi milele, kuna mwisho wake, kuna kuanguka, wangapi walikuwepo, walikuwepo Firauni, walikuwepo nani anaishi, ameondoka. Kwa hivyo msitengeneze Sheria ambayo inatizamwa leo, tengenezeni Sheria ambayo inakwenda wazi nikupe mifano ya vifungu kuna mambo tulikubaliana na Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati ndio maana nikasema hizi *gains* ambazo tumezipata kwenye Kamati sizikatai lakini zilipaswa ziwepo kwa sababu zimekuja *unconfussion* zimekuja *with a lack of democracy* ndio maana tuka-*gain* kwenye Kamati, Kamati illtumia akili. Yuko mtu simtaji hapa alisema, vifungu vingine vitaipeleka CCM ikashindwe asubuhi Mahakamani, Mahakamani mtakwenda kushindwa asubuhi hata mchana haifiki. Ndio maana baadhi ya viongozi, katika baadhi ya Viongozi baadhi ya Wabunge mle, wakasema, tusahihishe, na nimefurahi Serikali imekubali, lakini vingine wamekataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumezungumza katika suala la kutoa elimu, tumezungumza kwamba kuwe na muda Mheshimiwa Msajili anakujibu, haikuwa-*reflected* humu ukipeleka mafunzo yako unayotaka kufanya hakuambiwa muda gani atajibu, lakini kingine tumesema kwamba tunataka tupewe orodha ya mambo ambayo hayahusiki katika mafunzo ili orodha ile iwe *reference* kwetu katika kutengeneza mafunzo, tukaomba iwe *schedule* iwe na *scheduled* haikuja hapa, unatarajia tufanye nini sasa tumpelekee Msajili halafu tukae tu tusubiri, achague muda anaotaka yeeye kutujibu?

Mheshimiwa Spika, kingine ni suala la *merge* na *coalition*, hili ni eneo ambalo pana kichekesho kikubwa sana kwa sababu unatengeneza mazingira unaamini kama vile CCM hutotarajii kuungana na chama chochote kile,

unajitoa katika *merge* unasema kwa hili chama tawala hakihusiki. Lakini unasahau kwamba ilikuwa ni *challenge* tuliowapa baada ya kuja na sheria Kifungu kibovu katika kifungu hiki, walikuwa wana-*argue* wenzetu wa CCM kwamba ukisha-*merge* vyama vife tukawaambia sawa, vyama vitakufa, lakini vyama vikifa na Rais anakufa kwa sababu Rais hana chama, wakasema Rais haondoki kwa sababu Rais analindwa na Katiba tukasema *what comes first?*

Mheshimiwa Spika, Katiba au Rais wake, au kuwa mwanachama wa chama, *definitely* unachaguliwa kuwa mwanachama wa chama, mwanachama kisha anachaguliwa, kwa hivyo tutakuwa na *President less country* ambayo itakuwa ni *chaos*. Tukasema kingine tukawaambia kwamba *merge* hi itakwenda kuonesha kwamba wanasesma Wabunge ukifika muda wao, wanakufa, tukawaambia sawa wanakufa, lakini je, ikitokea dharura, unataka kuwaita Wabunge, utawaita Wabunge kwa chama gani? Hili halijasahihishwa tunakwenda kwenye *merge*, CCM ndio wameshasema wao chama dume sijui chama gani, wao hawamo, haya, tuseme tumekubali, lakini hawa Wabunge je, Wabunge kumetokea dharura hakukufanyika uchaguzi, hakujafanyika uchaguzi, utawaita kwa Mamlaka gani? Na wakati umesema vyeo vyao vimekufa? Lakini pili ni kuhusu *coalition*, *coalition* tulipendekeza lakini *schedule* iliyouja haikupita kwenye Kamati imekuja...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh.
(Makofii)

Bahati nzuri ulikuwa Mjumbe wa Kamati kwa hiyo mambo mengi mmeyaangalia kwenye Kamati, na tunawashukuruni sana, Mheshimiwa Ngeleja tafadhali, Mheshimiwa Ngeleja hajaingia, nakata jina lake, Mheshimiwa Lusinde tafadhali badala ya Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mungu kupata nafasi hii, ya kutoa mchango kwa ajili ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Nikushukuru kwa sababu nilikuwa mionganoni mwa wajumbe wa hiyo Kamati ambayo walichakatachakata kidogo na ndio maana unaona hata namna yangu ya kuzungumza sasa ni ya Kisheria zaidi kuliko ambavyo siku zote huwa nazungumza kwa verse za kisiasa zaidi. Kwa hiyo, leo nitajikita kwenye kuongea kwa Kisheria na kushawishi Wajumbe, Waheshimiwa Wabunge, waiunge mkono hoja hii kwa ufasaha wake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu muafaka kabisa, Muswada umelenga kuvimarisha zaidi Vyama vya Siasa, kutoka kwenye vingine kuwa Vyama shinikisho kuwa Vyama vnavyotetea hoja ndogondogo na kwenda kuwa Vyama vya Kisiasa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, tunaishukuru sana Serikali kwa kuleta Muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ujio wa Muswada huu, na namna ambavyo tulisaidiana sana na Wanasheria kama Kaka yangu Mheshimiwa Ally Saleh alikuwepo hapo, walikuja wakina Mheshimiwa Zitto Kabwe na wote tulitoka mle tukiwa tumekubaliana kwamba Muswada huu sasa uende kama ulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi, kuna vipengele hapa ukiondoa kimoja unaharibu maudhui yote ya Muswada mzima, kwa hiyo, ndio maana tunasema Muswada huu upite kama ulivyo kwa sababu vipengele vinabebana na kuleta maana kulingana na umuhimu wa Muswada. Na hii maana yake nini? Wanasiasa Watanzania sasa tukomae, tufahamu kwamba nchi hii ina Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wazee wetu wametetea uhuru wa nchi hii na Sheria peke yake zinatungwa ndani ya Bunge, sio kwenye korido za Mabalozi tusiende kuwapotenza muda Waheshimiwa Mabalozi tukafikiri labda kwenye korido zao ndio zinatungwa Sheria, hapana, Sheria

ya nchi hii inatungwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka niwakumbushe tu, maana kuna wengine mpaka viatu vilishaisha soli kila siku Ubalozi huu, Ubalozi huu kuzungumzia Muswada huu. Huu Muswada sasa unataka Vyama Misaada yote ambavyo Vyama vitapata, Serikali ijue Misaada hii ina lenga kuimarisha nini kwenye Chama hiki. Maana yake nini? maana yake Muswada huu sasa unakiimarisha Chama, unajua anayetunza mara nyingi kwenye ngoma ndio anachagua wimbo, sasa ukiacha Vyama vipewe pesa, bila Serikali kujua maana yake wale wanaotoa pesa ndio watachagua nyimbo za kuimbwa na hivyo Vyama, Muswada huu unakataa hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unavitaka Vyama kutambua nembo za Kitaifa, hivi kuna ubaya gani? Waheshimiwa, utambue Mwenge wa Uhuru, utambue Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huu Muswada watu wanauzungumzia juu juu hawajaingia ndani, huu Muswada unakwenda kuviiimarisha Vyama vya Siasa Tanzania, kuzungumzia mambo ya msingi ya Kitaifa. Ndio maana nimesema vipengele vyake vyote vilivyomo humu vипитишве kama vilivyo, Muswada huu unakwenda kumpa nguvu Msajili sasa, Msajii alikuwa akihudhuria Mikutano Mikuu ya Vyama vya Siasa kama mwalikwa tu, lakini Sheria haimtambui. Sasa anahudhuria na kusimamia demokrasia kuona inafanyika ndani ya Vyama hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu sana, Watu wanasema oooohh! Muswada huu unampa Mamlaka makubwa Msajili ya kumbana Mwanachama mmoja mmoja, jamani, kama Shirikisho la Mpira tu Duniani linaweza, mpira una adhabu zake, una kadi ya njano, una kadi nyekundu lakini mpira huo huo, unakufungiwa maisha, kwa hiyo shabiki ambaye atakuwa anakiuka mambo yaliyowekwa kwa ajili ya kuhakikisha mchezo wa mpira wa mguu unafanyika

salama, sasa itakuwa sembuse kwenye Chama cha Siasa! Chama cha Siasa lazima kiwe na Sheria ambayo inawatazama Wanachama, na sasa Watu wajue uhuni tena kwenye kufanya mambo ya siasa haupo, sasa tufanye kwa ukomavu huku tukijua kwamba kuna Sheria inayo tu-guide kuhakikisha kwamba tunatekeleza mambo haya kwa kufuata utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nishukuru sana, kwa namna ambavyo Muswada umeletwa na namna ambavyo vipengele muhimu vimewekwa kama ulinzi na usalama, Watu wanapotosha wanafikiri Muswada huu unakataza Mtu kulindwa, hapana mlinzi wa kwako binafsi wa kumuajiri kutoka *group four* ukamlipa Mshahara kitambulisho kikapelekwa kwenye Wizara ya Kazi kwamba nimemuajiri mlinzi Muswada haukatazi, haukatazi, hakuna mahali Muswada huu unakataza mlinzi binafsi, tusipotoshe, huu Muswada unakataza vikundi vya Kijeshi vya Ulinzi, ambavyo vilikuwa vinapewa mafunzo porini tunavijua kwa hiyo tunasema Muswada huu haujamkataza Mtanzania kulindwa. Naomba utulie, tulia, mama watoto tulia, tulia, mimi nakujua, huyu ni mama watoto wangu kwa hiyo achana naye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, eehe! Jamani mambo ya mapenzi hayaingii kwenye Chama jamani.

Mheshimiwa Spika, ulinzi binafsi mtu akatazwi, anaruhusiwa kujilinda, ye ye mwenyewe kwa kuajiri mlinzi lakini sio chama, kianzishe kundi la vijana kiliite Kundi la ulinzi hiyo Muswada huu umekataza, kwa hiyo mimi nimesimama hapa kusema mambo ya msingi kwanza Muswada huu umetambua nembo za Kitaifa, Mwenge wa Uhuru pamoja na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka Muswada huu uspite bila kusema, kwamba Sheria sasa zinatungwa, sisi ni nchi huru jamani na wote diplomasia waliokuwa kwenye nchi yetu watuheshimu kwamba hili ni Taifa huru linajifanyia mambo yake lenyewe na hatujawahi kuingilia nchi yoyote kwenye kutunga Sheria za nchi zao, nilitaka niseme kwa sababu

wenyewe wapo, wasikie kwamba Mbunge amesisitiza watuachie uhuru wetu na sisi tutaheshimu uhuru wa nchi zao, na Waheshimiwa Wabunge wajue Sheria zinatungwa ndani ya Bunge sio kwa Mabalozi, hayo nilitaka yaeleweke vizuri halafu mambo ya vifungu sasa nawaachia Wanasheria asante sana.

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja. (*Makofi/ Kicheko*)

SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde, tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, na atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba, eeehe, haya Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa na mimi nafasi niweze kuchangia huu Muswada ulio mbele yetu wa Sheria ya Vyama vyta Siasa. Kwanza nianze ku-*declare interest* kwamba ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, kabla sijasahau huko nitakakohitimisha nianze kwa kusema naunga mkono Muswada huu kwa asilimia 100, (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Ibara ya 4(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa ruhusa yako naomba niisome kwa sababu sio ndefu sana, inasema hivi; "Vyombo vyenye mamlaka ya utendaji vitakuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki vitakuwa ni Mahakama ya Serikali ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na pia namalizia kwa kusema na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma vitakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi."

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma utangulizi kwanza nilisoma utangulizi, nilisoma wote lakini kwenye utangulizi hapa wenzetu wanajaribu kuwashawishi sio Bunge

tu na hata ambao waliopo nje kwamba Muswada huu unapitishwa wengine wakiwa ndani, kuna wengine wako ndani, kuna Viongozi wako ndani wamewataja majina.

Mheshimiwa Spika, sijaona *best practice* yoyote ambayo wameiandika hapa kwamba kuna Serikali duniani ambayo hata kama mtu ana uhalifu uko nje basi siku kuna Muswada basi anaachiwa aje achangie halafu arudi kule ndani, sjawahi kuona. Ndio maana nimesoma hii Ibara ili kuangalia hivyo Vyombo vitatu kila moja ana madaraka yake, sasa Bunge hili, haliwezi kuingilia wale walioko ndani, hatujui wamefanya nini, ili waweze kuchangia na hiyo haifanyi muswada uwe batili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini, niseme kifungu 6A(3) ambacho kinazungumzia kukasimu Madaraka. Wakati wachangiaji wengine wakizungumza hapa mmoja wa wachangiaji hapa alikuwa anasema mbona Vyama vingine vinaruhusu Kamati Kuu ya Vyama vyao Kukasimiwa Madaraka na Halmashauri Kuu ya Chama.

Mheshimiwa Spika, ni kweli lakini kinachoongeleta hapa kuna vyama vingine tumeona hiyo Kukasimu Madaraka wanaweza wakawa ni watu wawili tu au watatu wamejifungia basi wamekasimiwa Madaraka, hiki ndio kinachoongeleta hapa. Kwa sababu chama ni cha watu wengi, na wanachama wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali imefanya marekebisho mengi ya Muswada ambao walikuwa wameleta mara ya kwanza tulikaa na Serikali kama ambavyo Serikali wamezungumza, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kuna sehemu nydingi sana ambazo tulikubaliana na wenzetu wakiwepo kwa mfano, Kifungu cha 7(6A) (6B) hiki cha *pressure groups* tulikubaliana kitoke kikatoka Serikali ni sikivu ikasikia ikatoa. Lakini tulikuwa na vifungu ambavyo Kifungu kwa mfano cha Sheria hii Kifungu 24(7) cha kuhusu hati, hati chafu, na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana tutoe neno *qualified* tubaki na *disclaimer* tulikubaliana, lakini vitu vingi, na kimoja ameongelea mwenzangu hapa ametoka kuongea Mheshimiwa Ally Saleh ambacho nacho kimetoka cha kuunganisha vyama iki-*merge* Kifungu hiki nacho tulipinga pamoja. Sasa hawa wenzetu wanakwenda nje wanaenda kusema eti, sisi Chama cha Mapinduzi tumekubali ushauri wao, kutoka wapi? Kwa sababu haya yalikuwa ni mawazo yetu sisi kwenye Kamati, na sio kutoka Upinzani, kitu hiki si kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kuna jambo moja, kuna andiko moja nimelisoma mahali kuna mahali andiko lile shetani anawangaa wanadamu, shetani anasema mimi nawashangaa wanadamu, wanadamu hawa ukiwapa kitu cha moto wanakipooza, lakini ukiwapa tena kitu cha baridi nacho wanakipasha moto. Sasa shetani haelewi kwamba wanadamu wanataka nini, wenzetu wameleta mawazo yao kwenye Kamati yamekuwa *absorbed* tumejadili tukakubaliana. Leo wanaanza kusema haya ni mawazo yao, la kwanza, kitu ambacho si kweli. Lakini la pili tulikubaliana sasa leo mtu anapokuja kusema hii Sheria haifai, nashindwa kuelewa hicho kitu ametoa wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ni suala hili la mali za chama, kwanza nilidhani wenzetu katika Kifungu hiki, ndio wangeunga mkono kwelikwelii kwa sababu hapa sisi Chama cha Mapinduzi unajua kabisa hili suala la mali ya chama hata kwetu Chama cha Mapinduzi, mali za chama zinahakikiwa, sasa hapa kuna ubaya gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili linakwenda sambasamba na suala la ruzuku, kama mtu anataka kusaidia au kikundi kinataka kusaidia kudhibiti kitu ambacho ni cha watu wengi, leo mtu anakataa, huyu ana ajenda ya siri. Unataka mali zako zisijulikane kwa nini? Unaflicha nini, nashangaa kwa sababu nilifikiria Kifungu hiki wangeweza kukfurahia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine wameongelea suala la mwenge. Wenzetu katika kitabu chao wanaandika

kwamba wao wanadhani mwenge kazi yake yake iliisha lakini niwakumbushe Bunge hili, siku moja nadhani kama sio Mheshimiwa Haonga lakini kuna Mheshimiwa hapa alizungumzia nembo ya Taifa na akamsema yule ambaye inasemekana au inasadikika kwamba yeze ndiye alianzisha au aliyechora nembo na akasema hapa Bungeni jamani tuenzi vitu vyetu vinavyotuweka pamoja, tumkumbuke na huyu aliyebungu hiki, leo wamegeuka wanasema mwenge tena hauna maana.

Mheshimiwa Spika, mtu anazungumza hapa kwamba tena hii ni ripoti ya chama kwamba mwenge umekwisha kazi yake, lakini hata pale kwenye nembo yetu iliyoandikwa uhuru na umoja mwenge upo pale na wanauona. Sasa leo wanaposema kwamba mwenge umekwisha kazi zake na nembo yake isiwepo, mimi nashindwa kuelewa *ideology*yao ni ipi, hapa ni kutaka kutupotosha.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme la mwisho, suala la ulinzi. Ulinzi wanaouongelea wao ambao ukiuangalia ulinzi huo kwenye taarifa yao wanazungumzia kwamba ulinzi huo lazima uhalalishwe, lakini kwenye ibara ya 20(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza vyama vya siasa ambavyo vina vikundi ambavyo vina mwelekeo wa kutumia nguvu. Sasa mtu anapoendelea kung'ang'ania vikundi viwepo wakati Jeshi la Polisi lipo mimi nashindwa kuelewa ana ajenda gani ya siri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kifungu hiki nakiafiki kibaki kama kilivyo na hivi vikundi visiwepo kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hizi haziathiri vyama vya upinzani tu, hakuna mahali ambapo sheria hizi tunasema Chama cha Mapinduzi iwe *exceptional*, hakuna wote tutaathiriwa na sheria hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa sheria hii tulipotoka sasa, maana, tukumbuke hii sheria imerekebishwa mara ya mwisho mwaka 2009 miaka kumi

sasa, hapa ni mahali pake sheria hii itatuathiri wote, ni nzuri sana, na nasema hivyo kwa sababu ya uzoefu wa kwenye hivi vyama.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuhusu hili suala la ufadhilli. Wenzetu wamesema kwenye vifungu mbalimbali hata nchi ambazo wamezitaja kwa mfano Ghana na Kenya kuna udhibiti. Leo uanze ufadhilli ambao hauwezi kudhibitiwa hiyo ni hatari kwa usalama wa nchi lakini pia ni hatari kwa usalama wa vyama vyetu nya siasa. Mimi naunga mkono ufadhilli wa kutoka nje uendelee kudhibitiwa na haitaathiri vyama nya upinzani tu, hata chama tawala kitaathirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, nilishamtaja Mheshimiwa Salome Makamba kwa dakika kumi.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kwenye sheria hii muhimu kwa Taifa letu inayohusu vyama nya siasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kulitaarifu Bunge hili kwamba Ibara ya 20(1) ya Katiba inatoa uhuru wa kuunda vyama nya siasa na Ibara ndogo ya (2) inaeleza mambo ambayo yanapaswa kuzingatia katika uundwaji wa vyama nya siasa na ukiyakiuka mambo haya basi chama hicho kinaweza kikafutiwa usajili. Vilevile ibara ya 3 inasema Bunge linaweza kutunga sheria inayoweka masharti yatakayohakikisha kwamba vyama nya siasa vinazingatia mipaka na vigezo vilivyowekwa katika Ibara ya 2 hapo juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Katiba hii hakuna hata sehemu moja inayoonesha kwamba Msajili anaweza kumfukuza mtu kufanya kazi za siasa kwa sababu

amemkosea, haipo hata sehemu moja, lakini muswada ulioletwa na Msajili wa Vyama vya Siasa unampa nafasi hiyo Msajili kinyume kabisa na Katiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikufahamishe kwamba jambo hili halijaja kwa bahati mbaya, tunamfahamu sote hapa Jaji Mutungi, Mheshimiwa Waziri Jenista, *Attorney General* na tunaifahamu Serikali vizuri hawa ni watu ambao wangeweza kukaa chini na kuleta muswada ambao unakwenda sawa na matakwa ya Katiba, lakini wamefanya hivi kwa makusudi kwa sababu Kanuni za Bunge zinataka, kwamba mapendekezo ya kamati yanayokwenda kwa Serikali yarudishwe kwenye kamati wapitie kama kweli wametimiza yale ambayo Serikali imekubaliana na Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumepata majibu ya mapendekezo ya Serikali leo asubuhi hapa Bungeni na kwa kukufahamisha tu kwenye mapendekezo ya Serikali yaliyoletwa yapo mambo mengi ambayo tuliafikiana kwenye Kamati hayajafanyiwa marekebisho. La yamefanyiwa marekebisho sivyo Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria walivyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, haya mambo hayafanyiki kwa bahati mbaya... (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Salome kidogo dakika mbili tu, utaendelea. Mheshimiwa Mchengerwa wewe ni Mwenyekiti wa Kamati.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, ndiyo...

SPIKA: Yuko wapi Mheshimiwa Mchengerwa?

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Haya maneno yanayosemwa ikoje maana yake tulikubaliana kwamba mtapitia kabla.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, Salome Makamba sio Mjumbe wa Kamati yangu kwa hiyo hana ufahamu wa yale ambayo yamerekebishwa na jedwali la Serikali. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana, sasa nimeelewa, kumbe Salome unaongea mambo ambayo... Salome endelea sikuwa na nia ya kumkata.

MBUNGE FULANI: (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

SPIKA: *No! no! no!* Mimi nilitaka Salome tu nielewe maana yake alikuwa anasema kwamba hakushirikishwa ndio maana nikamnyanyua Mwenyekiti katikati ya mjadala, endelea Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge mimi kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninayo haki ya kuingia Kamati yoyote na kwenda kushuhudia mwenendo wa Kamati na ikibidi naweza kutoa mapendekezo, kanuni inanikataza mimi kupiga kura tu. Kama Kanuni hii iko kwa bahati mbaya mimi naridhia na sitokwenda kwenye Kamati yoyote... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa yaani mimi ninachoona kabisa hujajandaa. (*Makofi*)

Eh kabisa kabisa kwa sababu hakuna cha kuficha, ninamuuliza huyu Mwenyekiti nimekukata makusudi nimuulize kwa sababu niliagiza kwamba hii nanii ya Serikali ikishamalizika muione kabla hatujaenda Bungeni na amethhibitisha. Sasa wewe ambaye hukuwa Mjumbe hebu iache ajenda hiyo maana yake unapotosha, eeh. Hiyo ajenda yaani iache tu, wenyе Kamati yao wapo sio vizuri sana kupotosha mambo ambayo; wewe sema unataka kusema nini Salome?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haimruhusu Msajili wa Vyama vya Siasa kumzuia mtu kutengeneza chama cha siasa eti kwa sababu wazazi wake wote wawili si Watanzania, hairuhusu. Hayo ni masharti yalipo kwenye muswada mpya unaokuja na haya ni marekebisho baada ya mara kwanza kuwekwa sharti kwamba mtu haruhusiwi kutengeneza chama cha siasa ikiwa ye ye mwenyewe si raia wa Tanzania kwa kuzaliwa. Yamefanyika marekebisho sasa wameleta aina nyingine wanasesma ni lazima wazazi wako wote wawili wawe raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi siamui nani anizae hapa duniani, kuzaliwa na wazazi wote Watanzania sio *discretion power* niliyonayo, ninajikuta nimezaliwa na wazazi mmoja si Mtanzania na mwininge ni Mtanzania. Hiki kifungu hakikubaliki; kwanza ni kinyume na Katiba, lakini pili Msajili hana hayo mamlaka ya kumuamulia mtu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi katika *section 26(2)* ya muswada huu Msajili amevikwa mamlaka makubwa zaidi ya kufuta chama.

Mheshimiwa Spika, leo kwako, kesho kwangu, lakini nakuhakikishia dua la kuku halimpati mwewe, hii sheria leo tunaitunga kwa kuangalia kesi zilizopo mahakamani za CUF, leo tunaangalia kwa sababu CHADEMA ni chama cha upinzani, lakini ninakuhakikishia wanasesma hii sheria itakuja kuwachinja walioitunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sidhani kama ni sahihi Bunge lako tulipotoshe kwa kumpa mamlaka makubwa namna hii Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kudhani kwamba tunakomesha upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa kazi yake kubwa na namba moja ni kulea vyama vya siasa. Ukiangalia sheria hii mpya iliyokuja kwako vifungu vingi vinafanya kazi ya kubadilisha kazi ya siasa kuwa ni kazi ya jinai. Kosa dogo humu mtu anaweza akajishtukia

amefungwa jela miaka mitatu mpaka miaka 20, kwa kosa dogo tu. Sheria hii inakwenda kupita kimya namna hii tunaruhusu, kazi ya siasa ni kazi ya kujitolea, hakuna watu wanaolipwa kwa ajili ya kufanya kazi ya siasa, lakini tunaruhusu mtu afungwe jela kwa kosa dogo miaka mitatu mpaka karibu miaka 20 na faini juu au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Si ungekuwa unatoa mifano Salome ili watu wakuelewe unasema kwa kosa fulani...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Nimesema *section 26(2)* isomwe pamoja na Ibara ya 8(c) na (e) ya marekebisho na *section* zingine zinazofanana na hizo, zipo nyingi sana. kwa ajili ya *interest* ya muda naomba nitaje hizo chache.

Mheshimiwa Spika, tulisema wazi kwamba ili kuepuka mgogoro kama uliojitokeza kwenye kikokotoo, namna ya kutengeneza *coalition terms and conditions* zielezwe kwenye sheria moja kwa moja na sio kwenye kanuni, tunalieleza hilo. Katika eneo la *coalition* nyuma tumeweka *schedule* tumeonesha namna gani muungano wa vyama vya siasa unaweza kuundwa, lakini katika sheria hii *minister* anakwenda kutafsiri yale yaliyoandikwa kwenye sheria mama juu ya muungano wa vyama vya siasa. Tunayo sababu ya kuliangalia hilo kwa kina kabla hatujafunga muswada huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kwenda haraka niende kwenye suala la kufuta vikundi vya ulinzi. Mawakili na wanasheria wenzangu wamepotosha suala lilioandikwa kwenye Katiba la uundwaji wa majeshi. Vipo vikundi mbalimbali vya binafsi vya ulinzi tena vinakwenda mbali zaidi wanapewa *rank* za kijeshi, wanabeba silaha na wanapewa mafunzo ya kijeshi. Vikundi vya ulinzi tunavyoviongelea hapa ni vile vya mtu kujilinda mwenyewe au wanachama kulinda mali zao cha chama.

Mheshimiwa Spika, leo tunasema hao wamekatazwa na katiba, katiba haijakataza Wabunge wenzangu kwenye hili lazima tusome kwa makini kwa sababu tutapotoshana, haijaelezwa hivyo. Tunao *KK Security* na *Ultimate Security* hivyo ni vikundi vya ulinzi na viro kwa mujibu wa sheria na Katiba. Kwa hiyo, sitaki kuamini kama vikundi vya ulinzi leo eti ni kosa kuwa navyo kisheria mpaka Msajili wa Vyama vya Siasa anataka kuvifuta.

Mheshimiwa Spika, ninachokiona hapa tunalo ombwe kubwa sana juu ya Serikali yetu upande wa Jeshi la Polisi kuwalinda raia. Sijawahi kumuona Katibu Mkuu wa CHADEMA Ndugu Vincent Mashinji anaongozwa na kimulimuli cha polisi wala kulindwa na polisi, tunamlinda wenyewe Katibu Mkuu wetu, lakini juzi Mizengo Pinda amefanya maandamano jambo ambalo limezuiliwa, amesindikizwa na polisi. Bashiru akizunguka mikoani anasindikizwa na polisi... (*Makofi*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Sijawahi kuona hata siku moja viongozi wa Chama cha CHADEMA...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ...au chama chochote cha upinzani...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Viongozi wa Chama cha CHADEMA au chama chochote cha upinzani wanasingikizwa na polisi...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wawili wa wastaafu wapo CHADEMA...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Kuhusu utaratibu.

SPIKA: Salome dakika mbili tu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nimweleze mwenzangu kwamba kwanza amepotosha utaratibu kwamba...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: ...sio kosa la kikatiba kuwa na vikundi nya kijeshi, kilichozuiliwa na muswada huu ni vikundi nya kijeshi sio kujilinda. Imeelezwa kabisa anaweza ndio maana wanapewa ruzuku, ukipewa ruzuku unaweza ukaenda *KK Security* ukachukua kikundi cha kukulinda, lakini watofautishe na wanaposema jeshi letu halilindi, hata leo mpaka tunafika hapa kilichotufikisha hapa tukawepo ni Jeshi la Polisi limetulinda ndio maana tuko salama mpaka sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa amekuwa mara nyingi akijirudia kupotosha kuhusu katiba, katiba iko wapi na vitu vilivyokatazwa na bahati mbaya tu wenzangu hapa wanajaribu kuridhisha watu fulani wanaokutana nao kwenye makorido kama alivyosema Lusinde hapa sasa hivi, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Baada ya kelele hizi sijui kama Salome unaweza kusikia vizuri. Anachosema ni kwamba ruzuku mnayoipata badala ya kuitumia kwa mazingira mengine mnachukua

vyombo au kampuni ambazo zimekubalika zinawalinda kwa sababu hela mnayo, endelea Salome. (*Makofi*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wako wa Kamati ya Kanuni, mtu anaposimama anataka kutoa utaratibu anatakiwa ataje kwanza kanuni gani, wewe ndiye umenifundisha hayo, mimi naachana nayo.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) tunao Mawaziri Wakuu wawili wastaafu, lakini wanatembea/wanafanya ziara kwenye Taifa hili hakuna hata mmoja amewahi kwenda na hicho kimulimuli. Kwa hiyo, kabla hatujaenda kwenye suala la kupitisha kwamba polisi ndio watulinde nafikiri tuanze kujadili impartibility ya *Police Department* kwenye taifa hili. Nafikiri huo ni mjada mpana ambao ni lazima tuujalidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Salome, Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru...

SPIKA: Una dakika 15.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO:...kwa kupata nafasi ya kuchangia muswada huu ambao Serikali imeuleta mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati najiandaa kuchangia napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakumbuke mwaka 1933 aliyekuwa kiongozi wa Ujeruman Adolf Hitler alipeleka ndani ya Bunge la Ujerumani muswada wa sheria ambao kiingereza unaitwa *Enabling Act* ambao Wabunge wa Chama chake cha Nazi na wa vyama vingine isipokuwa chama kimoja tu Chama cha SDP waliunga mkono. Illichukua miezi sita tu muswada ule baada ya kuanza kutumika, Ujerumani haikuwa na chama cha siasa kwa

sababu Hitler alitumia sheria ile ile ambayo ilitungwa na Bunge la Ujerumanî kuhakikisha si tu vyama vimefutwa bali wanasiasa au wamekimbilia uhamishoni ama wameuawa kutokana na mazingira mabovu yaliyokuwa ndani ya sheria hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ndio hali ambayo Bunge lako tukufu inayo sasa hivi; kwamba tuna muswada hapa ambao kwa *nature* ya majadiliano unaonekana ni muswada kati ya chama kinachotawala na vyama vya upinzani, lakini utekelezaji na madhara yake yanakwenda zaidi ya ushindani wa chama kinachotawala na vyama vya upinzani. Hii ni kwa sababu sisi sote ni wanasiasa na tunajua mamlaka ambayo tunataka kumkabidhi Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa sheria hii ni mamlaka yatakayotengeneza hali ngumu sana ya kisiasa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikukumbushe, wewe ni Mwalimu wa Historia. Nchi yetu hii kabla ya Mfumo wa Vyama Vingi kuanza na wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere, kwa sababu watu hawakuwa huru kuzungumza kisiasa, kulikuwa na majoribio ya mapinduzi manane. Baada ya Mfumo wa Vyama Vingi kuanza, nchi yetu haina rekodi ya jaribio la mapinduzi hata moja kwa sababu watu wakiwa na hasira watakwenda Mwembeyanga, watakwenda Songea, watakwenda Kigoma, watazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mazingira yanayojengwa sasa hivi...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Waheshimiwa tumwache aendelee.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, mazingira yanayojengwa sasa hivi, iwapo watu watakosa uhuru wa *ku-vent out* na milango ikafungwa, wakaamua kupita madirishani, tusilaumiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja hapa ya; ni wakati gani na kwa namna gani Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza akafuta chama. Katiba yetu imeelezwa vizuri na bahati nzuri nilishiriki vikao vya Kamati ya Katiba na Sheria, namshukuru Mwenyekiti aliniruhusu; na tunampongeza sana Mheshimiwa Chenge, alijitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuweza kutupitisha katika kila kifungu na vifungu vya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukawa na Katiba inayoruhusu *freedom of association* halafu ukawa na mtu ambaye unampa mamlaka peke yake ya kuamua kwamba wakati huu sasa hii *freedom of association* inafutwa. Katika hali ya kuonesha kwamba inawezekana vyama vikafanya makosa vikatakiwa kufutwa, tulipendekeza ndani ya Kamati kwamba kuwepo na *tribunal*. Kwamba Msajili anapoona chama kimefanya makosa, sio ye ye tu aamue, kuwe na *tribunal*, halafu vyama vipelekwe kule viweze kuwa *tried* na *tribunal* ile iweze kuamua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pamoja na marekebisho, hakuna *tribunal*. *Best examples* zimetajwa na Mwenyekiti wa Kamati. *Best examples* zimetajwa kuna *tribunal*. Ghana ambayo imezungumziwa kwa kina sana katika Muswada huu, ina *tribunal*; Kenya ina *tribunal*; ni nini ambacho sisi tunakiona ni hatari kuweka *tribunal* ili kuhakikisha kwamba wote tuone haki inatendeka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba na Wabunge wenzangu walitazame hili, tuone uwezekano wa kufanya mabadiliko. Badala ya mamlaka haya ambayo tumemkabidhi Msajili peke yake kuyafanya peke yake, yaundiwe *tribunal* ambayo itayafanya na bado hata hiyo *tribunal* inateuliwa na watu wa Serikalini humo humo tu; *it's not a problem*, tunachokitaka, tuwe na uhuru wa kuweza kuzungumza na kuweza kutoa maoni yetu kwa jinsi ambavyo inastahili.

Mheshimiwa Spika, *democracy* siyo uadui. Nchi yetu imefaidika sana na *democracy*. Nitakupa takwimu kidogo tu. Kati ya mwaka 2007 na mwaka 2012, jumla ya

Watanzania milioni moja waliondolewa kwenye *poverty*. Wewe unajua. Hiki ndicho kipindi ambacho demokrasia ilikuwa imeshamiri sana katika nchi yetu, hiki ndicho kipindi ambacho tulikuwa na uhuru mpana zaidi wa mawazo na ndicho kipindi ambacho Serikali inakuwa *responsive* kwa watu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *data za juzi za World Bank*, ndani ya miaka mitatu toka utawala huu uingie madarakani, Watanzania milioni mbili wame-fall into poverty, kwa sababu kuna *correlation* kati ya demokrasia na maendeleo ya watu. Tunachopaswa kufanya leo, miaka 25 toka tumeingia katika Mfumo wa Vyama Vingi siyo kubana zaidi demokrasia, ni kuipanua zaidi demokrasia. Tungepaswa leo tuleteewe Muswada ambao unapanua zaidi badala ya kudhibiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunadhibitiwa mpaka kwenye elimu ya uraia, kwamba unapokuwa na *a sister party* au *any other organization* ambayo mnafanya nayo kazi, tunaweka udhibiti. Siyo taasisi za nje tu, maana yake inawezekana watu wakadhani; na wakati naingia hapa nimekuta Mbunge mmoja kutoka Tabora Mjini anazungumza, anadhani kwamba ni taasisi za nje ndiyo zitakuja, zitaleta tatizo kwenye nchi yetu, hapana. Hata taasisi za ndani tunaweka udhibiti wa elimu ya uraia.

Mheshimiwa Spika, unapotunga sheria kuna jambo ambalo liliikuepo unataka kulitatua. Naomba Serikali inieleze, kabla ya kuweka vifungu hivi inavyovi-propose vya elimu ya uraia kudhibitiwa na Msajili, kulikuwa kuna tatizo gani katika nchi yetu? Kwa sababu *a new bill* ina lengo la kwenda kutibu tatizo ambalo limetokea. Naomba Serikali inieleze, kulikuwa kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Spika, hatujaona tatizo lolote la elimu ya uraia, *NGOs* zimekuwa zikitoa elimu ya uraia, vyama vimkuwa vikitoe mafunzo kwa wanachama wake. Kwa nini sasa tutake kudhibiti katika Muswada huu ambao unakuja hapo mbele yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tuongozwe na maslahi mapana ya nchi yetu. Tusiongozwe na kubanana. Tusitunge sheria kwa kuwatazama watu. Kuna vifungu humu nya sheria vimetungwa kwa kutazama watu, ndio maana watu hawaogopi kubadilisha Katiba, hawaogopi kwenda kutunga kifungu ambacho kiko kinyume na Katiba. Tulikubaliana sisi ndani ya Kamati, Wajumbe wa Kamati, mimi nilikuwa mwalikwa kwamba *the reference* ya uraia itumike *reference* ya uraia ya ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Schedule of Amendments* iliyokuja, labda Mheshimiwa Jenista aseme amekosea. Ni tofauti kabisa na lile ambalo lilikubaliwa ndani ya Kamati. Kwamba leo wewe ukiwa umezaliwa na mzazi mmoja ambaye sio Mtanzania unaweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, unaweza kuwa Makamu wa Rais, unaweza kuwa Mbunge, unaweza kuwa Waziri Mkuu, lakini huwezi kuanzisha chama cha siasa. *It is ridiculous!* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *consensus* ndani ya Kamati. Kitendo cha ile *consensus* ya ndani ya Kamati kutorejeshwa kwenye *Schedule of Amendments* lazima kuna watu wanaokuwa-*targeted*, huwezi kutunga sheria kwa *ku-target* watu. Naomba Bunge lako Tukufu lifanye *amendment* kwenye eneo hilli. Tutumie *provision* ya Katiba katika hayo. Tunaelewa ni muhimu kuweza kuwa na Watanzania halisi katika uanzishaji na uendeshaji wa vyama, lakini tunayo *guidance* yetu ambayo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni *section 19(c)*, sijaiona kwenye *Schedule of Amendments*, lakini tulikuwa tumekubaliana kwamba ifanyiwe marekebisho kwenye Kamati. Kifungu cha 19(c) kinasema: "Msajili wa Vyama, wakati wowote ule akiona kwamba chama kiliundwa na kikasajiliwa, yeye akiamini *fraudulently* anakifuta chama kile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzisha chama haupati cheti cha usajili wa chama kama mchakato huo haukuidhinishwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama. Sasa mtu ambaye ndio ametoa cheti cha usajili, ameidhinisha, huyo huyo eti akiwaza tu kwamba hii ni *fraudulent*, anaweza akakifuta chama. Sasa *who is fraudulent there?* Ina maana ni Msajili mwenyewe kwa sababu ye ye ndio ambaye ametoa ile *certificate*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chama cha kwanza ku-suffer kwenye hili itakuwa ni Chama cha Mapinduzi...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Tulitoa mwongozo asubuhi kwamba tuvumiliane. Mheshimiwa Naibu Spika alipokuwa hapa, nafikiri alieleza vizuri. Karibu tunafika mwisho, tuvumiliane tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Simbachawene, kitu muhimu ni kwamba mnaofuata mnafuatilia, mnapangua hizo hoja, yaani usikae unasubiri kuchangia yale ya kwako. Kama kuna matundu sasa hapo utajua. Mheshimiwa Ngeleja utafuata, kama kuna matundu mnarekebisha, hakuna shida. (*Kicheko*)

Malizia dakika mbili za mwisho.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo, nashauri kifungu hiki, tuliomba kwenye Kamati na Mheshimiwa Mtemi Chenge akapewa jukumu la kukitazama, sijakiona kwenye *Schedule of Amendments*, kama kipo mtaniwia radhi; kitazamwe, kifutwe, kwa sababu hakina maana yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, chama cha kwanza kuingia kwenye mgogoro huo kitakuwa ni Chama cha Mapinduzi kwa sababu hakikusajiliwa, hakikufuata mchakato ambao vyama vyote vilifuata kwenye usajili. Chama cha Mapinduzi kilitungwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo ninyi mpo madarakani, mna *majority* ndani ya Bunge, kesho mnapoteza *majority* hata ya Mbunge mmoja, *the first act* ya kiongozi yeyote atakayeingia madarakani, mmepoteza *majority* hata ya Mbunge mmoja, anakwenda kuwafuta, hamkuuata sheria. Sasa mnajitungia sheria hata ya kuwanyonga ninyi wenyewe? Naomba hiki Kifungu cha 19(c) kifutwe kwa sababu hakina maana yoyote. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni huu mjadala wa vikosi vya ulinzi, naomba Mbunge yeyote wa Chama cha Mapinduzi hapo alipo atazame kazi ya kwanza ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi ni nini? Mbunge yeyote yule wa CCM, najua kuna Wabunge ambao wameingia hawakupita kwenye hiyo michakato ya... (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zitto, dakika zako zimekwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa George Simbachawene, tafadhalii. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kuipongeza Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuleta Muswada huu mzuri ambao kwa hakika unataka kuiokoa nchi hii ili isipate matatizo ambayo nchi za wenzetu zimepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulianza Mfumo vya Vyama Vingi mwaka 1992 na kwa hiyo, kutoka 1992 mpaka sasa ni takribani miaka 27. Tumefanya chaguzi mara tano na katika chaguzi hizi tumeshuhudia mambo mengi. Tumeshuhudia watu wakiumizana, watu wakifa, watu wakimwagiwa tindikali na fujo nyingi sana. Vile vile tumeshuhudia kutokuwepo demokrasia ndani ya vyama vya siasa. Katika kipindi hiki tumeshuhudia pia rasilimali za vyama kuwa rasilimali za watu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vipo vyama inawezekana likitokea la kutokea, watu wawili au watatu tu wakiondoka, wakiwa hawapo, hivyo vyama vinakosa mali kabisa kwa sababu hata hawajui ziko wapi. Katika mazingira haya na upungufu huu, bila shaka ndiyo maana Serikali ikaamua kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni matokeo ya kujifunza kwetu mambo mengi yanayotokea. Nimewasiliza wachangiaji waliopita na hasa rafiki yangu Mheshimiwa Zitto, amezungumza juu ya jambo la demokrasia, lakini demokrasia bila mipaka ni fujo. Demokrasia ni mfumo au utaratibu unaoweka utawala kwa uchaguzi na ukishauweka huo utawala kwa uchaguzi kuna mifumo mingi; iko *constitutional democracy*, iko *representative democracy* na iko *direct democracy*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *indirect democracy* inakuwa kila jambo lazima mpige kura; katika *representative democracy* wanachaguliwa viongozi kama hivi tulivyo sisi kwa niaba ya Watanzania wengine kwa ajili ya kuamua mambo yao na kusimamia masuala ya utawala. Katika mazingira haya, mnapomaliza uchaguzi, shughuli zote za siasa zinakuja Bungeni. Zikija Bungeni huku ndiyo tumepewaa mpaka na kinga ya kusema tunayotaka tuseme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawaambia pande zote mbili, kama uchaguzi umekwisha, kwa nchi maskini kama yetu ambayo bado wako watoto wanakaa chini, ambayo bado kuna matatizo watu hawapati dawa, tunataka tuendelee kulumbana na kufanya siasa wakati uchaguzi umepita, tutaendelea kuwa masikini na hatuwezi kutoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata aliyeshindwa ana haki yake na aliyeshindwa ana haki yake. Wakati wewe umeshinda; tuchukulie Mheshimiwa Zitto umeshinda uchaguzi, unaongoza nchi, halafu sisi akina Simbachawene tunaanzisha *Movement for Change*, tunaanzisha Sangara, tunaanzisha operesheni, nchi haitulii, nchi inahema juu kwa juu, utaongoza vipi? Utaiiongozaje hiyo nchi? Kwa hiyo, ni

vigumu sana haya mambo kuya-equate unapochukulia nadharia za kidemokrasia na hali halisi ya dunia ya leo...

SPIKA: Mheshimiwa Simbachawene, bahati nzuri Mheshimiwa Zitto hawezi kuwa Rais wa Nchi, haiwezekani. Endelea tu Mheshimiwa. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, hakika tunapaswa tuijilize, maana ziko nchi ambazo hazina hata vyama vingi. China kuna chama kimoja kikubwa kinafanya vizuri; na China sasa ndiyo Taifa kubwa lenye uchumi mkubwa duniani. Sasa katika mazingira haya lazima na sisi tuijilize, vyama vyetu lazima viwekewe mipaka na kurekebishwa baadhi ya mambo ili twende sawa. Ndiyo maana Serikali inaleta Muswada kama huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa ndio referee na *role* yake ni *impartial*. Unapozungumzia juu ya vikundi vya ulinzi, wote tunajua humu, mbona hatutaji tu! *CUF* wana *blue guard*, *CHADEMA* wana *red brigades*, *CCM* wana *green guard*; hivi vitu ni hatari kwa Taifa. Kwa hiyo, huwezi kusema Muswada huu unapendelea upande mmoja, sheria inakata kotekote. Humu tupo Wabunge wengi wa CCM, lakini tunasema, tunaona umuhimu wa kutunza amani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo yameguswa na Muswada huu ambayo kwa kweli kabisa na hasa yanayompa nguvu ya kusimamia mchezo huu wa siasa, yanayompa nguvu Msajili kufanya kazi ya u-referee wake vizuri, ni ya muhimu sana, lakini unashangaa yanapingwa.

Mheshimiwa Spika, unasema *training* na *capacity building* za *ideology*; *ideology* ni kitu cha hatari sana. Ndicho tunachozungumza, leo hii tuijilize *Janjaweed* ilitokea wapi? *It was ideology teachings. Janjaweed* ambayo leo hii *Western Sudan* na *Eastern Chad* ni matatizo makubwa na inasambaa kote; leo hii *Al-Qaeda* ni tatizo la dunia, *it is these teachings* ambazo hazikuwa *controlled* ndizo zilizotufikisha hapo, ndizo zilizoifikisha dunia hapo. Kuna

Mungiki, imewatesa wenzetu wa Kenya vibaya mno; lakini /Simemwondoa Gaddafi kwa kumuua kinyama kweli kweli. Wanasema wanapigania *ideology* ya Uislam, wakati na Gaddafi ni Muislam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, siasa ina vitu vingi, ukiviachia hivi kama huvioni unakuja kulia baadaye. Hizi *ideology, teachings* hazikatazwi kwa mujibu wa sheria hii, tumesema zitolewe taarifa kwa Msajili watakavyofundisha na wanachotaka kufundisha halafu ataruhusu au atakataa kulingana na hali ilivyo ya hizo *ideologies* wanazotaka kufundisha au itikadi au vyovyote mnakavyoweza kusema. Hazijakatazwa, kuwekewa utaratibu huu tu ndiyo jambo bayal Hapana, bila shaka pengine wengine wanafikiri tuna nchi nyingine ya kwenda, lakini nchi yetu ndiyo hii hii, tusipoilinda ilivyo, hatuna pa kwenda sisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wanazungumzia suala la uzingatiaji wa matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vya Siasa katika kutekeleza na kufanya shughuli zetu zote za uendeshaji wa demokrasia nchini. Jambo hili ndilo limekuwa tatizo kubwa kwamba wengine wanafuata kidogo, wengine wanajitahidi, tunataka kuwe na uwanja ulio sawa. Napo hapa kuna tatizo?

Mheshimiwa Spika, vipo vyama hapa viliungana *vika-form coalition*, sina uhakika kwenye ugawanaji wa baadhi ya makubaliano waliyoyafanya kama wengine hawakuumizwa. Muswada huu unaweka *schedule* ambayo inaweka utaratibu wa makubaliano ambapo waliopata madhara ni vyama ambavyo tunajua, lakini kama mtu aliyeumia anasema yeye hajaumia, inakuwa vigumu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikiangalia nikiwa upande wa CCM na nikiwaangalia wenzetu, naona wao wanauhitaji zaidi Muswada huu na Sheria hii kuliko sisi, wana hali mbaya sana hawasemi. Sasa kama hivyo ndivyo na hawaoni hii, bila shaka sasa hiki kinachotaka kufanywa na sheria hii

ambacho kinataka kunyanya zaidi *institutional party*, badala ya chama cha mtu, wenzetu wanaiona hiyo siyo sawa, bila shaka hawajui wanachokifanya. Mimi ninavyoona angalau CCM tuna *an institutional system political part*, lakini si ajabu wao wanahitaji zaidi kwa kweli, kwa maoni yangu wanahitaji zaidi Sheria hii kuliko tunavyohitaji sisi CCM. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi yamesemwa lakini moja kati ya masuala mengine ya msingi yanayoletwa na sheria hii, ni masuala ya vyama kuzingatia Katiba zao. Kumekuwa na tatizo la vyama kutokuzingatia Katiba na wakati huo huyo *Referee* aliyepewa hiyo kazi anakuwa hana uwezo, Sheria hii inampa uwezo wa kusema sasa bwana fuata Katiba yako ulisema hivi, lakini pia wameweka na nyongeza nyingine ya kwanza hapa ambayo inasema italeta *basic matters for which provisions of the constitution of the parties shall contain*. Hasa Katiba zitakuwa na mfumo ambao unafafana, zina mfumo ambao vitu muhimu vyote vipo na hivyo Msajili itakuwa ni rahisi sana kuvisimamia vyama hivyo na kuamua hata ugomvi ambao umeweza kutokea hapa na Msajili anashindwa kupata namna ya kufanya. Sasa nadhani kama nilivyosema vyama vingine vinahitaji zaidi Sheria hii kuliko pengine hata CCM.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inazungumzia kumzuia mtu asiye raia kujishughulisha na masuala ya siasa za nchini mwetu. Hivi wewe leo kweli unaweza ukatoka hapa ukaenda Marekani ukasema wewe unataka kupata haki ya kuanzisha chama, unataka kupata haki ya kufanya nini, ni ngumu mno. Sisi hatuwezi kuacha milango hii wazi na ndiyo maana Sheria hii inakuja kuuziba huu mwanya kwa sababu tunajua yanayotokea. Nami niseme tu ukicheka na nyani, utavuna mabua. Tunajua yanayotokea, tunajua ambavyo vyama hivi vinaweza vikatumika katika kuingiza watu wasio na nia njema na nchi yetu, tunapozima mianya hii ubaya wake ni nini na wameonesha kidole sana kwa upande wa CCM, lakini nasema hivi, wana haki ya kufanya hivyo kwa sababu nchi hii ikiparaganyika watakaodaiwa na Watanzania ni sisi CCM, maana ndiyo tunaoongoza nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo niwasihii na niwaombe wana CCM wenzangu tushikamane na tuhakikishe kwamba sheria hii inapita kwa sababu ya uhuru wa nchi yetu, amani ya nchi yetu na kwa sababu ya uimara wa demokrasia katika nchi yetu. Tusipofanya hivyo sisi ndiyo tutakaoulizwa kuliko mwengine yejote yule, wenzetu wengine wanaweza wakawa wanatafuta namna ya kuingia kiurahisi, lakini sisi tunaona suala la siasa ni lingine lakini maisha ya nchi yetu, maisha ya watoto wetu na maisha ya wajukuu zetu ndiyo kitu cha maana kuliko hata mchezo wa siasa tunaocheza humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata mchezo wa mpira wenyewe una sharia, mchezo wowote duniani una sharia na taratibu zake na hata kuna kadi unapewa ya njano, baadaye unapigwa *red*, kwa nini? Kwenye utaratibu wa kuendesha jambo *sensitive* hili ambalo linatunza mhimilli wa amani na utulivu wa nchi tusiliwekee utaratibu, ni jambo zuri na naunga mkono hoja, sheria hii Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Wabunge tuipitishe kama ilivyopendekezwa kwa marekebisho ya Serikali. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene. Mheshimiwa Zitto naona karatasi karibu zote hizi mlikuwa mnaandikiana Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kama rafiki yao wanasema kwamba walitarajia utaunga mkono mabadiliko haya kwa asilimia 100, kwa sababu upungufu wa Sheria iliypita ndiyo uliosababisha ukafukuzwa CHADEMA hivihivi kwa kuonewa tu. (*Makofi/ Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tulivyokuwa tumegawa muda *CUF* walikuwa na nafasi moja dakika 15, amezitumia Ally Saleh dakika kumi na mwenzake Mheshimiwa Musa dakika tano wakawa wamemaliza, CHADEMA walikuwa na dakika 30, wao wamezigawa kwa dakika kumi, watatu wameshaongea wawili, Mheshimiwa Halima na Mheshimiwa Salome na dakika zilizobaki ni huku CCM. Sasa Chadema bado Saed Kubenea wa mwisho katika upande huo,

dakika kumi, Mheshimiwa Chenge utafuata karibu Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nitachangia kwa kifupi sana. La kwanza, sisi kwenye Kamati ya Katiba na Sheria na jambo hili umemuuliza Mwenyekiti wetu kwamba hayo marekebisho ya mwisho ya Serikali yalikuja kwenye Kamati? Sasa mimi sitaki kuwa Jaji, lakini nikuombe utumie mamlaka uliyonayo ufanye uchunguzi Serikali walileta marekebisho ya mwisho kwenye Kamati? Kwa ufahamu wangu mimi hawakuleta; sasa nakuachia wewe, vyombo unavyo, kamera zipo kwenye Bunge, Mawaziri wapo hapa, Mwenyekiti yupo, Katibu wa Kamati wapo, waulize maelekezo yako walitekeleza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, Sheria yoyote inapotungwa huwa ni lazima iwe inatafuta tiba na imetolewa mifanoi hapa nchi ya Ghana, ya Kenya na humo mote Sheria ilipotungwa kulikuwa na matatizo ambayo yalilazimisha kutungwa hiyo Sheria; Rwanda walipotunga Sheria ya Vyama vya Siasa walikuwa wanazuia mauaji ya kimbali yasiendelee, Kenya walikuwa wanazuia mauaji ambayo yalitokea mwaka 2007 ambayo yalizaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa kumbe hapa nilivyosikia Waheshimiwa Wabunge sijui kama ndiyo dhamira ya Serikali, lakini nilivyomsikia Mheshimiwa Simbachawene na nilivyowasikia Wabunge wengine kumbe kuna tishio la nje ambalo mimi silioni la kuletwa Muswada huu Bungeni. Kwa sababu ukiuangalia huu Muswada ulivyokuja kwenye Kamati mwanzo unashangaa kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametambulishwa leo Bungeni hapa ni Profesa, Waziri wa Katiba na Sheria ni Profesa, Msajili wa Vyama vya Siasa ni Jaji wa Mahakama Kuu, hawa watu wanaletwa Muswada Bungeni unapingana na Katiba ya nchi yaani sisi ambao siyo Wanasheria ndiyo tunakuja kuona vifungu vinavyopingana na Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana ikawa ni nia ovu na wamesema Mheshimiwa Ally Saleh amesema. Wameleta kifungu ambacho sasa hivi kwenye jedwali la marekebisho

la mwisho kimeondolewa na Serikali ambalo limeletwa hapa mchana. Kifungu ambacho kilikuwa kinaruhusu vyama viungane, lakini Mheshimiwa Rais aliyeo madarakani alikuwa anapoteza madaraka yake, tunawaauliza kwenye Kamati ninyi mnaruhusu vyama viungane, wanasesma wote watapoteza nafasi zao, lakini Rais atabaki. Tunawaauliza kwa Sheria ipi? Wanasesma kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 42(3) lakini Ibara ya 42(3) wanaoitaja inasoma pamoja na masharti ya Katiba hii, masharti yaliyomo kwenye Katiba ni lazima uwe mwanachama wa chama cha siasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tungekuwa tunaingia kwenye nchi ambayo Mheshimiwa Rais akiamua kuunganisha vyama watu wakienda Mahakamani wanamzuia wanamwambia wewe siyo Rais. Hivyo vitu hawavioni! Sasa hivi wameondoa kabisa maana yake nini, maana yake wanataka Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa mfano akitaka kuhama chama kwa sababu Mwalimu Nyerere alisema kwamba nafuata chama kwa sababu ya sera na usafi wake na uadilifu wake, nikikikuta chama hiki CCM kimepoteza malengo hayo mimi nitakihama kwa sababu CCM, siyo baba yangu mzazi, wala siyo mama yangu mzazi. Sasa Mheshimiwa Rais Magufuli leo kwa Muswada huu hata akiiona hii CCM chafu kweli kweli na haisafishiki hawezi kutoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inawezekana hawa watu walioleta huu Muswada wameona kwamba pengine wapo watu wanataka kumpinga Mheshimiwa Rais 2020 ili Mheshimiwa Rais akitoka aende na chama chake na wale awaache kule wamemzuia, yaani Muswada, dhamira inayoonekana. Kwa hiyo... (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Kubenea, naomba ujielekeze tu kwenye Muswada maana hayo unayoyasema utapata tabu, sasa hivi watasema uthibitishe yatakupa tabu kwa sababu siyo ya kweli. Endelea Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni jambo la ajabu kwamba Msajili wa Vyama ndiye anakuwa mlalamikaji, Mheshimiwa Zitto ameeleza

kidogo, Msajili wa Vyama anakuwa mwendesha mashtaka, Msajili wa Vyama anakuwa Jaji na Msajili wa vyama anakuwa bwana Jela. Tumewaambia kwenye Kamati kwamba mnatoa mifano ya vyama vya mipira; ultolewa mfano na mdau mmoja kwamba hata Chama cha Mpira wa Miguu kinaadhibu, tukasema sawa, lakini kwenye Chama cha Mpira wa Miguu kuna Kamati za Nidhamu, Kamati za Rufaa na Kamati mpaka za ligi, kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa hata Baraza la Vyama vya Siasa halikushirikishwa katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamekuja kwenye Kamati wakati wa kutoa maoni yao, wamekushukuru sana, sana na shukrani hizo zilitolewa na Mheshimiwa Shibuda kwamba wewe ulifanya juhudini kubwa za kuwaita Viongozi wa Vyama vya Siasa na ukawawezesha kuishi Dodoma kutoa maoni yao, lakini Msajili wa Vyama ambaye anaunda Baraza la Vyama kwa mujibu wa Sheria alikataa kukutana nao na Muswada huu haukipitia kwenye baraza kwa mujibu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Msajili wa Vyama vya Siasa ni mlezi wa vyama, Msajili anapogeuka kuwa Hakimu, anapogeuka kuwa mwendesha mashtaka, anapogeuka kuwa Polisi, anapogeuka kuwa bwana Jela, dhamira njema...

MHE. AMINA S. MOELL: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Kubenea kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. AMINA S. MOELL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya (64)(b). Mheshimiwa Kubenea wakati anachangia amesema kwamba Baraza la Vyama vya Siasa halikuwahi kukutana. Nasema tu kwamba Baraza la Vyama vya Siasa lilikutana mwaka 2013 wakati limeanza kukusanya maoni. Baraza hili likaja kukutana Oktoba, 2014, lakini pia 2015 lilikutana na wakati huo 2014 baadhi ya

Wajumbe ambao sasa wapo katika Baraza la Vyama vyama Siasa hawakuwepo; kwa mfano, Shibuda wakati huo hakuwa kiongozi alikuwa ni Mbunge tu yuko CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwamba taarifa hizo siyo za kweli na naomba kiti chako kimwelekeze Mbunge anayechangia aweze kujikita kwa kusema taarifa ambazo ni za kweli. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kubenea iko hivi, lawama kwa Msajili kuhusu kutokupeleka Muswada huo kwenye Baraza kwa maana hiyo ni lawama za kumwonea kwa sababu gani? Muswada ukishasomwa mara ya kwanza hapa tayari ni *property* ya Bunge, siyo wa Msajili wala siyo wa Serikali, ni wa Bunge na ndiyo maana sisi Bunge tukafanya taratibu zote za kuhakikisha kila chama cha siasa kinafika mbele ya Kamati na *including* Wajumbe wa Baraza hilo walialikwa pia kufika mbele ya Kamati, kwa hiyo ni la Kamati zaidi. Mheshimiwa malizia tu muda wako maana naona bado kama dakika moja hivi. (*Makof!*)

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, muda wangu umebaki mwingi na naomba niendelee. Muswada huu amekuja kwenye Kamati Waziri kuhusu kipindi cha mpito cha utekelezaji wa Sheria hii, tukasema Serikali ilikuja na mapendekezo kipindi cha mpito kiwe miezi sita tukawaambia hivi miezi sita unaweza ukaitisha mikutano mkuu wa chama kwa sababu Muswada huu ukipita hapa Bungeni vyama vyote vinalazimika kubadilisha Katiba zao na hali ya vyama vyetu tunajua, hata chama tawala kimebadilisha ratiba za vikao vyake kwa sababu ya uwezo wa kiuchumi, ndivyo tulivyoambiwa. Sasa tukasema angalau basi uwe mwaka mmoja, angalau basi iwe tarehe 30 ya Septemba mwaka 2020 ili vyama vinapoitisha mikutano yao mikuu ya uteuzi wa wagombea zifanye pia mabadiliko ya Katiba zao, lakini maoni yale hayakuzingatiwa na Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba vyama vinaweza vikashirikiana, vyama vinaweza vikaungana, hiyo ya kuungana wameitoa wapi?

SPIKA: Ni kengele ya pili Mheshimiwa Kubenea, nakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ngeleja dakika kumi, Mheshimiwa Chenge dakika kumi ili tuweze kumaliza naona muda unazidi kwenda, tujitahidi kutumia muda huo tulionao, Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naungana na wenzangu kukupongeza sana wewe kwa namna ambavyo umesimamia zoezi la maandalizi ya Sheria hii ambayo tuna marekebisho ya Sheria tunayokwenda kuyafanya. Kwa mwongozo wako ndiyo kilichowezesha Kamati ikafanikisha kuzihusisha Taasisi kwa maana ya wadau 21, lakini watu binafsi zaidi ya 400 na kwa usahihi kabisa 410. Pia wewe umeturuhusu kwa utaratibu wa kikanuni za Bunge sisi Wabunge wengine kushiriki kwenye Kamati ya Katiba na Sheria kwenye maandalizi ya marekebisho haya ya Sheria hii ya Vyama vya Siasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuandaa marekebisho haya. lakini pia kwa namna ambavyo walikubali kushirikiana na Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na wadau wengine walioshiriki katika maboresho ya Sheria hii. Pongezi maalum kwa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mchengerwa kwa kufanya kazi kubwa na Wajumbe, lakini pia niwapongeze sana wadau wote nje ya Bunge hili, waliotenga muda wao kuja kutoa ushauri katika hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunatunga Sheria na kama ambavyo wenzangu wamesema sheria huwa hazitungwi tu lazima kuwe na jambo ambalo linatakiwa kurekebishiwa. Haya yamesema sana na wenzangu na mimi sitapenda kurudia, lakini ukweli kabisa ambao nataka kuusisitiza ni kwamba baada ya mashauriano makubwa yaliyofanyika kuanzia kwa wadau hadi kwenye Kamati na hapa tulipo sasa, sina wasiwasi wala sina mashaka kusema kwamba marekebisho haya tuliyonayo sasa ni bora zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo tulivyoanza kupokea Muswada wa marekebisho haya. Ndiyo maana tunafanya rejea ya vifungu vichache tu ili kukubaliana na marekebisho yaliyofanywa ili

hatimaye marekebisho haya yawe Sheria na yakatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, tumesikia na tume shauriana lakini wapo watu wana mashaka na kifungu cha 3(5)(c) kinachompa mamlaka Msajili wa Vyama kufuatilia chaguzi za ndani. Wapo wanaotia mashaka kwamba kwa nini Msajili huyu apewe mamlaka ya kwenda kuingilia mambo ya ndani, lakini Mheshimiwa Sixtus Mapunda asubuhi na wengine wametukumbusha sisi sote tuko katika Taifa hili, tunafahamu kinachoendelea hatuko tofauti na yanayofanyika katika uendeshaji wa vyama vyetu, si jambo la siri, ni jambo la wazi, migogoro imekuwepo katika chaguzi za ndani na mara kadhaa watu wameshapelekana Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunajenga *platform* na fursa ya kulishughullikia jambo hilo kabla halijafikia huko Mahakamani, kwa sababu huko tunakokwenda pia kunatumika rasilimali za Taifa na ndiyo msingi tunaoutaka kuufanya hapa kuimarisha hili eneo ili kupunguza ule uwezekano wa kuwa na migogoro katika chaguzi za ndani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 3(5)(g) elimu ya uraia kimelalamikiwa sana, lakini kimsingi Serikali imefafanua na Kamati imesema. Ukisoma maelezo yaliyotolewa na Serikali kuhusu lengo la kwa nini Msajili amepewa mamlaka haya ya kuratibu hiyo elimu ya uraia ambayo inaweza kutolewa na Taasisi za ndani na nje ya nchi tunaona kabisa kwamba nia ni njema na hatuhitaji kuwa na mashaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wamesema lengo lake moja ni kudumisha Umoja wa Kitaifa. Tunataka kuona kabisa kwamba hii elimu inayokwenda kutolewa haiendi kuperaganyisha Taifa. Pia wamesema kukuza uzalendo wa nchi yetu; kuzuia elimu inayolenga kupandikiza chuki mionganoni mwa jamii na mifarakan kati ya vyama vyaya siasa vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani. Ni jambo la kawaida, hivi ni kweli dhamira ambayo inaelezwa hapa mtu mwenye akili timamu kama sehemu ya Mtanzania mzalendo anaweza kupinga jambo hili? Hiyo ni fursa yetu

kushauriana lakini kwa hakika jambo hili halijakaa vibaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiki kinanipelekea nifuatilie kwa karibu alichokuwa anasema rafiki yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe hapa. Ametukumbusha na akafanya rejea ya mtu aliyeangamiza maisha ya wanadamu duniani, Hitler. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alichokuwa anakizungumza Mheshimiwa Zitto na nafahamu mazingira aliyokuwa nayo, samahani sana. Najua Mheshimiwa Zitto ameongea lakini alikuwa hajasoma marekebisho ya Serikali yaliyoletwa hapa. Ukisoma ukurasa wa tano ile 'R' ndiyo iliyorekebisha kifungu ambacho ulikuwa unakizungumzia Mheshimiwa Zitto, hupata nafasi ya kufuatilia lakini yalizingatiwa na tukasema mwongozo wa Katiba ndiyo utuongoze katika kufikia maamuzi yanayoweza kufanya na Msajili na hata maamuzi mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niwakumbushe Watanzania wanaofuatilia, nafahamu Bunge haliko /ivelakini teknolojia inaturuhusu, watu wataingia *Youtube*, watafuatilia mijadala hii. Wananchi wafuatilie sana, tusiendeshwe na *intensity* ya sauti inayopazwa hapa isipokuwa tuzingatie maudhui, ukweli na uhalisia wa michango inayotolewa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dada yangu Mheshimiwa Esther Bulaya ulisema lakini nataka nikurejeshe kwenye ukurasa wa 6 wa taarifa jambo ambalo ulikuwa unalilalamikia sana kwamba kwa nini Msajili anapewa mamlaka haya. Mheshimiwa Esther katika *paragraph* ya pili, ulichokuwa unakilalamikia kimetolewa ufanuzi pale. Wewe unapinga jambo hilo lakini unasema kama mamlaka haya ingepewa Tume ya Uchaguzi sisi tungeunga mkono. Sasa inawezekana jambo hapa ni tofauti na mitazamo kuhusu Msajili wa Vyama vya Siasa lakini siyo mantiki na umuhimu wa kifungu ambacho tunakizungumza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5A kuhusu taarifa ya siku 30 kabla ya zoezi la elimu ya uraia kutolewa, ni jambo la msingi tu na zuri. Pia limelalamikiwa kwamba endapo Msajili atakataa kutoa hicho kibali yeye atatoa sababu au anafanyaaje lakini jambo hili kwenye Muswada limesemwa. Ukienda kwenye Muswada wetu, ukurasa wa 5, kipo kifungu cha 5A(2) kinasema Msajili lazima atoe sababu kwa nini anapinga kutoa kibali hicho, sasa kwa nini tuendelee kubishana katika hili? Maana yake ni nini? kama Msajili wa Vyama anapewa masharti ya kutoa sababu maana yake ni kwamba yejote atakayeathirika na kifungu hicho anaweza kwenda Mahakamani kupinga sababu ambazo zimetolewa na Msajili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6A(5), umuhimu wa Mwenge na Mapinduzi ya Zanzibar, hili limezungumzwa lakini mimi nataka ninukuu maneno yallyosemwa mwaka 1961 na ambayo yamekuwa yakisemwa kila wakati ambapo Mwenge wa Uhuru unapandishwa kwenye Mlima Kilimanjaro, Mwalimu Nyerere pamoja na Waasisi wengine wamekuwa wakisema na yamekuwa yakirudiwa wanasesma: "Sisi tunataka kuwashaa Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro umulike nje ya mipaka yetu ili pale palipo na mashaka ulete matumaini, pale palipo na dharau ulete heshima na pale palipo na uonevu ulete haki". (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naamini sisi wote ni waumini hapa ama Mkristo ama Muislam inawezekana ukawa huna imani. Kule kwenye *Quran* na Biblia maandiko ni yale yale lakini ni kanuni ya maisha kwamba mambo mema tunakumbushana kila siku. Wanaoshauri kwamba jambo hili lingebaki kwenye maabara ama likabaki kwenye makumbusho hawaelewi kwamba changamoto za wananchi walizonazo hazijengi mazingira ya wao kujikumbusha na kuona kilichofanyika miaka ya 1940, 1960, 1970 iliyopita na ndiyo maana tunasema mwenge uzidi kuwakumbusha Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya yote, nini sasa langu, Serikali hii ni sikivu sana na imethibitisha usikivu wake katika Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria

kwa sababu ulivyokuja na ulivyo sasa ni tofauti kabisa. Wako watu wanaotumia maneno magumu sana kwamba Muswada huu una uharamu lakini wengine pia wanasesma una ujinai. Nataka niseme shughuli ya kisiasa siyo eneo ama siyo shughuli ambayo inajenga uficho wa watu kufanya mambo maovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mwanasheria mmoja hapa anahoji, kwa nini tumeweka vifungu vingi vya kuwachukulia hatua wale ambao watakiuka sheria hii. Kwa msingi wa kawaida wa utungaji wa sheria mnafahamu, makatazo yanapowekwa lazima kuwe na hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa kama kuna mtu atakiuka. Hili jambo hata huyu ambaye tunamwona kama ndiyo *central focus* katika mjadala huu, Msajili wa Vyama, akikiuka kifungu chochote na yeye inakula kwake. Hizi adhabu ambazo tumezitaja hapa hazijamuacha mtu ye yeyote salama kama atakiuka kifungu chochote katika sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema Taifa hili tunalijenga kwa pamoja lakini tusijifanye tunapokuwa hapa hatuyaoni mazuri yanayofanyika ndiyo maana nasema mimi na wenzangu naunga mkono kabisa mapendekezo yaliyoletwa na naamini kwa pamoja tutaendelea kujenga nchi yetu vizuri. Naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa William Ngeleja. Sasa Mheshimiwa Chenge tafadhalii dakika kumi. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kusema hukusu hoja hii. Mtaniwia radhi Waheshimiwa Wabunge kwa sauti yangu kwa sababu wiki mbili zote hizi zimekuwa na mahangaiko kwangu kutokana na Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na moja la kusema naunga mkono Muswada huu. Ni Muswada mzuri, umekuja kwa wakati na kwa shabaha na lengo zuri tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sheria hii imetungwa mwaka 1992, baadhi yetu tulikuwa humu Bungeni. Sheria hii tumeifanya marekebisho hapa katikati lakini hayakuwa marekebisho makubwa sana mpaka miaka 10 iliyopita 2009 tulipoleta marekebisho mengi kidogo. Lengo kubwa la kipindi hicho na mtakaokumbuka ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo inakubalika na hao wanasiasia ambao ndiyo viongozi wa vyama hivi au wanachama wake lakini pia mionganoni mwao au mionganoni mwa vyama hivyo vinapata bahati ya kuongoza nchi. Ndiyo maana katika sheria hiyo utakuta yale makatazo kama walivyosema wengine yanaanza kwenye Ibara ya 20(2) ya Katiba. Ndiyo maana masuala ya ubaguzi wa dini, maeneo unakotoka, kuhakikisha tunaulinda Muungano wetu, yote hayo yapo ndani ya Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kupitia Muswda huu imekubali kufanya marekebisho ambayo Bunge lilifanya lakini liikakosea. Bunge lina mamlaka ya kutunga sheria kwa jambo lolote la Muungano na kwa masuala mengine ambayo ni ya Tanzania Bara lakini Bunge halina mamlaka ya kutunga sheria ambayo inakwenda kinyume na Katiba. Hilo liko wazi kabisa na *concern* ya Waheshimiwa Wabunge nailewa, nawaheshimu sana wanaposema hivyo, wanatukumbusha vizuri tu. Mwaka 2009 tuliingiza kifungu mionganoni mwa sababu za kufuta chama cha siasa, nia ilikuwa ni nzuri lakini hatukufika katika kukiweka kwenye Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukikisoma kifungu hicho hata chenyewe maana kina makatazo kwamba chama kwenye Katiba yake kisiruhusu wanachama wake kutukana. Sasa kuna Katiba ya chama ambayo tutakuta imendikwa Katiba yangu itaruhusu wanachama wake kutukana?

MBUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, sasa na chenyewe ilikuwa ni kituko lakini kwa bahati nzuri sasa tumepata nafasi nzuri ya kuyasahihisha hayo. Mimi nashukuru sana Serikali imeliona hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana mtoa hoja, Mheshimiwa Jenista na timu yake, Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Kamati ya Katiba na Sheria. Mimi uliniruhusu nikakae nisikilize, nilikuwa mwakilishi wako msikivu, nilikaa kuanzia siku ya *public hearing* ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, wiki nzima tukahamia kwenye Kamati lakini na kule nilikuwa naweza kusimama tu pale Mwenyekiti anaponiomba nisaidie. Kwa hiyo, nashukuru sana Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye *Schedule of Amendments* ya Serikali sote tunaona ni kazi kubwa na siyo nyepesi. Mimi nasema tujipongeze lakini tujipongeze Serikali inapokubali hoja nzuri zinazoletwa na Waheshimiwa Wabunge. Hapo ndiyo tunaposema Serikali yetu ni sikivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa ni uwanja wa kulea viongozi wetu. Kupitia marekebisho haya tunaanza kuona matumaini mapya kwa nchi hii kupitia vyama vya siasa. Mimi sipendi kurudia yaliyosemwa lakini tukiweza kuyasimamia haya kwenye vyama vyetu, uwanja wa siasa Tanzania utaanza kuwa tambarare. Tunapoongelea utawala bora na demokrasia, lazima uanzie kwenye vyama vyenyewe vya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 6C(5) kinatamka wazi kabisa kwamba mwanachama kama sheria hii itapita hataweza kufukuzwa tu kama kiongozi anavyotaka. Lazima taratibu za Katiba zizingatiwe. Sasa unapolikataa na hilo sielewi lakini mimi naona ni mambo mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme mawili ya mwisho, la kwanza ni kuhusu vyama kuungana (*merging*) tumehangaiaka nalo sana na siyo suala rahisi. Niishukuru

Serikali kwa kuliona hilo kwa sababu hatuwezi kuandika sheria yenyé macho. Sheria inapaswa isiwe na macho itende haki kote kote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali imeliona hilo na hiyo ni kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania hairuhusu mwanachama kiongozi aliyepatikana kwa kupendekezwa na chama chake hapa katikati akaondoka kwenda chama kingine, lazima apoteze nafasi aliyonayo. Tulifanya yale makosa mwaka 2009, ndiyo kilikuwepo kifungu hicho, wengi walisema tulikikosea, ni kweli tulikikosea lakini sasa tumepata nafasi ya kukisahihisha, tukiondoe. Kikiendelea kukaa kitaweza kuleta mtikisiko wa Kidola maana haiwezekani nchi hii ikawa na *vacuum* katika uongozi wa nchi yetu. Rais wa Jamhuri ya Muungano akishapatikana isipokuwa kama atajiu zulu mwenyewe, atakuwa *impeached*, au atafariki dunia atasubiri mpaka uchaguzi mwininge kama ye ye ni mgombea ataendelea, kama siyo ye ye amsubiri amkabidhi Rais mteule, ndiyo Katiba hiyo. Kwa utaratibu wa *merging* unazaa chama kipyä, viongozi wapya wa vyama na wanachama wapya na ndiyo maana matokeo yake hayo yanafikisha kuleta *constitutional crisis*. Tumeliacha hilo ili Serikali iendelee kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, dunia ya leo siyo ya *merge* ya miaka ya TANU na Afro-Shiraz. Dunia ya leo ni ya mashirikiano ya *coalition* na ndiyo maana Ibara ya 51(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu nafasi ya Waziri Mkuu mtaona *concept* ile ni ya *coalition*. Iwapo chama cha Rais hakikupata Wabunge wengi humu, Waziri Mkuu hatapatikana kutokana na chama cha Rais, lazima Wabunge walio wengi kutoka vyama vingine washirikiane.

Mheshimiwa Spika, muda wangu ni huo lakini mimi naipongeza Serikali kwa kutuletea Muswada huu na kwa kukubali marekebisho mengi ya Waheshimiwa Wabunge. Yale ya Katiba tumejitätahidi sana kuhakikisha kwamba hatukiuki Katiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipo kifungu kidogo tu cha kiongozi anayetaka kuanzisha chama. Tunaweza tukaki-*justify* kama kilivyo kwa kwenda kusema kwamba kwa sababu hakuna haki au uhuru usio na mipaka, Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini mimi najaribu kuomba tuliangalie, tungeweza tu kusema huyu awe ni Mtanzania wa kuzaliwa basi. Ukiisoma Sheria ya Uraia wewe kama ni Mtanzania wa kuzaliwa maana yake moja ya wazazi wako ni wa kuzaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi ni Wabunge, tunatunga sheria lakini lazima tutunge sheria *from an informed position* kwa kuheshimu sheria zilizopo. Nisingependa tupate nafasi ya watu kwenda kusema kifungu hiki kinaleta ubaguzi wa aina fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nakushukuru sana. (*Makofi/Vigelegеле*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge. Hii ndiyo namna ya kuwa *Senator* katika Bunge.

WABUNGE FULANI: Ndiyo. (*Makofi*)

SPIKA: Vijana wanajifunza maana wengine wanafikiri kuwa mkali tu au kurusha makombora ndiyo, haiendi hivyo. Kwa kweli na mimi niwapongeze sana Kamati wamefanya kazi kubwa sana na Serikali imesikiliza kweli kweli. *Amendements* kurasa nane, vipengele kadhaa na mliachia Wabunge wengine wakaingia wakashirikiana nanyi, mmewasikiliza karibu watu wote waliotoka kwa Watanzania huko, vyama vya siasa, mmekaa saa nygingi sana. Hata hivyo, kuna kalawama kalitokea kidogo basi Mheshimiwa Mchengerwa usizidi dakika tano ili tuendelee, karibu Mwenyekiti.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, baada ya Mzee Chenge (Mtemi) kuzungumza, sidhani kama nitakuwa na maneno mazuri sana ya kuzungumza kwenye Bunge lako Tukufu lakini nitaomba *ni-respond*

kidogo kwenye baadhi ya mambo, nakushukuru sana kwa kunipa dakika tano.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wabunge wakajielekeza kwa mujibu wa Kanuni ambazo zinatuongoza katika Bunge letu hili Tukufu. Ukiisoma Kanuni ya 84(3), Kamati yangu baada ya kupokea maoni ya wadau ilikaa pamoja na Serikali na ikakubaliana hoja nydingi na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyo sema, kwa mara ya kwanza tunaipongeza sana Serikali kwa kukubaliana na ushauri wote wa Kamati iliyoutoa na maamuzi ya mwisho ya Kamati kukubalina na Serikali ilikuwa ni tarehe 24 Januari, 2019, nimuombe mjumbe Mbunge aliyezungumza kwamba Serikali haikuja kukubaliana na Kamati maneno haya ni ya uongo na nia ya uongo kabisa kwamba Kamati ilikubaliana na Serikali na msingi wa sheria hili angalau kwa dakika moja yapo maeneo ambayo Mheshimiwa Mzee Chenge ameyagusa na niipongeze sana Serikali kwa sababu ukilisoma jedwali la marekebisho ukurasa wa pili umekwenda kutibu tatizo lile ambalo Mheshimiwa Mzee Chenge alikuwa analisema hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, isipokuwa tu Serikali kwa huruma yake baada ya neno *by birth* iongeze *comer* ili sasa sentensi hizi sasa ziwe mbili nikiwa na maana ya kwamba kifungu cha 6B ambacho Mheshimiwa Mzee Chenge amekizungumza tayari Serikali imeshakiandika na ukikisoma kifungu hiki ili tuweze kutibu tatizo ambalo Mheshimiwa Mzee Chenge amelisema basi tunaweza kuongeza *comer* baada ya *by birth* na sentensi hili ikasomeka kwamba; "*that person is the citizen of United Republic by birth, and both parents of that person are citizen of United Republic*" tukiweza kufanya hivyo tutakuwa tayari tumetibu tatizo ambalo pengine ingetulazimu watu baadaye kwenda kukuomba tafsiri za Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kwa nini sasa Muswada huu ni muhimu wakati huu, ukisoma Ibara ya 5(c) ambayo yanaainisha majukumu ya msajili ndiko jukumu la kwenda

kusimamia chaguzi za ndani za vyama. Jukumu hili linasomeka sambamba na Ibara ya 7(6)(b) ambayo inazungumzia jenda na masuala mengine ya vijana na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, mimi na wewe *we are the living example* tujifunze yalitokea mwaka mmoja uliopita kiko chama Mbunge wake alikuwa na ulemavu baada ya kufariki chama hicho kikaleta Mbunge ambaye haendani na matakwa yalikuwepo hapo awali. Kifungu hiki kinakwenda sasa kutibu tatizo liliokuwepo na kumpa msajili Mamlaka ya kuwataka wanachama wa chama chochote kuhakikisha kwamba wanazingatia eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia majukumu ya msajili, msajili sasa anakwenda kusimamia Katiba ya nchi kwamba anakwenda kusimamia utekelezaji wa sheria za nchi ikiwa ni sambamba na Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wapo wanachama wa chama fulani walikwenda sehemu fulani wakatoa kauli ambazo zinakinzani na kanuni za adhabu sura ya 16 *penal code* sura ya 16 ukisoma kifungu cha (89) sheria inazuia mtu yoyote mtanzania kuvunja sheria kuzungumza maneno ambayo yanakwenda kuharibu amani.

Mheshimiwa Spika, yaani *the penal code* ukisoma sehemu ya tisa inazungumzia *offences against public tan quality. Offence* hizi siyo za mtanzania wa kawaida peke yake ni za watanzania wote sasa kwa kifungu hiki kinakwenda kumsaidia msajili kwenda kutibu matatizo ambayo yanajitokeza kwa mwanachama wa chama chochote ambaye anatoa kauli ambazo zinakwenda kuharibu amani ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yupo Mbunge alitoa kauli kwamba kule Rufiji watu 700 wamefariki, kauli hii ni mbaya sana na pengine kwa kutumia kifungu cha 89 Serikali ione uwezekano wa kulifanyia kazi jambo hili. Kwa sababu unaposema watu 700 wamefariki inamaanisha kwamba asilimia moja ya wa Rufiji wamefariki wameuwawa kauli hii

ni mbaya sana na pengine iwapo tutampa msajili mamlaka atakwenda kushughulika na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa ni uanzishwaji wa vikundi vyta ulinzi umezungumzwa katika Katiba sheria hii inakwenda kuzuia taasisi au mtu fulani kuanzisha kikundi cha ulinzi ambacho kinakwenda kuchukua mamlaka ya Jeshi la Polisi au Jeshi la Wananchi Tanzania, lakini vikundi vingine vyta kawaida havijazuiliwa kwa mujibu wa sheria hii, lakini sisi sote watanzania ni mifano halisi. Ukiangalia kilichotokea tarehe 27 Januari, 2001 kule Pemba watu walianzisha vikundi vyta ulinzi wakaenda wakamkamata Askari wakamchinja kama kuku mambo haya ni mambo mabaya na watu wa namna hiyo pia baada ya hapo hayakuishia hapo kikundi hiki cha ulinzi kilikwenda mbele zaidi na wakawa wanakunywa kwenye...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Ahsante sana nashukuru sana.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Ahsante sana *order, order* sasa kwa hali ilivyo Mheshimiwa Waziri tuko mahali pazuri *consensus* ni kubwa sana na Serikali ime-*consider* mambo mengi sana sioni kama kuna haja ya Mawaziri wengi kuongea.

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda kumshukuru Mungu hadi aliponifikisha hapa nilipo tukiwa wote ni salama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Muswada huu ambao utaboresha siasa ya nchi yetu ambayo ilikuwa na mwelekeo wa baadhi ya vyama kuleta vurugu ambazo

zinaugawa utaifa wetu na hata wananchi kukosa uzalendo na kuwajengea wananchi kuwa na maisha ya hofu ndani ya nchi yao. Kwa nyakati zifikapo wakati wa chaguzi za kubadilisha viongozi kwa mujibu wa Katiba na sheria zetu za muda wa uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Rais ndio Jemadari Mkuu wa Jeshi la Nchi, hali ilipofikia hata vyama kuwa na makundi ya vijana na kuwapa mafunzo ya ulinzi na usalama na kuwa chini ya viongozi wao wa vyama ndio majemadari. Ndio kulisababisha nidhamu na maadili ya vijana wa vyama hivyo viliporomoka na maadili ya vijana yalichanganyikana na kusababisha nchi kurejesha makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunao Polisi ambao wana jukumu la kuwalinda wananchi na mali zao pamoja na shughuli wazifanyazo katika makundi mbalimbali kwa madhumuni kadhaa wayafanyayo. Fahari wawili hawawezi kukaa pamoja na kufanya kazi moja kwa mafanikio, sio jambo linalowezekana kwa hiyo, Muswada huu utatujengea umoja. Tuwe na jeshi la ulinzi chini ya jemadari mkuu ambaye ni Rais wa nchi tu bila ya kuwa na vikundi vya vijana wa chama tumepoteza vijana wetu, sasa inatosha. Na kuwarejesha vijana kwenye maadili na nidhamu kwa nchi yetu ni ukamilifu wa Muswada huu na kupitishwa ndani ya kifungu hiki cha ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utofauti wa upatikanaji wa uhuru wetu na nchi nyingine ndani ya Afrika na ulimwengu, basi ni dhahiri mila, desturi, hata mzunguko wa maisha ya Wananchi husika yanatofautiana. Hivyo tukijua nchi yetu ina makabila zaidi ya mia moja hadi leo tuna miaka zaidi ya hamsini na tuwamoja, tuna imani na tunautaratibu kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria zilizomo ndani ya mwenendo na maisha ya wananchi wetu, tunaendeleza upendo na umoja.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekuwa na uhuru wa kutoa ushauri na maoni mbalimbali ya Kitaifa kwa

maendeleo ya nchi yetu, hata uhuru wa nani kuwa waongoza na kwa namna gani. Hii yote ni ubora wa demokrasia na hali hii ya kuboresha zaidi na kuwapa fursa kamili ya kutawala nchi yao, vinginevyo tutarejea kwenye kutawaliwa na hii itakuwa ni kosa na upungufu kwetu tulio madarakani, tusikubali bali tuhakikishe Muswada huu upite.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri tunaomba Muswada huu tuupitishe na utekelezwe kwa kufanyiwa kazi kwenye chaguzi zinazokuja 2019 na 2020. Naunga mkono hoja.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, naupongeza Muswada huu kwa lengo la kuweka nidhamu katika vyama pia kudhibiti utitiri wa vyama ambavyo havijakidhi vigezo vya kuunda chama cha siasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5A ni kifungu ambacho itadhibiti Elimu potovu ambayo inatolewa kwa wananchi na kuwapotosha kwa kutumia mgongo wa Elimu ya Uraia. Kifungu hicho kitadhibiti upotoshaji unaofanywa na baadhi ya vyama vya siasa kwa kupitia wafadhili wao kuwapotosha wananchi na kuwajengea chuki dhidi ya Serikali, viongozi na chama tawala.

Mheshimia Spika, Muswada huu utavitaka vyama vinavyoundwa kutambua umoja wa kitaifa na kuimarisha kwa kutambua Mwenge wa uhuru, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na kupongeza kifungu cha 6A kinachotaka vyama vya siasa kufuata katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar na Sheria nyininge za Jamhuri ya Tanzania. Pia katika vyama vya siasa na kuyatambua makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono marekebisho yote ya Muswada huu kwa Maslahi ya Wananchi wa Tanzania naipongeza Serikali yetu kuleta huuMuswada.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asante.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi katika Muswada wa Sheria ya Marekabisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu kwa kuleta Muswada huu katika Bunge lako Tukufu ili ujadiliwe na mwisho kupitishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwanza kuhusu tunu za nchi. Katika ulimwengu nchi zote zina ala, mila na desturi zake ambazo kila mwananchi analazimika kufuata na kuzikubali. Katika nchi yetu Mwenge wa Uhuru ni jambo ambalo linaonesha alama ya uhuru wa nchi yetu jambo hilli halipaswi kupuuzwa hata chembe.

Mheshimiwa Spika, pia Muungano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni kitu adhimu ambacho wenzetu wa nchi nyingine nyingi ulimwenguni wanakitamani. Ni jambo jema ambalo nalo halipaswi kubezwa hata chembe. Hii ni fahari ya Tanzania na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mapinduzi ya Zanzibar, hili ni jambo ambalo linapaswa kuheshimiwa na kutambuliwa na watu wote wa Tanzania. Mapinduzi ya Zanzibar ni kichocheo kikubwa cha Muungano wetu. Bila Mapinduzi ya Zanzibar tusingekuwa na Muungano ambao leo tunajisifia na kujivunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zote ambazo nimezitaja hapo juu pia Muswada huu unafaida zifuatazo:-

- (i) Kupanua wigo kwa Tanzania katika kushiriki siasa za nchi;
- (ii) Kudumisha amani na utulivu wa nchi; na
- (iii) Kushiriki katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%. Naipongeza Serikali kwa kuona haja ya kuleta marekebisho ya sheria hii muhimu kwa wakati. Ni jambo jema kumpa Mamlaka Msajili wa Vyama vy'a Siasa aweze kuwa na mamlaka ya kudhibiti mambo mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi kufanywa na vyama vy'a siasa.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya aina mbalimbali katika vyama kusimamiwa na Msajili ni jambo jema sana kwani mafunzo kufanywa na vyama wanaweza kutuletea mabeberu na watu wasioitakia kheri nchi yetu wakaingiza watu na kuwapa mafunzo yasiyo na maadili kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masharti ya kuundwa kwa chama cha siasa, Serikali imefanya jambo jema kufanya marekebisho hayo angalau kuwepo na utaratibu mzuri. Nchi yetu kuna baadhi ya watu walikuwa na tabia mbaya ya kuchafua vyama na yeye kwa maslahi yake anakimbia anaenda kuanzisha chama kingine. Masharti yaliyowekwa yamezingatia vigezo mbalimbali kwa hiyo sasa heshima itakuwepo kwa mwanachama na chama cha siasa. Pia Muswada umezingatia kuwekwa karibu kwa Msajili wa Vyama vy'a Siasa na vyama vy'a siasa, kwa hiyo sheria itasaidia kutuweka karibu na kuwa na ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inalenga kukagua fedha za vyama vy'a siasa (ruzuku). Fedha hizi zinatolewa na Serikali kama ruzuku lakini kuna baadhi ya vyama hawatumii vizuri fedha hizo nyingine zinaenda kwa viongozi na kuliwa tu, hakuna mahesabu endelevu ya kuonesha mapato na matumizi ya fedha hizo. Napongeza Serikali kuleta sheria hiyo ambayo itasaidia sana kudhibiti fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri anayeshughulikia Sera na Bunge na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuleta marekebisho haya ya sheria ya kumpa nguvu Msajili wa Vyama vy'a Siasa.

MHE. ZAINABU M. AMIRI: Mheshimiwa Spika, Muswada huu una mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, hivyo ni wa muhimu sana katika kuendana na wakati wa sasa wa kuendesha vyama vya siasa. Muswada huu umependekeza kuongezwa kifungu cha 5(A) katika sheria ya vyama kinachoweka masharti takwa la kumjulisha Msajili wa vyama juu ya dhamira ya kuendesha semina au mafunzo ya elimu kwa chama cha siasa. Kwa maandishi pia kinampa mamlaka Msajili ya kuzuia semina au mafunzo hayo. Hata hivyo wakati wa kuzuia Msajili atatakiwa kutoa sababu ya kuzuia.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya si mazuri, yataweka ugumu wa uendeshaji wa semina au mafunzo kwa kuzingatia kuwa Ofisi ya Msajili haina watendaji Mikoani na katika Kata, Kijiji wakati huo huo vyama vilivyosajiliwa vipo vingi na vinafanya siasa kuanzia vijijini ambako semina au mafunzo halijafika.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo, kifungu kiweke muda wa ukomo wa Ofisi ya Msajili kuwasilisha maamuzi yake kuhusiana na taarifa aliyopewa ya mafunzo. Kifungu kibakie ila kiwekewa ukomo wa masaa 24 ambayo Msajili atatakiwa kutumia mamlaka aliyopewa na kifungu hiki kuamua kama akatae kurishisha taarifa au aruhusu . hii itawezesha vyama kuwa na haki ya kuendelea na semina pindi wasipopata taarifa ya kuzuiwa kuendesha semina au mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu 5(B) cha Muswada huu kimeongezwa katika Sheria ya vyama kitakachompa mamlaka Msajili wa vyama kudai taarifa yoyote kutoka kwa vyama au viongozi wake. Maoni; kifungu hiki hakijatoa muda (*time frame*) ambao chama au huyo mtu akishindwa kuwasilisha taarifa itakuwa kosa la jinai na hiyo kutoa wigo mkubwa kwa watu kuadhibiwa kwa makosa kutotoa taarifa iliyohitajika wakati taarifa yenyewe inahitaji muda wa kutosha ili kupatikana na kuwasilishwa. Hivyo kifungu hiki kipitiwe tena na kutoa muda maalum wa kuwasilisha taarifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8(A). Muswada huu umependekeza kifungu hiki kufanyiwa marekebisho *subsection one* katika Sheria ya vyama kinachoweka masharti kwa *register*.

Mheshimiwa Spika, maoni kifungu hiki pamoja kina malengo mazuri kwa vyama na maslahi makubwa kwa Taifa hili. Kifungu 8(E) hikini kifungu kipyaa kinazuia vyama kuwa na kikundi cha ulinzi kifungu hiki .

Mheshimiwa Spika, maoni kiondolewe kwa sababu ulinzi ni jukumu la kila mtu kwa mujibu wa Katiba. Kuzuia ni kuendana na kinyume cha Katiba. Jukumu la kuachiwa Vyombo vyaa Usalama kulinda mali za vyama, viongozi na wanachama wake ni jambo gumu ukizingatia ufinyu wa askari wetu na ukubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vikundi hivi hulinda mali za chama pamoja na viongozi wake na hawatumii silaha na huwa wanajitolea kufanya shughuli hizo na ulinzi hivyo kifungu hiki kiondolewe ili kutoa fursa ya wanachama watifi kulinda mali za chama na viongozi wake. Ni matarajio yangu kwa maoni, ushauri na mapendekezo yangu yatazingatiwa ili kuweza kuwa na Taifa linalojali demokrasia ya vyama vyaa siasa na kuleta haki na usawa kwa vyama hivyo ili mradi visivunje Katiba ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania.

MHE. MAKAME MASHAKA FOUM: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka na malengo yake ni sahihi kwa mustakabali wa nchi yetu ya mfumo wa vyama vingi. Sheria hii imempa msajili kazi za kufanya, huko nyuma ilikuwa hazijaonyeshwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu 7(6) (b), vikundi vyaa ulinzi katika vyama vyaa siasa visiruhusiwe kwa sababu vyama vinaweza kuwafunza vijana mafunzo ya uasi na baadaye kusababisha vurugu katika nchi yetu. Mifano ipo kwa

baadhi ya vyama hasa siku za uchaguzi na siku za kampeni, wafuasi wa vyama hutumia nafasi hii kwa kuwamwagia tindikali watu wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya uraia inayotolewa katika vyama iratibiwe na Msajili. Kifungu hiki kiko sahihi kwa sababu taasisi ya vyama wanafundisha wanachama wao elimu ya kuchukia mambo ya uzalendo. Mifano ipo, kuna baadhi ya sehemu wanachama kuharibu miundombinu kama kuchoma moto barabarani, kuweka vinyesi kwenye visima, pia kuharibu na kukata mazao mashambani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima elimu inayotolewa, Msajili ahakikishe ni sahihi. Vile vile kwa Msajili kufuatilia uchaguzi wa vyama vyta siasa kwa viongozi wa juu, atawezekuona na kuhakikisha uhalali wa kupatikana viongozi wa vyama. Baadhi ya vyama havifanyi uchaguzi wa haki na huru na hii hupelekea mgogoro wa viongozi katika chama. Hivyo, Msajili atapata nafasi nzuri ya kulea vyama na kuepusha migogoro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku katika vyama, ni sahihi na naunga mkono vyama vyote vipatiwe ruzuku. Hii itavisaidia vyama kuijiendesha lakini pia fedha hizo zikaguliwe, kwani hizi ni pesa za wananchi. Baadhi ya vyama hutumia vibaya fedha hizi na kuwanufaisha wachache. Sasa Msajili apewe kazi ya kuhakikisha matumizi ya fedha.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maudhui ya kifungu cha 6(a)(5). Kifungu hiki ni muhimu sana kuwepo au kubaki katika mabadiliko hayo. Vyama vyote lazima vienzi tunu za Tanzania ili kuendeleza amani na utulivu lakini pia uzalendo na upendo wa nchi yetu. Kwa mfano, Mwenge wa Uhuru, Mapinduzi ya Zanzibar, Muungano wa Tanzania, Demokrasia yetu, Maadili, kupinga rushwa, umoja na amani yetu, utawala bora na kupinga ubaguzi wa *gender*.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia maudhui ya kifungu cha 8(e) cha marekebisho. Hii inahusu marufuku

ya vyama vya siasa kuhodhi majeshi au vikundi vya mgambo au vya ulinzi binafsi. Marufuku hii ni muhimu sana kuzuia:-

(a) Mwingiliano wa shughuli za ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

(b) Marufuku hii inarandana na marufuku inayowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania Ibara ya 147(1)(3) na (4)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Mwenyekiti wa Sekta Binafsi ya Ulinzi kwa miaka 10. Suala hili lilikuwa na changamoto nyingi. Vyama vya siasa vilishindwa kuweka mipaka ya mafunzo yao kati ya mafunzo ya Kipolisi, Kijeshi au taaluma kubwa zaidi za ulinzi, hivyo kuunda majeshi kinyume na Katiba. Kifungu hiki ni muhimu kibaki.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niishukuru sana Serikali kwa kuamua kutuletea marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Ni kweli kwamba sasa umefika wakati wa kurekebisha sheria hiyo kwani baadhi ya vyama vimekuwa vikijisahau sana iwe viongozi wa chama na hata wanachama wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, vyama vya siasa vimekuwa vikiongoza vyama vyao kwa njia za chuki, uhasama, migomo, hujuma, hasa pale inapofika nyakati za uchaguzi. Wanasiasa wengi wamekuwa wakijifanya kwamba hawafahamu yanayokuwa yakiendelea au kufanywa na wanachama wao, wakati mwininge kuwatuma pia kujifanya hawajui yanayoendelea. Hivyo, sasa Muswada huu utaweza kudhibiti yale yote yanayokuwa yakiendelea kwa kufanywa na baadhi ya vyama vya siasa kwa kusimamiwa na Msajili wa Vyama.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha kwanza; sina tatizo na jina la Muswada, naunga mkono liendelee kubaki. Pia

naunga mkono kwamba Muswada huu uwe chombo cha maamuzi na sio chombo cha utawala.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tatu; niungane na Serikali pia Kamati kuhusiana na suala la majukumu ya Msajili, kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha na kutoa elimu ya siasa inayohusiana na vyama vingi ili wanasiasa kuweza kupata uelewa mpana kuhusu vyama vyao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tano; nakubaliana na marekebiso ya Serikali. Mtu au taasisi iwe ndani au nje ya nchi akitaka kufanya jambo lolote ndani ya chama lazima atoe taarifa ndani ya siku 30 kwa Msajili wa Vyama. Pia Msajili kwa mujibu wa sheria hii ataweza kuangalia na kuititia mpango huo, lakini anaweza kuukubali au kuukataa, pia kama ameukataa atatoa taarifa za kukataa kwake. Nikubaliane na adhabu iliyoainishwa kwa wale watakaokiuka sheria hiyo. Niungane na Serikali kwamba Msajili anaweza kutaka taarifa yoyote kutoka kwenye chama kuititia kiongozi wa chama.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha sita; niungane na Serikali kuhusu kinga ya Msajili akiwa kwenye majukumu yake ya kazi yeye na wasaidizi wake. 6A (ambayo imekuwa 7) kuhusu suala la uundaji wa chama, kuwe na: Kuzingatia Katiba ya nchi na sheria zake; Zanzibar na Jamhuri ya Muungano; Utawala bora; Kutokuwa na ubaguzi wa masuala wanawake; na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, niungane na marekebiso haya ili vyama vya siasa wanapoanzisha vyama hivyo kuzingatia vigezo hivyo ili kuleta umoja, usalama na kudumisha uhuru wa Taifa, pia kutambua sheria zote za nchi.

Mheshimiwa Spika, pia Katiba zao za vyama pia kanuni na sera zao zizingatie kuenzi tunu za Taifa. Nasema hili kwa sababu baadhi ya vyama wamekuwa hawashiriki kikamilifu katika sherehe mbalimbali zinazohusiana na uhuru na mwenge wa uhuru, pia Mapinduzi ya Zanzibar hata

kwenye uzinduzi wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa sheria hii katiba, kanuni na sera zao zitaweza kutambua na kuondosha mizozo inayoendelea kuwepo siku hadi siku na watalazimika kushiriki kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Ningeshauri aongee Mwanasheria Mkuu, uongee wewe ili tuingine kwenye vifungu kama kuna mtu ana shida mahali tu-*concentrate* hapo, Mwanasheria Mkuu dakika kumi. (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuanza kuhitimisha hoja iliyoko mezani. Katika uchangiaji imbalimbali uliofanyika yameibuka masuala na hofu kwamba Muswada huu na hasa katika vifungu vyake fulani unaweza kuwa unakinzana na Katiba. Nafikiri ingefaa nikajielekeza tu zaidi katika yale maeneo ambayo kuna wasi wasi kwamba kuna ukinzani na Katiba.

SPIKA: Waheshimiwa naomba tusikilizane kwa sababu tukifika kwenye vifungu mtu mwengine ndio anaanza kunyanyuka na kurudia mambo yale ambayo yameshaelezwu vizuri hili jambo la mgongano na Katiba ni katika mambo muhimu tumsikilize Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, na nitazungumza mambo mawili jambo la kwanza ni hili takwa linalowekwa katika sheria kwa anayetaka kusajili chama cha siasa kwamba wazazi wake wote wawili wawe raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, na katika jambo hilo kumeibuka hisia kwamba kunaweza kuwa na ubaguzi katika hilo, kuna suala la kuwaganya raia katika matabaka ambayo ni muendelezo wa ubaguzi, kwamba kifungu hicho kinaweza kuwa kinavunja Ibara ya 39 ibara ndogo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Ibara ya 47, na kwamba kwa nini kifungu hiki kinaweka viwango vya juu

zaidi kwa nafasi ya yule anayetaka kuandikisha chama ukilinganisha na nafasi ya mtu anayekuwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika msuala hayo manne, tukianza na la kwanza suala la ubaguzi, limeelezwa vizuri sana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunapokuwa tunazungumza niombe niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kila wakati tukizungumza juu ya ubaguzi tuende Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo suala hilo limeelezwa vizuri sana. Lakini la msingi katika ibara hiyo ni maana ya neno ubaguzi na jambo gani linaingia katika wigo wa ubaguzi na jambo gani haliingii katika wigo wa ubaguzi hilo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa ukisoma ibara ndogo ya (5) katika ile Ibara ya 13 imeeleza vizuri sana suala la ubaguzi na imeeleza ni kitu gani hakitengenezi ubaguzi. Ukiisoma hiyo ibara ndogo ya (5) mambo ambayo hayatengenezi ubaguzi ni pale ambapo kumewekwa masharti au sifa za lazima za jambo fulani. Kwa mfano ukisema kwamba mwenye haki ya kupiga kura ni mtu mwenye miaka 18 hizo ni sifa za lazima, mtu anayeweza kupewa labda leseni ya kuendesha gari au awe na miaka 18 hizo ni sifa za lazima panapowekwa sifa au masharti ya lazima kwa kitu fulani huo sio ubaguzi hiyo ibara ndogo imeeleza vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, au panapochukuliwa hatua za makusudi ili kurekebisha matatizo mahususi katika jamiihi hizohatua zikichukuliwa siyo ubaguzi, vingenevyo kama tukisema hivyo ukieda katika ibara nyingi tu za Katiba utaona ubaguzi Ibara ya 39(1) inayozungumzia sifa za kuwa Rais imeeleza mambo mengi awe raia wa Tanzania wa kuzaliwa maana yake inabagua ambao siyo raia wa Tanzania wa kuzaliwa na imeeleza mambo mengi sana, awe na umri wa miaka 40 maana yake ambaye hajafikisha miaka 40 ha-*qualify* awe aliyependekezwa na chama cha siasa anazo sifa za kumuwezesha kuwa Mbunge. Na ukienda kwenye sifa za kuwa Mbunge na kwenyewe zipo sifa nyingi hajawahi kutiwa hatiani yote hiyo ni masharti yanayoweka sifa na hizi

ni sifa za lazima na hii imeelezwa kwenye hiyo Ibara ya 13 ibara ndogo ya tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, na hata ukienda kwenye ile *bill of white* kuanzia Ibara ya 12 mpaka ya 29 utaona baadhi ya ibara zinasema kila mtu ana haki, lakini baadhi ya ibara zinasema kila raia. Kwa hiyo, sasa hapo tena inabagua hazingumzii kila mtu inazungumzia pia raia na hizo ziko wazi Ibara ya 17, Ibara ya 22, Ibara ya 28, Ibara ya 29 hayo ni masharti ya lazima kwa ajili ya jambo fulani na hayo masharti yanapowekwa inakuwa siyo ubaguzi. Kwa hiyo, kinachokuja kuwekwa sasa kwa huyu atakayekuja kuandikisha chama cha siasa ni masharti ya lazima na inapokuwa ni masharti ya lazima siyo ubaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa spika, *otherwise* kumezungumzwa jambo la matabaka ya raia sheria hii haiweki matabaka ya raia kwa sababu sheria yenye ya uraia imezungumza aina tatu za uraia, kuna uraia wa kuzaliwa, kuna uraia wa kurithi, kuna uraia wa kuandikishwa. Sasa yako mambo ambayo ni lazima tutaje kwamba katika jambo hilli tunataka aina fulani ya raia, kwa mfano kwenye nafasi ya uraisi tunesema tunataka aina ya raia wa kuzaliwa, lakini kwenye nafasi ya Mbunge tunesema tu raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza kuwa katika zile aina tatu za uraia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halafu kuna mapendelekezo kwamba au kulikuwa na maoni kwamba unaposema wazazi wote wawe raia yanakinzana na ibara ya 39(1) ibara ya 47(4) si kweli hizi ibara zimeweka masharti ya lazima au *qualification* za lazima kwa nafasi ya Rais na Makamu wa Rais na tukisoma hiyo sehemu ya Katiba iko wazi inahusu nafasi ya Rais, inahusu nafasi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, ukisema kwamba kwa yule atakayekuja kuandikisha chama cha siasa tunapoweka masharti hayo yanakinzanana haya siyo sahihi kwa sababu haya masharti yanahusu tu nafasi ya Rais na hayahusu jambo jingine lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, labda nizungumzie hili suala la pili ambalo pia kumekuwa na wasiwasi kwamba msajili anapewa mamlaka *yaku-suspend* shughuli za chama nadhani ni kusitisha hivi au kusimamisha shuguhuli za chama na kwamba kufanya hivyo ni kuvunja Katiba. Naomba nikuthibitishie kwamba jambo hili halivunji Katiba hata kidogo. Kulitolewa hoja hapa nilisikia kwamba masharti mojawapo yaliwekwa ili chama kiweze kuwa *suspended* hayamo kwenye Ibara ya 20(2) ambayo imeorodheshwa kwamba mambo haya yakifanyika chama kinaweza kuwa *suspended* au kuwa *deregistered*.

Mheshimiwa Spika, tuisahau kwamba Katiba lazima isomwe kwa ujumla wake iko Ibara ya 26(1) inayozungumzia ulazima wa kila mtu na sasa hapa mtu anawea kusema ni mtu uksoma ile *version* ya kiingereza inasema *every person* na katika kiingereza *a person could be a legal person or natural person* kwa hiyo, kila mtu inamaanisha ama taasisi au mtu binafsi na kwamba ama taasisi au mtu binafsi anawajibu wa *ku-observe* sheria zote za nchi. Ana wajibu wa kuangalia kwamba sheria zote za nchi zinasimamiwa na kutelezwa ipasavyo na ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amelieleza vizuri sana hilo kwamba baadhi ya mambo pengine hayamo kwenye Katiba baadhi ya mambo ambayo yanakatazwa hayamo kwenye Katiba lakini yako kwenye sheria nyingine ikiwemo sheria ya kanuni ya makosa ya jinali na kwa hiyo ni sahihi kuiweka katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana namkaribisha Mheshimiwa Waziri na mtoa hoja uhitimishe hoja yako katika muda usiozidi nusu saa tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ili niweze kuja kuhitimisha hoja ambazo zimetolewa na

makundi mbalimbali katika mjadala huu mkubwa ambao utatupelekea leo kutengeneza historia ya kufanya mabadiliko ya nane ya sheria inayosimamia demokrasia ya vyama vingi katika nchi yetu ya Tanzania nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza mjadala huu vizuri lakini nimshukuru sana Naibu Spika kwa kukusaidia pia kuongoza mjadala huu vizuri katika siku hii ya leo. Lakini kwa kweli kwa dhati nishukuru sana wachangiaji wote nikianza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba ya Sheria kwa kazi kubwa waliyoifanya. Umeshuhudia hapa Serikali ikiwa imekubaliana na ushauri tuliopeokea kwa Kamati yako ya Katiba na Sheria, ninaweza kusema kwa kiasi cha 100% katika masuala makubwa yote ambayo Kamati ilikuwa imetushauri. Naishukuru sana Kamati yako namshukuru Mwenyekiti, nawashukuru na wajumbe wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya shukurani labda kwanza nianze moja kwa moja kwenye jambo kwenye hoja ambayo Mheshimiwa Zitto aliisema hapa wakati anachangia na alinipa tahadhalii mimi na Serikali lakini na wale wote wanaouna mkono Muswada huu leo upitishwe kuwa sheria. Kwamba sheria hii itakwenda kuanza kushugulika na Chama cha Mapinduzi kwa sababu Chama cha Mapinduzi bado hakijapata usajili. Ninaomba nimwambie tu Mheshimiwa Zitto aende akafungue sheria mama ya vyama vyaa siasa na akasome kifungu cha 7 kinasema nini na kile kitaenda kumpa kumhakikishia usalama wa Chama cha Mapinduzi mpaka sasa na si tatizo lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini labda pia nizungumzia kidogo tu kwanza suala la Mheshimiwa Kubenea amesema hapa kwamba Muswada huu hauna uhalali wa kuendelea kwa sababu ushiriki wa Baraza la Vyama vyaa Siasa katika kutoa maoni ya Muswada huu ulikuwa ni hafifu. Sitaki kurudia sana wadau walisema nini. Nikushukuru umelizungumza jambo hili kwa kiasi chake lakini naomba tu nikuthibitishie sheria mama ya vyama vyaa siasa namba 258 inasema Baraza

la Vyama vya Siasa ni mshauri wa msajili lakini Baraza kazi yake siyo kutunga sheria lakini itashauri maoni ambayo yanaweza kuchukuliwa kwenye kutunga sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Na kazi hiyo waliifanya vizuri tu na ninaomba nikukuhakikishie kwamba utaratibu ulioweka wa kukialika chama kimoja kimoja ulikuwa ni ushauri mzuri na maamuzi mazuri sana kwa sababu Kamati ilipata kukisikia chama kimoja, kimoja katika ya vyama vyote 19. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na wakati wa mchakato wa maandalizi ya kupokea maoni ya Muswada huu sisi wote Waheshimiwa Waabunge tutakumbuka vyama hivi 19 baada tu ya Muswada kuwa umesomwa mara ya kwanza hapa Bungeni viko vyama vilikwenda mahakamani kupinga Muswada huu usiletwe Bungeni. Viko vyama vilikuja hadharani vikasema Muswada huu haufai usiye Bungeni. Lakini viko vyama kati hivyo vyama 19 vikasema kwamba Muswada huu unafaa na ni lazima upitishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa hali tu ya kawaida kama vyama vilishakuwa na maoni tofauti, vingine vimeenda Mahakamani, vingine vimeita muswada huu tena vikauita majina tofauti ambayo wala siwezi kuyarudia, unavikusanyaje hivyo vyama tena vikae pamoja halafu vilete maoni ya pamoja?

Mheshimiwa Spika, halikuwa ni jambo la busara, jambo la busara ni lile ulilolisema kila chama kije kueleza mbele ya Kamati na walifanya hivyo. Niishukuru sana Kamati yako, walikuwa watulivu, walivisikiliza vyama vyote 19, na vile vyama 19 viko vyama viwili vilipokuja mbele ya Kamati ama Mwenyekiti wa Kamati alipinga muswada, Katibu wa Kamati akaunga mkono muswada. Vyama hivyo vilikuwa viwili na vyama vingine ulikuta kwamba chama kizima viongozi wote waliunga mkono muswada wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Wabunge ushiriki wa vyama katika kutoa maoni kwenye muswada huu kwa kweli nafasi ilikuwa kubwa na vyama

vinafanya kazi yao vizuri na mimi ninaomba kuvishukuru vyama. Wakati wote kila mtu anapopata nafasi ya kutoa maoni yake basi, wakati mwininge maoni ya wachache yatasikilizwa na maoni ya wengi yatachukuliwa na leo tunahitimisha shughuli hii, naishukuru sana Kamati yako.

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge, lakini na hasa Taarifa ya Kambi ya Upinzani imezungumza sana kifungu hiki cha 5(5)(A)(1), ambacho kinaweka masharti ya utoaji wa elimu ya uraia. Nataka niwatoe hofu tu Wabunge na hasa wale wanaoogopa kwa nini kifungu hiki kiletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme jambo moja, kwa sasa ndani ya Serikali yetu tunayo Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi inaipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kuratibu elimu ya mpiga kura inayotolewa kwa mpiga kura. Sasa kama tayari tunayo sheria ya namna hiyo tunaogopa nini kumpa Msajili madaraka ya kuratibu aina ya elimu ya uraia itakayotolewa kwa vyama vyaya? Tunaogopa nini na ni kitu gani kigeni hapo?

Mheshimiwa Spika, hakuna jambo geni na hakuna hofu yoyote. Mwenyekiti wa Kamati ametuambia ziko sheria katika nchi nydingine tena ndani ya Bara la Afrika, sheria hizo pia zinaweka masharti magumu sana ya kuratibu elimu ya uraia ndani ya nchi zao. Kwa hiyo, jambo hilo wala sio geni kwa nchi yetu tu, limeshafanywa kwenye nchi nydingine na sisi tunaenda kufanya jambo hilo, tunaulizwa hapa tumeona kuna ombwe gani mpaka tunaleta kifungu hiki?

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu asiyejua kwamba dunia na ulimwengu mzima umebadilika. Hali ya usalama katika dunia hii imebadilika na kila jambo katika dunia hii kila nchi inajifunza kutoka kwa jirani yake ama kwa Taifa lingine. Ni wakati muafaka sasa elimu ya uraia katika nchi yetu ya Tanzania inayoingia katika vyama vyetu ni lazima iratibiwe na ikiratibiwa itatusaidia kudumisha umoja na usalama wa Taifa letu, pamoja na kuendelea kuangalia mwenendo wa

shughuli za demokrasia na uendeshaji wa shughuli za vyama katika Taifa letu.

Kwa hiyo, niwaombe tu Wabunge wasiwe na hofu na wale wenzetu wenye hofu itabidi tuanze kuwashangaa kwa nini wanakuwa na hofu? Kulikuwa na nini katika kutokuratibu elimu hiyo ya uraia kwenye vyama vyao? Hilo ni jambo ambalo tunatakiwa kujiuliza, unapokataa sana kuratibu jambo ambalo linaleta tija ulikuwa unaficha nini kabla ya sheria hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba wakati tunapokea maoni ya wadau yuko kiongozi wa chama kimoja cha siasa alituambia wakati wa kupokea maoni anasema yeye aliwahi kugombea Urais mwaka fulani katika Taifa letu, na akatuambia alikuwa hana fedha yoyote, hakuwa hata na senti tano, lakini alipata fedha, akaletewa kila kitu na taasisi mbalimbali kutoka nje ya nchi, lakini vilevile akatengenezewa uratibu wa kuratibu elimu ya uraia kupitia kwenye chama chake na taasisi mbalimbali. Sasa tushukuru Mungu tu labda huyo mgombea hakuwa na lengo baya kwenye Taifa letu, angekuwa na lengo baya tungepata shida. Kwa hiyo, wenyewe mapenzi mema watulie, wale ambao hawakuwa na mapenzi mema ni lazima wakubali sasa nchi yetu ni lazima mambo haya yaratibiwe ili tuwe na usalama na uhakika wetu.

Mheshimiwa Spika, muswada umelenga kudhibiti vyama vyaa siasa. Iko hoja hapa imeletwa na tumeambiwa kwamba kwa nini muswada huu unataka kudhibiti vyama vyaa siasa?

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tu niseme, kwamba muswada huu unalenga kwa kweli kukuza demokrasia na hasa kukabiliana na changamoto ambazo tulikuwanazo. Kifungu cha 6C(5); kifungu hiki kinaenda kuweka utaratibu sasa wa kuvikataza vyama kukasimu shughuli muhimu sana ambazo zitaleta umoja na demokrasia kwenye vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumeshuhudia hapa ndani ya mienendo ya vyama vyetu nya siasa kwamba mgombea wa Urais anaweza akapatikana tu labda kwa watu kumi ama 20 kukaa mahali na wanaamua huyu atakuwa mgombea wetu wa Urais bila ridhaa ya chama. Maamuzi hayo yanayofanywa na watu wachache yamekuwa yakileta mpasuko na migogoro mingi na migogoro mikubwa sana ndani ya chama, wote ni mashahidi. Sheria hii inapokuja kuweka mfumo na uratibu, kwa mfano mgombea Urais apatikane kupitia mikutano mikubwa ya vyama, mtu anasema sheria hii inabana vyama, haileti demokrasia.

Mheshimiwa Spika, ni lazima hapa ujiulize kinachotakiwa ni nini? Kwa hiyo, utaratibu wa mtu kuamua kukaa ndani ya ofisi na kuteua mgombea ndio demokrasia kuliko Mkutano Mkuu wa chama kuteuwa mgombea wa Urais?

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya kuijuliza. Sheria inakuja kuweka utaratibu Mwenyekiti wa Chama wa Taifa achaguliwe na Mkutano Mkuu wa Taifa na Mkutano Mkuu huo wa taifa uwe umeshaonekana kwenye mfumo wa kiuratibu wa katiba ya chama. Viko vyama hapa Wenyeviti wao wa Taifa hawachaguliwi na Mikutano yao Mkuu ya Taifa, vipo.

Mheshimiwa Spika, na ninakwambia kwamba sheria hii sasa inakwenda kutibu hayo na ukiona watu hawataki ujue ajenda hizi zilikuwa zinaendelea kwenye vyama vyao, kwa hiyo acheni tupate sheria ambayo itatusaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linadhihirisha kabisa kwamba sheria hii inaenda kukuza demokrasia. Kabla ya sheria hii chama kilikuwa kinaweza kuadhibiwa kwa makosa ya mwanachama, lakini katika sheria hii sasa tumekubaliana kwamba akifanya makosa mwanachama ataadhibiwa mwanachama mwenywewe na si chama chake, lakini watu nashangaa kwamba wanakataa wanasesma huu sio mfumo mzuri.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza demokrasia viko vyama vilikuwa vinabadilisha Katiba za vyama vyao ndani ya ofisi na wanachama hawana habari. Mtu akitaka kuongeza madaraka ya kukiongoza chama alikuwa na uwezo wa kuibadilisha Katiba mahali popote, sheria hii sasa inaenda kuweka utaratibu. Kwa hiyo, kama tunaweka utaratibu huo hiyo ni demokrasia na si kwamba tunenda kuminya demokrasia. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge muukubali muswada huu, ili haya matatizo yaweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, na mimi nikuhakikishie Ofisi ya Msajili wa Vyama ina malalamiko mengi kutoka kwa wanachama wa vyama mbalimbali wakilalamikia mienendo ya kunyimwa demokrasia ndani ya vyama vyao kwa aina moja ama nyngine. Sasa hapa tunaenda kutoa dawa na ninadhani sheria hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, hapa imezungumzwa kwamba muswada una nia ya kumpa Msajili nguvu kubwa na hiyo nguvu si sawa kwa muktadha wa siasa na demokrasia ya nchi yetu tulyonayo kwa sasa hivi. Ukiangalia mwenendo mzima wa shughuli za siasa zilivyokuwa zinafanywa ndani ya vyama vyetu, leo tunapoamua kumpa Msajili, kwa mfano, madaraka ya kufuatilia matumizi ya fedha ndani ya vyama ni jambo la msingi sana. Tumepokea hapa ripoti ya CAG na umeona ni kwa kiasi gani vyama vimeduwa vikifanya matumizi mabaya ya fedha na hakuna sheria ambayo illkuwa inavibana vyama hivyo katika kudhibiti matumizi ya fedha ambayo ni fedha za walipa kodi wa Tanzania na hasa vile vyama ambavyo vilikuwa vinapata ruzuku.

Mheshimiwa Spika, tuliona hapa na tuna malalamiko kwamba kuna baadhi ya vyama kwa viongozi wa vyama wanavikopesha vyama vyao fedha na wanapovikopesha hakuna kumbukumbu zozote za aina ya mikopo inayopelekwa kwenye vyama kutoka kwa viongozi na wala haielezi matumizi ya mikopo hiyo ni kwa ajili ya shughuli gani? Na Serikali inapotoa fedha za ruzuku baadhi ya viongozi wa vyama wamekuwa wakichukua fedha za ruzuku kujilipa

mikopo ambayo haina maelezo ilipelekwa kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiangalia haya yote yanayoenda kufanywa na huu muswada unagundua kabisa kwamba muswada huu sasa unaenda kutibu matatizo mengi katika uwanda wa demokrasia, lakini uwanda wa uendeshaji wa shughuli za kisiasa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, limesemwa jambo hapa kwamba, kwa nini kile kifungu kidogo cha 6A(5) kinaweka hii misingi na alama muhimu za taifa letu. Watu wamebeza mwenge wa uhuru na Mapinduzi ya Zanzibar kwamba hivi si vitu ambavyo vinastahili kukaa katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tuendelee kushangaana. Hawa hawa leo wanaoyakataa Mapinduzi matukufu ya Zanzibar wakitoka hapa wanaenda tena kuwashawishi Wazanzibar kwamba

wanapenda sana kuwatetea kwenye hoja zao. Lakini tujulize kuhusu historia ya muungano wa taifa letu, kwamba utawezaje kuzungumza muungano wa taifa hili bila kuzungumzia mapinduzi matukufu ya Zanzibar? Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, huwezi kuzungumza uhuru wa taifa letu la Tanzania bila kuuzungumzia mwenge wa uhuru, haiwezekani. Tunayo Sheria ya Nembo ya Taifa na Sheria ya Nembo ya Taifa inaweka mwenge kama alama mojawapo kwenye Nembo ya Taifa letu. Vilevile kinaenda kusisitiza kwamba vyama vyote wakati wa kutengeneza sera za vyama vyao ni lazima watambue hiyo misingi mikubwa na alama muhimu za Taifa letu zinazoonesha utaifa wetu pamoja na utawala bora, mambo ya amani na kukimbia rushwa. Leo tunasema tunaongeza na masuala ya jinsia kama ni masuala ya msingi sana katika uendeshaji wa vyama vyaa siasa, lakini watu wanaona jambo hili si jema pia.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo tumeona kabisa kwamba sasa tunakokwenda vyama vitakapoteuwa

wagombea wake, kama mgombea atayakataa mapinduzi yetu ya Zanzibar hatoshi kuwa kiongozi katika chama cha siasa. Kama mgombea katika uongozi wa chama cha siasa hatazungumzia masuala ya jinsia, masuala ya mapambano dhidi ya rushwa, masuala ya wenyewe ulemavu na masuala yote yanayozingatia utamaduni na uhuru wa Taifa letu, kiongozi huyo hatoshi, acheni tuweke hapa. Lakini niseme kama sera za vyama hivi vyote katika Taifa letu havitathamini mwenge wa uhuru kama alama ya uhuru wa Taifa letu ni lazima chama hicho tukishangae na tutajua chama hicho hakina nia njema ya kulinda uhuru wa Taifa la Watanzania, kwa hiyo jambo hili lazima lieleweke vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaona watu wamezungumza sana kuhusu kifungu cha 8E, kwa nini tunaondoa hivi vikundi vya ulinzi?

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge labda msome vizuri kwanza hicho kifungu kinasema nini. Kifungu hicho kinaenda sambamba na kifungu cha Katiba ambacho tumekieleza cha 147 kwa sababu gani! Kifungu hicho cha 8E(1) kimesema; "kiongozi au mwanachama asije akaandikisha wala kuunda vikundi vinavyofanana na vikundi vya kijeshi", kifungu ndicho kimesema hivyo. Kama wewe unaona kwamba unataka kulindwa nenda huko kachukue hizo taasisi zilizoanzisha vikundi vya ulinzi na usalama watakulinda, lakini tunasema wewe kama chama, kiongozi, usianzishe kikundi kinachofanana na kikundi cha kijeshi ndani ya chama chako, hilo jambo limepigwa vita hapa wazi kabisa ama usianzishe hicho kikundi kitakachofanya kazi zinazofanana na taasisi ambazo zinashughulika na ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa umeshaambiwa usifanye, usianzishe vikundi ambavyo vinafanana na taasisi za ulinzi na usalama nchini, sasa wewe unataka kuanzisha kikundi kinafanana na polisi, kinafanana na wanajeshi, kinafanana na kikundi cha makomandoo. Kuna Mbunge mmoja alisema wao hawachukui silaha wanapigana kwa mikono, sasa kama wanapigana kwa mikono, lakini wanafanana na vikundi vya

kijeshi, nduguzanguni machafuko yote katika nchi za wenzetu yalianzishwa kwa sababu ya kutokuzingatia kifungu hiki ambacho kiliruhusu vikundi vyta namna hiyo kwenye vyama vyta siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwathibitishie wanasiasa wenzangu, tumeona mfano dhahiri wakati wa uchaguzi, kila mgombea Urais katika nchi hii anakuwa analindwa na polisi tena ni polisi wa Serikali hii hii, hakuna mgombea wa Urais hata mmoja wakati wa uchaguzi amelindwa na *green guard* ama amelindwa na *red brigade* ama amelindwa na *blue brigade*. Wagombea wote wa Urais, Makamu wa Rais wakati wa uchaguzi wote wamelindwa na polisi hawa hawa wa Tanzania na hakuna aliyepata matatizo hata mmoja. Leo tunasema kwamba, hatuna imani na Polisi wa Tanzania katika kuwalinda wanasiasa tunaanza wapi?

Mheshimiwa Spika, ninaomba ndugu zangu tuendelee kukipitisha kifungu hiki. Tuondoe vikundi hivyo ambavyo mwisho wa siku vinaweza kuleta matatizo makubwa ya usalama, amani katika nchi yetu ya Tanzania. Ndugu zangu kama tunaendelea kung'ang'ania hivi vikundi kila mtu atatuuliza tuna ajenda gani ya kuwatumia hawa?

Mheshimiwa Spika, na Mjumbe mmoja amesema tunawapa mafunzo kweli kweli. Sasa hayo mafunzo mwisho wa mafunzo inaweza kuwa ni shida kubwa kuliko kuendeleza amani na utulivu kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 tumetoa maelezo sasa hivi kuhusu vyama kuweka mashirikiano. Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge muunge mkono kifungu hiki. Tumeshuhudia vyama vikishirikiana bila kuwa na utaratibu na matokeo ya kufanya mashirikiano bila kuwa na utaratibu yameleta migogoro mikubwa sana ndani ya vyama vyta siasa nchini.

Mheshimiwa Spika, ilifikia hatua, vyama vya siasa vinafanya ushirikiano halafu vinatumia ushirikiano huo ambao siyo rasmi kurasimisha shughuli ambazo zinaenda kinyume na sheria tulizonazo nchini. Jambo hili halipaswi kufumbiwa macho. Sheria sasa inasema, kila chama kitakachotaka kufanya ushirikiano, kitamtaarifu Msajili, kwani shida ipo wapi? Nendeni tu mkatoe taarifa kwa Msajili kwamba mnataka kufanya ushirikiano na lengo la ushirikiano wenu. Sasa shida ipo wapi? Kutoa tu taarifa kwamba tunataka kushirikiana, shida haipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani sasa kifungu hiki kitatusaidia kuratibu ushirikiano huo, kila chama kifanye ushirikiano katika malengo wanayoyataka lakini kitatusaidia pia kuondoa migogoro. Sasa sheria inataka hao wanaotaka kufanya ushirikiano, ni lazima kwanza ushirikiano huo upitie kwenye Mikutano yao Mikuu ya Taifa na siyo watu wanakutana wapi au wapi wanashirikiana, hapana. Hiyo itasaidia sana kuondoa migogoro kwenye vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, labda kwa kumalizia kwa sababu ya muda, ni huu utaratibu ambao umewekwa na Kifungu cha 21(e), nilisema pale mwanzo, haya ni Mamlaka ya Msajili kushungulikia Mwanachama anayekiuka Katiba ya chama chake lakini pia anakiuka sheria za nchi na hasa Sheria za Vyama vya Siasa. Huko mwanzo nilisema, mwanachama huyu akikiuka Sheria ya Vyama vya Siasa chama chake ndiyo kilikuwa kinapata taabu na kuadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki sasa kimeweka vizuri sana, kinamfanya Msajili, akigundua Mwanachama amekiuka sheria, Msajili atakiandikia chama chake, jamani mtu wenu huyu amefanya mambo ambayo siyo sawa sawa, ni kinyume cha sheria na atakiagiza chama chake kichukue hatua. Kisipochukua hatua, Msajili sasa apate nguvu na yeye ya kumchukulia hatua huyo Mwanachama na kukiacha chama kibaki salama. Hapo kuna tatizo gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie kwamba kwa kukiweka kifungu hiki, vyama vingi vitakuwa salama,

nyie mmekuwa ni mashahidi, wanachama wa vyama vyetu wamekuwa wakileta fujo bila kutumwa na vyama vyao na mwisho wa siku chama kilikuwa kinaadhibiwa na mwanachama anajificha ndani ya chama. Kwa hiyo, Kifungu cha 21(e) sasa kinaweka utaratibu mzuri, chama kitakuwa salama, mwanachama atakayeshughulika kuvunja sheria, yeche ndiye atakayebeba dhamana ya kushughulikiwa na chama chama chake kwanza, lakini baadaye atakuja kushughulikiwa na Msajili kwa utaratibu mzuri kabisa ambao umewekwa na sheria hii ambayo leo mkiipitisha itatusaidia sana kuweka utaratibu huo wa kutoa nidhamu kwa vyama vyetu.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema yafuatayo: watu wamechangia na wamesema kwamba sisi wote tunatakiwa wote tunatakiwa kusimama kwenye misingi ya demokrasia, lakini hakuna demokrasia yenye uhuru ambayo hauna mipaka. Demokrasia nchini imeendelea kukua, haya mabadiliko tunayoyafanya ni mabadiliko ya nane na Sheria hii ya Vyama vya Siasa wala hajjafanyiwa mabadiliko mara ya kwanza kwenye mwaka huu, lakini mwisho wa siku tunaamini baada ya sheria hii, haki usawa na uendeshaji wa shughuli wa vyama vya siasa na shughuli za siasa katika nchi yetu zitaratibowi vizuri. Wenyе nia njema wataonekana na wasio na nia njema wataonekana. Mwisho wa siku Taifa hili ni la kwetu sisi wote. Kama Taifa hili ni letu wote, kama tutafanikiwa kuweka mfumo na utaratibu mzuri wa uendeshaji wa demokrasia, uratibu wa shughuli za siasa nchini, sisi wote ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tutakuwa salama. Tusipofanya hivyo, tutapata shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwashawishi sana Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja hii, tupitishe hii sheria ikatusaidie kusimamaia masuala ya demokrasia na utaratibu na uratibu wa vyama vya siasa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja yangu lakini naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja litolewa lamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tumeona jinsi hoja inavyoungwa mkono kwa nguvu kubwa, ahsante sana. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Moja kwa moja sasa tunaendelea naomba ushirikiano wenu. Katibu.

RAMADHANI ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa Mwaka 2018 [The Political Parties (Amendments) Bill, 2018]

Ibara ya 1

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 2

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia bado una maneno?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Naomba kufanya marekebisho katika kipengele cha 3(c) kama sitaridhika nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono, wajadili.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Msajili wa Vyama asipewe jukumu la ku- *monitor intraparty elections and nomination processes* na badala yake napendekeza Msajili wa Vyama vyta Siasa apewe kazi ya ku-*observe*.

Mheshimiwa Spika, natambua majukumu makubwa aliyonayo Msajili wa Vyama vyta Siasa na ninajaribu kui-*imagine* kama atapewa kazi ya ku-*monitor elections* na hiki kifungu *specific* hakijasema katika ngazi ipi, ana-*monitor election* kwenye tawi, kwenye kata au kwenye msingi? Badala yake inasema huyu mtu/Msajili huyu apewe mamlaka ya ku-*observe* ambayo ku-*observe* sasa haimwongezi madaraka makubwa sana. Badala yake, kwa kuwa sasa Msajili ana nafasi iwapo wale ambao kwenye mchakato wa uchaguzi hawajaridhika wanaweza kupeleka malalamiko yake, nashauri hiki kipengele kisiwe ku-*monitor* badala yake tu-*replace* neno *observe*.

MWENYEKITI: Kwanza nikupe ushauri wa jumla Mheshimiwa Anatropia, kwenye mfumo wetu wa Bunge hapa tunayo Idara maalum kabisa ambayo inasaidia masuala ya *drafting* kama haya. Kwa hiyo, wakati mwingine utakapokuwa na kitu kama hiki, unawaenda wanakuweka katika utaratibu ule ambao ndiyo hasa unatakiwa kukaa vizuri. Hilo ni kwa Wabunge wote pia. Tunao usaidizi wa kisheria hapa.

Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi upande Serikali tunaomba kifungu hiki kibaki kama kilivyo kwa sababu ukimwita huyu ni *observer* humpi yale mamlaka kamili ya kufuatilia *compliance*, kwa sababu tumempa madaraka kwenye huu muswada wa kuhakikisha kwamba Sheria ya Vyama vyta Siasa inatekelezwa. Sasa

akiwa *observer*, kazi yake ni kuangalia, hachukui hatua yoyote; lakini akiwa *monitor*, pale atakapogundua kwamba labda katika uchaguzi fulani uliofanyika utaratibu haikuafuatwa, Sheria ya Vyama imekiukwa, atapata nafasi ya kuona ni kifungu gani cha sheria kilikiukwa na hata mashtaka yatakapoletwa kwake atakuwa na nafasi nzuri ya kutatua hilo ambalo lilijiri katika uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uzoefu unaonyesha, kama ni kumfanya huyo awe *observer*, alishakuwa anafanya hiyo kazi, hawa wenyewe wanajuwa mikutano yao mikuu yote walikuwa wanamwalika na alikuwa anakwenda huko. Sasa kifungu hiki sasa hivi kinatengeneza kazi ambazo zitatambulika rasmi kisheria zitakazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Vyama. Kwa hiyo, naomba hili jambo libaki kama liliyuo.

SPIKA: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, anachokisema Mheshimiwa Waziri, *application* yake ipo *theoretical*. Bado pia hajaeleza, hata kama *ana-monitor*, *ana-monitor* katika *level* gani? Hicho kipengele bado kinabaki kuwa *wide*. Unasema *ata-monitor intraparty election*, nina uchaguzi tawi Kisiwani, Msajili anahusika? Awe *very specific* na ndiyo maana tukasema *ku-observe it is a bit mandatory*, anaweza kuja, anaweza asije lakini akaletewa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani watu wengine watoe maoni yao kwa sababu kwa maoni yangu naona huyu mtu tayari ana majukumu, lakini kama ikitokea hatujaafikiana huko chini kwenye uchaguzi ni lazima twende kwa Msajili kwa sababu tayari huu muswada unampa majukumu ya kuingilia na *ku-settle disputes* zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba...

MWENYEKITI: Mpaka hapo hoja yako ni nini? Hoja yako ni kwamba iwekwe ngazi ambayo yeye *ata-monitor* au hoja yako ni nini hasa?

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ku-*observe*, tuondoe neno *monitor* tumfanye *observer*. Naomba kutoa hoja watu wajadili.

MWENYEKITI: Haya. Nitachukua CUF mmoja, hapa mbele ambaye hajaongea Mheshimiwa Selasini na CCM wawili, nitamchukuwa Mheshimiwa Angella Kairuki na Mwenyekiti wa Kamati kule mwisho. Tuanze na...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu baada ya bundi kuonekana ndani ya Ukumbi wa Bunge)

MWENYEKITI: Kuna nini? Bobali au nani?

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Bobali.

MWENYEKITI: Tunaanza na Mheshimiwa Bobali. Hayo mambo ya kawaida yasiwape shida.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Wamwache yupo kazini.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa hoja mbili, hoja ya kwanza...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba tusivuruge kikao. Tuendelee na kikao, msiwe na wasiwasi. Hao ni wanyama wetu katika Taifa, kwa hiyo, isiwababaishe, endelea Mheshimiwa. (*Makofi*)

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa hoja mbili.

MWENYEKITI: Huyo ni mgeni wa Spika, mwacheni.
(*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Angekaa *Speaker's Gallery*.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sheria kama alivyosema Mheshimiwa Anatropia kwamba ilivyoweka ni kama *the limit is the sky*, yaani ipo tu haijaweka msingi kwamba ata-*monitor* kuanzia *level* gani? Kwa hiyo, ni vyema tukasema *observer* kuanzia labda kwenye *national level*/kwa sababu nategemea Ofisi ya Msajili namna ilivyo ikiwekwa tu hivi kuanzia kule chini inaweza ikawa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba sisi tunategemea kwa sheria hii, tukishagombana huko kwenye vyama tukimbilie kwenye Ofisi ya Msajili. Sasa kama ata-*monitor* kwenye shughuli za kiuchaguzi *let's say*, halafu baadae twende tena kwake ye ye ambaye alishiriki moja kwa moja ni kama atakuwa anakosa ule uhalali, *justification* ya kutatua zile changamoto. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Chaguzi katika vyama vyetu ni *process* inayoanza kwenye mashina mpaka ngazi ya Taifa. Sasa Msajili kwa jinsi ile ofisi ilivyo sasa hivi, yupo pale Msajili na Msaidizi wake tu, hakuna *manpower*. Sasa huyu Msajili atakuwa na uwezo gani wa ku-*monitor process* ya vyama hivi vyote 19 ambavyo vinafanya uchaguzi kwa nyakati mbalimbali? Isitoshe, hii ni gharama pia inaingia kwenye Taifa, kwa sababu kama tumeamua lazima hili liwe, ina maana lazima Ofisi ya Msajili iwekewe watu wa kuweza kufanya hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Katiba za vyama vyote zina utaratibu wa kukata rufaa kama mgombea wa nafasi yoyote ana mashaka. Kwa hiyo, nashauri, hii nafasi ya ye ye kuwa *monitor* iondolewe. Akiwa *observer* anaweza akatengeneza utaratibu wa kuwa...

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili tulilitazama kwa kina sana na tumediriki kuazima maneno ya kiingereza tupate tafsiri fasaha ya neno "*monitor*" na tukagundua kwamba *to monitor is to observe*, isipokuwa sasa yule anaye-*monitor* anakwenda mbele zaidi ya kuweka misingi na kusimamia yale matakwa ya katiba ya vyama uhusika. Kwa hiyo, eneo hili mimi naiunga mkono Serikali kwa sababu *to monitor is to observe*. Pengine tatizo hapa ni kizungu tu, labda tafsiri ya maneno ya kizungu yanawasumbua watu, lakini *monitor* na *observer* ni neno lile lile isipokuwa *monitor* ataendelea kufanya kazi ile na *observer* atafanya kazi kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuzingatia kwamba sheria hii inakwenda kuanziswa Ofisi mpya ya Msajili ya kuongeza majukumu mapya ya Msajili, uazishwaji wa nafasi ya Naibu Wasajili. Inamaanisha kwamba wapo watendaji wataongezeka katika Ofisi ya Msajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiunga mkono Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kabisa na mimi niunge mkono kwa namna ambavyo Serikali imeleta pendekero lake. Ukiangalia kwanza *monitor* ni *concept* pana zaidi, anaweza hata asiwepo pale, lakini bado anaweza kufuatilia kila kinachoendelea na akapata taarifa na mambo yakaenda sawa. Unapoweka ku-*observe* tu, kwanza anakuwa *limited* na ni lazima awepo pale *physically* na kuwe na *physical presence*. Kwa hiyo, *monitor* ni neno sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitabaki na msimamo wangu kwamba atakavyokuwa ana *limited scope*, maana yake anatuachia nafasi sisi kwamba kama hatujaridhika na mchakato tunaenda kwake, lakini tukimpa *scope* yote aka-*exhaust* nguvu zake zote aka-*exhaust* na shughuli zake zote tutakuwa hatuna uwezo tena wa kukata rufaa kwake kwa sababu amehusika kwenye mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaachia Wajumbe waamue.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Hoja Iliamulliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia jambo lako limekataliwa, linabaki liliivyo.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

MHE. PENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kabla...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Upendo ni kinyume na utaratibu, tumeshamaliza hilo. Sasa kutokana na maandishi yako Mheshimiwa Anatropia hayakuwa mazuri, ile *clause 3* tunaondoka pale. Yaani jinsi ulivyoandika inatosha, tunakwenda mbele. Ulikosa ushauri mzuri wa kuiweka vizuri *amendment* yako hiyo.

Tuendelee Katibu.

Ibara ya 4

(Ibara iliyotajwa hapo juu imefutwa na Serikali)

Ibara ya 5

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napendekeza kwamba baada ya Kifungu cha 5(A)1 ninapendekeza kije Kifungu cha 5B kwa maana kifungu cha pili. Kuna cha kwanza tayari, cha pili. Msingi wa kupendekeza, Mheshimiwa Waziri alikuja kwenye Kamati nami nilipata fursa ya kushiriki na tulimpa *concern* yetu kwamba watu wanavyoambiwa wapeleke taarifa za kutoa mafunzo au *training* ya aina yoyote, lakini kuna kipengele kinachofuatia kinawaambia Msajili anaweza kukubali au akakataa, inatuacha kwenye *dilemma*. Pia marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanatoa muda wa siku wa 30 huo mchakato ukamilike.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia hebu soma kwanza kitu gani unachokipendekeza hicho kipyta maana yake hiki Kiingereza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, najenga hoja halafu nakusomea kifungu.

MWENYEKITI: Aaa, soma bwana, fuata ninachokwambia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Sawa inasema B; "*training or capacity building to political parties will not involves terrorism, radicalism training, money laundering, rebellion, homosexuality and all other behavior that are not in conformity with Tanzanian Society*". napendekeza hicho kifungu kije kama cha pili kwamba anayeomba kuwafanya mafunzo, akiomba katika *basis* ya hivi vitu hatakubaliwa, ndio msingi wa kifungu changu.

MWENYEKITI: Hapa hueleweki kabisa unataka kusema nini maana yake lazima tuangalie *exactly* ulichokiandika ni kitu gani, hatujadili vitu vingine vinavyotoka hewani eeeh. Hii hata nikimpa Mheshimiwa Msigwa hapa, atapata tabu sana jinsi ya kukuunga mkono.

Kwa hiyo kwa hili nadhani kama nilivyosema mwanzo, ni vizuri wakati mwingine unawaona vijana wetu wale wanakuweka au una watu ndani ya kambi yako ni vizuri kuwaona wakakuwekea vizuri kidogo. Hatuwezi tukawa na kifungu cha aina hii cha Kiingereza hiki.

Jamani Waheshimiwa nadhani nipo sahihi?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Kabisa kabisa. Sasa nitawahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

(Ibara iliyotajwa hapo juu illifutwa na Serikali)

Ibara ya 7

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia tena kwako kifungu cha 7.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 kinatoka kwenye section 6A ambayo inapendekeza vitu mbalimbali ambayo mimi kwa maoni yangu napendekeza ku-delete neno *uhuru torch*. Nakubaliana na mambo mengine lakini naomba kuondoa kitu kimoja tu kinatwa *Uhuru torch* na nieleze msingi wa kutokukubaliana nayo. Nadhani Mheshimiwa Hayati Mwalimu Baba wa Taifa aliyohamasisha Mwenge na alitushauri tuweke juu ya Mlima Kilimanjaro. Nadhani sisi wote humu ndani tunakubali Mwenge tuupeleke juu ya Mlima Kilimanjaro, lakini zama pia zimebadilika leo watu Wanaheshimu kilichotokea lakini hatuamini kama bado kinaishi leo. Naamini vyama hatupaswi kuvi-compel/kuweka au kufanya mambo ambayo yameelezewa kwenye kifungu hiki yaki-base katika vitu vingine, nakubaliana navyo ukiondoa *uhuru torch* huo ndio msingi wa kukiondoa au kuondoa neno linaitwa *uhuru torch*.

MWENYEKITI: Sasa Anatropia baada ya maelezo yote yaliyotoka hapa kweli bado unasimama na jambo hilo hilo tu, maana uhalali wa maneno yako siuoni uko wapi. Yaani nashindwa, nadhani nihoji tu moja kwa moja kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Anatropia

*(Hoja Iilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

MWENYEKITI: Anatropia pia ana marekebisho, lakini marekebisho yake ni kifungu cha 8(e) ambacho kwenye Muswada huu hakipo kabisa na ndiyo maana nasema ungekuwa unashirikisha kidogo, ungejikuta upo mahali pazuri kidogo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

MHE. KABWE R. Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kifungu cha 11 ambacho kili-introduce kifungu kipywa cha 8C ukishuka nayo mpaka (3)"*A Political Party which fails to comply...*" na kinaendelea. Kifungu hiki kinaangukia kwenye vifungu ambavyo tulikubaliana kwenye

Kamati kwamba ni *unconstitutional*, kwa hiyo nadhani Serikali ilisahau kukifuta kwa sababu vyote vinyofanana na hiki vilifutwa. Naomba nipate maelekezo ya Serikali kuhusiana na hiyo 8C(3), tafadhalii.

MWENYEKITI: Mwenyekiti wa Kamati au niende kwa Waziri, ni kweli endapo kulikuwa na makubaliano hayo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza hatufahamu juu ya makubaliano hayo, lakini jambo la pili Mheshimiwa Zitto angelisaidia Bunge kwa kueleza hivyo *unconstitutionality* iko wapi?

MWENYEKITI: Nakuruhusu kwa vile jambo unalotaja linahusu Katiba.

MHE. KABWE R. Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa Kamati tulisema kwamba vifungu vyote ambavyo vinaenda kinyume na vifungu vyta Katiba viondolewe na moja ya *principle* ni kwamba vifungu vyote ambavyo vinahusiana na *suspension* na kadhalika viweze kutoka.

Sasa ukitazama lbara ya Katiba ya 20 ukisoma chote kile, maeneo mengi sana tulifanya *reference* kwa lbara ya 20 na ukisoma hiki kifungu cha 8C kwamba chama kinaweza kuwa *suspended*, msingi hasa Katiba *hai-provide suspension* na ndio maana vifungu vyote vinyohusiana na *suspension* vyote na Wajumbe wa Kamati watakumbuka, tumevifuta kwenye huu Muswada na jedwali la marekebisho ambayo Serikali imelileta limevifuta vifungu vyote na Mwenyekiti anaweza akaulizwa na aka-*confirm* hapa *reference* ni ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo nahisi Serikali ilisahau tu vifungu tulivyokuwa tunafuta ni vingi tu. Kwa hiyo, wakubali na hiki waweze kukifuta kama vingine pia.

MWENYEKITI: Jamani hata Wajumbe wa Kamati wenyewe, sio lazima awe Mwenyekiti au nani hiki kinachosema kama mnakubaliana kipo? Mwenyekiti wa Kamati amesimama.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti yale maaneo ambayo tulikubaliana Serikali ilifanya marekebisho na katika eneo hili la 8C Kamati illi-overlook, hatukuliona eneo hili kwa kina. Kwa hiyo naomba nikiri Kamati na Serikali, sote hatukuliona.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *just information*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *just point of information*, ukisoma taarifa ya Kamati page 36 ina specify hilo jambo kufuta ibara 12(2)(f) – (g) ifutwe kwa kuwa maadhui ya kifungu kidogo...

MWENYEKITI: Subiri kidogo maana yake akina Selasini, sijui nani wamesimama, akina Lema sijui nani, kuna nini jamani, kwa nini tusikae chini twende pamoja. Anza tena Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti kwenye taarifa ya Kamati kifungu hiki kimekuwa *mentioned* kabisa na *page*namba 36 ya taarifa ya Kamati inasema ibara ya 12(2)(f) na (g) ifutwe kwa kuwa maadhui ya kifungu hiki hayaendani na maudhui ya Ibara ya 20(2) ya Katiba ya nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka nitoe taarifa hii kwa sababu hili jambo limekuwemo, inawezekana ni kweli Serikali im-overlook.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Serikali

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Bashe sasa anatutoa kabisa. Hicho anachozungumza Mheshimiwa Bashe sicho hiki ambacho tunacho sasa hivi, hicho ni kingine kabisa sicho hiki ambacho tunacho sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ameliweka vizuri sana. Mambo haya yanayozungumzia, Katiba *custodian* wa kusimamia kuona uvunjifu wa Katiba au kutokuwepo uvunjifu ni *Attorney General*/ndani ya Serikali. Baada ya *Attorney General*/kupitia kifungu hiki na amekitolea maelezo ya kila hapa ndani ya Bunge kwamba hiki kifungu hakivunji Katiba, haya ni maelezo yaliyotolewa na *Attorney General* wakati akijibu maswali leo kabla ya kuingia kwenye hoja ya Kamati.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima
bila mabadiliko yoyote)*

*(Hapa Mhe. Kabwe R. Z. Zitto na Mhe. Upendo F. Peneza
walisimama wakitaka kuzungumzia kifungu
kilichopitishwa hapo juu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto tumeshafanya maamuzi tuendelee Katibu.

Ibara ya 12

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Upendo sema.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuzungumzia kifungu hicho cha 12 ambacho Mheshimiwa Bashe alikwishakianza kwa kuongelea tulipokuwa tunazungumzia kifungu cha 11 sasa mimi naona nikizungumze kwenye 12. Tulikubaliana kwenye Kamati kwamba kifungu (f) na (g) vifutwe kwa sababu haviendani na Katiba ya Muungano wa Tanzania katika Ibara hiyo ya 20. Kigezo ambacho kipo ni kwamba kama tunahitaji hiyo (f) na (g) iwepo basi marekebisho ilibidi yafanyike awali katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, sasa kwa sababu haya mabadiliko hayapo huko, basi hatuwezi tukaweka katika sheria hii hiyo (f) na (g).

MWENYEKITI: Umeelewaka. Wanadai kuwa mlikubaliana mliokuwepo huko. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12(f) kinazungumza mambo ya *any party data allows its leaders and members to utter or use obscene language, vindictive, defamatory or inciting words.....*" na kadhalika pia (g) "*it uses or accept the use of or advocates for the use of religion or religious organisations to further its objectives*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleweke vizuri ibara ya 26(1) iko wazi, inamtaka kila mtu kuzingatia sheria za nchi hii. Pia tukasema haya yote yaliyozungumzwa hapa yamewekwa pia kwenye sheria nyingine zikiwemo Sheria za Makosa ya Jinai, kwa hiyo hakuna *unconstitutionality* hapa. Tukienda (g) hiki kifungu kinabebwa na Ibara ya 20(2) ukienda kwenye Katiba Ibara ya 20(2) imebeba mambo hayo hayo, hakuna *unconstitutionality*.

MWENYEKITI: Nilitaka kushangaa sana, kwa hiyo ndio nakupa nafasi ya upendeleo.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Hebu halalisha ulichotaka kusema.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningependa kusema kwenye hili suala tunachoongelea hapa ni kuhusu suala la vyama vyaya siasa na siyo kwa maana ya Ibara hiyo. Kwa hiyo tunachoongelea kama tunatunga sheria ya kuhusu vyama vyaya siasa kipengele tunachokiangalia kwenye Katiba ni Ibara ya 20(2) na mambo ambayo kimetaja kinazuia vyama vyaya siasa kufanya. Sasa kama kwenye hicho kipengele cha

katiba hakijataja haya maneno ambayo yapo kwenye (f) na (g) hatuna ulazima sasa wa kutunga sheria ambayo inaonyesha vitu ambavyo Ibara hiyo 20(2) haijataja. Kwa hiyo kuna sheria za nchi ambazo zinazungumzia na ndio maana watu sasa hivi wanaoongea maneno mabaya, wanatukana wana pelekwa mahakamani kwa sababu kuna sheria hiyo. Hata hivyo, hatuwezi tukaifanya hiyo ikawa sehemu ya chama cha siasa kwa sababu hii ni sehemu ya uwajibishaji kwa chama cha siasa, lakini kama ni watu kwa maana ya lugha ambazo mtu anavunja sheria, kuna sheria ambazo zinawapeleka mahakamani katika makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hili suala lilifanyika kwa maelezo mengi sana kwenye Kamati na tulikubaliana kwa ujumla na Mheshimiwa Chenge akiwa ndio kiongozi wetu mkuu tulipata mwongozo mzuri sana katika hili suala na tulikubaliana kimsingi kama Kamati na Serikali ikatuletea jedwali hili hapa, hili ni la Serikali sio la Kamati. Serikali ikikubali kwamba imekubali kufuta (f) na (g), sasa leo itakuwa suala la kushangaza. (*Makof*)

MWENYEKITI: Liko wapi hilo jedwali?

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti hili hapa.

MWENYEKITI: Hebu leteni wale watu wangu wahini basi na nyie muwe mnatawanyika mnakaa mahali pamoja wote.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, hili hapa ni ukurasa wa 22.

MWENYEKITI: Mpe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashe ulikuwa unaongelea hapa kwenye 12, hebu rudia tena.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisoma kwenye taarifa ya Kamati ambayo aliisoma

Mwenyekiti, kwamba katika page namba 36 ya taarifa ya Kamati inasema hivi; "Ibara ya 12(2)(f) na (g) ifutwe kwa kuwa maudhui ya kifungu hiki hayaendani na maudhui ya Ibara ya 20(2) ya Katiba ya nchi."

MWENYEKITI: unajua ndio hiyo niliyokuwa nasema kuwa Mwenyekiti wa Kamati kwamba mkija hapa Kamati na Serikali kidogo mnatufanya Bunge zima tukose namna ya kwenda au basi Mwenyekiti unakumbuka maana yake hotuba yako inasema.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti msingi ya Kanuni ya 84(3) inaitaka Kamati kuishauri Serikali na kukubaliana baadhi ya hoja. Kwa hiyo inawezekana tulishauri Serikali ikaona hakuna msingi wa mashauriano tuliyotoa kanuni inaruhusu Serikali kuendelea na utaratibu kuendelea.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Naomba sana tusikilizane kwa sababu fujo hazisaidii chochote *no, no, no* tupeane nafasi mta-/loose track ya jambo ambalo labda ni muhimu kwa sababu tu ya kukosekana nidhamu. Ni jambo ambalo si sawa Mwenyekiti malizia au ulikuwa umemaliza?

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni msingi wa mjadala, ukiangalia kanuni 84(3) inaitaka Kamati kuishauri tu Serikali, kwa hiyo sisi tumeishia katika kushauri na ushauri huo upo kwa mujibu wa maandiko ambayo yapo, maandiko ambayo yamewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, jukumu la kukubali au kukataa ni jukumu la Serikali, hivyo, tunaafikiana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto kwa dakika tatu tu.

MHE. KABWE R. Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo kwenye Kamati ya Mheshimiwa Mchengerwa, mambo ambayo Kamati iliyapendekeza yalikwenda Serikalini, Waziri akaja na jedwali ambalo linaeleza ushauri wa Kamati na mambo ambayo Serikali imekubaliana na Kamati na ndio hilo ambalo umeletewa hapo mbele. Taarifa hii ukiisoma ibara zote za taarifa hii zimeleta yale mambo ambayo Kamati na Serikali wamekubaliana, humu hamna *controversy, problem ni kwamba schedule of amendment* imekuja tofauti na yale mambo ambayo yamekubaliwa ndani ya Kamati na ndio maana kila jambo tunakupa na *reference* ya hotuba ya Kamati kwamba hiki tumekubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ututoe hapo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi halafu tutarudi kwa Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nakuja kwenye misingi wa uendeshaji tu. Kwa kawaida na siku zote haijawahi kutokea kwamba maoni ya Kamati yakawa ni uamuzi. Haijawahi kutokea humu ndani kwamba maoni ya Kamati yakawa ndiyo maoni ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Wajumbe wa Kamati pamoja na kwamba Serikali iko ndani wanaweza wakapendekeza mengi na baadaye Serikali ikachambua ikaleta maoni tukaja kubishana, vinginevyo sasa kungekuwa na maoni ya pande mbili ya nini?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ndiyo maana kitabu hiki kimeandikwa maoni siyo uamuzi. Kwa hiyo, mimi nakwenda kwenye misingi tu haya ni maoni...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Yanaweza kuwa yalisemwa lakini Serikali ime-digest imeona siyo sahihi. Kwa hiyo, haya ni maoni. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Taarifa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Tafadhalii sana, nimetoa zaidi ya hata ambacho kwa kawaada inaruhusiwa, sasa mumsikilize Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuna taarifa ya Kamati na tuna Jedwali la Serikali ndani ya Kamati, Jedwali linarudi Serikalini na linaporudi Serikalini linakwenda kuandika Jedwali la Marekebisho ya Muswada. Unaporudi kuandika Jedwali la Marekebisho, *custodian* anayatunza Katiba ya nchi ndani ya Serikali ni AG. AG ameshatuambia Serikalini kwamba kifungu hiki hakivunji Katiba na amekizungumza wakati anazungumza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi sasa wa Jedwali hili kuja hivi ilivyo ni mwongozo unaotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na amesema jambo hili toka mwanzo. Hivi ndivyo ilivyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Tunavuka sasa Waziri ameshamaliza tunafanya maamuzi.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

(Ibara iliyo tajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zillipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa
Mwenyekiti, naondoa maoni hayo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zillipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 21

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

Ibara ya 22
Ibara ya 23

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 24

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 25

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 26

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto.

MHE KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni moja ya Ibara ambayo Wajumbe wa Kamati wamekubaliana, Serikali ikakiri kwamba imekubali, *Schedule of Amendment* iliyotoka jana saa sita mchana ikaonekana kwamba wamekubali na naomba nifanye *reference* ya Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, ukurasa wa 40. Anasema: "Ibara ya 26(2) ifutwe kwa kuwa kifungu hiki hakina mantiki kwa kuzingatia kuwa Msajili alishajihakiki kuhusu taarifa za chama husika kabla ya kutoa usajili wa kudumu. Aidha, masharti haya siyo sehemu ya masharti yaliyoainishwa katika Ibara ya 20(2) ya Katiba ya nchi." (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumza hoja hii na wewe ulisisitiza hapa Wajumbe wanaofuata waje kujibu. Mheshimiwa Ngeleja akaja kujibu akasema tutazame *Schedule of Amendment* jambo hilo limekuwa *taken into consideration*. Jambo hilo halijawa *taken into consideration*, halipo.

MBUNGE FULANI: Wamerudisha tena.

MHE KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, ni wazi kwamba endapo kama mtu ye yeyote atatoa taarifa ya uongo, ya kugushi kwa lengo la kumu-*induce* mtu mwingine kufanya maamuzi, yale maamuzi ya huyo mtu siyo maamuzi huria, Wanasheria wanasema sio *free consent*. Pale yatakapotambulika kwamba maamuzi haya yalipatikana kwa ulaghai, ndipo hapo hapo uhalali wa maamuzi yale unafutika, hii ni kanuni ya kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukirudi kwenye Ibara ya 20(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, endapo yale maelezo yote chama kilighushi, kilifanya ulaghai, pale itakapo julikana kwamba huu ni ulaghai uhalali wake unafutwa kwa sababu kile ni *fraud*. Sasa huwezi ukasema kwa sababu mtu amemdanganya Msajili leo, kesho Msajili amegundua basi asirekebishe kwa sababu alidanganywa jana, haitawezekana. Kwa hiyo, hii iko sahihi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Labda niseme neno moja, kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, ninyi mnatuvuruga, mnatuvuruga kabisa. (*Makofii*)

Kamati mnapokuja tofauti ya Serikali tena kwa kuandika humu ndani maana yake ni kwamba Serikali, natumia tu maneno yale ya kienyeji, Serikali imekuwa kiburi kule ndani kwa jambo la msingi.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Kwa hiyo, mnapotuandikia hapa mnatuletea jambo ambalo mnapendekeza kama Wajumbe wa Kamati,

kwa kawaida yetu ya Bunge mnataka sisi tuwaunge ninyi mkono dhidi ya Serikali ambayo haikuwasikiliza kule. Sasa mnayaandika ya nini? Kwa hiyo, wakati mwingine mjitahidi kuandika vitu ambavyo vina msingi. Siyo mnatushawishi kama Kamati maana yake ninyi ndiyo Bunge letu dogo kula, halafu mkija huku tena inakuwa taabu sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa imeandikwa kwenye *schedule* yetu na sisi tunaomba Bunge lako tukufu lipitishe hiyo *schedule* kama ilivyoandikwa. Tunasema hivyo kwa sababu unaweza ukakuta mazingira ambayo labda wakati chama kinakwenda kufanya usajili, labda *desk officer* atakayeshughulikia usajili wa chama hicho hapo akakutana na mazingira ambayo chama *kikam-corrupt*, usajili ukapatikana, baada ya hapo jambo hilo likaonekana limefanywa *in a fraud manner*, sasa utaacha tu kwa sababu chama kilishasajiliwa? Haiwezekani. Huo ndiyo msingi wa hii hoja ambayo imejitokeza hapa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, yaani nimewaelewa vizuri kabisa, sasa nachoshangaa kwa nini Kamati inatushawishi sisi? (*Makofii/Kicheko*)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 27

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 28

Ibara ya 29
Ibara ya 30

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 31
Ibara ya 32

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Jedwali la 1
Jedwali la 2

(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Sasa naagiza Katibu uhakikishe unavipa namba upya vile vifungu tulivyovipitia kwa mujibu wa marekebisho ya vile vilivyofutwa na vinginevyo, kufanya *renumbering* vizuri wakati tutakapokuwa tunamaliza zoezi hili la uwekaji sawasawa wa Muswada wetu na kilichopitishwa na Bunge kihalsia, Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.
Mheshimiwa Waziri, nakuomba utoe taarifa.

T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika,
kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa taarifa

kwamba Kamati ya Bunge imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Vyama vyा Siasa wa mwaka 2018 (*The Political Parties (Amendments) Bill, 2018*) kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, wajibu wangu ni kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vyा Siasa wa Mwaka 2018 sasa tuufanyie maamuzi.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Nadhani walioafiki wameshinda. (*Makofii*)

Tunaendelea, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vyा Siasa kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo (*A Bill for an Act to Amend the Political Parties Act in order to keep the Law updated with challenges observed in the implementation*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tunapofikia mwisho wa zoezi hili. Nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali kwa usikivu, kwa kweli marekebisho ambayo mmeefanya ni mengi sana, mmezingatia mambo mengi yaliyoongelewa na wadau wakiwepo na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile Kamati yetu ya Katiba na Sheria kama nilivyosema mmeefanya kazi nzuri sana, sana, tunaendelea kuwapa moyo muendelee kuchapa kazi na Kamati nyingine zinazofuata nazo zijiandae vizuri.

Ushauri wangu tu ni ule ule kwamba Kamati mnapotuletea jambo hapa yaani *traditions* za Kibunge ni kwamba Kamati mnapotushawishi kuelekea upande fulani mara nyingi sisi ndiyo tunatakiwa tufanye maamuzi kuelekea upande huo. Sasa mkitoa mjadala wenu kule mkatuletea hapa inatupa shida. Kwa hiyo, ndiyo maana mambo yenu mnapaswa kuyamaliza kule la sivyo siyo lazima mulandike. Vinginevyo nawapongezeni sana, najua jinsi ambavyo mmeefanya kazi *overtime* na kufika hapo.

Nimpongeze Msajili wa Vyama vyta Siasa na timu yake yote na vyama vyote vilivyoandikishwa katika nchi yetu ambavyo vilishiriki kwa namna moja ama nyingine katika mchakato mzima huu. Mheshimiwa Waziri mwenyewe nikupongeze sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu kazi yako hii tunakupongeza sana, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu zenu zote za *drafting*. Kwa maana hiyo, kwa kuwa sisi tumemaliza, tutapeleka Muswada huu kwa Mheshimiwa Rais ili ikimpendeza atoe kibali chake kwa mujibu wa Ibara ya 97(1) ya Katiba yetu.

Kwa vile shughuli zote zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika tena kwa wakati, kwa uendeshaji wa kisayansi, mtaona muda uko pale pale. Basi nichukue nafasi hii sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano,
Tarehe 30 Januari, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*